# BUNGE LA TANZANIA

___________

## MAJADILIANO YA BUNGE

___________

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 17 Aprili, 2020

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge yaani hii meza hapa utafikiri hospitali, maana *disinfectant* wanazotumia ni zile tunazozisikia hospitali. Utafikiri meza ya daktari, lakini yote haya ni kwa ajili ya *COVID-19*. Natumaini tunaendelea kuchukua *precautions* mbalimbali.

Natumaini tunaendelea kutembea na *sanitizer* zetu na kama kuna maoni ya nini cha kufanya ili kuhakikisha tunaimarisha hali, basi tuendelee kupeana. Nasi tunatafuta mitambo ambayo mtu akipita, basi inampuliza pande zote. Ninaamini katika muda usiozidi wiki moja tutakuwa nayo na sisi katika baadhi ya maeneo. Tunajali sana afya zenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa 3 Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko huo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

## MASWALI NA MAJIBU

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 93

### Hitaji la Shule ya Kidato cha Tano na Sita – Jimbo la Geita Vijijini

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

(a) Jimbo la Geita Vijijini halina Shule kwa ajili ya Kidato cha Tano na Sita: Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Shule za Kidato cha Tano na Sita katika Jimbo hili?

(b) Shule za Sekondari Bugando na Rubanga zipo tayari kwa ajili ya ujenzi wa madarasa hayo: Je, Serikali iko tayari kutoa fedha za ujenzi kwenye shule hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imepatiwa kiasi cha shilingi milioni 215 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa manne na mabweni mawili katika Shule ya Sekondari Bungando ambayo inatarajiwa kuanza kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano katika mwaka wa fedha 2020/2021. Shule nyingine zilizobaki zitaendelea kujengwa kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

Na. 94

## Kuondoa Magugu Maji - Ziwa Babati

**MHE. ESTER A. MAHAWE** aliuliza:-

Magugu maji yaliyopo Ziwa Babati yanahatarisha uwepo wa Ziwa hilo:-

Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya kuondoa magugu maji hayo ili kunusuru Ziwa hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, magugu maji yaliyopo kwenye Ziwa Babati pamoja na maziwa mengine kama Ziwa Victoria yameenea kwenye kingo za maziwa hayo na hivyo kuhatarisha mifumoikolojia na bioanuai ya maziwa hayo. Kuenea kwa magugu maji hayo kumechangiwa zaidi na kuongezeka kwa virutubishi *(nutrients)* ziwani vinavyotokana na shughuli za kilimo kisichozingatia hifadhi ya mazingira hasa kinachohusisha matumizi makubwa ya mbolea na viuatilifu. Aidha, uchungaji holela wa mifugo kando ya ziwa umechangia kushamiri kwa magugu hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia suala hilo, Ofisi imewasiliana na Wizara ya Kilimo ili kuondoa Kanuni za Udhibiti ya Magugu Maji ya Mwaka 1999 iliyoandaliwa chini ya Sheria Na. 13 ya Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea ya Mwaka 1997. Lengo la Kanuni hii ilikuwa ni kuzuia uvunaji wa magugu maji kwa ajili ya matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, tumeshauri kwa vile kanuni hizo zimedumu zaidi ya miaka 20, ni vema sasa zikaondolewa ili kuruhusu uvunaji wa magugu maji ambayo ni mengi na athari

zake ni kubwa katika maziwa ikiwa ni pamoja na Ziwa Babati. Aidha, magugu maji haya yana faida kubwa ikiwa ni pamoja na kutumika kutengeneza rasilimali kama karatasi, nishati mbadala, mifuko mbadala wa plastiki kama inavyofanyika katika nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeandaa Mkakati na Mpango Kazi wa Kusimamia Viumbe Vamizi (2019-2029) ikiwemo magugu maji ambao pamoja na mambo mengine umeweka lengo la kuhakikisha tunahuisha masuala ya udhibiti na usimamizi wa magugu maji katika sheria ili kudhibiti kuenea kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali inakamilisha mwongozo utakaobainisha shughuli ambazo zinaweza kufanyika ndani ya mita 60 kutoka kwenye fukwe za bahari na kingo za maziwa, mito na mabwawa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kifungu cha 57 (4), ili kudhibiti shughuli zinazochochea kushamiri kwa magugu maji.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzihamasisha Wizara za Kisekta, taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi kuhakikisha zinadhibiti kuenea kwa magugu maji kwa kutekeleza miongozo na mikakati iliyopo.

Na. 95

**Tatizo la Majisafi na Salama Tunduma**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi wa Tunduma maji safi na salama ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa Tunduma na wageni wanaoingia kila siku?

(b) Utekelezaji wa miradi hiyo itaanza lini na mfadhili wake ni nani?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Jimbo la Tunduma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wananchi wa Tunduma wanapata huduma ya majisafi na salama, Serikali inaendelea kutekeleza miradi miwili (2) katika Mtaa wa Mpandekati ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; na katika Mtaa wa Chipaka umefikia asilimia 92.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa miradi hiyo kutahudumia jumla ya watu wapatao 7,000 na kuongeza asilimia 4.38 ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama. Aidha, Serikali imechimba visima vitano katika maeneo ya Nandanga, kimoja; Chapwa, viwili; Ipito, kimoja; na Majengo kimoja; ambapo usanifu umefanyika na ujenzi utaanza mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika kuboresha huduma ya maji Tunduma, kupitia programu ya malipo kwa matokeo, Serikali inatekeleza mradi mmoja katika Mitaa ya Chapwa – Mpemba - Katete ambapo ujenzi wa miundombinu ya maji umeanza na umefika asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi huu kutahudumia jumla ya watu wapatao 25,789 na kuongeza asilimia 16.16 za upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama.

Na. 96

**Kukamilisha Vipande vya Mradi wa Maji wa Mkwiti**

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA** aliuliza:-

Ili kutatua ukosefu wa maji katika Vijiji vyote vilivyoko Kaskazini mwa Wilaya ya Tandahimba na baadhi ya Vijiji vya Wilaya ya Newala Serikali imeanzisha mradi wa Mkwitu. Katika mradi huo vipande viwili vipo katika hatua za utekelezaji lakini kipande cha tatu hakijafanyiwa kazi yoyote:-

Je ni lini Serikali itakamilisha vipande vyote vitatu ili wananchi walioko katika eneo la mradi waweze kupata maji?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tandahimba eneo la Kaskazini lina jumla ya Vijiji 21. Kati ya hivyo, Vijiji vitano vinapata huduma ya maji safi na salama na Vijiji 16 vya Mkwiti Juu, Mkwiti Chini, Mmeda, Libode, Litehu, Mabeti, Naanala, Mkuti, Nanjanga, Mangombya, Ngunja, Namindondi Juu, Namindondi Chini, Chidede, Mahoha na Mkola Juu wenye jumla ya wakazi 21,384 vinatarajia kupata huduma ya maji kupitia mradi wa Maji wa Mkwiti.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 6.712 na kutekelezwa kwa muda miezi 36. Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika vipande *(lots)* vitatu.

Mheshimiwa Spika, kipande cha kwanza *(Lot No. 1)* kinagharimu kiasi shilingi bilioni 2.772. Utekelezaji wake umefikia asilimia 60 na kinatarajia kukamilika mwezi Juni, 2020. Kipande cha pili kitakachogharimu shilingi bilioni 1.8, kinahusisha ujenzi wa njia kuu ya bomba kutoka Kijiji cha Idomnole hadi Kijiji cha Mangombya umbali wa mita 17,200 ambacho utekelezaji wake umefikia asilimia 93 na kinatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2020.

Mheshimiwa Spika, kipande cha tatu kimepangwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo kitahusisha ulazaji wa mabomba yenye mtawanyo wa maji yenye urefu wa kilometa 42.375 na ujenzi wa vioski 42.

Na. 97

**Ving'amuzi (*VTS*) Kupunguza Ajali**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Serikali kupitia Wakala wake *LATRA* imeanzisha mfumo wa kuratibu mwendo wa magari hususani mabasi ili kupunguza ajali kwa kufungwa ving'amuzi *(VTS).*

Je, vifaa hivyo vimepunguza ajali kwa kiasi gani?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *Vehicle Tracking System* (*VTS*) ni kifaa maalumu kinachofungwa kwenye gari ili kufuatilia mwendo wa gari barabarani, kuonyesha eneo na mahali. Kifaa hiki hakipunguzi mwendo wa gari bali hutoa ishara kwa dereva endapo atakuwa amezidi mwendo ulioidhinishwa kisheria na hivyo kumfanya dereva kupunguza mwendo ili kufikia *speed* iliyopendekezwa na iliyoidhinishwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, takwimu za ajali zilizosababishwa na mwendokasi kwa magari ya abiria (Mabasi) yanayofanya safari za mikoani zimeendelea kupungua kwa kiwango kikubwa. Mathalan, katika mwaka 2016 kulikuwa na ajali 730, mwaka 2017 kulikuwa na ajali 509 na mwaka 2018 kulikuwa na ajali 364 na mwaka 2019 zimetokea ajali 231. Mfululizo huu wa upunguaji wa ajali unaonyesha mafanikio yanayopatikana kutokana na matumizi ya ving'amuzi kwenye mabasi ya abiria.

Na. 98

**Kuhakiki Leseni za Bodaboda na Bajaji**

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR** aliuliza:-

Je, Serikali haioni ni wakati sasa wa kuhakiki leseni za bodaboda na bajaji ili kuhakikisha kwamba zimepatikana kisheria kwa kuwa ajali nyingi zinatokana na bajaji na bodaboda?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainabu Mussa Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhakiki wa leseni za madereva ikiwa ni pamoja na madereva wa bodaboda na bajaji unaofanywa na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani umesaidia kupunguza ajali za barabarani ikiwa ni pamoja na za bodaboda na bajaji. Mathalan, mwaka 2014 zilitokea jumla ya ajali 4,169, vifo 928 na majeruhi 3,884. Mwaka 2015 zilitokea jumla ya ajali 2,626, vifo 934 na majeruhi 2,370. Ukilinganisha takwimu hizi kwa kipindi cha miaka hiyo miwili kinaonyesha upungufu wa ajali 1,543 sawa na asilimia 37%, ongezeko la vifo sita sawa na asilimia 0.64% na upungufu wa majeruhi 1,514 sawa na asilimia 38.9%.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwaka 2017 zilitokea ajali 1,459, vifo 728 na majeruhi 1,090 ambapo mwaka 2018 zilitokea ajali 876, vifo 366 na majeruhi 694. Mlinganyo wa takwimu hizi unaonyesha kwa kipindi hicho cha miaka miwili kinaonyesha kupungua kwa ajali 583 sawa na asilimia 39%; kupungua kwa vifo 366 sawa na asilimia 50.2%; na upungufu wa majeruhi 396 sawa na asilimia 36.3%

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kinafanya operesheni za kuwakamata madereva

wote ikiwa ni pamoja na bodaboda na bajaji wanaokiuka sheria na kanuni za usalama barabarani. Aidha, Kikosi pia kinafanya ukaguzi wa leseni za madereva ili kuhakikisha kuwa leseni zote zimepatikana kwa kufuata utaratibu na kwa mujibu sheria kupitia mashine maalum kwa kuingiza namba ya leseni na kutoa taarifa za uhalali wa leseni.

Na. 99

**Barabara Inayounganisha Wilaya za Malinyi na Namtumbo**

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI** aliuliza:-

Kipande cha barabara kutoka kwa Mpepo Wilayani Malinyi hadi Londo darajani kinaunganishia Wilaya hiyo na Wilaya ya Namtumbo na ndicho kiungo cha Mkoa wa Ruvuma na Morogoro katika barabara Kuu ya Lumecha – Kitanda – Londo – Kilosa kwa Mpepo – Lupiro – Ifakara – Mikumi:-

(a) Je, kipande hicho kitafunguliwa lini?

(b) Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami kama iliyoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya 2015/2020?

(c) Je, ni lini upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mtwara Pachani – Lusewa – Lingusenguse – Nalasi – Tunduru utakamilika?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Edwin Amandus Ngonyani, Mbunge wa Namtumbo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ilifungua kipande cha

barabara kilichokuwa kinabakia katika sehemu ya kutoka Kilosa kwa Mpepo hadi Londo katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017 na Wizara kupitia *TANROADS* inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hiyo kwa mwaka ili iweze kuendelea kupitika vizuri.

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Lumecha – Kitanda – Londo – Kilosa kwa Mpepo – Lupiro – Ifakara – Mikumi imekamilika. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Lumecha ya Mikumi – Londo – Ifakara.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Mikumi hadi Kidatu yenye urefu wa kilometa 35 na Daraja la Kilombero (384m) na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 9.14. Aidha, kwa sasa ujenzi wa sehemu ya Kidatu hadi Ifakara yenye urefu wa kilometa 66.9 na Daraja la mto Ruaha Mkuu unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Upembuzi Yakinifu, Usanifu wa Kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mtwara Pachani – Lingusenguse – Nalasi – Tunduru yenye urefu wa kilometa 300 ulisainiwa tarehe 23 Agosti, 2017 kati ya Wakala wa Barabara *(TANROADS)* na Mhandisi Mshauri aitwaye *Advance Engineering Solution Ltd (AESL).* Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni ilikamilika Februari, 2020.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI**: Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutoa majibu. Hata hivyo, jibu la kipande cha barabara cha kutoka Londo hadi Kilosa kwa Mpepo kidogo halijaeleweka. Naomba Serikali itujibu kuhusu kufungua kipande hicho. Kwa sasa hakipitiki kwa magari ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuhusu barabara ya Mtwara Pachani hadi Nalasi hatua inayofuata ya kuijenga kwa kiwango cha lami itaanza lini?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyojibu katika jibu la msingi, kipande cha barabara kutoka Kilosa kwa Mpepo hadi Londo kilifunguliwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hivi sasa Serikali kupitia Wakala wa Barabara nchini inaendelea kuifanyia ukarabati barabara hiyo hatua kwa hatua kadri ya upatikanaji wa fedha ili kuiimarisha. Hadi mwezi Februari, 2020, jumla ya kilometa 20 zimekamilika kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Mtwara Pachani hadi Nalasi. Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa Nyaraka za zabuni kazi ambayo imekamilika Februari, 2020. Kufuatia kazi hiyo kukamilika, Serikali imejua gharama za ujenzi na sasa inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Hivyo, ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza mara baada ya fedha za ujenzi kupatikana.

Na. 100

**The Great North Road**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Barabara iliyopewa jina la "*The Great North Road*" hapa nchini ilipita njia ya Tunduma – Mbeya – Chunya – Itigi – Manyoni – Singida – Babati – Arusha hadi Namanga.

Je, ni sababu zipi zimefanya Serikali kubadili njia hiyo kupitia *GN* na kuweka Mbeya – Iringa – Dodoma – Babat – Arusha na Namanga?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haina kumbukumbu zinazoonesha kuwa barabara iliyopewa jina la *"The Great North Road"* hapa nchini ilipita njia ya Tunduru – Mbeya – Chunya – Itigi – Manyoni – Singida – Babati – Arusha hadi Namanga.

Mheshimiwa Spika, Barabara Kuu ya Kaskazini (*The Great North Road*) inaanzia *Cape Town* nchini Afrika Kusini na kupita Botswana – Zimbabwe – Zambia – Tanzania – Kenya – Ethiopia – Sudan na kuishia *Cairo* nchini Misri (kilomita 10,288). Kwa upande wa Tanzania barabara hii inapita katika Mikoa ya Songwe – Mbeya – Njombe – Iringa – Dodoma - Manyara na Arusha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa "*The Highway Ordinance Cap. 167, First Schedule, Main Road G.N. No. 471* ya Mwaka 1962, Barabara Kuu ya Kaskazini hapa nchini inapita Tunduma – Mbeya – Iringa – Dodoma – Babati – Arusha hadi Namanga na ina urefu wa kilometa 1,222. Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya zamani ya barabara *(The Highway Ordinance Cap. 167*) ya Mwaka 1932, Barabara Kuu ya Kaskazini inapita katika maeneo niliyoyataja hivi punde.

Na. 101

**Kufungua Barabara ya Liwale – Ulanga**

**MHE. DUA W. NKURUA** aliuliza:-

Katika kutekeleza mpango wa kuunganisha mikoa yote nchini kwa barabara za lami.

Je, ni lini Serikali itafungua barabara ya Liwale – Ulanga ili kurejesha mawasiliano kati ya Mkoa wa Lindi na Morogoro?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dua William Nkurua, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara ya Liwale – Ulanga yenye urefu wa kilomita 215 inapita kwenye Hifadhi ya Wanyama ya *Selous*. Kutokana na kupita kwenye Hifadhi ya Wanyama, sehemu hii ya kuunganisha mikoa ya Lindi na Morogoro itafanyiwa upembuzi wa awali ambao ndiyo utakuwa msingi wa maamuzi ya kuendelea na hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na hatimaye kujenga barabara hiyo.

Na. 102

**Kujenga Miundombinu ya Umwagiliaji Bonde la Bugwema-Musoma Vijijini**

**MHE. AMINA NASSORO MAKILAGI** aliuliza:-

Bonde la Bugwema Musoma Vijijini katika Mkoa wa Mara ni bonde zuri sana kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji?

**MHE. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa Bonde la Bugwema ulianza mwaka 1970 chini ya iliyokuwa Mamlaka ya Pamba Tanzania *(Tanzania Cotton Authority-TCA)* ili kuweza kumwagilia zao la pamba, kwa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulioanza mwaka 1974 na kukamilika mwaka 1978 na kuanza ujenzi ambao ulisitishwa mwaka 1985 kwa kukosekana fedha za ujenzi. Aidha, hadi

wakati huo jumla ya hekta 450 zilikuwa zimeendelezwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1992 Serikali ililiagiza Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kukamilisha ujenzi na kuuendesha mradi huo lakini kazi hiyo haikufanyika na mradi ukasitishwa. Aidha, Serikali imeshafanya upembuzi yakinifu na inaendelea na taratibu za kufanya usanifu wa kina kabla ya kuanza ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma iliingia makubaliano *(MOU)* na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* mwaka 2019 chini ya usimamizi wa Mkoa wa Mara kwa ajili ya kuendeleza Bonde la Bugwema.

Mheshimiwa Spika, katika makubaliano hayo, kumeonesha namna Benki, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma na wanachi kutoka vijiji vinavyozunguka bonde hilo vya Masinono na Bugwema watakavyoshiriki katika uendelezaji wa bonde hilo kupitia utaratibu wa ubia *(Public-Private Partneship-PPP)*.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa *TADB* inaendelea na ufuatiliaji wa nyaraka mbalimbali kama michoro ili kujiridhisha na namna ya kuitekeleza kazi hiyo. Aidha, lengo la Serikali ni kujenga mradi huo kwa haraka kibiashara ili kuongeza vipato vya wakulima na Taifa kwa ujumla.

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa nikukaribishe Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ili uweze kuwasilisha hoja yako, tafadhali Mheshimiwa Waziri endelea sasa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, shukurani na pole; awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na fadhila kwa kutujalia afya njema ya kuweza kuwa hapa leo kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka Fedha wa 2020/2021. Aidha, kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kuitumikia Serikali ya Awamu ya Tano katika nafasi ya Waziri wa Katiba na Sheria. Naahidi kuitumikia nafasi hiyo kwa uadilifu, uaminifu na unyenyekevu mkubwa kwa maslahi mapana ya Taifa na wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa majonzi makubwa nikupe pole wewe, Bunge lako, familia na wananchi wote wa Jimbo la Newala Vijijini kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar aliyefariki tarehe 15 Januari, 2020. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa familia za watu waliopoteza maisha kutokana na madhara ya mvua kubwa zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, salamu za pongezi, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa jitihada zenu za dhati katika kuisimamia na kuishauri Serikali. Bunge lako limeendelea kutoa ushauri na maelekezo ambayo yamewezesha kuboresha utendaji kazi wa Serikali wa kuwatumikia wananchi kwa kuhakikisha

haki na huduma mbalimbali za kisheria zinaendelea kuboreshwa na kutolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ushauri na maelekezo ya Bunge lako yametuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Aidha, Wizara imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa umakini na kwa kuzingatia, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015, Sera, Mipango, Mikakati na Sheria mbalimbali zilizopo ikiwemo Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021. Malengo ya Maendeleo ya Afrika 2063, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030, Mikakati mbalimbali ya Wizara, Idara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, pia tumetekeleza maelekezo na ahadi mbalimbali za viongozi wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanazozitoa katika nyakati mbalimbali katika kutekeleza majukumu yao. Kutokana na mafanikio hayo, Wizara itaendelea kuongeza juhudi katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi kwa nia ya kufanikisha lengo kuu la nchi yetu la kujenga Taifa lenye uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Taifa limepiga hatua kubwa katika kutimiza lengo hili, tuendelee kushikamana na kulinda umoja na uzalendo wetu, kufanya kazi na kutekeleza wajibu wetu katika safari iliyobaki kuelekea uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Tuliahidi kwa pamoja, tukapanga, tukatekeleza, tuendelee kuchapa kazi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa,(Mb) na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo ameweka msingi wa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa

fedha 2020/2021. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako hasa kwa kipindi hiki ambapo tunakabiliwa na janga la Corona na pia na madhara yaliyotokana na mvua nyingi na mafuriko katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba niwapongeze Wenyeviti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi kwa uongozi wao mahiri na kuziwezesha kamati wanazoziongoza kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi. Wizara yangu inayo imani kubwa kwao na itaendelea kuwapatia ushirikiano unaostahili katika kipindi chote cha uongozi wao. Vilevile, natoa shukrani za dhati kwa kamati hizo kwa kazi kubwa ya kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Nilihakikishie Bunge lako kuwa wizara yangu inatambua na kuthamini mchango wa kamati hizi katika kuhakikisha Sekta ya Sheria inachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni, mazingira na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia hayo wizara itandelea kuongeza juhudi katika kutekeleza majukumu yake kwa bidii na weledi ili kufanikisha lengo kuu la nchi yetu la kujenga Taifa lenye uchumi wa kati na unaochangiwa na maendeleo ya viwanda ifikapo mwaka 2025. Hivyo, tunapoelekea kwenye uchumi huo wa kati ifikapo mwaka 2025 wizara inaendelea kufanya mageuzi na maboresha ya kuwa na mfumo imara wa kikatiba, kisheria na utoaji haki ambayo itahakikisha kwamba kama Taifa tuendelee kushikamana, kudumisha uzalendo na kulinda umoja wetu.

Mheshimiwa Spika, Dira na Dhima, Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na Dira ambayo ni Katiba na Sheria wezeshi kwa Maendeleo ya Taifa. Aidha, Dhima ya Wizara ni

kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na sheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa. Dira na dhima hizi zinalenga kuweka mazingira rafiki ya kisera na ya kisheria ya kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa, kudumisha hali ya amani, utulivu na utangamano wa kitaifa ambazo ni nguzo muhimu kwa mstakabali wa ustawi wa jamii na taifa letu na katika kujenga mazingira wezeshi ya upatikanaji haki na huduma bora za kisheria kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Muundo na Majukumu ya Wizara; Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Muhimili wa Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto. Aidha, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 144A la tarehe 22 Aprili, 2016 wizara imeendelea kutekeleza majuku yake ya kuhakikisha kuwa nchi inaongozwa kwa katiba, sheria, kanuni na taratibu zilizopo kupitia taasisi zilizotajwa. Majukumu ya wizara yameelezwa kwa kina katika ukurasa wa tano wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha 2015/ 2016 hadi 2019/2020. Kama unavyofahamu mwezi Oktoba, 2020 tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu na hivyo hii ni taarifa yangu ya mwisho katika kipindi hiki. Hivyo, nimeona ni muhimu kutoa japo kwa kifupi tathmini ya masuala ambayo wizara yangu na taasisi zake imeyatekeleza katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2019/2020. Taarifa hiyo ya utekelezaji imeoneshwa kwenye ukurasa wa sita hadi wa saba na maelezo ya kina yanapatikana katika Kiambatisho A cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Mpango wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, wizara yangu ilibainisha

maeneo mahsusi ya kipaumbele kwa msingi wa kutekeleza dhima ya wizara katika kutoa huduma bora za kisheria nchini. Maelezo kuhusu maeneo hayo ya kipaumbele yanapatikana katika Kiambatisho B cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 wizara ilijielekeza zaidi katika kutekeleza jumla ya maeneo 25 ya kipaumbele yafuatayo:-

(i) Kutunga sheria zinazohusu masuala ya kisheria na kusimamia utekelezaji wake;
(ii) Kushughulikia masuala ya kikatiba;
(iii) Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki;
(iv) Kuendesha mashtaka, uandishi, urekebu na ufasili wa sheria,
(v) Uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi,
(vi) Utoaji wa ushauri wa kisheria,
(vii) Usimamizi wa mikataba, mikataba ya kikanda na kimataifa;
(viii) Utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria, haki za binadamu na haki za watu;
(ix) Mapitio ya sheria mbalimbali,
(x) Urejeshwaji wa wahalifu na ushirikiano wa kimataifa katika makosa ya jinai;
(xi) Usajili wa matukio muhimu ya binadamu, kuratibu masuala ya utajiri na maliasili za nchi;
(xii) Mafunzo ya uongozi wa mahakama kwa utoaji haki,
(xiii) Mfunzo ya wanasheria kwa vitendo;
(xiv) Kutembelea na kufanya ukaguzi wa magereza na sehemu za kuhifadhia watuhumiwa katika vituo vya polisi;
(xv) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mahakama;
(xvi) *Program* ya kutenganisha upelelezi na uendeshaji wa mashtaka;
(xvii) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kimahakama;
(xviii) Program ya maboresho ya Sekta ya Sheria, maboresho ya mfumo wa haki jinai, maendeleo ya rasilimali watu na kushughulikia janga la ugonjwa wa *COVID-19* linalosababishwa na maambukizi ya virusi vya corona.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara pamoja na mafanikio yaliyopatikana yanaonekana kuanzia katika ukurasa wa 8 hadi ukurasa 46 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara na Taasisi zake imeendelea kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha kwamba inawajibika ipasavyo kwa wananchi kupitia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015, ikiwemo ahadi na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa. Miongoni mwa ahadi hizo ni pamoja na kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma; kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na kuendeleza utawala wa sheria; na kuimarisha mfumo wa utoaji haki. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa ahadi hizo yanapatikana katika ukurasa wa 46 hadi 56 wa hotuba yangu*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtiririko wa Mapato na Maduhuli ya Serikali ya mwaka wa fedha 2019/2020; Makusanyo ya Maduhuli; katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ilipanga kukusanya jumla ya Sh.12,606,487,000 kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara ilikusanya jumla ya Sh.9,248,652,497.00 sawa na asilimia 73.36 ya lengo, maelezo zaidi kuhusu makusanyo ya maduhuli yanapatikana katika jedwali namba moja kwenye ukurasa wa 57 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, fedha Zilizoidhinishwa na Kupokelewa kwa Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo; katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa na Bunge jumla ya Sh.181,337,627,874 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo Sh.77,755,166,000 ni za mishahara na Sh.3,532,963,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Sh.30,049,498,874 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya

fedha za Maendeleo jumla ya Sh.16,248,363,000 ni fedha za ndani na Sh.13,801,135,874 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara ilipokea jumla ya Sh.130,934,893,787 sawa na asilimia 72 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo Sh.55,419,744,545 ni mishahara na Sh.63,043,351,265 ni matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo ni Sh.12,469,797,977 sawa na asilimia 41 ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa. Kati ya hizo Sh.6,037,318,052 ni fedha za maendeleo za ndani na Sh.6,432,479,725 ni fedha za maendeleo kutoka nje. Mtiriko wa fedha zilizopitishwa na Bunge na kiasi kilichopokelewa kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 kwa Mafungu ya Wizara ni kama inavyooneshwa katika majedwali namba mbili na namba tatu yanayopatikana kuanzia ukurasa wa 58 hadi 60 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 ni pamoja na, Kuongezeka kwa imani ya wananchi juu ya utendaji kazi wa Taasisi na mifumo ya kusimamia Sheria na utoaji haki nchini. Maelezo zaidi kuhusu mafanikio yaliyopatikana yamefafanuliwa katika ukurasa wa 60 hadi 63 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana ni juhudi za pamoja kati ya Wizara, Idara, Taasisi na wadau wetu wakiwemo washirika wa maendeleo katika sekta ya Sheria. Hivyo, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano mzuri uliopo kati yetu na Washirika wa Maendeleo ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake *(UN Women),* Jumuiya ya Ulaya *(EU),* Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Nchi ya Uingereza *(DfID),* Shirika la Maendeleo Kimataifa la Nchi ya Canada *(CDC)* na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Nchi ya Denmark *(DANIDA)* pamoja na wadau wengine ikiwemo Kampuni ya Simu ya TIGO. Napenda niwahakikishie kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini uhusiano mzuri uliopo kati yetu na

wadau hawa na tutahakikisha kuwa, unaimarishwa kwa maendeleo ya sekta ya Sheria na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Julai, 2019 na Machi, 2020, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo nimezieleza kwa kina katika ukurasa wa 63 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, mikakati ya kutatua changamoto; katika kutatua changamoto hizo, Wizara iliendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana nazo ili kutimiza malengo tuliyojiwekea kufanikisha mipango ya maendeleo ya Taifa. Mikakati hiyo imeeleza kwenye ukurasa wa 63 hadi 64 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021; katika mwaka wa fedha 2020/ 2021, Wizara itaendelea kutekeleza dhima yake na hivyo kuendelea kuboresha utoaji wa huduma za sheria kwa umma. Ili kufikia azma hiyo Wizara yangu imeainisha maeneo mahsusi ya kipaumbele na kuyawekea malengo na shabaha kwa ajili ya utekelezaji. Maeneo hayo ya kipaumbele yameelezwa kwa kina katika ukurasa wa 65 hadi ukurasa wa 69 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha Sh.14,634,533,235 ikiwa ni maduhuli ya Serikali. Maelezo ya kina ya kuhusu ukusanyaji wa kiasi hicho cha maduhuli yanapatikana katika ukurasa wa 69 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, kwa mwaka 2020/2021; ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vyake, Wizara inaliomba Bunge lako kuidhinisha jumla ya Sh.73,684,796,059 katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa Fungu 12, 16, 19, 35, 41, 55 na 59. Ufafanuzi wa maombi haya kwa kila Fungu tajwa

yameonyeshwa kwenye ukurasa wa 70 hadi ukurasa wa 72 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, niliomba Bunge lako liidhinishe kiasi cha Sh.176,437,977,000 kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama ambapo matumizi ya kawaida ni Sh.106,562,577,000 na matumizi ya maendeleo ni Sh.69,875,000,000. Katika fedha za matumizi ya kawaida; Sh.50,543,864,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Mahakama; Sh.2,264,771,000 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na Sh.53,754,381,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Mahakama. Kwa upande wa fedha za maendeleo, kiasi cha Sh.39,000,000,000 ni fedha za ndani na Sh.30,875,000,000 ni fedha za nje. Mchanguo wa matumizi ya bajeti kwa Mfuko wa Mahakama nimeonesha kwenye ukurasa wa 72 na 73 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, shukrani; nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya uwaziri. Hakika, ni kutokana na ushirikiano huo nimeweza kusimama leo hivi mbele ya Bunge lako kueleza mafanikio, mipango na mikakati tuliyonayo katika kuhudumia wananchi wetu. Hivyo, kipekee nimshukuru Profesa. Sifuni Ernest Mchome, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria; Bwana. Amon Anastas Mpanju, Naibu Katibu Mkuu; Mheshimiwa Profesa Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania; Mheshimiwa Adelardus Lubango Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania; Bwana. Mathias Bazirinkangu Kabunduguru, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama; Mheshimiwa Waziri Martin Chuma, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania; Bwana. Biswalo Eutropius Kachele Mganga, Mkurugenzi wa Mashtaka; Bibi Emmy Kalomba Hudson, Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini; Dkt. Julius Clement Mashamba, Wakili Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani, January Henry Msoffe,

Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria; Bwana Casmir Sumba Kyuki, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Mheshimiwa Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mathew Mhina Mwaimu, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; Bibi Fatuma Iddi Muya Kaimu, Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa bado dakika moja sasa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mahiga, lakini inabidi utoe hoja ili uungwe mkono.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI DKT. AUGUSTINE PHILLIP MAHIGA (MB), WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA, AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa zilizowasilishwa leo katika Bunge lako na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

***Shukurani na Pole***

**2. Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na fadhila kwa kutujalia afya njema ya kuweza kuwa hapa leo

kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka fedha wa 2020/2021. Aidha, kipekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini kuendelea kuitumikia Serikali ya Awamu ya Tano katika nafasi ya Waziri wa Katiba na Sheria. Naahidi kuitumikia nafasi hiyo kwa uadilifu, uaminifu na unyenyekevu mkubwa kwa maslahi mapana ya Taifa na wananchi wote.

**3. Mheshimiwa Spika;** kwa majonzi makubwa nikupe pole wewe, Bunge lako, familia na wananchi wote wa Jimbo la Newala Vijijini, kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar, aliyefariki tarehe 15 Januari, 2020. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

**4. Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa familia za watu waliopoteza maisha kutokana na madhara ya mvua kubwa zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, niwape pole Watanzania wote ambao wamepoteza ndugu zao katika ajali mbalimbali ambazo zilitokea katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2019/2020.

***Salamu za Pongezi***

**5. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa jitihada zenu za dhati katika kuisimamia na kuishauri Serikali. Bunge lako limeendelea kutoa ushauri na maelekezo ambayo yamewezesha kuboresha utendaji kazi wa Serikali wa kuwatumikia wananchi kwa kuhakikisha haki na huduma mbalimbali za kisheria zinaendelea kuboreshwa na kutolewa kwa wakati. Ushauri na maelekezo ya Bunge lako yametuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Aidha, Wizara imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa umakini na kwa kuzingatia, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015, Sera, Mipango, Mikakati na Sheria mbalimbali zilizopo ikiwemo

Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021); Malengo ya Maendeleo ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030; Mikakati mbalimbali ya Wizara, Idara na Taasisi zake. Pia tumetekeleza maelekezo na ahadi mbalimbali za viongozi wetu – Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - wanazozitoa katika nyakati mbalimbali katika kutekeleza majukumu yao. Kutokana na mafanikio hayo, Wizara itaendelea kuongeza juhudi katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi kwa nia ya kufanikisha lengo kuu la nchi yetu la kujenga Taifa lenye uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Hadi sasa, Taifa limepiga hatua kubwa katika kutimiza lengo hili; tuendelee kushikamana na kulinda umoja na uzalendo wetu, kufanya kazi na kutekeleza wajibu wetu katika safari iliyobaki kuelekea uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Tuliahidi, kwa pamoja tukapanga tukatekeleza, tuendelee kuchapa kazi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

**6. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri ambayo imeweka msingi wa mwelekeo wa kisera katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako.

**7. Mheshimiwa Spika**, kwa ridhaa yako naomba niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Omari Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kwa uongozi wao mahiri na kuziwezesha kamati wanazoziongoza kutekeleza majukumu yake kikamilifu na ufanisi. Wizara yangu inayo imani kubwa kwao na itaendelea kuwapatia ushirikiano unaostahili katika kipindi

chote cha uongozi wao. Vilevile, natoa shukrani za dhati kwa Kamati hizo kwa kazi kubwa ya kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Nilihakikishie Bunge lako kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini mchango wa Kamati hizi katika kuhakikisha Sekta ya Sheria inachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni, mazingira na teknolojia.

**8. Mheshimiwa Spika,** naomba kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri walioteuliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kuziongoza wizara mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda kumpongeza Mhe. George Boniface Simbachawene (Mbunge wa Kibakwe) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mbunge wa Ilala) kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira. Pia, nimpongeze Mhe. Hussein Mohamedi Bashe (Mbunge wa Nzega Mjini), kwa kuteuliwa kushika nafasi ya Naibu Waziri wa Kilimo. Niwatakie wao na wengine wote walioteuliwa na Mhe. Rais, kushika nafasi mbalimbali katika utumishi wa umma, kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya ya kuwatumikia wananchi kupitia wizara wanazoziongoza.

## B. DIRA NA DHIMA

**9. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria inaongozwa na Dira ambayo ni ***Katiba na Sheria wezeshi kwa maendeleo ya Taifa***. Aidha, Dhima ya Wizara ni ***kuwa na mfumo madhubuti wa kikatiba na Sheria wenye kufanikisha utekelezaji wa sera na mipango kwa maendeleo ya Taifa***. Dira na dhima hizi zinalenga kuweka mazingira rafiki ya kisera na ya kisheria ya kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Taifa, kudumisha hali ya amani, utulivu na utangamano wa kitaifa ambazo ni nguzo muhimu kwa mstakabali wa ustawi wa jamii na Taifa letu katika kujenga

mazingira wezeshi ya upatikanaji haki na huduma bora za kisheria kwa wakati.

## C. MUUNDO NA MAJUKUMU YA WIZARA

**10. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha Mhimili wa Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, RITA, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto. Katika kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kuwa nchi inaongozwa kwa kuzingatia Katiba, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa, Wizara yangu na taasisi zake imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Hati ya Mgawanyo wa Majukumu kwa Mawaziri, kupitia Tangazo la Serikali Na. 144A la tarehe 22 Aprili, 2016 na sheria nyingine za nchi. Majukumu hayo ni:-

i. Kutunga Sera zinazohusu masuala ya kisheria na kusimamia utekelezaji wake;

ii. Kushughulikia mambo ya kikatiba;

iii. Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki;

iv. Uandishi wa sheria;

v. Kuendesha mashtaka;

vi. Kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na mikataba mbalimbali inayohusu Serikali na uratibu wa sheria za kimataifa;

vii. Kushughulikia masuala ya haki za binadamu na msaada wa kisheria;

viii. Kurekebisha sheria;

ix. Kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai;

x. Kusajili matukio muhimu ya binadamu (vizazi, vifo, ndoa, talaka na uasili), ufilisi na udhamini;

xi. Kuboresha utendaji na maendeleo ya rasilimali watu iliyo chini ya Wizara; na

xii. Kuratibu shughuli za taasisi, mipango na miradi chini ya Wizara. Aidha, kulingana na Mabadiliko ya muundo wa Wizara ya mwaka 2018 Wizara imeongezewa jukumu la kuratibu masuala ya utajiri na maliasilia za nchi kulingana na matakwa ya Ibara ya 9 na 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Sura ya 2) ili kuhakikisha rasilimali hizo zinalindwa, zinaendelezwa, zinatumika, na zinasimamiwa kwa ajili ya mtakabali wa maendeleo ya Taifa na ustawi wa jamii kwa ujumla.

## D. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 HADI 2019/2020

**11. Mheshimiwa Spika,** kama unavyofahamu, mwezi Oktoba mwaka wa 2020 tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu na hivyo hii ni hotuba yangu ya mwisho katika kipindi hiki. Nichukue fursa hii kutoa taarifa kuwa tathmini ya ujumla ya mambo ambayo Wizara yangu na taasisi zake imeyatekeleza katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2019/2020 inaonesha mafanikio makubwa na ya kuridhisha katika maendeleo ya sheria na utoaji wa huduma za kisheria. Tumepata mafanikio katika maeneo mbalimbali ikiwemo kusimamia kwa ukaribu maboresha ya mfumo wa haki na utoaji haki ambapo kesi mbalimbali zimeshughulikiwa na kuamuliwa na mahakama na vyombo vingine vya utoaji haki; tumeandaa na kuandika miswaada ya sheria mbalimbali, ikiwemo ya kurekebisha baadhi ya sheria kwa ajili ya kuboresha mfumo wa sheria nchini na kiumarisha misingi ya utoaji haki (overiding principles); tumesimamia kesi za jinai, kuratibu upelelezi na kuendesha mashtaka ya aina mbalimbali na hivyo kuendelea kuchangia katika kuhakikisha

nchi iko salama, watu na mali zao wako salama, na pia nchi ina utulivu na amani; tumeratibu, kusimamia na kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na mikataba mbalimbali inayohusu Serikali; tumeratibu masuala mbalimbali ya sheria za kimataifa; tumeratibu na kushughulikia masuala mbalimbali ya haki za binadamu na haki za watu ikiwemo huduma ya msaada wa kisheria; tumeratibu na kushughulikia urejeshwaji wa wahalifu na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai; tumesajili matukio muhimu ya binadamu hususan vizazi, vifo, ndoa, talaka na uasili, ufilisi na udhamini na kuifikisha huduma hii karibu zaidi na wananchi na hivyo kuongeza idadi ya matukio yanayosajiliwa; tumeboresha miundo ya ofisi mbalimbali ikiwemo ya Wizara yangu na Idara mahususi za kuratibu na kushughulikia masuala ya haki za binadamu na haki za watu na masuala ya utarjiri na maliasilia za nchi kwa ajili ya ustawi wa jamii na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

**12. Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imerekebisha muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hivyo kuwa vyombo mahsusi vya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inayoshughulikia kesi za daawa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inayoshughulikia kesi za jinai ikiwemo uratibu wa upelelezi; tumesimamia kwa umakini na ukaribu utendaji wa watumishi, maadili na maendeleo yao ili kuhakikisha kwamba tunatekeleza misingi ya utawala bora na kuchukua hatua pale panapoonekana kuna shida; tumeratibu shughuli za taasisi, mipango na miradi yetu mbalimbali ikiwemo kujenga mahakama mpya katika ngazi za Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama za Hakimu Mkazi, na Mahakama Kuu ili kufikisha huduma ya mahakama karibu na wananchi, kujenga mifumo mbalimbali ya TEHAMA ili kurahisisha utoaji huduma kwa wakati na kumpunguzia gharama mteja; na tumeendelea kufungua ofisi za mashtaka katika ngazi ya wilaya ili kufikisha huduma ya sheria kwenye masuala ya kesi za jinai ili ziende haraka na wale wenye hatia wapate haki yao na wale ambao hawana hatia wachiwe na kuendelea na majukumu yao ya kulijenga Taifa; na tumeboresha baadhi ya mifumo ya haki jinai kwa kuongeza njia mbadala ambazo zinaweza kutumika na kumaliza kesi kwa haraka, ikiwemo *plea*

*bargaining,* upatanishi na ufifishaji wa baadhi ya makosa. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha 2015/2016 hadi 2019/2020 yameambatishwa katika **KIAMBATISHO A.**

## E. MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

13. **Mheshimiwa Spika,** sasa nijielekeze kwenye utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara yangu ilibainisha maeneo mahsusi ya kipaumbele kuwa msingi wa kutekeleza Dhima ya Wizara katika kutoa huduma bora za kisheria kama yalivyoainishwa katika **KIAMBATISHO B**. Katika kutekeleza mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/ 2020 masuala yaliyotekelezwa ni pamoja na yafuatayo:-

### I. Kutunga Sera Zinazohusu Masuala ya Kisheria na Kusimamia Utekelezaji Wake

14. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekamilisha maandalizi ya rasimu ya Sera ya Taifa ya Sheria ambapo kwa sasa ipo kwenye hatua ya kuandaa nyaraka mbalimbali kwa ajili ya kuwasilishwa katika vikao vya maamuzi vya Serikali kabla ya kupitishwa kuwa sera kamili. Aidha, mikakati ya utekelezaji wa sera hii wakati itakapopitishwa pia imeanza kuandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

### II. Kushughulikia Masuala ya Kikatiba

15. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara na wadau wake waliendelea kushughulikia masuala mbalimbali ya kikatiba ikiwemo haki za binadamu na haki za watu, utoaji wa haki kwa wakati, utoaji wa taarifa mbalimbali ikiwemo katika vyombo vya kitaifa, kikanda na kimataifa. Jukumu hili lilitekelezwa ikiwemo kujibu na kuwaelimisha wadau kuhusu hoja mbalimbali wanazozitoa kuhusiana na masuala ya kikatiba. Changamoto kubwa ambayo tunaendelea kuiona na ambayo Wizara yangu inaendelea kuishughulikia na wadau

wake ni uelewa mdogo wa masuala mbalimbali ya kikatiba. Baadhi ya vitu vinavyozungumziwa katika maeneo mbalimbali tayari vipo katika Katiba yetu na kinachohitajika ni kujenga uelewa wa pamoja ili kupunguza upotoshaji ambao umekuwa ukijitokeza mara kwa mara. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wake itaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya masuala mbalimbali ya kikatiba kwa kutumia vyombo na njia mbalimbali ili kila mmoja wetu apate uelewa mpana wa masuala haya.
Aidha, Wizara yangu imeendelea kushiriki na kutoa mchango wake katika vikao vya mbalimbali vya ushirikiano katika kudumisha Muungano wetu, hususan katika masuala mbalimbali ya sheria. Muungano wetu unaendelea kuwa imara na mfano wa kuigwa ulimwenguni kote.

## III. Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki;

16. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama ya Tanzania imeendelea kutekeleza mkakati wake wa kupunguza mlundikano wa mashauri ili kuhakikisha wananchi wanapata haki zao kwa wakati. Kwa upande wa usikilizaji mashauri, katika mwaka 2019 Mahakama ilianza na mashauri **67,811** na kusajili mashauri mapya **272,326** na kumaliza mashauri **271,214** ambapo yalibaki mashauri **69,648** ilipofikia mwezi Desemba, 2019. Kwa upande wa Mahakama ya Rufani, ilianza mwaka 2019 na mashauri **3,248**, ikasajili mashauri **1,836** na kumaliza mashauri **1,309** na kufunga mwaka 2019 na mashauri **3,775**. Aidha, kwa upande wa Mahakama Kuu na Kanda zake, ilianza mwaka 2019 na mashauri **14,814** na mashauri mapya yaliyosajiliwa ni **13,342** na kumaliza mashauri **14,421** na kufunga mwaka ikiwa na mashauri **13,735**. Divisheni za Mahakama Kuu zilianza mwaka na mashauri **5,087** zikasajili mashauri **4,755** na kumaliza mashauri **4,651** na kufunga mwaka na mashauri **5,191**. Vilevile, kwa kipindi cha Januari 2020 hadi Machi 2020, Mahakama ya Rufaa ilikuwa na kesi **228** na imemaliza kesi **215** hivyo kubaki na kesi **3,788**; Mahakama Kuu ilikuwa na kesi **2,262** na imemaliza kesi **202** hivyo kubaki na kesi **20,986**; Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya zilikuwa na kesi **2,517** na zimemaliza kesi **934** hivyo kubaki na kesi **12,780**; na Mahakama za Mwanzo zilikuwa na

kesi **26,480** na zimemaliza kesi **24,061** hivyo kubaki na kesi **18,281**. -

17. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka, 2019 Mahakama za Hakimu Mkazi kwa Mikoa ya Tanzania Bara, zilianza na mashauri **9,862** na kusajili mashauri **17,736** ambapo mashauri **16,401** yalihitimishwa na kufunga mwaka na mashauri **11,197**. Aidha, Mahakama za Wilaya zilianza na mashauri **18,486** na katika kipindi husika, mahakama zilisajili mashauri **39,599**. Jumla ya mashauri **39,658** katika ngazi hii ya mahakama, yalihitimishwa katika kipindi hicho na kufunga mwaka na mashauri **18,427**. Kwa upande wa Mahakama za Watoto, zilianza na mashauri **470** na zilisajili mashauri mapya **1,967** ambapo idadi ya mashauri **1,701** yalihitimishwa na kufunga mwaka na mashauri **725**. Aidha, Mahakama za Mwanzo zilianza na mashauri **15,844** zikasajili mashauri **193,091** na kumaliza mashauri **193,073** ambapo zilifunga mwaka 2019 na mashauri **15,862**.

18. **Mheshimiwa Spika**, Wizara pia imeendelea kutekeleza wajibu wake katika utoaji haki na wananchi kuifikia haki. Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa wananchi ambao kwa namna moja au nyingine walishindwa kufungua kesi mahakamani ndani ya muda uliowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Ukomo (Sura ya 89) na wanakidhi vigezo vilivyowekwa na sheria hiyo, wanapatiwa nafasi nyingine tena kwa kuruhusiwa kufungua mashauri Mahakamani nje ya muda. Katika kipindi hiki, Wizara ilipokea na kushughulikia jumla ya maombi **214** ya kuongeza muda wa kufungua mashauri ya madai nje ya muda. Hata hivyo, nitumie fursa hii kutoa rai kwa wananchi kwa ujumla kuzingatia muda uliowekwa na sheria kwa ajili ya utatuzi wa migogoro mbalimbali. Endapo mwananchi anakabiliana na mgogoro wowote ni vyema akachukua hatua mapema na ahakikishe anapata ushauri au mwongozo juu ya mgogoro huo kutoka kwa wakili, au mtoa huduma ya msaada wa kisheria na mtu mwingine mwenye uelewa wa masuala ya utatuzi wa migogoro aliyepo katika eneo lake. Njia hii itamsaidia kuondokana na kadhia ya kuchelewa kuumaliza mgogoro huo ndani ya muda uliopo kisheria na hivyo kuhitaji kupata

kibali cha Waziri mwenye dhamana na mambo ya sheria ili afungue kesi yake nje ya muda.

19. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na maombi ya kuongeza muda wa kufungua mashauri ya madai nje ya muda, Wizara imepokea taarifa za maendeleo ya wagonjwa **50** wa afya ya akili wanaohifadhiwa katika Taasisi ya Magonjwa ya Afya ya Akili baada ya kuthibitika walitenda makosa mbalimbali wakiwa wagonjwa wa akili na sasa wamepona. Katika kupitia taarifa hizo, Wizara imetoa jumla ya Amri **50** za kuwaachilia huru hao waliothibitika kuwa wanaendelea vizuri ili wakaungane na familia zao na kuendelea na uangalizi na matibabu katika maeneo wanakotoka. Wito wangu ni kwa wananchi, ndugu, jamaa na marafiki wa wagonjwa wa afya ya akili ambao wamepona na kuachiwa kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (Sura ya 20) kuhakikisha kuwa wanawasimamia watu hao kundelea kutumia dawa zilizoelekezwa na Madaktari ili afya zao ziendelee kuimarika na hatimaye kuendelea na shughuli za ujenzi wa Taifa, na hivyo, kupunguza, kama si kuondoa kabisa, matukio ya jinai yanayosababishwa na ugonjwa wa afya ya akili katika jamii zetu.

20. **Mheshimiwa Spika,** kupitia marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai (Sura ya 33) yaliyofanywa mwaka huu wakati Bunge linashughulikia suala la usuluhishi, ni takwa la kisheria sasa kwamba watu wanaoingia kwenye migogoro ya daawa, kabla ya kwenda Mahakamani, wahakikishe wamechakua hatua za makusudi za kutatua mgogoro wao nje ya mahakama. Hatua hizi ni pamoja na kutoa notisi na kuutarifu upande mwingine suala lenye mgogoro kwa nia ya kuhitaji kuusuluhisha; kutoa majibu mahsusi kwa notisi iliyotolewa na upande mwingine; kutoa taarifa na nyaraka sahihi kuuwezesha upande mwingine kuelewa mgogoro na namna mgogoro unavyoweza kutatuliwa; na kuangalia kama mgogoro unaweza ukatatuliwa kwa njia nyingine nje ya ile ya Mahakama kama vile maridhiano, majadiliano, upatanishi, usuluhishi au kufanya tathmini kupitia wathaminishaji.

21. **Mheshimiwa Spika,,** nitumie fursa hii kutoa rai kwa wananchi wenye migogoro mbalimbali ya daawa kuufuata utaratibu huu na hivyo kupunguza kesi zinazokwenda mahakamani.. Hata hivyo, kulingana na Ibara ya 107 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Mahakama ni chombo cha mwisho cha utoaji haki, hii ikiwa na maana kwamba wahusika katika migogoro mbalimbali ni vema watumie njia mbalimbali kama zilivyobainishwa na sheria katika kutatua migogoro yao kabla ya kukimbilia mahakamani. Kwa kufanya hivyo, migogoro itatatulika kwa haraka na gharama nafuu na kuziacha Mahakama kushughulikia masuala makubwa ambayo hayana namna zaidi ya kuyafikisha hapo.

22. **Mheshimiwa Spika**, kupitia marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (Sura ya 20) yaliyofanyika katika mwaka wa fedha 2019/2020, mfumo wa ufifilishaji na upatanishi kwenye makosa ya jinai umeimarishwa kwa makosa yanayoruhusiwa kisheria kufifilishwa au kupatanishwa kwa masharti na utaratibu uliowekwa. Makosa mengi yanayoangukia katika mamlaka za Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya yapo katika kundi hili. Makosa haya ni pamoja na yale ya kiudhibiti ambayo sheria imetoa mamlaka kwa mkamataji au Afisa anayehusika, ikiwemo Wakuu wa Vituo vya Polisi, kufifilisha endapo mtuhumiwa atatoa ushirikiano na kukubali kwa hiari yake mwenyewe. Aidha, masuala ya upatanishi yaliyoruhusiwa kisheria yanahusu makosa madogo ambayo adhabu yake haizidi kifungo cha miaka mitano jela kwa mujibu wa Vifungu vya 163 na 170 vya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20.

23. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuwataka Maafisa wote walioruhusiwa na sheria kufifilisha makosa na Mahakimu wote walioruhusiwa kupatanisha watu wanaokoseana katika makosa yaliyoruhusiwa kupatanisha kutokusita kufanya hivyo kwani huo ni wajibu wa kisheria ambao hauna budi kutekelezwa. Aidha, natoa rai kwa wananchi kuondokana na dhana iliyoanza kuenea ya kuamini kwamba kosa linapofifilishwa ama watu wanapopatanishwa basi kutakuwa

na kiashiria cha rushwa ama kitendo ambacho ni kinyume na sheria. Huu ni utaratibu uliopo kisheria ambao wenye dhamana hawana budi kuutekeleza kwa mujibu ya matakwa ya sheria. Kwa kufanya hivyo tutapunguza adha ya mahakama kuwa na kesi nyingi, baadhi zikiwa ni kesi ndogo ndogo ambazo zingeweza kumalizika kwa utaratibu wa kufifilisha au upatanishi. Magereza pia yatapunguza msongamano wa mahabusi na wafungwa hivyo kupata fursa ya kushughulikia masuala makubwa ambayo yatasababisha wahusika kupelekwa gerezani. Utaratibu huu wa utatuzi wa migogoro katika jamii unaakisi aina ya maisha yanayokwenda sawia na dhana ya uchumi wa kati unaolenga kutatua migogoro kwa wakati na kwa gharama nafuu.

## IV. Kuendesha Mashtaka

24. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kutekeleza jukumu la uratibu na usimamizi wa shughuli za upelelezi, ilishughulikia majalada **16,039** kutoka vyombo vya uchunguzi na upelelezi. Kati ya hayo, majalada **9,477** yaliandaliwa hati za mashtaka; majalada **782** yalifungwa na majalada **2,776** yalirejeshwa kwa uchunguzi na upelelezi zaidi; hivyo kufanya majalada yaliyofanyiwa kazi kuwa **13,035** sawa na asilimia **81**. Aidha, majalada **3,019** sawa na asilimia **19** yalikuwa yanaendelea kufanyiwa kazi kote nchini.

25. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pia iliendesha kesi za jinai katika Mahakama za Wilaya, Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Jumla ya kesi za jinai **20,420** zilishughulikiwa katika Mahakama za Wilaya na Hakimu Mkazi ambapo, kesi **9,035** zilihitimishwa. Kati ya hizo, kesi **5,508** zilihitimishwa kwa washtakiwa kutiwa hatiani, ikiwa ni sawa na asilimia **61** ya kesi zote zilizohitishwa. Ofisi iliendesha jumla ya kesi za jinai **4,453** katika Mahakama Kuu ya Tanzania. Kati ya hizo, kesi **1,959** ni za vikao vya Mahakama Kuu na kati ya hizo, kesi **636** sawa na asilimia **32** ziliitimishwa na kesi **1,323** sawa na asilimia

**68** zinaendelea katika hatua mbalimbali. Aidha, kesi **2,494** zilihusu rufaa za Mahakama Kuu ambapo kesi **1,043** sawa na asilimia **42** zilihitimishwa na kesi **1,451** sawa na asilimia **58** zinaendelea katika hatua mbalimbali. Aidha, jumla ya rufaa **658** za jinai zilishughulikiwa katika Mahakama ya Rufani ambapo kati ya hizo, rufaa **201** sawa na asilimia **31** zilihitimishwa na rufaa **457** zilikuwa zinaendelea katika hatua mbalimbali.

26. **Mheshimiwa Spika,** Washtakiwa waliotiwa hatiani kutokana na kesi za jinai walipewa adhabu mbalimbali zikiwemo vifungo, faini, na mali mbalimbali kutaifishwa. Kiasi cha Shilingi **2,848,664,926.42** na Dola za Marekani **593,315.78** sawa na Shilingi **1,385,451,677.58** zililipwa mahakamani kama faini katika kesi **4,146**. Mali zinazokadiriwa kuwa na thamani ya Shilingi **3,605,169,186** na Dola za Marekani **831,759.61** sawa na Shilingi **1,942,241,865.31** zilitaifishwa kwa amri ya Mahakama. Baadhi ya mali hizo ni pamoja na madini ya dhahabu na vito, magari **10**, mbao vipande **1,203** mafuta ya dizeli lita **1,110** na petroli galoni **39**.

27. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali dhidi ya changamoto ya ucheleweshaji wa upelelezi na tuhuma za ubambikizwaji wa kesi. Nichukue fursa hii kuvitaka vyombo vyote vya ukamataji, upelelezi, mashtaka, maamuzi na wananchi wote kuchukua hatua za haraka katika kutatua changamoto na tuhuma hizi. Napenda kulitaarifu Bunge lako kwamba, wote watakaobainika kujihusisha na vitendo vya ubambikizaji kesi watachukuliwa hatua za kisheria na Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya sheria ili kukabiliana na hali hii. Tunahitaji, kama Taifa, watu wote waelekeze nguvu zao katika kutenda haki na kuachana na vitendo vya kuwabambikia watu mashtaka, kitu ambacho hakikubaliki katika zama hizi. Hali kadhalika, ili kukabiliana na changamoto za upelelezi kuchelewa kupita kiasi, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani na wadau wengine, ikiwemo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na TAKUKURU ambao ndiyo wenye wajibu wa kuratibu upelelezi, ili kulipatia suala hili ufumbuzi wa kudumu.

## V. Uandishi, Urekebu na Ufasiri wa Sheria;

28. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara imewezesha kutungwa kwa Sheria ya Usuluhishi ya mwaka 2020 na kufanya marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (Sura ya 20) na Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Daawa (Sura ya 33) ili kuongeza wigo wa utoaji haki kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo majadiliano, maridhiano, upatanishi na usuluhishi. Ni dhahiri kwamba kutungwa kwa Sheria ya Usuluhishi na kurekebisha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai na Sheria ya Mwendo wa Mashauri ya Daawa kumeweka misingi na miongozo madhubuti ya utatuzi wa migogoro kwa kuhakikisha kwamba mashauri yanatatuliwa kwa haraka na kwa maelewano hivyo kupunguza muda na gharama za utatuzi wa migogoro. Aidha, Wizara, kwa kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetekeleza maelekezo ya kuandaa miswada ya sheria mbalimbali na hivyo kuwezesha Bunge kutunga na kurekebisha sheria za sekta mbalimbali kwa ajili ya kuweka mfumo madhubuti wa kisheria wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya nchi.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mfumo wa utoaji haki na utendaji wa Sekta ya Sheria, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Serikali iliwasilisha Bungeni mapendekezo ya marekebisho ya sheria **30** kupitia Miswada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4, Na.5, Na. 6, Na. 7 na Na. 8 ya mwaka 2019 ambayo ilipitishwa na Bunge kuwa sheria. Aidha, marekebisho hayo yalilenga kuondoa upungufu ambao umejitokeza katika utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo. Ufafanuzi wa sheria iliyotungwa na zilizofanyiwa marekebisho katika mwaka 2019/2020 umeoneshwa katika **KIAMBATISHO C.**

30. **Mheshimiwa Spika,** Serikali pia imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuhakikisha kwamba Sheria za nchi zinakwenda na wakati na zinaakisi Sera, mila, desturi, maadili na vipaumbele vya Taifa. Katika Mwaka wa Fedha wa 2019/ 2020 Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa Miswada ya Sheria **15** na kujadiliwa na Bunge

ambapo Miswada ya sheria tisa **(9)** ilipitishwa na Bunge kuwa Sheria. Miswaada ya Sheria sita (**6)** inaendelea katika hatua mbalimbali kulingana na utaratibu. Aidha, Sheria ndogo **755** ziliandaliwa na kuchapishwa kwenye Gazeti la Serikali. Sheria hizo zilijumuisha Kanuni, Amri, Taarifa na Matamko. Vilevile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetafsiri Sheria mama **18** na Sheria Ndogo **29** kutoka lugha ya Kiingereza kwenda Lugha ya Kiswahili ili kuongeza uelewa wa sheria kwa wananchi kama zilivyoambatishwa katika **KIAMBATISHO D.** Hii ni pamoja na kufanya urekebu wa Sheria **91** ili kukidhi mahitaji ya sasa ya jamii **KIAMBATISHO E**.

## VI. Uendeshaji wa Mashauri ya Madai na Usuluhishi

31. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kuendesha wa mashauri ya madai (ikiwemo mashauri ya Haki za Binadamu, Uchaguzi, na mengine ya Kikatiba) na usuluhishi ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Ofisi ilikuwa na jumla ya mashauri ya madai **2,728,** ambapo ilishughulikia jumla ya mashauri ya madai **569** na mashauri **333** yalihitimishwa. Kati ya mashauri yaliyohitimishwa, Serikali imeshinda mashauri **278** na kuokoa kiasi cha Shilingi **249,238,064,721.75**.

32. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020, kulikuwa na jumla ya mashauri **46** ya kikatiba, kati ya mashauri hayo, tisa **(9)** ni mashauri mapya na yaliyofunguliwa katika kipindi hicho. Kati ya hayo, mashauri **35** yapo Mahakama Kuu, mashauri mawili **(2)** Mahakama ya Rufaa na Mashauri nane **(9)** yamehitimishwa. Aidha, hadi Mwezi julai, 2019 kulikuwa na jumla ya mashauri **21** ambayo yalisajiliwa kwenye Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika Mashariki. Katika kipindi cha julai hadi Machi, 2020, mashauri **manne (4)** yamesajiliwa. Mashauri manne **(4)** yamesikilizwa na yanasubiri maamuzi ya mahakama na mashauri **21** yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Kwa upande Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, jumla ya mashauri **138** yalikuwa yamesajiliwa katika Mahakama hiyo, dhidi ya Serikali ya Tanzania hadi kufikia Mwezi Julai

2019. Aidha, katika kipindi cha Julai 2019 na Machi, 2020, Ofisi ilisajili mashauri nane **(10)** na Mashauri **31** yalihitimishwa, mashauri **117** yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji.

33. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya mashauri **81** ya usuluhishi ya kitaifa na kimataifa yalikuwa katika Mabaraza ya usuluhishi. Mashauri **60** kati ya hayo ni ya kitaifa na **21** ni ya kimataifa. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Mashauri **(sita) 9** ya kitaifa yalihitimishwa na mengine **51** yanaendelea katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Vilevile, katika kipindi husika mashauri **7** ya kimataifa yamehitimishwa na mengine **14** yanaendelea katika hatua mbalimbali za usikizwaji. Katika mashauri yaliyomalizika Ofisi imeweza kuokoa kiasi cha **Shilingi 6,757,739,630.28** na Dola za Kimarekani **4,766,310,020.81** sawa na Shilingi **11,129,810,529,359.90**.

34. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuboresha Mfumo wa utunzaji wa taarifa za mashauri kwa kutumia TEHAMA. Kukamilika kwa mfumo huu kutarahisisha ukusanyaji wa takwimu za mashauri, kufanya ufuatiliaji wa mienendo ya mashauri, na utoaji wa taarifa mbalimbali kuhusu mwenendo wa Mashauri kwa matumizi ya ofisi, wadau mbalimbali pamoja na umma kwa ujumla. Aidha, katika kipindi husika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kusisitiza matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa mawasiliano ya nyaraka na majalada ya ofisi.

## VII. Utoaji wa ushauri wa kisheria

**35. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wakala na Taasisi nyingine za Serikali na Mashirika ya Umma. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya maombi ya Ushauri wa Kisheria **934** yalipokelewa, napenda kutoa taarifa ya kwamba maombi yote yalishughulikiwa.

## VIII. Usimamizi wa Mikataba

**36. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kufanya majadiliano na upekuzi wa mikataba mbalimbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya mikataba ya kitaifa na kimataifa **770** sawa na asilimia **57** ilifanyiwa upekuzi kati ya Mikataba **1,333** iliyokuwa imepangwa. Kati ya Mikataba **770** iliyofanyiwa upekuzi, Mikataba **345** ilikuwa imethaminishwa katika sarafu mbalimbali. Mikataba **262** ilikuwa na thamani ya Shilingi **4,645,372,100,000.00,** Mikataba **61** ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani **6,011,297,150.38** sawa na **Shilingi 14,036,979,975,852.30** mikataba **22** ilikuwa na thamani ya Euro **118,566,870.31** sawa na Shilingi **299,508,463,074.41.** Mikataba hiyo ilihusisha masuala ya manunuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo, utoaji wa huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, hospitali na barabara.

**37. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeunda vikosi kazi vinavyohusisha wataalamu kutoka Taasisi zinazohusika na mikataba ya utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia na mafuta na uzalishaji umeme ili kufanya mapitio ya mikataba hiyo kwa lengo la kubaini kama ina maslahi mapana kwa Taifa. Aidha, hadi mwezi Machi, 2020 Ofisi imefanya mapitio ya mikataba **13** ya Utafutaji na uzalishaji wa Mafuta na Gesi. Hivi sasa Ofisi imeshaanza mapitio ya mikataba mingine takriban **70** inayohusu Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Songo Songo na mikataba mingine **11** ya wazalishaji wadogo ya umeme.

## IX. Mikataba ya Kikanda na Kimataifa

**38. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Maazimio **nane (8)** ya Bunge ya kuridhia Itifaki na Mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa yaliwasilishwa na kupitishwa na Bunge. Orodha ya Itifaki na Mikataba hiyo ni kama inavyoonesha katika **KIAMBATISHO F**

## X. Utoaji wa Huduma ya Msaada wa Kisheria

**39. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu

utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Sheria (Sura ya 21) kwa kusajili jumla ya Watoa Huduma ya Msaada wa Sheria **126** na Wasaidizi wa Kisheria wapatao **498** ambao orodha yao pamoja na maeneo wanakofanyia kazi ni kama inavyooneshwa katika **KIAMBATISHO G.**

Aidha katika kipindi hicho Wizara, kupitia Maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria yaliyofanyika mwishoni mwa mwezi Novemba 2019, ilitoa elimu kuhusu msaada wa kisheria kwa umma kwa njia ya televisheni na radio kwa muda wa wiki mbili mfululizo. Sambamba na elimu iliyotolewa kupitia vyombo vya habari, wananchi wapatao **1,185** walipatiwa huduma za msaada wa sheria ana kwa ana zikiwemo ushauri pamoja na kuandaliwa nyaraka muhimu za kimahakama. Aidha, watendaji wa Serikali katika Mkoa wa Simiyu, wakiwemo maafisa wa Jeshi la Polisi, Jeshi la magereza, mahakimu, Washauri wa mahakama za mwanzo, wajumbe wa Mabaraza ya kata na Vijiji, Kamati za Ulinzi na Usalama, Wenyeviti wa Kamati za Shule, Watendaji wa Kata na Vijiji na Wajumbe wa menejimenti ya Sekretarieti ya Mkoa walipatiwa mafunzo maalum ya kisheria kulingana na majukumu yao. Jumla ya Watendaji waliopata mafunzo hayo katika wiki ya msaada wa kisheria ni **1,389**. Wakati wa mafunzo haya ilibainika wazi kuwa, bado elimu ya kisheria inahitajika sana kwa watendaji wa ngazi zote ili waweze kuwahudumia wananchi na pia kutekeleza majukumu yao kulingana na sheria, kanuni, taratibu na miongozo. Vilevile, Wizara ilitoa elimu ya kisheria kwa wanafunzi waliokuwa katika makambi ya kitaaluma mkoani Simiyu kati ya mwezi Septemba na Oktoba, 2019 ambapo wanafunzi walipata fursa ya kuelewa masuala muhimu ya kisheria yanayogusa jamii. Jitihada hizo zitaendelea katika mikoa mingine.

**40. Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kufikisha huduma ya msaada wa kisheria karibu na wananchi, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais- TAMISEMI imeteua Wasajili Wasaidizi katika kila mamlaka ya Serikali za Mitaa **185** ili kusajili, kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma hiyo nchini. Jambo hili ni la kujivunia kwa kuwa idadi ya wananchi waliokuwa wanasafiri kuja Wizarani kuwasilisha maombi ya msaada wa

kisheria sasa imepungua tangu kuanza kutekelezwa kwa sheria hii.

**41. Mheshimiwa Spika**, katika kupanua wigo wa utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria zipo baadhi ya taasisi na vyuo vya elimu ya juu ambavyo vimejisajili na kuanzisha Kliniki za Msaada wa Kisheria kwa lengo la kuwa na uendelevu wa utoaji wa huduma za msaada wa kisheria. Kupitia huduma hii wananchi wengi wameanza kuifikia haki kwa gharama nafuu na kwa wakati, hivyo kuwawezesha kupata muda wa kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Mwelekeo huu unakwenda sambamba na azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwawezesha wananchi kwa njia mbalimbali ili waweze kuchangia na kuwa sehemu ya kukuza uchumi wa viwanda na kuleta usawi wa jamii kwa ujumla.

**42. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imeendelea kuimarisha mfumo wa utoaji wa msaada wa kisheria kwa makundi maalum. Kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Tanzania na Jeshi la Magereza Tanzania, Wizara imeandaa Mwongozo wa kutoa huduma za msaada wa kisheria katika maeneo ambayo mahabusi na wafungwa wanashikiliwa. Lengo ni kuruhusu huduma hii kuwafikia wafungwa na mahabusi kama sheria inavyotamka na kutimiza azma ya Serikali ya kupunguza mlundikano katika maeneo hayo. Aidha, mafunzo yameendelea kutolewa kwa Maafisa wa Jeshi la Polisi na Maafisa Jeshi la Magereza ili kuwajengea uwezo katika masuala ya msaada wa kisheria. Pamoja na kuweka miongozo Wizara pia imesaini makubaliano na Wizara ya mambo ya Ndani ya Nchi kwa niaba ya Jeshi la Polisi Tanzania na Jeshi la Magereza Tanzania ya kushirikiana katika kutekeleza sheria ya msaada wa kisheria. Makubaliano ya aina hii pia yalisainiwa baina ya Mahakama ya Tanzania na Wizara ya Katiba na Sheria na yanaendelea kutekelezwa kwa Mahakama ya Tanzania kuwaelekeza mawakili kuwapatia msaada wa kisheria wadaawa wanaoonekana kuhitaji huduma hiyo.

**43. Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, maeneo ambayo yameonekana kuwa kero kwa wananchi ni pamoja na

migogoro ya ardhi, mirathi na ndoa. Wengi kati ya waliotafuta huduma kupitia vyombo vya habari na maeneo ya huduma wakati wa maonesho hayo ni wanawake **711** ambapo asilimia **60** walilalamikia kunyimwa haki ya kurithi mali za waume zao waliofariki. Kati ya hao **711**, wanawake **640** sawa na asilimia **90** hawakuwa na uelewa wa taratibu za kufuata kudai haki hizo wakati wanawake **71** sawa na asilimia **10** wamefika mahakamani lakini bado wanaendelea kukabiliwa na changamoto za kupata haki zao kutokana na sababu mbalimbali. Kati ya wananchi waliopatiwa huduma, wapo vijana wa kike na wa kiume ambao wamekosa haki ya kurithi mali za wazazi wao kutokana na kudhulumiwa na ndugu za marehemu. Katika kundi hili pia wapo wanawake walionyang'anywa watoto na watalaka/wenzi wao ambapo huko walipo watoto hao wanakosa matunzo na malezi stahiki.

**44. Mheshimiwa Spika,** Wizara, kwa kushirikiana na wadau, mbalimbali, ikiwemo Mahakama ya Tanzania, Wizara nyingine, Idara Taasisi za umma na zile zisizo za kiserikali, inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kupunguza changamoto zinazowakabili wananchi katika maeneo mbalimbali.

## XI. Haki za Binadamu na Haki za Watu

**45. Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu la kusimamia na kuratibu masuala ya haki za binadamu na haki za watu kwa niaba ya Serikali pamoja na kuhakikisha mifumo ya sheria inachangia katika kukuza, kulinda na kuendeleza haki za watu, haki za binadamu, utawala wa sheria na utawala bora nchini. Serikali ya Awamu ya Tano pia inatambua na kuheshimu wajibu ilionao wa kulinda, kukuza na kuendeleza haki za binadamu na haki za watu nchini kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia.

**46. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha na kutekeleza haki za watu kama ifuatavyo; haki ya watu kujitawala kwa kuhakikisha kwamba Taifa linaendelea kutafsiri uhuru tulioupata mwaka 1961 kwa vitendo ikiwa ni pamoja

na kuhakikisha kuwa utawala wa sheria na utawala bora unazingatiwa katika shughuli mbalimbali na kuchukua hatua pale panapoonekana kuna upungufu, hali kadhalika, inatumia utajiri wake, maliasilia na rasilimali zake kwa ustawi wa watu wake na Taifa kwa vizazi vya sasa na vijavyo kama ambavyo Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Sura ya 2) inavyotaka; haki ya watu ya uchumi endelevu kwa kuhakikisha kwamba nchi inajiwekea mipango, mikakati, sheria na mazingira bora ya kuendeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuhakikisha kwamba ubadhirifu au uhujumu uchumi kwa namna yoyote ile unachukuliwa hatua kwa wakati; haki ya watu kuwa na amani na usalama kwa kuhakikisha kwamba vyombo vya dola vya ulinzi na usalama vinaendelea kuboreshwa ili kwenda na wakati na kufanya kazi zake kwa weledi katika kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama, yenye amani na utulivu; haki ya watu ya mazingira salama kwa kuendelea kuhakikisha kwamba mazingira katika maeneo mbalimbali ikiwemo ya maji, kazi, migodi, viwanda, makazi, na mengineyo yanaendelea kuwa salama na rafiki kwa wanaoyatumia.

**47. Mheshimiwa Spika;** Serikali imeendelea pia kulinda, kukuza na kuendeleza haki za binadamu kama ifuatavyo:- haki ya binadamu wote kuzaliwa huru na sawa kwa kuhakikisha kwamba kila mtu yuko huru na sawa katika jamii jambo ambalo linakwenda sambamba na haki ya mtu kutokubaguliwa kwa namna yeyote ile ikiwemo kwa minajili ya siasa, rangi, jinsia, jinsi, kabila, kipato ama mahali anapotoka au misingi mingine ya kibaguzi; haki ya binadamu ya kuishi kwa kuhakikisha kwamba vitendo vyote vinavyoweza kuondoa maisha vinachukuliwa hatua na vyombo vya dola lakini pia kuhaikisha kuwa mazingira hatarishi yanarekebishwa kwa wakati ikiwemo upatikanaji wa dawa na tiba katika jamii; haki ya binadamu dhidi ya utumwa kwa kuhakikisha kwamba hatua zinachukuliwa kwa vitendo vyote vinavyojielekeza katika mazingira ya utumwa ikiwemo biashara na usafirishaji haramu wa binadamu au kuwatumikisha watu isivyo halali, hususan watoto na wanawake, vinadhibitiwa na wahusika kuchukuliwa hatua; haki ya binadamu ya kutokuteswa au kudhalilishwa kwa

kuhakikisha kwamba mtu au kikundi cha watu hakimtesi au kumdhalilisha mtu mwingine.

**48. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kulinda, kukuza na kuendeleza haki ya binadamu ya kutambuliwa mbele ya sheria kwa kuhakikisha kwamba vizazi vyote vinavyotokea nchini vianaendelea kutambuliwa na kuandikishwa kupitia mifumo ya RITA na utambulisho wa watu wazima unafanyika kupitia NIDA; haki ya binadamu ya usawa mbele sheria ya vyombo vya haki, ikiwemo kusikilizwa, kwa kuendelea kuviboresha na kuhakikisha kwamba vyombo vya kutoa haki ikiwemo Mahakama ya Tanzania na vyombo vingine vya haki vinawapa watu wote wanaofika mbele yake fursa sawa ya kujieleza, kujitetea, kutoa ushahidi au kuleta mashahidi na vielelezo vingine kadri inavyohitajika; haki ya binadamu ya faragha kwa kuhakikisha kwamba sheria zinawekwa na kufuatwa na watu wote katika kulinda haki ya faragha na utu wa mtu; haki ya binadamu ya kuishi au kwenda popote kwa kuhakikisha kwamba watu wanapata fursa ya kuwa na makazi au kwenda popote kwa mujibu wa sheria za nchi zilizowekwa na Bunge na kwa ajili ya kulinda maslahi mapana ya watu na nchi ya kiulinzi, kiusalama na maendeleo kwa ujumla; haki ya binadamu ya kupata hifadhi kwa kuhakikisha kwamba Taifa linaendelea kuwapatia hifadhi wale wanaopatwa na majanga mbalimbali ikiwemo wakimbizi kulingana na vigezo vya sheria za nchi na mikataba ya kikanda na kimataifa; haki ya binadamu ya uraia kwa kuhakikisha kwamba wote wenye kukidhi vigezo vya uraia wa Tanzania wanaendelea kufaidi uraia wao kwa mujibu wa sheria; haki ya binadamu ya mwanaume kuoa au mwanamke kuolewa na kuanzisha familia kwa kuendelea kuruhusu mwanamme na mwanamke ambao wametimiza vigezo vya kijamii na kisheria na wanapenda kuoana kiserikali, kidini, kimila au kuishi tu pamoja kama wenza wafanye hivyo na ili kuweza kupata watoto na kuendeleza familia zao; haki ya binadamu ya kumiliki mali za aina mbalimbali kwa njia halali kwa kuhakikisha kwamba kila mtu ana haki ya kutafuta na kujipatia mali kwa njia halali na kupewa hati au nyaraka mbalimbali kuthibisha au kurasimisha umiliki huo; uhuru wa

kuabudu kwa kutoa uhuru kwa watu kuwa au kutokuwa waumini wa madhehebu mbalimbali kulingana na sheria.

**49. Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na hoja kuhusu haki ya kuoa au kuolewa na kuanzisha familia kwa walio na umri chini ya miaka kumi na nane. Ieleweke kwamba Sheria ya Ndoa (Sura ya 29) inatoa wajibu na mazuio mbalimbali kwa watu katika kutekeleza haki ya kuoa au kuolewa. Ni wazi kwamba, pamoja na Sheria ya Ndoa kutoa fursa ya kuoa au kuolewa kwa mtu mwenye umri chini ya miaka 18, pia inamtaka mtu huyo ambaye yupo chini ya miaka 18, kwanza, iwapo ni mwanamke, apate ridhaa ya wazazi au mlezi na, pili, iwapo anayetaka kuoa yupo chini ya miaka 18 (kwa mwanaume) au kuolewa na yupo chini ya miaka 15 (kwa mwanamke), lakini kwa wote wawili wasiwe chini zaidi ya miaka 14, basi apate ridhaa ya Mahakama ili mwanaume huyo aoe au mwanamke aoelewe. Lakini pia wakati wa kutoa ridhaa hizo Mahakama, wazazi, walezi na hata wafungishaji ndoa wanaoongozwa na sheria mbalimbali za nchi ikiwemo Sheria ya Elimu (Sura ya 353) ambayo inamtaka kila mzazi au mlezi kumpeleka mtoto wake shuleni ili asome na hivyo kutoa adhabu kali kwa mtu yeyote ambaye atamzuia mwanafunzi kwenda shule au kuendelea na masomo yake ama kwa kuoa au kuolewa.

**50. Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa bila uwepo wa ridhaa iliyowekwa na Sheria ya Ndoa, na ridhaa hiyo kuzingatia sheria nyingine za nchi, mtu yeyote haruhusiwi kuingia kwenye mahusiano ya ndoa na kuanzisha familia kwa kuwa ndoa hiyo itakuwa ni batili. Pia, ni sharti la sheria kwamba kabla ya kutekeleza nia ya kuoa au kuolewa, wahusika wenyewe wawe wamefikia uamuzi huo kwa uhuru na watoe Notisi ya kuwajulisha wana jamii kwamba sasa wana nia ya kuoana. Hivyo, nitumie fursa hii kutoa rai kwa waliopewa wajibu huu wa kuwalinda watoto na vijana wetu, wakati wa kutoa ridhaa wahakikishe kuwa wanatekeleza wajibu huo vizuri na kwa busara ili kila mtoto au kijana aweze kupata haki zake mbalimbali kabla ya kuingia kwenye masuala ya ndoa na kwamba watendaji wote katika maeneo yao, ikiwemo wale wanaofungisha ndoa, wahakikishe hawakiuki misingi

iliyowekwa na sheria katika masuala ya ndoa. Nitoe rai pia kwa wanandoa wote kuhakikisha kuwa ndoa zote zinaandikishwa kulingana na sheria na pia miongozo mbalimbali inayotolewa na Kabidhi Wasii Mkuu kupitia RITA ili kuondoa uwezekano wa mtu kwenda kinyume na sheria, kanuni, taratibu na miongozo; au kukosa haki yake iwapo ndoa hiyo itapata misukosuko na kuvunjika, au mmoja wa wanandoa kufariki; lakini pia kudhibiti watu wasiokidhi vigezo kuoa au kuolewa. Ni imani yangu kuwa endapo, sheria zitatekelezwa ipasavyo na watu wote wakaelemika na kuitii sheria bila shuruti, tatizo la ndoa za watu wenye umri mdogo kuoa au kuolewa litapungua na kwisha kabisa. Serikali itaendelea kushirikiana na wadau katika kuendelea kuweka miongozo na kutoa elimu kwa jamii kwa ajili ya utekelezaji endelevu wa sheria hizi na nyingine kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

**51. Mheshimiwa Spika,** haki ya binadamu ya kutoa mawazo kupitia njia na vyombo mbalimbali kwa mujibu wa sheria, maadili na utamaduni wetu; haki ya binadamu ya kukusanyika na kuhakikisha kuwa mikusanyiko kwa ajili ya masuala mbalimbali ikiwemo ya kijamii, kiutamaduni, michezo, kisiasa na mengine yanafanyika kwa mujibu wa sheria na taratibu, na kwamba wakati wa uchaguzi wa kitaifa au wa Serikali za Mitaa, watu wanapata fursa ya kushiriki, kuchagua au kuchaguliwa kwa uhuru, haki na uwazi, na kwamba demokrasia nchini haki ya kupata taarifa na habari inaendelea kukua na kuimarika; haki ya binadamu ya kupata hifadhi ya jamii hususan kwa wazee, watoto na wenye mahitaji maalum; haki ya binadamu ya kufanya kazi kwa kuhakikisha kwamba fursa anuai za ajira zinaendelea kuongezeka ili kila mtu afanye kazi halali, apate ujira au kufaidi matunda ya jasho lake, lakini pia kuhakikisha kwamba watu wanaheshimu kazi kama njia pekee katika kupata maendeleo yao wenyewe, jamii na Taifa kwa ujumla; haki ya binadamu ya kupumzika au kupata likizo kwa wale ambao ni waajiriwa kwa kuhakikisha kwamba muda na siku za kufanya kazi ambao umewekwa na sheria za kazi unazingatiwa na kwamba kipindi cha likizo kikifika taratibu zinafuatwa ili mhusika aende likizo kwa mujibu wa sheria; haki

hizi nazo zimeendelea kulindwa, kukuzwa na kuendelezwa kulingana na uwezo wa Taifa letu na mazingira yake.

**52. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuzingatia wajibu wake katika haki ya binadamu ya huduma za jamii ikiwemo afya, maji, elimu, mafunzo, michezo, na sanaa kwa kuhakikisha kwamba huduma hizo zinawafikia watu wote katika maeneo yao au kwa umbali mfupi na kuendelea kuimarisha ubora wa huduma hizo kadri Taifa linavyoendelea kupata maendeleo na jamii kustawi. Haki hizi za binadamu na haki za watu ambazo nimezieleza kwa kirefu zinakwenda sambamba na wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha kwamba haki za watu na haki za mtu mmoja mmoja zinalindwa, kukuzwa na kuendelezwa ili nchi nzima iwe ni nchi yenye umoja, amani, usalama na utulivu ili ustawi wa jamii uweze kuendelea. Katika hili, utu na uzalendo wetu pamoja na uzingatiwaji wa maadili na utamaduni wetu kama watanzania ni muhimu.

**53. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza wajibu wa Serikali wa kulinda na kuendeleza haki za binadamu na haki za watu, Wizara iliiwakilisha nchi katika mikutano mbalimbali ikiwemo Kikao cha 41, 42 na 43 cha Baraza la Haki za Binadamu, Geneva, Uswisi miezi ya Julai na Septemba, 2019 na Machi, 2020 mtawalia. Madhumuni ya kushiriki kwenye Mikutano hii ni pamoja na kuonyesha namna Serikali inavyotekeleza mikataba ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu na haki za watu iliyoridhia. Katika kikao hicho Wizara iliwasilisha Taarifa ya Nchi ya Hali ya Haki za Binadamu ya mwaka 2019 na 2020. Taarifa hiyo pamoja na mambo mengine ilionyesha jinsi Serikali inavyoendelea kukuza na kulinda haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Pamoja na mambo mengine taarifa hiyo ilibainisha kwamba katika kulinda na kukuza haki za kiraia Serikali itaendelea kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuwa na Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba 2020 ambao utakuwa huru, wazi na sawa. Kwa kuthibitisha hilo Watazamaji wa Uchaguzi wa kimataifa, kikanda na wa ndani ya nchi wataalikwa kushuhudia uchaguzi huo.

**54. Mheshimiwa Spika**, Katika kukuza haki za kisiasa taarifa hiyo ilionyesha kwamba, Serikali inatambua jukumu kubwa la vyama vya siasa katika kujenga demokrasia na hivyo ilirekebisha Sheria ya Vyama vya Siasa (Sura ya 258). Sheria hiyo inatoa mwongozo kwa vyama vya siasa na masuala ya kuzingatia wakati wa kutekeleza kazi zao ambayo ni pamoja na kudumisha misingi ya kidemokrasia, utawala bora, usawa wa kijinsia, amani ya nchi pamoja na dhana nyingine muhimu wakati wa kuleta maendeleo nchini. Aidha, katika kuhakikisha usawa mbele ya sharia, Jaji Mkuu alitunga Kanuni zilizochapishwa kwenye Tangazo la Serikali Na. 110 la tarehe 01 Machi, 2019 zinazoelekeza kwamba mashauri yote yanayohusu wanawake, watoto na watu wenye ulemavu kuhitimishwa ndani ya miezi sita.

**55. Mheshimiwa Spika**, Katika taarifa iliyowasilishwa, uwepo wa uhuru wa habari na uhuru wa kujieleza ulielezwa kwa kufafanua kwamba hadi mwaka 2019 kulikuwa na takriban vyombo vya redio zilizosajiliwa **152** ambavyo kati ya hivyo vitatu (**3**) ni vya Serikali na vingine **149** ni vya sekta binafsi. Vilevile, kati ya vyombo vya televisheni **34** vilivyopo viwili (**2**) ni vya Serikali na **32** vinamilikiwa na sekta binafsi. Aidha, taarifa ilibainisha kuwa kulikuwa na jumla ya takriban leseni **172** za magazeti yaliyosajiliwa ambapo asilimia **90** zinamilikwa na sekta binafsi. Vilevile, taarifa hii ilibainisha kuwa Serikali inathamini kazi inayofanywa na vyombo vya habari na mchango wake kwenye maendeleo ya nchi na hii ilikuwa moja ya chanzo cha kutunga Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa (Sura ya 149) na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari (Sura ya 229). Sheria hizi zimekusudia kulinda ustawi wa wanahabari katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa masuala ya mishahara, bima, na pensheni yanazingatiwa ipasavyo.

**56. Mheshimiwa Spika**, Taarifa hiyo pia ilibainisha kuwa katika kukuza haki za kiutamaduni na kijamii, Serikali inahakikisha kila mtoto anaenda shule kwa kupitia elimu bure na kwamba Serikali imekuwa ikitenga kiasi cha **Shilingi Bilioni 23.8** kila mwezi kuendeleza sekta ya elimu. Aidha, ilielezwa kwamba huduma za afya zinasogezwa karibu na wananchi ambapo

katika kipindi cha miaka mitano (2015-2019) jumla ya zahanati **423**, Vituo vya Afya **451** na Hospitali za Wilaya **70** zimejengwa, pamoja na watumishi wa afya **13,479** waliajiriwa ili kuboresha huduma za afya nchini. Aidha serikali inatarajia kuongeza Madaktari wengine **1000** wa afya kufuatia ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika Mkutano wa Madaktari pamoja na watumishi wa sekta ya afya tarehe 20 Machi 2020. Kuhusu huduma ya maji, taarifa hiyo ilieleza kwamba huduma za maji zimeboreshwa na upatikanaji wa maji mwaka 2019 ulifikia asilimia **60** vijijini na asilimia **78** mijini.

**57. Mheshimiwa Spika**, kuhusu haki za Kiuchumi taarifa ilibainisha shughuli za kimaendeleo zinazotekelezwa nchini na jitihada za kufikisha Tanzania iwe Nchi ya Uchumi wa Kati. Aidha, ilielezwa na kusisitiza kwamba maendeleo yetu yana sura ya haki za binadamu lakini pia yamebeba haki za watu katika ujumla wake. Hivyo, Serikali inahakikisha kwamba sambamba na kasi ya mipango yake ya maendeleo, haki za kiuchumi zinalindwa na kukuzwa kwa usawa, bila kupendelea au kutoa kipaumbele kwa kundi moja la haki za binadamu zaidi ya lingine. Ilifafanuliwa pia kwamba katika suala la utawala bora ni muhimu kuhakikisha maendeleo ni endelevu na yanazingatia misingi ambayo mataifa yamekubaliana kupitia mikataba na mipango mbalimbali ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030 na Ajenda ya Afrika 2063. Hivyo, Serikali imeimarisha taasisi za haki za binadamu na zile za haki za watu, na pia katika kuhakikisha utawala bora, utawala wa sheria na mapambano dhidi ya rushwa yanakwenda sawia na mambo mengime muhimu katika ujenzi wa Taifa na ustawi wa wananchi. Pia taarifa hiyo ilieleza namna Serikali inavyotambua mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika kuimarisha haki za binadamu, haki za watu na kuleta maendeleo nchini.

**58. Mheshimiwa Spika,** Wizara inakamilisha Mpango Kazi wa Pili wa Kitaifa wa Haki za Binadamu wa mwaka 2020 - 2025 unaojumuisha mapendekezo yaliyokubaliwa chini ya Mfumo wa Umoja wa Mataifa wa Mapitio wa Kipindi Maalum. Lengo

la mpango huu ni kuiwezesha Serikali kuwa na mwongozo unaoonesha vipaumbele kwenye masuala ya haki za binadamu na kurahisisha utekelezaji wa mapendekezo ambayo Serikali ilikubali kuyatekeleza chini ya Mfumo huo wa Umoja wa Mataifa wa Mapitio wa Kipindi Maalum. Tunatarajia Mpango Kazi huo uanze kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi 2024/2025.

**59. Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilipata Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wapya ambao waliapishwa mwezi Novemba 2019 na kuanza kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria. Aidha, Tume iliendelea kupokea na kufanya uchunguzi wa malalamiko yanayohusu uvunjifu wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora nchini. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi mwezi Machi, 2020 Tume ilipokea malalamiko mapya **243** na hivyo kufanya idadi ya malalamiko kufikia **6,663** (ya zamani na mapya) yaliyokuwa yanaendelea na uchunguzi. Kati ya malalamiko hayo, **1,982** yamefanyiwa uchunguzi na kuhitimishwa. Malalamiko mengine **4,681** yanaendelea na uchunguzi katika hatua mbalimbali.

**60. Mheshimiwa Spika,** Tume iliendelea kuelimisha umma kuhusu haki za Binadamu na Utawala na jinsi ya kutumia huduma za Tume, kupitia vyombo mbalimbali vya habari, mikutano, maadhimisho ya kitaifa na kimataifa, machapisho na warsha mbalimbali. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya nakala **5,000** za vipeperushi na machapisho mbalimbali zilisambazwa kwa wananchi na taasisi mbalimbali. Vilevile, Tume iliendelea kuelimisha umma kupitia wanafunzi katika jumla ya sekondari **23** na vyuo vya ualimu vitatu (**3**) katika mikoa ya Pwani, Morogoro na Singida. Kupitia utaratibu huu jumla ya wanafunzi **11,050** na walimu **780** walifikiwa katika kipindi hiki.

**61. Mheshimiwa Spika,** katika kutetea haki za makundi maalumu nchini, Tume ilifanya uchunguzi na tafiti mbalimbali. Uchunguzi uliofanyika ni pamoja na uchunguzi kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika mikoa ya Mara na

Singida. Utafiti uliofanyika ulihusu unyanyasaji wa kingono dhidi ya wanafunzi wa kike katika vyuo vikuu na utafiti kuhusu ufikiaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu katika taasisi za elimu ya juu. Taarifa na mapendekezo ya uchunguzi na tafiti hizo zimewasilishwa Serikalini na zinaendelea kufanyiwa kazi.

**62. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilifanya ukaguzi kuhusu uzingatiwaji wa haki za binadamu kwenye Magereza **29** na Vituo vya Polisi **14**. Taarifa za ukaguzi na mapendekezo ya Tume zinaendelea kufanyiwa kazi na serikali kama sheria inavyoelekeza.

## XII. Mapitio ya Sheria Mbalimbali

**63. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria inawajibu wa kufanya mapitio na tafiti na kupendekeza maboresho ya sheria mbalimbali ili ziende na wakati na kuakisi hali halisi ya mabadiliko na maendeleo katika nyanja za kiraia, kisiasa, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Tume ya Kurekebisha Sheria, imeendelea kufanya mapitio na utafiti kuhusu; Mfumo wa Sheria unaosimamia Uwakilishi wa Kisheria Mahakamani, Mfumo wa Sheria unaosimamia Wazee wa Mahakama, Mfumo wa Sheria unaosimamia Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi na Mfumo wa Sheria unaosimamia Utatuzi wa Migogoro ya Kazi. Katika kuhakikisha kwamba wadau wanashirikishwa katika kupendekeza maboresho ya sheria katika maeneo hayo, Tume ilifanya mikutano **24** katika mikoa **12** kwa madhumuni ya kukusanya maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu mapitio hayo. Mikutano hiyo ilifanyika katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Iringa, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Songwe, Tabora na Tanga.

**64. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata elimu ya sheria kuhusu mabadiliko mbalimbali ya kisheria yaliyotokea, Tume ilitoa elimu kwa umma kupitia wiki ya sheria, maonesho ya Sabasaba na Nanenane, vipindi vya

redio na vipeperushi. Tume pia ilifanya tathmini ya utekelezaji wa sheria mbalimbali kwa lengo la kubaini changamoto za utekelezaji na kutathmini kama malengo yaliyokusudiwa wakati wa kutungwa kwa sheria hizo yamefikiwa. Tathmini hizo zimefanywa katika Sheria za Mahakama za Migogoro ya Ardhi, Sheria ya Taasisi za Kazi, Sheria ya Misitu na Sheria ya Mabaraza ya Kata. Mapendekezo ya Tume katika tathmini hizi yapo katika hatua mbalimbali za uchambuzi na utekelezaji serikalini.

## XIII. Urejeshwaji wa Wahalifu na Ushirikiano wa Kimataifa Katika Makosa ya Jinai

**65. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipokea jumla ya maombi mawili (**2)** ya kurejesha watuhumiwa wa makosa mbalimbali ya jinai waliokimbilia nchini baada ya kutenda makosa kwenye nchi zao. Maombi hayo yapo katika hatua mbalimbali za kushughulikiwa kwa mujibu wa Sheria ya Urejeshwaji wa Wahalifu (Sura ya 268). Kwa upande wa Serikali yetu, Wizara iliwasilisha ombi la kumrejesha mhalifu aliyekimbilia nje ya nchi ambaye anakabiliwa na kosa la mauaji. Ombi hilo bado linaendelea kufanyiwa kazi na mamlaka za nchi husika. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na mataifa mengine katika kubadilishana mashahidi na vielelezo ambapo ilipokea ombi la kukusanya ushahidi na vielelezo kutoka nchi nyingine. Ombi hilo linaendelea kushughulikiwa kwa mujibu wa Sheria ya Kusaidiana katika Masuala ya Jinai (Sura ya 256). Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020, Wizara ilikamilisha ukusanyaji wa vielelezo na nyaraka za maombi mawili (**2**) na kuyawasilisha katika nchi zilizoomba**.** Kwa upande wa Serikali ya Tanzania, Wizara iliwasilisha nje ya nchi maombi mawili (**2**) ya kukusanya ushahidi na vielelezo ambayo yanaendelea kushughulikiwa na mamlaka husika za nchi hizo.

## XIV. Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu

**66. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini, iliendelea kuimarisha shughuli za usajili wa vizazi, vifo, ndoa, talaka na

watoto wa kuasili ikiwa ni haki ya msingi ya kusajiliwa na upatikanaji wa takwimu kwa ajili ya maendeleo. Katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini ulisajili vizazi **1,247,640;** vifo **16,056;** ndoa **31,084;** talaka **181** na hati **21** za watoto wa kuasili. Aidha, jumla ya wosia 4**3** zimeandikwa na kuhifidhiwa na Bodi za Wadhamini **62** zimesajiliwa. Wakala unaendelea na utekelezaji wa mpango wa usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano katika Mikoa ya Morogoro, Pwani na Ruvuma. Jumla ya Watoto **702,773** walisajiliwa na kupatiwa vyeti ikiwa ni sawa na asilimia **87** ya lengo la kusajili Watoto **802,871** wa umri huo katika mikoa hiyo. Aidha, Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo Sura 108, ambapo pamoja na mambo mengine marekebisho hayo yamelenga kuhakikisha usajili wa matukio muhimu ya binadamu unaenda sambamba na mabadiliko ya kuboresha na kusogeza huduma za usajili wa matukio muhimu ya binadamu karibu na wananchi.

**67. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini imeendelea kuhakikisha kwamba huduma za usajili zinatolewa kwa kutumia TEHAMA kwa mfumo wa kielekroniki uitwao ***Birth Registration Fourth Generation (BR4G)***. Katika kipindi hicho, Wakala umefunga mfumo huo katika Wilaya za Chemba, Malinyi, Bahi, Buhigwe, Kakonko na Kalambo na hivyo kukamilisha ufungwaji wa mfumo huo katika wilaya zote **139** za Tanzania Bara. Aidha, Wakala umeingia Makubaliano ya kubadilishana taarifa za usajili wa matukio ya Vizazi na Vifo kwa kutumia TEHAMA baina yake na Idara ya Uhamiaji ikiwa na lengo la kuongeza tija katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

**68. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na uelewa kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini, Wizara kupitia Wakala imendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma zinazotolewa na Wakala kwa kupitia vyombo vya habari vikiwemo magazeti. Katika kipindi hicho, jumla ya makala **85**

yalichapishwa na vipindi **23** vya mahojiano vilifanyika katika redio mbalimbali. Aidha, vipindi vya mahojiano **19** vilifanyika katika vituo vya luninga na Vipeperushi **12,000** vimechapishwa na kusambazwa kwa wananchi kwa lengo la kutoa elimu, hamasa, gharama na maelekezo ya jinsi ya kupata huduma. Kati ya hivyo, vipeperushi **3,000** vinahusu vizazi na vifo, **3,000** vinahusu ndoa na talaka, **3,000** vinahusu miunganisho ya wadhamini na vipeperushi **3,000** vinahusu wosia.

## XV. Kuratibu Masuala ya Utajiri na Maliasilia za Nchi

**69. Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imebarikiwa kuwa na utajiri wa asilia na pia maliasilia za aina mbalimbali. Kwa mujibu wa sheria ya Mamlaka ya Nchi juu ya Utajiri na Maliasilia za Nchi (Sura ya 449), utajiri na maliasilia hizi zinajumuisha vitu vyote ambavyo vipo kiasilia nchini mwetu kama udongo na matabaka yake, gesi asilia, mafuta, madini, vito, maji, mito, maziwa, bahari na eneo lake, anga, hewa asilia, mimea, misitu, wanyama, ndege, samaki, wadudu wa aina na ukubwa mbalimbali, maeneo mbalimbali ya vivutio vya asilia, na vitu vyote vinavyoishi na visivyoishi katika eneo huru la bahari la kibiashara ambavyo vinaweza kuchimbwa, kutumiwa au kumilikiwa kwa ajili ya manufaa ya kiuchumi bila kujali kama vimeongezewa thamani au la. Kama tunavyofahamu, rasilimali hizi zinasimamiwa na sekta mbalimbali, kila moja ikiwa na eneo lake mahsusi la kushughulikia.

**70. Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 9(i) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Sura ya 2) inasema kwamba Mamlaka ya Nchi na vyombo vyake vyote vinawajibika kuelekeza sera na shughuli zake zote katika lengo la kuhakikisha kwamba matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi, na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada ya kuondosha umaskini, ujinga na maradhi. Ibara ya 27 inaongezea nguvu Ibara hii ya 9(i) kwa kueleza kuwa kila mtu ana wajibu wa kulinda maliasilia za nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi na kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhilifu,

na kuendesha uchumi wa Taifa kwa makini kama watu ambao ndiyo waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa lao. Aidha, Ibara ya 8(1)(c) inaitaka Serikali kutekeleza lengo kuu linaloiongoza ambalo ni ustawi wa wananchi. Kwa muktadha huu, Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani, na katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015, ilianza kulifanyia kazi kwa nguvu zake zote eneo la utajiri na maliasilia.

**71. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, kazi na majukumu mbalimbali yaliendelea kutekelezwa katika tasnia ya utajiri na maliasilia za nchi na mafanikio kuendelea kupatikana ambayo hatma yake ni kuhakikisha Ibara ya 8, 9 na 27 za Katiba, zikisomwa kwa pamoja, zinatekelezwa. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki ni pamoja na kukamilisha majadiliano katika mikataba mitatu (**3**) ya uwekezaji ya madini na gesi asilia ambapo pamoja na mambo mengine imeliwezesha Tanzania kusaini makubaliano na Kampuni ya Barrick ya kuanzishwa kwa Kampuni ya Madini ya Twiga ambapo imesaidia Taifa kumiliki hisa asilimia 16 kwenye kampuni ya madini ya Twiga na vilevile kuiwezesha serikali na mmliki kupata faida ya asilimia 50 kwa 50 itakayotokana shuhuli za madini katika maeneo ya uwekezaji. Aidha, makubaliano hayo yatakiwezesha Chuo Kikuu cha Dar es salaam kupata Dola za Kimarekani milioni **10** kwa kipindi cha miaka 10 kwa ajili ya kuwasomesha vijana wetu katika tasnia ya madini. Makubaliano hayo pia yatawezesha ujenzi wa barabara ya Bulyanhulu hadi Mwanza na pia uwekaji wa mpango wa maendeleo ya jamii kwa kuanzisha fursa mbalimbali za kiuchumi kwa wakazi wa eneo linalozunguka migodi hiyo. Hii ni hatua kubwa na majadiliano bado yanaendelea katika maeneo mengine. Hali kadhalika Wizara iko kati maandalizi ya kuanzisha mfumo wa Kieletroniki wa usajili na ufuatiliaji wa mikataba inayohusu utajiri asili na rasilimali za nchi kwa lengo la kurahisisha kazi ya uratibu katika eneo hili.

## XVI. Mafunzo ya Uongozi wa Mahakama na Utoaji Haki

**72. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, kimeendelea kusimamia shughuli za

taaluma ya Uongozi wa Mahakama. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 kwa mwaka wa masomo 2019/2020 Chuo kilidahili wanafunzi **677** wa ngazi ya Astashahada na Stashahada ikilinganishwa na wanafunzi **656** wa mwaka wa masomo 2018/19. Udahili huu utasaidia kuongeza rasilimaliwatu kwenye sekta ya sheria na hivyo kuongeza tija na ufanisi.

**73. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Chuo Uongozi wa Mahakama Lushoto, chini ya ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) imetoa mafunzo ya Taratibu za Uendeshaji wa Mashauri ya Mtoto kwa Maafisa wanaohusika na usikilizaji wa mashauri. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 mafunzo hayo yameendelea kutolewa kwenye Kanda sita **(6)** za mahakama na katika mkoa mmoja **(1).** Kanda hizo ambazo ziliwekwa kwenye mpango wa mafunzo wa miaka miwili **(2)** ni Kanda ya Mahakama Kuu Moshi, Shinyanga, Bukoba, Sumbawanga, Mtwara na Songea, ikiwa ni pamoja na mkoa wa Geita. Mafunzo hayo yalijumuisha washiriki **332** ambao ni Mahakimu, Mawakili wa Serikali, Waendesha Mashtaka na Maafisa Ustawi wa Jamii kutoka katika kanda hizo. Mafunzo hayo yanalenga kutoa haki kwa wahusika wakiwa ndani na nje ya mahakama kwa kundi lenye mahitaji maalum la watoto.

**74. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania iliendesha mafunzo ya namna bora ya kusikiliza na kushughulikia kesi za rushwa na uhujumu uchumi kwa Waheshimiwa Majaji, Naibu Wasajili wa Mahakama na Mahakimu Wakazi wapatao **36**. Aidha, Chuo kiliendesha Mafunzo ya Wakufunzi juu ya namna bora ya kuandika hukumu kwa Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani ya Tanzania na Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania wapatao **26**, lengo likiwa ni kuongeza tija katika kuandika hukumu.

**75. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) kilitoa mafunzo kuhusu utatuzi wa

migogoro ya ardhi kwa njia ya usuluhishi katika wilaya za Ulanga, Malinyi, Ifakara, Kilosa na Mvomero Mkoani Morogoro. Jumla ya washiriki **140** walinufaika na mafunzo hayo. Mafunzo hayo yalijumuisha; wanasheria wa Halmashauri, Wenyeviti wa Wilaya, Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi, Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuwajengea uwezo wahusika namna bora ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa njia ya usuluhishi.

**76. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi kufikia Machi, 2020, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ilisajili Kituo cha Msaada wa Kisheria ambacho kinatoa msaada wa kisheria kwa wahitaji na hivyo kusaidia kufanikisha lengo la Serikali la kufikisha huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi kwa wakati na kwa gharama nafuu. Aidha, Chuo katika kuhudumia jamii inayokizunguka, kilitoa msaada wa kisheria kwa jumla ya wananchi **240** wa Halmashauri za Lushoto, Bumbuli, Korogwe na Mlalo. Sambamba na hilo, Chuo kimetoa mafunzo ya weledi wa namna bora ya kufanya kazi kwa wadau wa mahakama, ambapo Madalali wa Mahakama **41** na Wasambaza Nyaraka za Mahakama 2**7** walifuzu mafunzo hayo yenye lengo la kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa amri za mahakama na vile vile kuboresha taswira ya Mahakama na kurudisha imani ya wananchi kwa Mahakama.

**77. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kiume la ghorofa tano **(5)** lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi **300.** Hadi kufikia Machi, 2020 mradi huu ulikuwa katika hatua ya ukamilishaji baada ya kuezekwa na kupaka rangi ya awali.

## XVII. Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo

**78. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo kwa wahitimu wa shahada ya sheria kutoka vyuo

vikuu mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Taasisi imedahili wanafunzi **1,357** wa kundi la 29 na 30. Idadi hii ni sawa na ongezeko la asilimia **13.1** ya lengo la usajili wa wanafunzi **1,200** kwa mwaka 2019/2020. Aidha, mafunzo ya uanasheria kwa vitendo yalitolewa kwa wanafunzi **1,323** kwa Kundi la 29 na 30 sawa na ongezeko la asilimia 10.3 ya malengo ya utoaji mafunzo kwa wanafunzi **1,200** kwa mwaka Jumla ya wanafunzi **606** wa kundi la 28 waliwezeshwa kwenda kufanya mafunzo ya vitendo sehemu za kazi ambapo zoezi la kuwasimamia na kuwapa miongozo mbalimbali lilifanyika. Vilevile, matokeo ya mitihani ya jumla ya wanafunzi **1,693** yalitolewa ambapo wanafunzi **515** sawa na asilimia **30.4** walifaulu, wanafunzi **1,062** sawa na asilimia **62.7** wanatakiwa kurudia mitihani, wanafunzi **99** sawa na asilimia **5.8** walishindwa mitihani na wanafunzi **17** sawa na asilimia moja **(1)** waliahirisha kufanya mitihani.

**79. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kutoa mafunzo kwa watoa huduma za msaada wa kisheria na kutoa msaada wa kisheria kwa wahitaji, Wizara kupitia Taasisi hiyo, iliandaa Mtaala wa mafunzo na kuuwasilisha Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi kwa ajili ya kupitishwa na kuanza kutumika. Mtaala huu utawawezesha watoa huduma za msaada wa kisheria kupata ujuzi wa namna bora ya kutoa huduma hizo. Aidha, katika kipindi hicho Taasisi ilisajili Kituo cha Msaada wa Kisheria kitakachotoa huduma ya msaada wa kisheria kwa wahitaji na hivyo kusaidia kufikia lengo la Serikali la kutoa msaada wa kisheria kwa wahitaji nchini.

**80. Mheshimiwa Spika**, kama mnavyofahamu, wengi wa wahitimu wetu wa shahada ya sheria wanatoka katika Vyuo Vikuu vya hapa nchini. Ili kuendelea kuhamasisha utoaji wa elimu bora ya taaluma ya sheria nchini na inayokwenda sawa na azma yetu ya kujenga uchumi wa viwanda na hatimaye kulifikisha Taifa katika kundi la nchi zenye uchumi wa kati, Wizara, ikishirikiana na Baraza la Elimu ya Sheria na Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo ya Tanzania, mwezi Machi 2020, ilifanya ziara katika vyuo vya elimu ya juu saba (**7**) vinavyotoa shahada ya sheria ambavyo ni Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kukuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha

Kiislamu Morogoro, Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Makumira, Chuo Kikuu Kishiriki cha Mtakatifu Jordan, Chuo Kikuu Iringa na Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Ruaha. Lengo la ziara hii ni kuona hali halisi ya utoaji wa taaluma ya Sheria katika Vyuo hivyo. Kwa ujumla Wizara ilibaini kwamba vyuo hivyo vinaendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na kuwajengea wanafunzi uwezo wa kumudu utoaji wa huduma za sheria, kujieleleza na kujiamini. Hata hivyo, baadhi ya changamoto zilibainishwa ikiwa ni pamoja uelewa usioridhisha wa lugha ya kiingereza ambayo inatumika katika kufundishia masomo ya sheria; baadhi ya wanafunzi kutokuwa makini katika masomo na hivyo kuwafanya kutofanya vizuri katika masomo yao wanapojiunga na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, na uhaba wa waalimu wenye sifa na uzoefu stahiki kwa ujumla. Pamoja na changamoto zilizopo, kutokana na umuhimu wa sekta ya sheria katika maendeleo endelevu, Wizara imetoa rai kwa vyuo hivyo kuondokana na dhana za zamani za ufundishaji kwa lengo la kufaulu mtihani na kuajiriwa na kuanza kuwajengea wanafunzi uwezo wa kujiajiri ili kuendana na mwelekeo wa sasa wa dunia na muelekeo wa nchi yetu kuelekea uchumi wa viwanda. Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine katika jitihada za Taifa letu za kuboresha na kuimarisha elimu nchini. Aidha Wizara imeliagiza Baraza la Elimu ya Sheria nchini kuzifanyia kazi changamoto mbalimbali zilizopo katika mfumo mzima wa elimu ya taaluma ya sheria kwa kushirikiana na wadau na kuishauri Serikali namna bora ya kuzishughulikia changamoto hizo kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya sheria. Zoezi hili litaendelea kwenye Vyuo Vikuu vilivyosalia ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo ya Wizara wakati wa ziara hizo.

## XVIII. Kutembelea na Ukaguzi wa Magereza na Sehemu za Kuhifadhia Watuhumiwa katika Vituo vya Polisi

**Mheshimiwa Spika,** Wizara na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilitekeleza wajibu wake wa kukagua Magereza na Vituo vya Polisi. Lengo la ukaguzi huu ilikuwa kuainisha changamoto za kiutendaji na upelelezi na kutoa maelekezo stahiki ya

kutatua changamoto hizo. Katika kipindi husika, Magereza **99** na Vituo vya Polisi **129** vilikaguliwa. Lengo la kutembelea na ukaguzi wa maeneo haya ni kuhakikisha kwamba sheria, kanuni, taratibu na miongozo kuhusu watuhumiwa inavyotekelezwa na kufuatwa katika vituo vya Polisi na kwamba sheria, kanuni, taratibu na miongozo pia inafuatwa katika Magereza kuhusu mahabusu na wafungwa na kuchukua hatua ili kurekebisha pale panapoonekana kuna kasoro. Orodha ya Vituo vya Polisi na Magereza vilivyokaguliwa katika kipindi hicho imeoneshwa katika **KIAMBATISHO H.**

## XIX. Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama

**81. Mheshimiwa Spika,** kuhusu miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama, katika kipindi cha Julai 2019 na Machi, 2020, Mahakama iliendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Kuboresha Huduma za Mahakama ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi mbalimbali nchini. Katika kutekeleza hilo, Mahakama imekamilisha ujenzi wa jumla ya majengo **21** yakiwemo majengo ya Mahakama Kuu mawili **(2)** katika Mikoa ya Kigoma na Mara; ujenzi wa majengo mawili **(2)** ya Mahakama ya Hakimu Mkazi katika mikoa ya Simiyu na Manyara; ujenzi wa Mahakama za Wilaya **10** katika Wilaya za Longido, Chato, Geita, Bukombe, Bariadi, Njombe, Ruangwa, Kilwa, Chunya, Kondoa na kuendelea na ujenzi katika Wilaya saba **(7)** za Kasulu, Wanging'ombe, Bunda, Makete, Sikonge, Kilindi na Rungwe. Aidha, Mahakama imekamilisha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo sita **(6)** za Mlowo, Magoma, Uyole, Mtowisa, Msanzi, na Mkunya. Vilevile ujenzi wa Mahakama za Mwanzo tisa **(9)** za Ngerengere, Mang'ula, Mlimba, Laela, Mtowisa, Msanzi, Uyole, Mtae, na Lugarawa upo kwenye hatua za mwisho kukamilika. Aidha, ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania Jijini, Dodoma unatarajiwa kuanza katika mwaka wa Fedha 2019/2020. Maelezo na orodha ya Mahakama hizo yanapatikana kwenye **KIAMBATISHO I.** Aidha, ujenzi unatarajiwa kukamilika katika Mahakama za Mwanzo 4,

Mahakama za Wilaya 6; Mahakama za Hakimu Mkazi 2 na Mahakama Kuu 1 inayokarabatiwa ifikapo Juni, 2020.

**82. Mheshimiwa Spika,** Mahakama imekamilisha Ujenzi wa jumla ya nyumba nne **(4)** zikiwemo mbili **(2)** za Majaji Mkoani Kigoma na mbili **(2)** za Mkoani Mara ambapo ujenzi wa nyumba mbili za Hakimu Wilayani Loliondo uko katika hatua za umaliziaji. Aidha, ujenzi wa vituo Jumuishi vya Haki umeanza katika mikoa ya Mwanza, Morogoro, Dar es salaam, Arusha na Dodoma.

**83. Mheshimiwa Spika,** Mahakama inaendela na taratibu za ujenzi wa jengo la makao makuu ya Mahakama Jijini, Dodoma. Hadi sasa kazi zilizofanyika ni pamoja na maandalizi ya michoro na makisio ya awali ya gharama za ujenzi wa jengo hilo. Aidha, Serikali imeipatia Mahakama kiasi cha **Shilingi bilioni 10.5** kwa ajili ya kuanza ujenzi huo ambapo taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga jengo husika zinaendelea kufanyika. Kwa ujumla, kazi za ujezi katika Mhimili wa Mahakama zitaendelea kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 ili kufikia malengo tuliyojiwekea katika mpango mkakati wa kuboresha miundombinu ya Mahakama ya Tanzania.

## XX. Progamu ya Kutenganisha Upelelezi na Uendeshaji Mashtaka

**84. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza matakwa ya kisheria, Serikali imeendelea kutekeleza Progamu ya Kutenganisha Upelelezi na Uendeshaji Mashtaka kwa kusogeza huduma za mashtaka karibu na wananchi katika ngazi za Wilaya. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2019 hadi Machi, 2020, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilifungua Ofisi zake katika Wilaya za Kondoa mkoani Dodoma, Ilala mkoani Dar es Salaam, Ilemela mkoani Mwanza na Korogwe mkoani Tanga na hivyo kufanya jumla ya Ofisi za Wilaya zilizofunguliwa kuwa tisa **(9).** Serikali itaendelea kutekeleza Programu hii kwa kufungua Ofisi katika Wilaya zilizobaki kadri fedha zitakavyopatikana.

## XXI. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kimahakama

**85. Mheshimiwa Spika,** Mahakama imeendelea kutumia TEHAMA katika utoaji wa huduma. Katika kuboresha huduma hiyo Mahakama imeanzisha mifumo na kufanya maboresho mbalimbali ya Mifumo ya kielektroniki ambayo ni Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri (JSDS), Mfumo wa Kuwasimamia Mawakili (TAMS) na Mfumo wa Utambuzi wa Mahakama na Majengo yake (JMAP). Mifumo hii imeongeza ufanisi katika utoaji haki nchini na kuwezesha utambuzi wa taarifa na takwimu mbalimbali za Mahakama katika kutafsiri sheria na kutoa haki nchini.

## XXII. Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria

**86. Mheshimiwa Spika,** Wizara, kwa kushirikiana na Taasisi ya UONGOZI imempata Mtaalam Mwelekezi ambaye hivi sasa anaendelea kuhakiki taarifa na takwimu zilizobainishwa na wadau wa sekta ya sheria ili kuandaa rasimu ya Awamu ya Pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria. Programu hii yenye lengo la kuboresha Sekta ya Sheria ni ya miaka mitano na itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021.

## XXIII. Maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai

**87. Mheshimiwa Spika,** katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuhakikisha kwamba mfumo wa Haki Jinai unaimarishwa ili haki iweze kupatikana kwa wakati, kwa gharama nafuu na kwa usawa, Wizara imeendelea kubuni mbinu na mikakati mbalimbali ya kuboresha mifumo ya haki jinai. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wizara kupitia mradi wa *Programu Endelevu* ya *Kuzuia Rushwa Nchini* **(Building Sustainable Anti-corruption Action in Tanzania - BSAAT**), inaratibu uandaaji wa Programu ya Maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai nchini kwa kushirikiana na wadau. Malengo makuu ya programu hii ni pamoja na kuimarisha mifumo na taratibu katika mnyororo wa Haki Jinai ikiwemo uzuiaji wa uhalifu; kubaini uhalifu unapotokea; taratibu za ukamataji wa

wahalifu; upelelezi wa makosa ya jinai; uendeshwaji na usikilizwaji wa mashauri mahakamani; utaratibu wa utoaji wa adhabu na urekebishaji wahalifu na ufuatiliaji wa mienendo ya wale wanaokamilisha adhabu zao au wanaoachiwa kwa sababu mbalimbali. Hivi sasa, Wizara inaendelea kukamilisha andiko kwa ajili ya kuwasilisha mapendekezo ya maboresho ya programu katika vikao vya maamuzi.

## XXIV. Maendeleo ya Rasilimaliwatu

**88. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia watumishi wake ili kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma. Wizara imechukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi waliokiuka maadili ya kazi kwa baadhi yao kupewa onyo, na wengine kufukuzwa kazi. Aidha, Wizara iliajiri watumishi wapya **171**, kuwathibitisha watumishi **259**, kuwapandisha cheo watumishi **72**. Katika kipindi hicho Wizara kupitia Tume ya Utumishi wa Mahakama Tanzania imejadili na kufanya maamuzi juu ya masuala **42** ya nidhamu kwa watumishi wa kada mbalimbali wa Mahakama ambapo watumishi **18** walifukuzwa kazi, watumishi watano **(5)** walirejeshwa kazini na watumishi **19** alipewa onyo kama inavyooneshwa katika **KIAMBATISHO J**.

**89. Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha utendaji wa Mahakama, katika kipindi hicho Tume ya Utumishi wa Mahakama ilimshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu ambapo uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu **12,** Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Msajili Mkuu wa Mahakama, Msajili wa Mahakama ya Rufani na Msajili wa Mahakama Kuu ulifanyika. Pia Tume kwa mamlaka iliyopewa na Sheria iliwezesha uteuzi jumla ya Naibu Wasajili **11** kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Mahakama.

**90. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Tume ya Utumishi wa Mahakama imeendelea kuimarisha Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama kwa kukamilisha Mwongozo wa Uendeshaji wa Kamati za Maadili ya Maafisa wa Mahakama za Mikoa na Wilaya. Aidha, hali ya nidhamu na maadili ya

watumishi na utendaji wao wa kazi kwa ujumla imeendelea kuimarika.

## XXV. Janga la COVID 19 au Virusi vya Korona

**91. Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu, dunia imekumbwa na janga la Virusi vya Korona na mataifa yanaendelea kupambana na janga hili kwa nguvu zote. Napenda kulihakikishia Bunge lako kuwa Wizara yangu na taasisi zake imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na janga hili kadri ya maelekezo ya viongozi wetu wakuu na wataalam wa afya na tiba yanavyotolewa. Nipende pia kuwaasa wananchi wote wanaohitaji au wanaopatiwa huduma mbalimbali za sheria ikiwemo za utoaji haki kuzingatia maelekezo yote wanayopewa katika maeneo husika ili kuendelea kuudhibiti ugonjwa huu. Afya yako, afya ya mwenzako na uhai wetu sote ni haki za binadamu. Kila mmoja wetu atekeleze wajibu wake, na kwa pamoja, tuendelee kuienzi haki hii.

## F. UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA MWAKA 2015

**92. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara na taasisi zake imeendelea kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha kwamba inawajibika ipasavyo kwa wananchi kupitia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015, ikiwemo ahadi na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa. Miongoni mwa ahadi hizo ni pamoja na kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma; kukuza, kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na kuendeleza utawala wa sheria; na kuimarisha mfumo wa utoaji haki.

### I. Kuendeleza Mapambano Dhidi ya Rushwa na Ubadhirifu

**93. Mheshimiwa Spika,** Serikali ilifanya marekebisho ya sheria ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 kupitia Sheria Na. 3 ya mwaka 2016 na kuwezesha kuanzishwa

ndani ya Mahakama Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Divisheni hii ilisajili jumla ya kesi **49** za rushwa na uhujumu uchumi ambapo kesi **40** zimetolewa maamuzi. Aidha, thamani ya mali zilizorejeshwa au kutaifishwa kutokana na kesi hizi ni jumla Shilingi **bilioni 29.9** zikiwemo magari mawili (**2)**, nyumba **1**, Ghorofa **1** na fidia ya Shilingi bilioni 26.3

**94. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendesha jumla ya kesi kubwa tano **(5)** katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ambapo washtakiwa waliotiwa hatiani kutokana na kesi hizo walipewa adhabu mbalimbali zikiwemo vifungo, faini, fidia kwa Serikali na mali mbalimbali kutaifishwa. Kiasi cha **Shilingi 32,534,528,871.20** kilipatikana kama fidia kwa Serikali, **Shilingi 205,500,000.00** kilipatikana kama faini na nyumba mbili **(2)** zilitaifishwa kuwa mali ya Serikali kwa amri ya Mahakama.

**95. Mheshimiwa Spika**, Katika kuendesha kesi za jinai na kuhakikisha kuwa nchi ina kuwa salama na kuwa wahalifu hawanufaiki na uhalifu, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kushirikiana na wadau wake, imeendesha kesi na kufanikiwa kupata amri ya Mahakama kutaifisha jumla ya kilo **398.145** za Dhahabu zenye thamani ya **Shilingi 32,295,101,922.67** zilizokuwa zinatoroshwa na kuikosesha Serikali mapato. Licha ya Dhahabu, madini mengine yaani madini bati na madini vito aina ya Almas, Tanzanite, Amethyst, Rhodolite, Bati, Blue Sapphire, Grossularite, Tsavorite, Green Garnet, Spessartite, Cintrine, Grossular, Supphire, Spinel, Ruby, Tourmaline, Acuamarine nayo yametaifishwa. Jumla ya thamani ya madini yote yaani Dhahabu na madini vito yaliyotaifishwa pamoja na faini zilizolipwa na washitakiwa ni **Shilingi 42,266,619,537.67**. Jumla ya **Shilingi 33,937,044,074.74** ikiwa ni fedha zinazohusiana na uhalifu zimetaifishwa na kuwekwa kwenye akaunti ya *Asset Forfeiture Recovery* iliyoko Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, baada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 11 ya mwaka 2019, katika zoezi la washitakiwa kukiri makosa yao (plea bargain), jumla ya **Shilingi 15,638,464,678.17** zimeshalipwa kama kodi iliyokwepwa, faini

na fidia baada ya washitakiwa **381** kukiri makosa yao na kulipa fedha katika akaunti maalum iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na zoezi la urejeshaji wa fedha kwa wale ambao hawajamaliza linaendelea. Kwa ufupi mpaka sasa jumla ya thamani ya madini yote pamoja na fedha zilizolipwa au kutaifishwa ni **Shilingi 91,842,128,286.58.** Pamoja na fedha hizo, Serikali imepata amri ya kutaifisha nyumba **24** , magari **65**, viwanja tisa (**9**), mashamba mawili (**2**), mbao **6,894**, Jahazi moja (**1**), XRF mashine mbili (**2**) za kupima ubora wa madini. Katika kipindi kati ya Julai 2019 na 8 Machi, 2020 jumla ya washitakiwa **2,916** waliokuwa mahabusu wamefutiwa kesi na Mkurugenzi wa Mashtaka katika zoezi la ukaguzi wa Magereza na kusikiliza changamoto za wafungwa na mahabusu.

## II. Kukuza, Kulinda na Kuhifadhi Haki za Binadamu na Haki za Watu

**96. Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza katika taarifa yangu, Serikali ya Awamu ya Tano inatambua na kuheshimu wajibu ilionao wa kulinda, kukuza na kuendeleza haki za binadamu na haki za watu nchini kwa mujibu wa Katiba, Sheria za nchi na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, kama nilivyoeleza katika hotuba hii Serikali imetekelea jukumu hili kwa jitihada kubwa. Nitaje baadhi ya shughuli zilizofanyika.

a) Kuhusu haki za watu, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa:

i. Uhuru wa nchi na watu wake unaendelea kulindwa na nchi pia imeendelea kuwa na uhuru wa kuamua masuala yake ya ndani kwa mujibu ya Ibara ya 2 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa 1945. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimeendelea kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ambayo tumejiewekea kama Taifa. Majeshi yetu yako imara na yanaendelea kulinda mipaka yetu na kufanya kazi mbalimbali za maendeleo kama ambavyo tumejionea wenyewe katika ujenzi wa miundombinu muhimu ya umma. Aidha, katika kuhakikisha kwamba uhuru, mamlaka na

maslahi ya nchi katika kutumia utajiri wake na maliasilia zake yanaendelea kulindwa, Serikali imefanya majadiliano na wawekezaji kwenye mikataba iliyopo ya uvunaji wa utajiri na maliasilia zilizopo na tayari mikataba mikubwa mitano (**5**) imeshapitiwa na mitatu (**3**) kati ya hiyo, imekamilishwa na kuleta manufaa makubwa kwa nchi na watu wake.

ii. Nchi imeendelea kuwa na amani, utulivu ni salama. Uhalifu umeendelea kudhibitiwa kikamilifu na wananchi na mali zao wanaendelea kuwa salama, na pale penye uhalifu hatua zinachukuliwa kama ambavyo dunia imeendelea kuitambua nchi yetu kama "**kisiwa cha amani na utulivu**". Baba wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitujengea misingi ya umoja na alikuza uzalendo na utaifa baina yetu. Viongozi wote wameendelea kuhamasisha uzalendo, utaifa, umoja na utangamano wa kitaifa bila kujali itikadi na vyama vyetu. Amani, utulivu na usalama wa nchi hauna chama, wala itikadi, kabila, dini au jinsi. Amani, utulivu na usalama ni haki ya watu wote katika Taifa lao.

iii. Maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii vinaendelea kutiliwa mkazo na kutekelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2015/2016 hadi 2020/2021 na ile ya mwaka mmoja mmoja, ikiwemo huu tunaoumaliza sasa wa 2019/2021 na ule unaofuata ambao Bunge lako limeuridhia wa 2020/2021, na hivyo kuendelea kuelekea kwa vitendo kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ambapo miradi mikubwa ya kimkakati ya kitaifa katika kujenga uchumi imara na endelevu imebuniwa na kuendelea kutekelezwa kulingana pia na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya 2030. Aidha, Serikali imeendelea kuwawezesha wafanyabishara wadogo wadogo kwa kuwapatia vitambulisho vya kufanya biashara na kuwaseheme baadhi ya kodi ili waweze kumudu biashara zao na hivyo kuchangia katika maendeleo ya familia, jamii zao, na Taifa kwa ujumla. Vilevile kupitia sheria za utajiri na maliasilia wananchi wameendelea kunufaika na utajiri na maliasilia za nchi, hususan kupitia uanzishwaji wa mifumo imara ya usimamizi na pia uanzishwaji wa masoko, hasa ya madini na vito, katika sehemu mbalimbali nchi. Kama ilivyo kwa suala la amani na usalama wa nchi, maendeleo

ya kiuchumi pia hayana chama, wala itikadi, au kabila, au dini au jinsi na vitu vingine vya aina hiyo. Maendeleo ni haki ya watu wote na jamii kwa ujumla.

iv. Mazingira yanaendelea kulindwa kwa nguvu zote ili kuhakikisha watu wanaendelea kuishi na kufanya shughuli zao za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiraia na kiutamaduni katika mazingira salama. Moja ambalo linaendelea kutekelezwa kwa ufanisi ni pamoja na kuzuia utumiaji wa mifuko ya plastiki, jambo ambalo limepokelewa na kutekelezwa na wananchi wote ikiwa ni ishara njema ya kujali mazingira yetu. Aidha, tumeshuhudia mvua kubwa zikiendelea kunyesha nchini na kuleta athari mbalimbali kwa mtu mmoja mmoja au jamii husika. Tunawapa pole wote walioathirika na mvua kwa namna moja ama nyingine. Serikali imeendelea kuchukua hatua kukabiliana na athari za mvua zinazoendelea. Wizara zinazohusika na kilimo, mifugo na uvuvi zinaangalia uwezekano wa kujenga mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji, maendeleo ya malisho, kunyeshea mifugo na ufugaji wa samaki wakati wa kiangazi. Mvua hizi zinaweza kuwa neema iwapo tutazitumia vizuri. Hata hivyo niendelee kuwaasa wananchi kuepuka maeneo hatarishi kama ya mabondeni ili kuepuka athari zinazoweza kuletwa na mvua. Niwatake wananchi wote tuendelee kuunga mkono juhudi za mbalimbali za kulinda mazingira yetu kwani hii ni haki ya watu wote.

b) Kuhusu haki za binadamu, Serikali imeendelea kuboresha huduma na kuhakikisha kuwa:

i. Watoto wote wanazaliwa katika mazingira bora, huru na salama na kuweka mifumo ya huduma mbalimbali katika maendeleo ya mtoto na ukuaji wake, ikiwemo usajili, chanjo, tiba na huduma za ushauri kwa wazazi ili waendelea kumlea mtoto vizuri na kumpatia makuzi mema;

ii. Watu wote wanaishi katika mazingira salama na kwamba vitendo vyote vinavyohatarisha maisha na uhai wa mtu vinadhibitiwa na kuchukuliwa hatua;

iii. Vitendo vyote vinavyoweza kumfanya mtua kuwa mtumwa ikiwemo biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, au kuwatumikisha binadamu, hususan watoto, wanawake na wazee, kinyume na sheria vinadhibitiwa;

iv. Vitendo vyote vya utesaji, udhalilishaji na unyanyasaji wa binadamu mahali popote nchini unaendelea kudhibitiwa na hatua kuchukuliwa pale vinapojitokeza;

v. Watu wote wanakuwa sawa mbele ya sheria na kila mtu anapata haki ya kutotendewa jambo lolote kinyume na taratibu zilizowekwa ikiwemo haki ya kusikilizwa, kujieleza, kujitetea, kutoa ushahidi, kuleta mashahidi, na vielelezo vingine kadri inavyohitajika na mahakama na vyombo vingine vya utoaji haki; na hivyo, tumeendelea kujenga Mahakama sehemu mbalimbali, kutunga sheria na kuimarisha mifumo ya utoaji haki kwa ujumla wake;

vi. Haki ya faragha inalindwa kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyowekwa ili kuhakikisha kwamba utu wa mtu pia unalindwa;

vii. Watu wote wameendelea kuishi na kwenda mahali popote wanapotaka ili kujipatia au kufaidi fursa mbalimbali za kiuchumi, kijamii na nyingine kwa mujibu wa sheria za nchi;

viii. Kutoa hifadhi kwa wananchi waliopatwa na majanga mbalimbali ikiwemo mafuriko yaliyotokea katika mikoa ya Tanga, Lindi na Mtwara; na pia Taifa limeendelea kuwapa hifadhi wakimbizi wanaokidhi vigezo kutoka maeneo mbalimbali kwa mujibu wa sheria za nchi, mikataba ya kikanda na kimataifa;

ix. Wanawake wanaotaka kuolewa au wanaume wanaotaka kuoa ili kuanzisha familia kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi, na ndoa zao zinatambuliwa na kusajiliwa;

x. Watu wote wanaohitaji kumiliki mali za aina mbalimbali kwa njia halali ikiwemo haki ya kutafuta na kujipatia mali

kwa njia halali na kupewa hati au nyaraka mbalimbali kuthibisha au kurasimisha umiliki huo wanapata haki hiyo;

xi. Watu wote wanapata haki ya kutoa mawazo kupitia njia mbalimbali au kuabudu kwa uhuru na kwa mujibu wa sheria za nchi;

xii. Watu wote wanapata haki ya kukusanyika na kufanya shughuli mbalimbali kwa kuhakikisha kuwa mikusanyiko kwa ajili ya masuala mbalimbali ikiwemo ya kijamii, kiutamaduni, michezo, kisiasa na mengine yanafanyika kwa mujibu wa sheria;

xiii. Wakati wa uchaguzi kitaifa au katika Serikali za mitaa, watu wanapata fursa ya kushiriki, kuchagua au kuchaguliwa kwa haki, uhuru na uwazi kama ilivyofanyika kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwezi Novemba, 2019;

xiv. Uwepo wa hifadhi ya jamii, hususan kwa wazee, watoto na wenye mahitaji maalum na wanaokidhi vigezo vya kisheria na taratibu kwa kupitia programu mbalimbali kama vile TASAF, bima ya afya na taasisi zingine za serikali na zisizo za Serikali zikiwemo za kidini unawanufaisha wananchi wanaokidhi vigezo vya huduma hizo;

xv. Watu wote wanapata fursa ya kufanya kazi kwa kuhakikisha kwamba fursa anuai za ajira au kujiajiri zinaendelea kuongezeka ili kila mtu afanye kazi halali, apate ujira na kufaidi matunda ya jasho lake lakini pia kuhakikisha kwamba watu wanaheshimu kazi halali kama njia pekee ya kupata maendeleo yao wenyewe, jamii na Taifa lao kwa ujumla;

xvi. Huduma za jamii ikiwemo afya, elimu na mafunzo zinapatikana kwa kuhakikisha kwamba hatua mbalimbali zinachukuliwa ili huduma hizo ziwafikie watu wote katika maeneo yao au kwa umbali mfupi na kuendelea kuimarisha ubora wa huduma hizo kadri jamii inavyostawi na taifa kupata maendeleo, hivyo tunaendelea kujenga na kuimarisha shule, vyuo, zahanati, hospitali na

maeneo mengine ili kila mmoja wetu awe sehemu ya maendeleo tuonayoyahitaji kama ambavyo Ibara ya 8 na 9 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Sura ya 2) inavyotuelekeza.

**97. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, inakamilisha Mpango Kazi wa Pili wa Kitaifa wa Haki za Binadamu wa mwaka 2020-2025 utakaobainisha masuala mbalimbali katika kipindi cha utekelezaji wake na hivyo kuwa na mwongozo unaoonesha vipaumbele vya muda mfupi, kati na mrefu kwenye masuala ya haki za binadamu na haki za watu.

**98. Mheshimiwa Spika,** nichukue nafasi hii kuzishukuru Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na zile zisizo za Serikali kwa kutekeleza majukumu yao mbalimbali ambayo yamewezesha kazi ya Serikali katika kulinda, kukuza na kuendeleza haki za binadamu na haki za watu nchini kuendelea kuwa endelevu kama Katiba na mikataba mbalimbali inavyotaka. Aidha, naomba niushukuru pia Mhimili wa Mahakama kwa kufanya kazi yake ya kuzitafsiri sheria hizi na kutoa haki kwa muktadha wa ustawi wa jamii na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Natambua kuwa kazi hiyo siyo rahisi lakini imekuwa ikifanywa kwa weledi mkubwa. Naomba pia nilishukuru Bunge kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri kupitisha mipango, bajeti na sheria mbalimbali ambazo zimewezesha utekelezaji wa jukumu la kulinda, kukuza na kuendeleza haki za binadamu na haki za watu nchini kuendelea kufanikiwa.

**99. Mheshimiwa Spika,** kuhusu shughuli ya uendeshaji wa mashauri ya ukiukwaji wa haki za binadamu kikatiba, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wizara kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliendesha mashauri nane **(8)** mapya ya haki za binadamu kikatiba hivyo kufanya mashauri hayo ya haki za binadamu kikatiba yaliyoshughulikiwa kufikia **45**. Kati ya mashauri hayo, mashauri 35 yapo Mahakama Kuu, mashauri mawili **(2)** yapo Mahakama ya Rufani kwa ajili ya rufaa na mashauri 8 yamehitimishwa.

**III. Kuimarisha Mifumo ya Utoaji Haki**

**100. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki kwa kuweka mifumo mipya na kuboresha mifumo iliyopo na kupata matokeo ambayo ni pamoja na:-

i. Kuwezesha wananchi kufungua mashauri na kufuatilia taarifa mbalimbali kwa njia za kielektroniki, jambo ambalo limewawezesha kupunguza gharama zinazohusiana na uendeshaji wa mashauri;

ii. Kuwezesha mamlaka na wenye kesi kufuatilia mwenendo ya kesi mbalimbali tangu zinapoanza hadi zinapohitimishwa na kuchukua hatua pale ambapo inaonekana kuna tatizo;

iii. Kuwezesha jamii kutambua mawakili kupitia mfumo wa kusajili mawakili na hivyo kutatua changamoto iliyokuwa ikijitokeza kwa baadhi ya watu wasio waaminifu kufanya kazi ya uwakili pasipo kuwa na sifa hizo;

iv. Kuwezesha mashauri kuendeshwa na kuhitimishwa kwa kutumia njia ya mawasiliano ya kielektroniki (video conference) na hivyo kuongeza kasi ya kuhitimisha mashauri na kupunguza gharama; na

v. Kuwezesha wananchi katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza kupata haki zao kwa wakati kwa kutumia mfumo wa mahakama zinazotembea.

**101. Mheshimiwa Spika**, shughuli za ujenzi wa majengo ya mahakama zinazoendelea katika maeneo mbalimbali ya nchi zimewawezesha wananchi kufikia huduma za mahakama kwa urahisi katika maeneo yao. Katika kipindi cha Julai, 2019, hadi Machi, 2020, ujenzi wa mahakama zifuatazo ulikamilika na baadhi yake zimeanza kufanya kazi:-

(i) Mahakama ya Hakimu Mkazi katika mikoa ya Simiyu na Manyara;
(ii) Mahakama za Wilaya katika Wilaya za Longido, Chato, Geita, Bukombe, Bariadi, Njombe, Ruangwa, Kilwa, Chunya na Kondoa; na

(iii) Mahakama za Mwanzo za Mlowo, Magoma, Uyole, Mtowisa, Msanzi na Mkunya, Ngerengere, Mang'ula, Mlimba, Laela, Mtowisa, Msanzi, Uyole, Mtae na Lugarawa.

**102. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, shughuli za ujenzi wa majengo ya mahakama katika maeneo kadhaa zitakamili ifikapo mwisho wa mwaka huu wa fedha lakini tunaendelea kwa mwaka 2020/2021 na ujenzi katika maeneo mbalimbali ya nchi kulingana na mpango kazi wa kuboresha miundombinu ya serikali.

## G. MTIRIRIKO WA MAPATO NA MATUMIZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

### I. Makusanyo ya Maduhuli

**103. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 12,606,487,000** kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara ilikusanya jumla ya **Shilingi 9,248,652,497.00** sawa na **asilimia 73.36** ya lengo la makusanyo kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:-

**Jedwali Na. 1: Taarifa za Maduhuli kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020**

| Fungu | Maduhuli yaliyoidhinishwa (Shilingi) | Maduhuli yaliyokusanywa (Shilingi) |
|---|---|---|
| 12 | | 0 |
| 16 | 3,332,000 | 13,654,300.00 |
| 19 | 1,002,000 | 0 |
| 35 | 14,432,000 | 19,599,000.00 |
| 40 | 12,571,199,000 | 9,204,618,197.00 |
| 41 | 16,520,000 | 10,781,000.00 |
| 55 | 2,000 | 0 |
| 59 | | 0 |
| **JUMLA** | **12,606,487,000** | **9,248,652,497.00** |

## II. Fedha Zilizoidhinishwa na Kupokelewa kwa Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

**104. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa na Bunge jumla ya Shilingi **181,337,627,878** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya hizo **Shilingi 77,755,166,000** ni za mishahara, **Shilingi 73,532,963,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 30,049,498,878** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo jumla ya **Shilingi 16,248,363,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 13,801,135,878** fedha za nje.

**105. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 130,934,893,787.11** sawa na asilimia **72** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo **Shilingi 55,419,744,545.02** ni mishahara na **Shilingi 63,045,351,264.98** ni matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo ni **Shilingi 12,469,797,977.11** sawa na asilimia **41** ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa. Kati ya hizo **Shilingi 6,037,318,051.88** ni fedha za maendeleo za ndani na **Shilingi 6,432,479,925.23** ni fedha za maendeleo za nje. Mtiriko wa fedha zilizopitishwa na Bunge na kiasi kilichopokelewa kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 kwa mafungu ya Wizara ni kama zinavyooneshwa katika majedwali yafuatayo:-

**Jedwali Na.2 Mtiririko wa Bajeti kwa Wizara kwa Kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020**

| Na. | Maelezo | Bajeti Iliyoidhinishwa (Shilingi) | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mishahara ya watumishi | 77,755,166,000 | 55,419,744,545.02 |
| 2. | Matumizi mengineyo | 73,532,963,000 | 63,045,351,264.98 |
| 3. | Fedha za maendeleo (Ndani) | 16,248,363,000 | 6,037,318,051.88 |
| 4. | Fedha za Maendeleo (Nje) | 13,801,135,878 | 6,432,479,925.23 |
| | **JUMLA** | **181,337,627,878** | **130,934,893,787.11** |

| Fungu | Bajeti Iliyoidhinishwa (Shilingi) | Kilichopokelewa Hadi Machi, 2020 (Shilingi) |
|---|---|---|
| **12** | [illegible] | [illegible] |
| **16** | 3,332,000 | 13,654,300.00 |
| **19** | [illegible] | [illegible] |
| **35** | [illegible] | [illegible] |
| **40** | 12,571,199,000 | 9,204,618,197.00 |
| **41** | 16,520,000 | 10,781,000.00 |
| **55** | 2,000 | 0 |
| **59** | | 0 |
| **JUMLA** | **12,606,487,000** | **9,248,652,497.00** |

**Jedwali Na. 3: Mtiririko wa Bajeti kwa kila Fungu la Wizara kwa Kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **16** | Matumizi ya Mishahara | 3,013,570,000 | 2,099,341,800.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 3,618,731,000 | 3,112,692,497.67 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | 0 | 0 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Nje) | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **6,632,301,000** | **5,212,034,297.67** |
| | | | |
| **19** | Matumizi ya Mishahara | 1,641,327,000 | 1,533,811,167.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 5,398,637,000 | 5,396,995,156.03 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | 0 | 0 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Nje) | 248,363,000 | 0 |
| | **Jumla** | **7,288,327,000** | **6,930,806,323.03** |
| | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **35** | Matumizi ya Mishahara | 10,980,893,000 | 6,779,502,515.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 6,723,265,000 | 4,653,712,100.00 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | 0 | 0 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Nje) | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **17,704,158,000** | **11,433,214,615.00** |
| | | | |
| **40** | Matumizi ya Mishahara | 52,523,182,000 | 38367817367.02 |
| | Matumizi Mengineyo | 51,481,382,000 | 45089869778.99 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | 15,000,000,000 | 6,037,318,051.88 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Nje) | 7,157,900,576 | 2,581,204,853.24 |
| | **Jumla** | **126,162,464,576** | **92,076,210,051.13** |
| | | | |
| **41** | Matumizi ya Mishahara | 5,567,737,000 | 3,969,589,184.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 2,765,859,000 | 2,074,294,270.76 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | 1,000,000,000 | 0 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Nje) | 4,075,853,500 | 3,475,057,389.99 |
| | **Jumla** | **13,409,449,500** | **9,518,940,844.75** |
| | | | |
| **55** | Matumizi ya Mishahara | 2,716,729,000 | 1,791,566,632.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 1,566,080,000 | 1,302,468,480.00 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | 0 | 0 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Nje) | 2,567,381,802 | 376,217,682.00 |
| | **Jumla** | **6,850,190,802** | **3,470,252,794.00** |
| | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **59** | Matumizi ya Mishahara | 1,006,766,000 | 626,784,000.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 979,009,000 | 716,456,000.00 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Ndani) | 0 | 0 |
| | Matumizi ya Maendeleo (Nje) | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **1,985,775,000** | **1,343,240,000.00** |

## H. MAFANIKIO

**106. Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 ni pamoja na:-

(i). Kuongezeka kwa imani ya wananchi juu ya utendaji kazi wa taasisi na mifumo ya kusimamia sheria na utoaji haki nchini. Mathalani, Mpango wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Mahakama pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Mahakama ya Tanzania kuwashirikisha wadau ikiwemo wananchi katika uboreshaji wa huduma za Mahakama, umeongeza taswira chanya ya Utendaji kazi wa Mahakama na Serikali kwa ujumla. Aidha, jitihada za kusogeza huduma ya kutenganisha shughuli za Upelelezi wa makosa ya Jinai na Uendeshaji wa Mashtaka nchini unaojumuisha kusogeza huduma hii karibu na wananchi katika ngazi za Wilaya kumewezesha majukumu na utendaji kazi wa Ofisi hii ya Taifa ya Mashtaka kufahamika zaidi na wananchi wengi, na pia imani ya wananchi wengi kuhusu utendaji wa Ofisi hii, imeongezeka.

(ii). Mipango na Mikakati mbalimbali inayotekelezwa na Wizara, hususani Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto, umefanikisha kuongeza hamasa kwa wananchi kushirikiana na Serikali katika kubaini ukatili huo na kudhibitiwa kwa haraka na hivyo kudumisha amani katika jamii na kuimarika kwa ulinzi wa haki za Mtoto.

(iii). Utekelezaji na usimamizi imara wa Sheria ya Msaada wa Kisheria, (Sura ya 21), umewezesha wananchi wengi kupata huduma za kisheria kwa urahisi na haraka katika kuifikia haki na kwa gharama nafuu na hivyo kuendelea kudumisha utawala wa sheria. Aidha, mtandao wa huduma za msaada wa kisheria umepanuka na kufikia kila Wilaya ya Tanzania Bara kwa kutumia mfumo jumuishi ambao unasimamiwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika maeneo yao. Maafisa hawa wameanzisha kundi lao la mtandao wa kijamii ambao unawawezesha kubadilishana habari na uzoefu wa jinsi ya kujipanga na kushulikia kero mbalimbali katika maeneo yao. Mfumo wa Usajili, Tathmini na Ufuatiliaji wa Utoaji Msaada wa Kisheria au ***Web-based Registration and Performance Monioring System*** pia umerahisisha kazi ya kuwaunganisha watoa huduma na kufuatilia kile kinachoendelea katika maeneo yao.

(iv). Utoaji wa mafunzo ya Sheria kwa vitendo na kuwajengea uwezo watumishi wa mahakama na mawakili wa Serikali kumefanikisha kuongezeka kwa wataalam, ufanisi na kuimarika kwa utaalam wa sheria nchini.

(v). Kutungwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Utajiri na Maliasilia (Sura ya 449) na Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri na Maliasilia za Nchi (Sura ya 450), sambamba marekebisho ya Sheria ya Madini (Sura ya 123) na kuanza kutekelezwa kwa sheria hizi ili kuhakikisha kwamba wananchi wanafaidika na rasilimali zao na kukuza pato la Taifa, kumefanikisha kufunguliwa kwa jumla ya masoko ya madini **28** pamoja na vituo vidogo **28** nchini kote. Lengo la masoko haya ni kuwezesha biashara ya madini na vito kufanyika kwa uwazi kwa zingatia sheria, kanuni na taratibu ili kuleta tija ya kiuchumi kwa maendeleo ya Taifa na kwa manufaa ya watanzania wote hususan wachimbaji wadogo. Aidha, utekelezaji wa sheria hizi kumewezesha Serikali kutambua kwa uhakika mchango wa sekta ya madini kwenye ukuaji wa uchumi ikiwa ni pamoja na manufaa yake kwa wananchi.

(vi). Ulindaji, ukuzaji na uendelezaji wa haki za watu na haki za binadamu ikiwemo demokrasia na utawala wa sheria unaendelea kuimarika siku hadi siku; na

(vii). Kuimarika kwa viwango vya usajili wa Vizazi kitaifa hususan kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano kwa kusogeza huduma karibu kwa wananchi.

**107. Mheshimiwa Spika,** mafanikio haya na mengine ambayo sikuyataja hapa yanaoneshwa kwamba dira na dhima ya Wizara zimeendelea kutuongoza na kutekelezwa vyema na kwamba nchi yetu inaendelea kupiga hatua katika maeneo mbalimbali. Tuendelea kushikamana ili tufike salama kwenye safari yetu ya kujenga uchumi na ustawi wa jamii imara ifikapo mwaka 2025.

## I. CHANGAMOTO

**108. Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Julai, 2019 na Machi, 2020, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na zifuatazo:-

(i). Baadhi ya wananchi kuhamasishwa kudai haki pasipo kuzingatia wajibu wao mbele ya sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa;

(ii). Wananchi katika baadhi ya maeneo ya nchi, kuendelea kushindwa kuifikia haki kwa wakati, kutokana na kukosekana kwa huduma za kisheria, hususan huduma za mahakama ambazo ni chache ikilinganishwa na idadi ya wananchi wanaohitaji huduma hizo; na

(iii). Kuendelea kuwepo na malalamiko ya wananchi kuhusu kubambikiwa kesi, ucheleweshwaji wa upelelezi na uchunguzi wa tuhuma za makosa ya jinai hususan kwa wananchi, walio kwenye mahabusu na selo za vituo vya polisi.

## J. MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO

**109. Mheshimiwa Spika,** katika kutatua changamoto hizo, Wizara iliendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali

ya kukabiliana nazo na kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na mfumo imara wa kikatiba na kisheria muda wote ili kufanikisha mipango ya maendeleo ya Taifa. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i). Kuelimisha wananchi na umma kwa ujumla kuhusu kutimiza wajibu wao wakati wa kutafuta haki na huduma nyingine za kisheria;

(ii). Wizara kuendelea kusogeza karibu na wananchi huduma za utoaji haki kwa kuongeza miundombinu ya mahakama kwa kujenga majengo ya mahakama katika kuanzia Mkoani mpaka mahakama za mwanzo, kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki ikiwa ni pamoja na mahakama zinazotembea, kuendelea kutekeleza Programu ya kutenganisha shughuli za Upelelezi na Uendeshaji wa Mashtaka ili kuharakisha utoaji haki na kuendelea kusajili watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria;

(iii). Kuupitia mfumo wa haki jinai kwa lengo la kubaini changamoto zilizopo na kuzipatia ufumbuzi.

**110. Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana ni juhudi za pamoja kati ya Wizara, Idara, Taasisi na wadau wetu ikiwemo washirika wa maendeleo katika sekta ya sheria. Hivyo, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa ushirikiano mzuri uliopo kati yetu na Washirika wa Maendeleo ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN Women), Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (DfID), Serikali ya CANADA na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Denmark (DANIDA) pamoja na wadau wengine ikiwemo kampuni ya simu ya TIGO. Napenda niwahakikishie kuwa Wizara yangu inatambua na kuthamini uhusiano mzuri uliopo kati yetu na wadau hawa na tutahakikisha kuwa unaimarishwa kwa maendeleo ya sekta ya sheria na taifa kwa ujumla.

**111. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya uwaziri. Hakika, ni kutokana na ushirikiano huo nimeweza kusimama leo hii mbele ya Bunge lako kueleza mafanikio, mipango na mikakati tuliyonayo katika kuwahudumia wananchi wetu. Hivyo, kipekee nimshukuru Prof. Sifuni Ernest Mchome, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bw. Amon Anastas Mpanju, Naibu Katibu Mkuu, Mhe. Prof. Ibrahimu Hamisi Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Adelardus Lubango Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Bw. Mathias Bazirinkangu Kabunduguru Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Mhe. Wilbert Martin Chuma, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Bw. Biswalo Eutropius Kachele Mganga, Mkurugenzi wa Mashtaka, Bibi Emmy Kalomba Hudson, Kaimu Kabidhi Wasii Mkuu na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Dkt. Julius Clement Mashamba, Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani January Henry Msoffe, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Bw. Casmir Sumba Kyuki, Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Mhe. Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania Mathew Mhina Mwaimu, Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bibi Fatuma Iddi Muya Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Dkt. Zakayo Ndobir Lukumay, Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Mhe. Jaji Dkt. Jerald Ndika, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto, Mhe. Jaji Dkt. Paul Faustine Kihwelo, Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, Watendaji Wakuu, Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake.

## K. MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

**112. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara itaendelea kueteleza dhima yake na hivyo kuendelea

kuboresha utoaji wa huduma za sheria kwa umma. Ili kufikia azma hiyo Wizara yangu imeainisha maeneo mahsusi ya kipaumbele na kuyawekea malengo na shabaha kwa ajili ya utekelezaji. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara imeainisha vipaumbele muhimu kama ifuatavyo: -

**Fungu 41: *Wizara ya Katiba na Sheria***

i. Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria;

ii. Kukamilisha na kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria (LSRPII);

iii. Kukamilisha na kuanza kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu;

iv. Kuboresha na kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo;

v. Kuanzisha na kuendesha mafunzo ya watoaji huduma za msaada wa kisheria;

vi. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji majukumu ya mashtaka na upelelezi na maboresho mengine yanayoendelea katika mfumo wa mashtaka nchini;

vii. Kuweka mfumo wa kusimamia masuala ya utajiri na maliasilia, kuratibu mapitio ya mikataba mbalimbali na kubainisha maeneo yenye masharti hasi ili yarekebishwe;

viii. Kutekeleza Mkakati wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu; na

ix. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria.

**Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama**

i. Kufanya ukaguzi na kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati za Maadili za Maafisa wa Mahakama;

ii. Kufuatilia na kuhakikisha kuwa watumishi wanaostahili kuajiriwa au kuteuliwa kujaza nafasi wazi katika Utumishi wa Mahakama wanapatikana kwa kuzingatia vigezo;

iii. Kufanya Vikao vya Tume pamoja na Kamati ya Ushauri ya Ajira kwa wakati; na

iv. Kuboresha mazingira ya kazi pamoja na kuwezesha mafunzo kwa watumishi wa Tume.

**Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

i. Uendeshaji wa Ofisi za mikoani;

ii. Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mikoani;

iii. Mapitio ya Sheria, Uandishi wa Sheria na ufasiri wa sheria;

iv. Kufanya majadiliano na mapitio ya Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa;

v. Utoaji wa ushauri wa Kisheria kwa Serikali na taasisi zake;

vi. Kuimarisha Mifumo ya TEHAMA.

**Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

i. Kuiwakilisha Serikali pamoja na Taasisi zake katika kuendesha mashauri ya Madai (Mashauri ya Haki za binadamu, Kikatiba, na Uchaguzi) na Usuluhishi kitaifa na kimataifa kwa kuzingatia viwango vya ubora;

ii. Kuhakikisha kuwa mifumo ya TEHAMA inaimarishwa ikiwa ni pamoja na mfumo wa usimamizi wa Mashauri na udhibiti wa ubora;

iii. Kuimarisha Masijala na Maktaba ya Sheria ili kuzifanya za kisasa na kuhakikisha kuwa maktaba inakuwa na vitabu vinavyohitajika pamoja na uwepo wa Maktaba Mtandao;

iv. Ujenzi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Dodoma na kuanzisha ofisi katika mikoa 10 ya Tanzania Bara;

v. Uboreshwaji wa mazingira ya kufanyia kazi na ununuzi wa vitendea kazi pamoja na kuhakikisha kuwa matengenezo ya vifaa hivyo yanafanyika kwa wakati.

**Fungu 35: Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

i. Kuratibu upelelezi wa vyombo vya uchunguzi na kuendesha mashtaka;

ii. Utenganishaji wa shughuli za upelelezi na mashtaka kwa kufungua ofisi za Wilaya sita (**6)**;

iii. Kuimarisha mfumo na shughuli za utaifishaji na urejeshaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu;

iv. Kuimarisha utendaji kazi wa ofisi kwa kununua vitendea kazi;

v. Maendeleo ya rasilimali watu ikiwa ni pamoja na kujaza nafasi – ikama, mafunzo kwa watumishi na motisha.

**Fungu 40: Mfuko wa Mahakama**

i. Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (Backlog);

ii. Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji wa huduma;

iii. Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;

iv. Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;

v. Kuanza kwa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania ili kuhamia Dodoma; na

vi. Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki.

**Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

i. Kupokea na kufanya uchunguzi wa malalamiko ya ukiukwaji wa misingi ya utawala bora na uvunjifu wa haki za binadamu hususan kwa makundi maalumu, sehemu wanamozuiliwa watu na maeneo yenye migogoro ya ardhi;

ii. Kuimarisha utoaji wa elimu kwa umma na mfumo wa TEHAMA, kuitangaza Tume na kusikiliza kero za wananchi katika maeneo yao;

iii. Kuimarisha ushirikiano na wadau wa haki za binadamu na utawala bora ndani na nje ya nchi;

iv. Kufanya ufuatiliaji wa Uchaguzi Mkuu wa 2020; na

v. Kuwajengea uwezo watumishi wa Tume, kuendeleza ubunifu na maarifa ili kutoa huduma kwa weledi na tija zaidi.

**Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria**

i. Kukamilisha Utafiti wa Mfumo wa Sheria Zinazosimamia Masoko ya Mazao ya Kilimo;

ii. Kufanya Utafiti wa Mfumo wa Sheria unaosimamia Usajili wa Vyama vya Kijamii;

iii. Kufanya Utafiti wa Mfumo wa Sheria zinazohusiana na Usajili wa Udhamini;

iv. Kufanya Utafiti wa Mfumo wa Sheria zinazohusiana na Makosa ya Uhujumu Uchumi; na

v. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sheria Nchini.

***Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali***

**113. Mheshimwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 14,634,533,235** ikiwa ni maduhuli ya Serikali, kama ifutavyo:-

**Makisio ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2020/2021**

| Fungu | Jina la Fungu | Kiasi (shilingi) |
|---|---|---|
| 12 | Tume ya Utumishi ya Mahakama | 0 |
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 3,332,000 |
| 35 | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 15,000,000 |
| 40 | Mfuko wa Mahakama | 14,571,199,235 |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 45,000,000 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,000 |
| 59 | Tume ya Kurekebisha Sheria | 0 |
| | **JUMLA** | **14,634,533,235** |

***Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo***

**114. Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vyake, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 73,684,796,059** katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Jumla ya makadirio ya bajeti kwa mafungu ya Wizara na taasisi zake ni kama ifuatavyo:

**MAPENDEKEZO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

| NA. | MAELEZO | BAJETI (SHILINGI) |
|---|---|---|
| **1.** | Mishahara ya watumishi | 25,614,416,000 |
| **2.** | Matumizi mengineyo | 34,859,640,000 |
| **3.** | Maendeleo (Ndani) | 4,433,200,000 |
| **4.** | Maendeleo (Nje) | 8,777,540,059 |
| **JUMLA** | | **73,684,796,059** |

**115. Mheshimiwa Spika,** kiasi hicho cha fedha kinaombwa kupitia mafungu ya bajeti kama ifuatavyo: -

**FUNGU 12: TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA**

| MAELEZO | BAJETI (SHILINGI) |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 603,148,000 |
| Matumizi Mengineyo | 2,000,000,000 |
| Fedha za Maendeleo (Ndani) | 0 |
| Fedha za Maendeleo (Nje) | 0 |
| JUMLA | 2,603,148,000 |

**FUNGU 16: OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

| MAELEZO | BAJETI (SHILINGI) |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 3,048,742,000 |
| Matumizi Mengineyo | 4,022,981,000 |
| Fedha za Maendeleo (Ndani) | 433,200,000 |
| Fedha za Maendeleo (Nje) | 0 |
| **JUMLA** | **7,504,923,000** |

**FUNGU 19: OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**

| MAELEZO | BAJETI (SHILINGI) |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 2,453,893,000 |
| Matumizi Mengineyo | 9,028,155,000 |
| Fedha za Maendeleo (Ndani) | 0 |
| Fedha za Maendeleo (Nje) | 0 |
| **JUMLA** | **11,482,048,000** |

**FUNGU 35: OFISI YA TAIFA YA MASHITAKA**

| MAELEZO | BAJETI (SHILINGI) |
|---|---:|
| Matumizi ya Mishahara | 10,104,098,000 |
| Matumizi Mengineyo | 12,068,944,000 |
| Fedha za Maendeleo (Ndani) | 3,000,000,000 |
| Fedha za Maendeleo (Nje) | 520,000,000 |
| **JUMLA** | **25,693,042,000** |

**FUNGU 41: WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

| MAELEZO | BAJETI (SHILINGI) |
|---|---:|
| Matumizi ya Mishahara | 5,839,127,000 |
| Matumizi Mengineyo | 4,665,271,000 |
| Fedha za Maendeleo (Ndani) | 1,000,000,000 |
| Fedha za Maendeleo (Nje) | 7,566,318,000 |
| **JUMLA** | **19,070,716,000** |

**FUNGU 55: TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA**

| MAELEZO | BAJETI (SHILINGI) |
|---|---:|
| Matumizi ya Mishahara | 2,809,256,000 |
| Matumizi Mengineyo | 2,850,280,000 |
| Fedha za Maendeleo (Ndani) | 0 |
| Fedha za Maendeleo (Nje) | 691,222,059 |
| **JUMLA** | **6,350,758,059** |

**FUNGU 59: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA**

| MAELEZO | BAJETI (SHILINGI) |
|---|---:|
| Matumizi ya Mishahara | 756,152,000 |
| Matumizi Mengineyo | 1,224,009,000 |
| Fedha za Maendeleo (Ndani) | 0 |
| Fedha za Maendeleo (Nje) | 0 |
| **JUMLA** | **1,980,161,000** |
| **JUMLA KUU** | **73,684,796,059** |

**107. Mheshimiwa Spika,** vilevile, naliomba Bunge lako liidhinishe kiasi cha **Shilingi 176,437,977,000** kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama ambapo matumizi ya kawaida ni **Shilingi 106,562,977,000** na matumizi ya maendeleo ni **Shilingi 69,875,000,000.** Katika fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 50,543,824,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Mahakama, **Shilingi 2,264,771,000** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto na **Shilingi 53,754,382,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Mahakama. Kwa upande wa fedha za maendeleo, kiasi cha **Shilingi 39,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 30,875,000,000 ni** fedha za nje. Mchanguo wa matumizi ya bajeti kwa Mfuko wa mahakama ni kama ifuatavyo:

| MAELEZO | BAJETI (SHILINGI) |
|---|---|
| Matumizi ya Mishahara | 52,808,595,000 |
| Matumizi Mengineyo | 53,754,382,000 |
| Fedha za Maendeleo (Ndani) | 39,000,000,000 |
| Fedha za Maendeleo (Nje) | 30,875,000,000 |
| **JUMLA** | **176,437,977,000** |

**116. Mheshimiwa Spika,** mchanganuo wa maombi ya fedha za bajeti ya kila Fungu umeainishwa kwenye vitabu vya KASMA za mafungu husika ambavyo vimegawanywa kwa Wabunge wote kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri hoja imetolewa na imeungwa mkono kweli kweli tunakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mahiga kwa kutuwasilishia hotuba yako vizuri kabisa kwa ufasaha mkubwa. Kwa kuwa hoja hii ni ya siku moja, inabidi twende haraka haraka kidogo, naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, una dakika 20 jielekeze moja kwa moja kwenye unayotaka kutuambia, Mheshimiwa Najma, Makamu wa Mwenyekiti, tafadhali.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote naomba taarifa ya Kamati iingizwe katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani. Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inahusu uchambuzi wa bajeti ya Mafungu saba yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria yanayoshughulikiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kama yalivyoainishwa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Maelezo ya Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini katika Mikoa ya Dodoma, Wilayani Kondoa, Manyara, Arusha na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhidhishwa kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa Majengo ya Mahakama kwa kuwa, ujenzi huo umetekelezwa kwa viwango vya kuridhisha na umezingatia masuala mengi yenye kurahisisha uratibu wa shughuli za Mahakama nchini.

Mheshimiwa Spika, Uzingatiaji wa Usawa wa Kijinsia, Haki za Mtoto na Mazingira rafiki kwa Watu wenye Mahitaji Maalum katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Mahakama; Kamati ilibaini kuwa, Ujenzi wa Majengo ya Mahakama kwa sasa umezingatia mfumo jumuishi, ikiwemo usawa wa kijinsia, haki za Watoto na Mazingira rafiki kwa Watu wenye mahitaji maalum kwa kiasi kikubwa, ambapo, kwenye kila jengo jipya la Mahakama kumejengwa vyumba maalum kwa ajili ya Afisa Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya ushauri,

mahabusu za Wanawake, mahabusu za Wanaume na Mahabusu za Watoto, pamoja na Ofisi za Huduma ya Msaada wa Kisheria. Aidha, Kamati ilibaini kuwa, katika Mahakama zilizotembelewa, zimeajiri Mahakimu na Maafisa wa Mahakama kwa kuzingatia jinsia zote, wanawake na Wanaume katika ngazi zote za Utumishi kwenye Mahakama hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliweza kubaini masuala hayo kwa kutumia ujuzi na mbinu tulizojifunza chini ya Mradi wa Bunge wa *LSP II,* hivyo, Kamati inaishukuru Ofisi ya Bunge kwa kuendelea kutumia Mradi wa *LSP II* katika kuziwezesha Kamati za Bunge katika kuchambua masuala mbalimbali na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ililiridhishwa na hatua hiyo ya kuzingatia Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Haki za Watoto kwenye Ujenzi wa Miundombinu na uratibu wa Shughuli za Mahakama. Hivyo, Kamati inashauri Wizara nyingine na Taasisi zake ziige mfano mzuri wa Mahakama katika kuzingatia masuala hayo muhimu kwa ustawi wa Taifa letu*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na Mpango wa Mahakama unaolenga kuongeza upatikanaji wa haki kwa Wananchi, ambao pia umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali na Mahakama kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa katika majengo mbalimbali ya Mahakama nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi na mazingira rafiki katika suala zima la utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake husika kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni wa kuridhisha. Hivyo, Kamati imeridhishwa na hatua

hiyo ya Wizara, na pia inashauri iendeleze jitihada hizo kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi Februari, 2020 mafungu yaliyosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake zilipokea asilimia 67.7 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida. Hivyo, Kamati inaipongeza Hazina kwa kutoa fedha kwa wakati hatua ambayo imerahisisha utekelezaji wa shughuli za Wizara na Taasisi zake kwa ufanisi uliokusudiwa. Maoni ya Kamati ni kwamba Serikali ihakikishe fedha zilizobaki zinapatikana kabla ya kuisha mwaka huu wa fedha 2019/2020 na ihakikishe fedha zitakazoidhishwa na Bunge zinapatikana kwa wakati kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa hadi Februari, 2020 fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni Sh.7,716,488,786 sawa na asilimia 26 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hivyo, mwenendo wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake, haukuwa wa kuridhisha katika robo tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020. Maoni ya Kamati ni kuwa, ni vyema Hazina ikatoa fedha za Bajeti hii ya Maendeleo kabla ya tarehe 30 Juni, 2020, ili Wizara na Taasisi zake iweze kutekeleza shughuli zake kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, pamoja na utolewaji usioridhisha wa Fedha za Miradi ya Maendeleo katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020, bado Mahakama imeendelea kuonyesha utendaji bora na wa

kuridhisha sana ambapo umeweza kusimamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Mahakama mbalimbali nchini kwa kutumia kiasi hicho kidogo cha fedha kilichopokelewa kwa ufanisi mkubwa. Maoni ya Kamati ni kuwa, miradi inayotekelezwa inaweza kukamilika kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa, endapo kiasi cha fedha za ndani kilichobaki kitatolewa kabla ya kuisha mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake inatarajia kukusanya kiasi cha Sh.34,334,000. Kamati imebaini kuwa, kupungua kwa makadirio ya maduhuli chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kunatokana na mabadiliko ya Sera ya Utoaji Haki nchini ambapo kwa sasa, gharama za ada mbalimbali zilizokuwa zikitozwa na Mahakama zimefutwa ili kupanua uwigo wa upatikanaji wa haki nchini kwa kila mwananchi, kwa bei nafuu na kwa wakati. Mchanganuo wa kiasi cha maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu husika ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.1 kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Katiba na Sheria inaomba jumla ya Sh.61,474,056,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, Sh.25,614,416,000 ni kwa ajili ya Mishahara; Sh.34,859,640,000 ni fedha za Matumizi Mengineyo. Mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ni kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na.2 kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa mwaka wa fedha 2020/2021. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake zinaombewa Sh.13,210,740,059 kwa ajili ya Mpango wa

Maendeleo. Pamoja na kupungua kwa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021, bado Kamati imeridhishwa na maboresho yanayoendelea katika Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa kuwa yamezingatia maoni na ushauri wa Kamati yaliyotolewa wakati wa kupokea na kujadili Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/ 2020.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama. Pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji kazi wa Mahakama katika jitihada zake za kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani, Kamati inaendelea kushauri kuwa, Waheshimiwa Majaji kwa kushirikiana na vyombo husika, waendelee kutekeleza utaratibu wao waliojiwekea wa kutembelea magereza pamoja na mahabusu nchini ili kujionea hali halisi ya mlundikano wa watuhumiwa na wafungwa, kwa lengo la kuchochea utekelezaji wa miongozo ya Mahakama kuhusu kusikiliza na kumaliza mashauri mbalimbali kwa wakati, kama sehemu ya utekelezaji wa moja ya vipaumbele vya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mahakama imeiridhisha Kamati na umma wa Tanzania kwa ujumla kuhusu namna inavyoendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya Mahakama katika Mikoa na Wilaya mbalimbali nchini, ikiwemo matumizi mazuri na ya kuridhisha ya fedha za umma inayotolewa na Hazina, na kwa kuwa, imebaini wazi kuwa endapo Serikali itatoa kiasi kilichobaki katika bajeti ya ujenzi wa majengo ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2019/ 2020, miradi hiyo inaweza kukamilika kwa wakati. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu na ulazima wa kutoa kiasi hicho cha fedha kilichobaki ili kuiwezesha Mahakama

kukamilisha miradi husika kwa wakati kwa lengo la kuboresha mazingira stahiki ya utoaji haki nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa, fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na fedha za Matumizi ya Kawaida zitolewe kwa wakati ili kuiwezesha Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi hususan utoaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu, kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha inaimarisha mfumo wa uandishi wa sheria na usimamizi wa masuala ya mikataba inayohusu rasilimali za nchi katika sekta zote nchini. Hii ni pamoja na kuongeza idadi ya rasilimali watu wa taaluma mbalimbali, kuwajengea uwezo kwa njia ya uanagenzi kupitia wadau mbalimbali wa maendeleo ndani na nje ya nchi, pamoja na kuboresha stahiki za Wanasheria wa Serikali na mazingira yao ya kazi kwa lengo la kuongeza weledi na ufanisi zaidi kwa watumishi hao katika kusimamia maslahi ya nchi na rasilimali zake.

Mheshimiwa Spika, Fungu 19 - Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji wenye tija kwa Ofisi hii muhimu na kwa kuwa Serikali imeanzisha Ofisi hii mahsusi kwa ajili ya ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa na rasilimaliwatu wa kutosha, iendelezwe pia na kupewa stahiki zenye kuridhisha ili kuimarisha uwezo wa Mawakili wa Serikali katika kushughulikia mashauri ya usuluhishi na ya madai kwa maslahi ya nchi na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Kwa kuwa Ofisi hii imeendelea kutekeleza ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu, kuhusu kufungua Ofisi zake katika Mikoa na Wilaya mbalimbali kwa lengo la kuongeza uwigo wa utoaji haki katika maeneo husika kwa kusogeza

huduma stahiki karibu na wananchi, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zote zilizoombwa na Ofisi hii kwa wakati, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Hii ni pamoja na kuendelea kuboresha mishahara na stahiki nyingine za Waendesha Mashtaka wa Serikali nchini ili kutoa motisha kwa watumishi hao waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 55 -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Kwa kuwa bado yapo malalamiko mengi kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu, ukiukwaji wa misingi ya utawala bora nchini pamoja na tuhuma za kushikiliwa watu magerezani, polisi na sehemu nyinginezo nchini pasipo kuwepo utoaji haki au majibu yanayoridhisha kwa wakati; na kwa kuwa hali hiyo inawakatisha tamaa wananchi katika kuwa na imani juu ya Serikali yao, hivyo basi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizotengewa kwa ajili ya Fungu 55, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Tume iendelee kufanya ukaguzi katika sehemu zote nchini zenye malalamiko ya ucheleweshaji wa haki na kutoa taarifa kwa mujibu wa sheria ili kutatua changamoto hizo endapo zitabainika kuwepo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria. Kamati inaendelea kuishauri Tume ya Kurekebisha Sheria kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na mfumo wa sheria nchini unaozungumza lugha moja yaani *(uniformity of law)* na hivyo kuondokana na mgogoro wa kisheria usio wa lazima ambao unajulikana kama *(unnecessary conflict of law)* unaoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji, kutokana na kazi kubwa ya kurekebisha sheria mbalimbali iliyotekelezwa na Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Spika, Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa kuwa Watanzania kama Taifa, tumeshuhudia changamoto za watu kutoendelea kukutana kwenye mikusanyiko mikubwa, kutokana na athari za ugonjwa

hatarishi wa *Corona*, hali ambayo inatoa ishara maalum kwa vyombo vya utoaji haki nchini kuanza kufikiri maboresho ya mfumo wa utoaji haki kwa wananchi, kwa kuzingatia mazingira yote ya kukutana au kutokutana. Hivyo basi, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Taasisi zote zilizo chini yake, kuhakikisha inaendelea kutekeleza Mpango wake wa matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki nchini pamoja na kusimamia mazingira wezeshi ya utoaji haki. Hatua hiyo, itarahisisha utoaji haki kwa wakati, kwa gharama nafuu na hata kwa mazingira ambayo hayaruhusu kukutana uso kwa uso, ikiwa ni pamoja na mfumo wa utaratibu wa mahabusu zote nchini kutokana na athari za magonjwa hatarishi kama vile *corona*, yanayoweza kutokea wakati wowote kama ilivyotokea sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Katiba na Sheria kuendelea kusimamia mipango ya kujenga majengo ya Mahakama yenye mfumo shirikishi wa utoaji haki, kwa lengo la kurahisisha utoaji haki kwa wananchi, kwa wakati na kwa bei nafuu, kama ilivyoidhinishwa katika Mpango kazi wa Miaka Mitano wa Mahakama ya Tanzania. Hii ni pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu ya utoaji haki wa Mahakama zote nchini kulingana na bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukupongeza wewe kwanza kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili kwa hekima na weledi mkubwa katika kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania. Napenda pia nimpongeze Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wote wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge la Kumi na Moja. Wote kwa pamoja nawaombea afya njema na uzima katika kutekeleza majukumu yao pamoja na Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mhe. Balozi Dkt. Augustine Mahiga, Waziri wa Katiba na Sheria kwa

ushirikiano anaoendelea kuutoa kwa Kamati, pamoja na timu yake ya Watendaji ikiongozwa na Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Amon Mpanju, Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kamati inawashukuru kwa ushirikiano wao mzuri wakati wote wa utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa ujumla, wakati wa ukaguzi wa miradi na uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango mizuri katika kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake. Naomba Majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kabisa lakini siyo kwa umuhimu wake, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi zake bila kukwama. Aidha, pia napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein; Wakurugenzi Wasaidizi Michael Chikokoto na Ndg. Gerald Magili; Katibu wa Kamati hii Ndg. Stanslaus Kagisa; na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Pia napenda kuwashukuru Watendaji wote wa Idara husika za Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati kwa wakati na kwa ubora wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI

---

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (2) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria jukumu la kusimamia shughuli za Wizara tatu ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Jukumu hili la Uchambuzi wa Bajeti linaendana sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa na kupokea fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu Ujenzi wa Mahakama nchini, kuanzia tarehe 12 hadi 17 Machi, 2020.

Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake tarehe 20 Machi, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inahusu Uchambuzi wa Bajeti ya Mafungu Saba (7) yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, yanayoshughulikiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, ambayo ni:-
i) **Fungu 12** – Tume ya Utumishi wa Mahakama,
ii) **Fungu 16** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
iii) **Fungu 19** – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,
iv) **Fungu 35** – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,
v) **Fungu 41** – Wizara ya Katiba na Sheria,
vi) **Fungu 55**- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, na
vii) **Fungu 59** –Tume ya Kurekebisha Sheria,

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo Manne yafuatayo:-
i) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, na;
iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

***Maelezo ya Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa***
**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilifanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Ujenzi wa Mahakama nchini katika Mikoa ya Dodoma Wilayani Kondoa, Manyara, Arusha na Morogoro.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhidhishwa kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa Majengo ya Mahakama kwa kuwa, ujenzi huo umetekelezwa kwa viwango vya kuridhisha na umezingatia masuala mengi yenye kurahisisha uratibu wa shughuli za Mahakama nchini.**

***Uzingatiaji wa Usawa wa Kijinsia, Haki za Mtoto na Mazingira rafiki kwa Watu wenye Mahitaji Maalum katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Mahakama;***

***Mheshimiwa Spika,*** *Kamati ilibaini kuwa, Ujenzi wa Majengo ya Mahakama kwasasa umezigatia mfumo jumuishi, ikiwemo usawa wa kijinsia, haki za Watoto na Mazingira rafiki kwa Watu wenye mahitaji maalum kwa kiasi kikubwa, ambapo, kwenye kila jengo jipya la Mahakama kumetengwa vyumba maalum kwa ajili ya Afisa Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya ushauri, mahabusu za Wanawake, mahabusu za Wanaume na Mahabusu za Watoto, pamoja na Ofisi za Huduma ya Msaada wa Kisheria. Aidha, Kamati ilibaini kuwa, katika Mahakama zilizotembelewa, zimeajiri Mahakimu na Maafisa wa Mahakama kwa kuzingatia jinsia zote, wanawake na Wanaume katika ngazi zote za Utumishi kwenye Mahakama hizo.*

***Mheshimiwa Spika,*** *Kamati iliweza kubaini masuala hayo kwa kutumia ujuzi na mbinu tulizojifunza chini ya Mradi wa Bunge wa LSP II, hivyo, inaishukuru Ofisi ya Bunge kwa kuendelea kutumia Mradi wa LSP II katika kuziwezesha Kamati za Bunge katika kuchambua masuala mbalimbali na kuishauri Serikali ipasavyo.*

***Mheshimiwa Spika, Kamati ililiridhishwa na hatua hiyo ya kuzingatia Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Haki za Watoto kwenye Ujenzi wa Miundombinu na uratibu wa Shughuli za Mahakama. Hivyo, inashauri Wizara nyingine na Taasisi zake ziige mfano mzuri wa Mahakama katika kuzingatia masuala hayo muhimu kwa ustawi wa Taifa letu.***

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ukaguzi wa Miradi husika, pia Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo juu ya ujenzi wa Mahakama katika Mikoa Mbalimbali nchini, inayoendelea kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati ni kuwa, endapo Serikali itatoa kiasi kilichobaki cha fedha za maendeleo zilizotengwa

na kuidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Ujenzi wa Majengo ya Mahakama zilizopangwa, unaweza kukamilika kwa wakati. Aidha, kukamilika kwa miradi hiyo kutaboresha mazingira ya utoaji haki nchini ikiwemo kupunguza usumbufu kwa baadhi ya Wananchi kutembea Kilomita nyingi kutoka Wilaya moja kwenda Wilaya nyingine ili kufuata haki ya Mahakama katika mashauri mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na Mpango wa Mahakama unaolenga kuongeza upatikanaji wa haki kwa Wananchi, ambao pia umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali na Mahakama kwa kuendelea kufanya maboresho makubwa katika Majengo ya Mahakama mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi na mazingira rafiki katika suala zima la utoaji haki.

## UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZAKE PAMOJA NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, tarehe 20 Machi, 2020. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

### *Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa

Mwaka wa Fedha 2019/2020 ulitazama mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2020. Lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu Mwenendo wa Mpango wa Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili kujua utekelezaji wa vipaumbele vya kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulitazama pia eneo la ukusanyaji wa Maduhuli kwa kulinganisha kiasi kilichokusanywa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 na ukamilishaji wa lengo la ukusanyaji lililowekwa wakati wa kupitisha bajeti Mwezi Aprili 2019. Lengo la uchambuzi wa namna hii ni kufahamu uwezo wa Serikali katika kukusanya Maduhuli. Kamati ilitumia njia mbalimbali katika uchambuzi wake ikiwa ni pamoja na kutazama hali halisi ya kila Taasisi, kujiridhisha na taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu kwenye Kamati.

***Uchambuzi wa Taarifa Kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Bunge liliidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili, Milioni Mia Sita na Sita, Laki Nne Themanini na Saba Elfu (12,606,487,000/=).** Hadi kufikia Februari, 2020 kiasi cha Maduhuli kilichokusanywa na Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake ni **Shilingi Bilioni Nane na Milioni Thalathini na Moja, Laki Tisa Thelathini na Tisa Elfu, Mia Tisa Themanini na Tano (8,031,939,985 /=)** sawa na **asilimia 64** ya lengo lililokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mwenendo wa ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake husika kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ni wa kuridhisha. Hivyo, Kamati imeridhishwa na hatua hiyo ya Wizara, inaishauri iendeleze jitihada hizo kwa mwaka huu wa Fedha 2020/2021.**

***Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina***

***Mheshimiwa Spika,*** *katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Mafungu yanayosimamiwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake yalitengewa* ***Shilingi Bilioni Mia Moja Hamsini na Moja, Milioni Mia Mbili Themanini na Nane, Laki Moja Ishirini na Tisa Elfu ( 151,288,129,000 /=)*** *kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo,* ***Shilingi Bilioni Sabini na Saba, Milioni Mia Saba Hamsini na Tano, Laki Moja Sitini na Sita Elfu ( 77,755,166,000 /=)*** *zilikuwa ni za Mishahara na* ***Shilingi Bilioni Sabini Tatu, Milioni Mia Tano Thelathini na Mbili, Laki Tisa Sitini na Tatu Elfu (73,532,963,000/=)*** *zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Februari 2020 Wizara na Taasisi zake zilipokea* ***Jumla ya Shilingi Bilioni Bilioni Mia Moja na Mbili, Milioni Mia Nne na Tatu, Laki Mbili Arobaini na Nane Elfu, Mia Tatu Hamsini na Nane (102,403,248,358/=) sawa na asilimia 67.7%*** *ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida.*

***Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonyesha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri na wa kuridhisha kuhusu upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida, hivyo Kamati inaipongeza Hazina kwa kutoa fedha kwa wakati hatua ambayo imerahisha Utekelezaji wa Shughuli za Wizara na Taasisi zake kwa ufanisi uliokusudiwa.***

**Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati ni kwamba Serikali ihakikishe upatikanaji wa fedha zilizobaki zinapatikana kabla ya kuisha kwa Mwaka huu wa Fedha 2019/2020 na ihakikishe fedha zitakazoidhishwa na Bunge zinapatikana kwa wakati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali kwa wakati na kwa ufanisi zaidi.**

***Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020,***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa Fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni Thelathini na Milioni Arobaini na Tisa, Laki Nne Tisini na**

**Nane Elfu, Mia Nane Sabini na Nane (30,049,498,878/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizi **Shilingi Bilioni Kumi na Sita, Milioni Mia Mbili Arobaini na Nane, Laki Tatu Sitini na Tatu Elfu (16, 248,363,000/=)** ni fedha za ndani na **Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Nane na Moja, Laki Moja Thelathini na Tano Elfu, Mia Nane Sabini na Nane (13,801,135,878/=)** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Februari, 2020 Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Saba Kumi na Sita, Laki Nne Themanini na Nane Elfu, Mia Saba Themanini na Sita (7, 716,488, 786/=) sawa na asilimia 26%** ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za ndani ni **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Moja Sitini na Moja, Laki Moja Hamsini na Nane Elfu, Mia Saba Thamanini na Sita (5,161,158,786/=)** sawa na **asilimia 32%** ya Fedha iliyokuwa imetengwa kama bajeti ya Ndani. Aidha, fedha za Nje zilizopokelewa hadi Mwezi Februari, 2020 ni **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tano Hamsini na Tano, Laki Tatu Thelathini Elfu (2, 555,330,000/=)** sawa na **asilimia 1.9%** ya fedha za nje zilizotengwa.

**Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, Mwenendo wa Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake, haukuwa wa kuridhisha katika robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. Maoni ya Kamati ni kuwa, ni vyema Hazina ikatoa fedha za Bajeti hii ya Maendeleo kabla ya tarehe 30 ya Mwezi Juni, 2020, ili Wizara na Taasisi zake iweze kutekeleza shughuli zake kama ilivyopangwa.**

***Yatokanayo na Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, pamoja na utolewaji usiyoridhisha wa Fedha za Miradi ya Maendeleo katika robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2019/2020**, bado Mahakama imeendelea kudhihirisha utendaji bora na wakuridhisha katika kusimamia utekelezaji wa Miradi ya ujenzi wa Mahakama mbalimbali nchini kwa kutumia kiasi kidogo cha fedha kilichopokelewa kwa ufanisi mkubwa.**

**Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ni kuwa, Miradi inayotekelezwa inaweza kukamilika kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa, endapo kiasi kilichobaki cha Fedha za ndani kitatolewa kabla ya kuisha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.**

**UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 umeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mpango ambao umelenga utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/2021).

***Uchambuzi wa Vipaumbele vya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria***

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021 umeainisha maeneo zaidi ya Thelathini (30) ya vipaumbele kwa Taasisi zote zilizo Chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, ya kiwemo;

i) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Sheria;
ii) Kukamilisha na kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria (LSRPII);
iii) Kukamilisha na kuanza kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu;
iv) Kuboresha na kutoa mafunzo ya uanasheria kwa vitendo;
v) Kuanzisha na kuendesha mafunzo ya watoaji huduma za msaada wa kisheria;
vi) Kufuatilia na kutathmini utekelezaji majukumu ya mashtaka na upelelezi na maboresho mengine yanayoendelea katika mfumo wa mashtaka nchini;
vii) Kuweka mfumo wa kusimamia masuala ya utajiri na maliasilia, kuratibu mapitio ya mikataba mbalimbali na kubainisha maeneo yenye masharti hasi ili yarekebishwe;
viii) Kutekeleza Mkakati wa usajili wa matukio muhimu ya binadamu na takwimu; na

ix) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria.

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na Vipaumbele viliyowekwa na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kwa sababu vinaendana na Mpango wa Taifa wa Mwaka 2020/2021 pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Aidha, Kamati imeridhika na vipaumbele hivi kwa sababu vinajumuisha maeneo yote ya Msingi ambayo yanaleta mantiki ya uwepo wa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake hapa nchini.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo Kamati inatoa rai kwa Wizara ya Katiba na Sheria inaendeleza jitihada zake katika kuhakikisha kwamba vipaumbele vyake vinaakisi udhibiti wa rasilimali za nchi, uharakishwaji wa utoaji haki, uboreshaji wa Taaluma ya Sheria, uboreshaji wa mazingira ya utoaji haki na upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu.

***Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Milioni Thelathini na Nne, Laki Tatu Thelathini na Nne Elfu (34,334,000/=).**

**Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, kupungua kwa makadirio ya Maduhuli chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kunatokana na mabadiliko ya Sera ya utoaji haki nchini ambapo kwa sasa, gharama za ada mbalimbali zilizokuwa zikitozwa na Mahakama zimefutwa ili kupanua uwigo wa upatikanaji wa haki nchini kwa kila Mwananchi, kwa bei nafuu na kwa wakati.**

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa kiasi cha Maduhuli kinachotegemewa kukusanywa kwa kila Fungu husika ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.1**

**JEDWALI NA.1: Mpango wa Ukusanyaji Maduhuli ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | KIASI CHA FEDHA KILICHOPANGWA KUKUSANYWA 2020/2021 |
|---|---|---|
| 12 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 0 |
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 3,332,000 |
| 19 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 1,002,000 |
| 35 | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 15,000,000 |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 16,000,000 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,000 |
| 59 | Tume ya Kurebisha Sheria | 0 |
| **JUMLA KUU** | | **34,334, 000** |

***Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria ya tarehe 20 Machi, 2020***

***Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ya Katiba na Sheria inaomba jumla ya **Shilingi Bilioni Sitini na Moja, Milioni Mia Nne Sabini na Nne na Hamsini na Sita Elfu (61, 474,056,000/=)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Ishirini na Tano, Milioni Mia Sita Kumi na Nne, Laki Nne Kumi na Sita Elfu (25,614,416,000/=)** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi Bilioni Thelathini na Nne, Milioni Mia Nane Hamsini na Tisa, Laki Sita Arobaini Elfu (34,859,640,000 /=)** ni fedha za Matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mchanganuo wa Mapato na Matumizi kwa kila Fungu chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.2.**

**Jedwali Na.2: Kiasi cha Fedha kinachoombwa kwa Mafungu ya Bajeti yaliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | KIASI CHA FEDHA KINACHOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 |
|---|---|---|
| 12 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 2,603,148,000 |
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 7,071, 723,000 |
| 19 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali | 11,482,048,000 |
| 35 | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka | 22,173,042,000 |
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 10,504,398,000 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 5,659,536,000 |
| 59 | Tume ya Kurekebisha Sheria | 1,980,161,000 |
| | **JUMLA KUU** | **61,474,056,000** |

***Chanzo: Taarifa ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Serikali ya Tarehe 20 Machi, 2020***

***Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;***
**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake zinaombewa **Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Mbili na Kumi, Laki Saba Arobaini Elfu na Hamsini na Tisa (13,210,740,059/=)** kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake imepungua kwa kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Sita, Milioni Mia Nane Thelathini na Nane, Laki Saba Hamsini na Nane Elfu, Mia Nane Kumi na Tisa (16, 838, 758,819/=) punguzo**

**ambalo ni sawa na asilimia 56% ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kupungua kwa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, bado **Kamati imeridhishwa na maboresho yanayoendelea katika Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kwa kuwa yamezingatia maoni na Ushauri wa Kamati yaliyotolewa wakati wa kupokea na kujadili Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/ 2020.**

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba sasa kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake.

***FUNGU 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama***

i) **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji kazi wa Mahakama katika jitihada zake za kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani, Kamati inaendelea kushauri kuwa, Waheshimiwa Majaji kwa kushirikiana na vyombo husika, waendelee kutekeleza utaratibu wao waliojiwekea wa kutembelea Magereza pamoja na Mahabusu nchini ili kujionea hali halisi ya Mlundikano wa Watuhumiwa na Wafungwa, kwa lengo la kuchochea utekelezaji wa miongozo ya Mahakama kuhusu kusikiliza na kumaliza mashauri mbalimbali kwa wakati, kama sehemu ya utekelezaji wa moja ya vipaumbele vya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

ii) **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Mahakama imeiridhisha Kamati na Umma wa Tanzania kwa ujumla kuhusu namna inavyoendelea kutekeleza Miradi ya Ujenzi wa Majengo ya Mahakama katika Mikoa na Wilaya mbalimbali nchini, ikiwemo matumizi mazuri na ya kuridhisha ya fedha za Umma inayotolewa na Hazina, na kwa kuwa, imebainika wazi kuwa

endapo Serikali itatoa kiasi kilichobaki katika bajeti ya Ujenzi wa Majengo ya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2019/ 2020, Miradi hiyo inaweza kukamilika kwa wakati, Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu na ulazima wa kutoa kiasi hicho cha fedha kilichobaki ili kuiwezesha Mahakama kukamilisha miradi husika kwa wakati, kwa lengo la kuboresha mazingira stahiki ya utoaji haki nchini.

iii) **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuwa, fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na fedha za Matumizi ya Kawaida zitolewe kwa wakati ili kuiwezesha Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi hususan utoaji haki kwa wakati na kwa gharama nafuu, kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

***Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhakikisha inaimarisha Mfumo wa uandishi wa Sheria na Usimamizi wa Masuala ya Mikataba inayohusu rasilimali za nchi katika Sekta zote nchini. Hii ni pamoja na kuongeza idadi ya Rasilimali Watu wa Taaluma mbalimbali, kuwajengea uwezo kwa njia ya Uanagenzi kupitia Wadau mbalimbali wa Maendeleo ndani na nje ya nchi, pamoja na kuboresha stahiki za Wanasheria wa Serikali na mazingira yao ya kazi kwa lengo la kuongeza Weledi na ufanisi zaidi kwa Watumishi hao katika kusimamia maslahi ya nchi na rasilimali zake.

***Fungu 19: Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali,***

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuridhishwa na utendaji wenye tija kwa Ofisi hii muhimu, na kwa kuwa Serikali imeanzisha Ofisi hii mahsusi kwa ajili ya ufuatiliaji wa mashauri ya madai ambayo Serikali ina maslahi ndani na nje ya nchi, Kamati inaendelea kuishauri Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa na rasilimali watu ya kutosha, iendelezwe na kupewa stahiki zenye kuridhisha ili kuimarisha uwezo wa Mawakili wa Serikali katika kushughulikia mashauri ya usuluhishi na mashauri ya madai kwa maslai ya nchi na kwa ufanisi zaidi.

***Fungu 35 - Ofisi ya Taifa ya Mashtaka***

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Ofisi hii imeendelea kutekeleza ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu, kuhusu kufungua Ofisi zake katika Mikoa na Wilaya mbalimbali kwa lengo la kuongeza uwigo wa utoaji haki katika maeneo husika kwa kusogeza huduma stahiki karibu na Wananchi, Kamati inashauri Serikali, kutoa fedha zote zilizoombwa na Ofisi hii kwa wakati, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hii ni pamoja na kuendelea kuboresha Mishahara na stahiki nyingine za Waendesha Mashtaka wa Serikali nchini ili kutoa motisha kwa Watumishi hao waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

***FUNGU 55 -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora***

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa bado yapo malalamiko mengi kuhusu uvunjwaji wa Haki za Binadamu, ukiukwaji wa Misingi ya Utawala Bora nchini pamoja na tuhuma za kushikiliwa Watu Magerezani, Polisi na sehemu nyinginezo nchini pasipo kuwepo utoaji haki au majibu yanayoridhisha kwa wakati, na kwa kuwa hali hiyo inawakatisha tamaa Wananchi katika kuwa na imani juu ya Serikali yao,

Hivyo basi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizotengewa kwa ajili ya FUNGU 55, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Tume iendelee kufanya ukaguzi katika sehemu zote nchini zenye malalamiko ya ucheleweshaji wa haki na kutoa taarifa kwa mujibu wa Sheria ili kutatua changamoto hizo endapo zitabainika kuwepo.

***FUNGU 59 -Tume ya Kurekebisha Sheria***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuishauri Tume ya kurekebisha Sheria kuendelea kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kunakuwepo na Mfumo wa Sheria nchini unaozungumza lugha moja *(Uniformity of Law)* na hivyo kuondokana na mgogoro wa kisheria usio wa lazima *(unnecessary Conflict of Law)* unaoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji, kutokana na kazi kubwa ya

kurekebisha Sheria mbalimbali iliyotekelezwa na Bunge la Kumi na Moja.

***FUNGU 41-Wizara ya Katiba na Sheria***

i) **Mheshmiwa Spika,** ***Kwa kuwa Watanzania kama Taifa, tumeshuhudia changamoto za watu kutoendelea kukutana kwenye mikusanyiko mikubwa, kutokana na athari za ugonjwa hatarishi wa CORONA, hali ambayo inatoa ishara maalum kwa vyombo vya utoaji haki nchini kuanza kufikiri maboresho ya mfumo wa utoaji haki kwa Wananchi,kwa kuzingatia mazingira yote ya kukutana au kutokutana,***

***Hivyo basi, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Taasisi zote zilizo chini yake, kuhakikisha inaendelea kutekeleza Mpango wake wa matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki nchini pamoja na kusimamia mazingira wezeshi ya utoaji haki.***

***Hatua hiyo, itarahisisha utoaji haki kwa wakati, kwa gharama nafuu, na hata kwa mazingira ambayo hayaruhusu kukutana uso kwa uso , ikiwa ni pamoja na mfumo wa uratibu wa mahabusu zote nchini kutokana na athari za Magonjwa hatarishi kama vile CORONA, yanayoweza kutokea wakati wowote, kama ilivyotokea sasa.***

ii) **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Katiba na Sheria kuendelea kusimamia Mpango wa kujenga Majengo ya Mahakama yenye mfumo shirikishi wa utoaji haki, kwa lengo la kurahisisha utoaji haki kwa Wananchi, kwa wakati na kwa bei nafuu, kama ilivyoainishwa katika Mpango kazi wa Miaka Mitano wa Mahakama ya Tanzania. Hii ni pamoja na kuendelea kuboresha miundombinu ya utoaji haki kwa Mahakama zote nchini kulingana na Bajeti ya Serikali.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda nikupongeze kwa umahiri wako katika kasi ya kuliendesha Bunge hili kwa Hekima na Weledi Mkubwa katika kuishauri vema Serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge la Kumi na Moja. Wote kwa pamoja tunawaombea afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza Mhe. Balozi Dkt. Augustine P. Mahiga, (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria kwa ushirikiano anaoendelea kuutoa kwa Kamati, pamoja na timu yake ya Watendaji ikiongozwa na Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Amon Mpanju, Watendaji Wakuu na Wataalam wote wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati inawashukuru kwa ushirikiano wao mzuri wakati wote wa utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa ujumla, wakati wa Ukaguzi wa Miradi na uchambuzi wa Bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake. **NAOMBA MAJINA YAO KAMA YALIVYO KATIKA TAARIFA HII YAINGIE KATIKA TAARIFA RASMI ZA BUNGE (HANSARD):-**

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb - **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe.Joseph Kizito Mhagama, Mb-Mjumbe;
4. Ally Saleh Ally, Mb - Mjumbe;
5. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb - Mjumbe;
6. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb - Mjumbe;
7. Mhe. Amina Saleh Mollel, Mb - Mjumbe;
8. Mhe. Wanu Hafidh Amer, Mb - Mjumbe;
9. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb - Mjumbe;
10. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb - Mjumbe;
11. Mhe. Nimrod Elirehemah Mkono, Mb - Mjumbe;
12. Mhe. Susan Peter Maselle, MB - Mjumbe;-
13. Mhe. Alfredina Apilinary Kahigi, Mb - Mjumbe;
14. Mhe. Latifah Hassan Chande,Mb - Mjumbe;

15. Mhe. Jacqueline K. Ngonyani Msongozi,Mb- Mjumbe;
16. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe;
17. Mhe. Sixtus Raphael Mapunda, Mb - Mjumbe;
18. Mhe. Hassan Seleman Kaunje, Mb - Mjumbe;
19. Mhe. Yahaya Omary Massare, Mb - Mjumbe;
20. Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb - Mjumbe;
21. Mhe. Emmanuel A.Mwakasaka, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Dkt.Suzan Alphonce Kolimba, Mb **–** Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, mwisho, kabisa lakini si kwa umuhimu napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, **Ndg. Stephen Kagaigai** kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi Michael Chikokoto na Ndg. Gerald S.Magili, Katibu wa Kamati hii, Ndg. Stanslaus Kagisa, na Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa kuihudumia vyema Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Napenda kuwashukuru Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuchapa taarifa hii. Napenda pia kushukuru Watendaji wote wa Idara husika za Bunge kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati hii kwa wakati na kwa ubora.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zilizo chini yake, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii.

Najma Murtaza Giga, Mb.
**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

17 APRILI, 2020

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Najma Giga ambaye umeipitia hotuba yako kwa niaba ya Wanakamati wenzako kwa umahiri mkubwa sana. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, una dakika zisizozidi ishirini.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama, Fungu 40 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 9(c) cha Sheria ya Bajeti Na.11 ya mwaka 2015 pamoja na Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya mwaka 2011, kifungu cha 59, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania ni moja kati ya mihimili mitatu ya dola na majukumu yake makubwa kwa mujibu wa Katiba ni kutafsiri sheria na kutolea maamuzi kesi mbalimbali zinazoletwa Mahakamani. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara 107A(1) Mahakama imepewa mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Mahakama hadi Februari, 2020 pamoja na

vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Mfuko wa Mahakama yaani Fungu 40 uliidhinishiwa na Bunge jumla ya kiasi cha Sh.126,162,464,756. Kati ya fedha hizo Sh.50,145,970,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Mahakama; Sh.2,377,212,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Sh. 51,481,382,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na Sh. 22,157,900,756 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Maendeleo, Sh.15,000,0000,000 ni fedha za ndani na Sh.7,157,900,756 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2020, Mahakama ilipokea jumla ya Sh.80,689,372,935 ambazo ni sawa na asilimia 63.9 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kati ya fedha hizo, Sh.39,130,875,169 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; Sh.32,664,474,980 kwa ajili ya Mishahara ya Mahakama; Sh.1,224,864,000 kwa ajili ya Mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; Sh.10,437,010,014) ni Fedha za Maendeleo. Kati ya hizo Sh. 5,161,158,786 ni fedha ndani na Sh. 2,508,000,000) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2019/2020 ulipanga kukusanya maduhuli ya Sh.12,328,200,862 ambapo hadi kufikia Februari, 2020 kiasi kilichokuwa kimekusanywa ni Sh.8,004,020,000) ikiwa ni sawa na asilimia 63.6 ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utekelezaji wa bajeti hadi kufikia mwezi Februari, 2020 ni wa kuridhisha isipokuwa kwa fedha za maendeleo za ndani na nje ambazo zimetolewa kwa asilimia 34.1. Aidha, fedha hizi zililengwa kwenda kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama. Hivyo kwa mwenendo huu, ni wazi kuwa Mahakama haikuweza

kutekeleza vipaumbele kwa ukamilifu na hivyo kufifisha jitihada za kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, Kamati inaendelea kusisitiza Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe kuwa fedha za Mfuko wa Mahakama zinatolewa kwa wakati kulingana na mahitaji ya mfuko huku ikizingatia maeneo yote ya vipaumbele vya mfuko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mahakama katika kutekeleza jukumu lake la msingi la utoaji haki ilijiwekea vipaumbele mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuharakisha usikilizaji wa mashauri, kuimarisha utawala bora, maadili na uwajibikaji, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, kujenga miundombinu na kuongeza matumizi ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utekelezaji wa bajeti ya Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Mahakama imefanikiwa kutekeleza vipaumbele vyake kama inavyosomeka kwenye taarifa yetu na naomba iingizwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Mahakama ilikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ambavyo pia tumeziorodhesha kwenye taarifa yetu. Aidha, changamoto hizo zinazoikabili Mahakama zimekuwepo muda mrefu na zimekuwa zikiripotiwa kila mara. Hivyo, wakati umefika sasa changamoto hizi zichukuliwe kwa uzito wake na kuweza kutatuliwa ili Mahakama iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, tuangalie Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha unaokuja 2020/2021. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kutekeleza Malengo ya Mpango Mkakati waliojiwekea.

Mheshimiwa Spika, katika matumizi ya kawaida; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa Mahakama

umepewa ukomo wa jumla ya shilingi 158,437,977,000/= ikiwa ni ongezeko la asilimia 25.68 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/2020. Kati ya fedha hizo, shilingi 50,543,824,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Mahakama, shilingi 2,264,771,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, shilingi 53,754,382,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 51,875,000,000 ni kwa ajili ya maendeleo, ambapo kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 39 ni fedha za ndani na shilingi 12,875,000,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ukomo huu umeongezeka ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/2020 hususani eneo la bajeti ya maendeleo. Nyongeza ya bajeti ya maendeleo ya fedha za ndani ni mahususi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama Dodoma. Aidha, kati ya fedha hizo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia ambao utaelekezwa katika kuboresha miundombinu ya Mahakama ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Mahakama Kuu, Mahakama za Mwanzo na za Wilaya. Ni matumaini ya Kamati kuwa ikiwa fedha hizo zitatoka kama ilivyotarajiwa, basi Mahakama itaondokana na changamoto ya uhaba wa miundombinu na hivyo kuleta karibu huduma za Mahakama kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi mengineyo. Kuna nyongeza ya shilingi bilioni 2,273,000,000/= ambazo ni mahususi kwa ajili ya kugharamia mashauri yanayotokana na Uchaguzi Mkuu kwa upande wa Wabunge na Madiwani, mashauri ambayo yana utaratibu maalum wa kuyashughulikia. Kwa kuzingatia umuhimu wa jambo hili, Serikali iliona umuhimu na haja ya kuiongezea Mahakama kiasi hicho cha fedha kwenye bajeti. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa suala hili na kulitengea fedha ili kuhakikisha kuwa mashauri ya namna hivyo yatakapojitokeza yanasikilizwa na kumalizwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuzungumzie kuhusiana na maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa Mahakama umepanga kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi 14,571,199,235/= ikiwa ni ongezeko la shilingi 2,000,000,000/=

ikilinganishwa na makadirio ya shilingi 12,571,199,235/= ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye maoni na ushauri wa Kamati. Kuhusiana na changamoto ya uhaba wa watumishi, Mfuko wa Mahakama unakabiiliwa na uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika kada mbalimbali hususani Majaji, Mahakimu na Makarani. Aidha, changamoto hiii imekuwa ya muda mrefu na kusababisha Mahakama kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi wanaohitajika kwa awamu kwenye kada mbalimbali kulingana na mabombi yaliyowasilishwa ili kusaidia kutekeleza majukumu ya Mahakama. Hatua hii iende sambamba na uongezaji wa mishahara na maslahi ya watumishi ili kuongeza tija katika utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na watumishi wenye maadili, Mahakama imekuwa na changamoto ya maadili kwa baadhi ya Watumishi wa Mahakama. Kwa kuwa Tume ya Utumishi wa Mahakama ndiyo yenye jukumu la kushughulika na maadili ya watumishi, Kamati inasisitiza Tume ya Utumishi kuwatambua na kuwachukulia hatua watumishi ambao wanaenda kinyume na maadili ya Utumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba utaratibu uliowekwa kisheria wa Kamati ya Maadili ya Wilaya chini ya Wenyekiti wa Mkuu wa Wilaya umekuwa haufanyiki kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha. Kamati hii ya Maadili ndiyo inahusika na kusikiliza tuhuma za uvunjifu wa maadili wa Watumishi wa Mahakama katika ngazi ya Wilaya na kuwachukulia hatua. Hivyo, ni wazi kwamba bila kutenga rasilimali fedha za kuwezesha vikao hivi kufanyika kikamilifu, tatizo la maadili kwa Watumishi wa Mahakama litaendelea kuwepo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inatenga fedha ili vikao vya Kamati ya Maadili vifanyike kama sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie maoni yetu kuhusiana na Mabaraza ya Mahakama. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuogezea posho zinazolipwa kwa Wazee wa Mabaraza ya Mahakama. Wazee wa Mabaraza wanalipwa kiasi cha shilingi 5,000/= kwa kila kesi, kiasi ambacho Kamati inaona ni kidogo lakini vilevile kimekuwa hakilipwi kwa wakati na hivyo kusababisha madeni. Wazee hawa kwa kuendelea kudai posho zao kunawaondolea heshima na kuweka mazingira ya kuhitaji rushwa kutoka kwa watuhumiwa. Hivyo, wakati Serikali inaangalia uwezekano wa kuongeza kiwango hicho, iangalie uwezekano wa kuhakikisha kuwa posho hizo zinalipwa kwa wakati na hakuna malimbikizo ya madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Mabaraza ya Usuluhishi; Mabaraza haya yalianzishwa kwa Sheria Na. 5 ya Mwaka wa 1985 kwa nia njema ya kusaidia utoaji haki katika maeneo ambayo hayajafikiwa na Mahakama lakini mabaraza haya badala yake yamekuwa yakiongoza katika kuwanyima wananchi haki kutokana na kutawala kwa rushwa na kutokuwa na uelewa wa masuala ya utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, aidha, mabaraza haya yanasimamiwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata na miongoni mwa Kanuni za Baraza ni baraza kuundwa na wananchi wa kawaida tu wasio na uelewa wa sheria suala ambalo linapelekea haki kutotolewa kwa usawa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hii, Kamati kwanza inaona haja ya kurejea na kupitia upya sheria iliyoanzisha mabaraza ya usuluhishi kwenye ngazi ya chini ili kubadili mfumo huu wa Mahakama ikizingatiwa sheria hiyo ni ya muda mrefu. Aidha, mabadiliko haya yanatakiwa kuwa na mawanda mapana zaidi kwa mabaraza mengine yanayotumika kutoa haki, mathalan Mabaraza ya Ardhi ili kuleta haki na usawa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali iimarishe usimamizi wa mabaraza husika kwani imebainika kuwa mabaraza haya hayana usimamizi mzuri na mengine kutokukaguliwa na

kufuatiliwa utendaji kazi wake na mwisho Serikali kuhakikisha kuwa uteuzi wa mabaraza yaliyopo yanazingatia sheria iliyozianzisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na miundombinu ya TEHAMA bado mahakama ina uhaba mkubwa wa viendea kazi hasa vitendea haki vya TEHAMA kwa upande wa vikao vifaa vya kuredi, mashauri ya vikao ambapo yanafanywa kwa kuandika kwa mkono. Majaji kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakiandika mashauri kwa mkono suala ambalo haliendani na hali halisi ya kidigitali iliyopo sasa hivi. Aidha, njia hii pia inachukua muda mrefu na hivyo kupelekea Mahakama kushindwa kuwa shindani na kufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa. Hivyo ni vyema Mahakama ikaanzisha program ya mifumo ya kurekodi mashauri haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na utoaji wa fedha za maendeleo, Mahakama inategemea kupata mkopo kutoka Benki ya Dunia ambao utaenda kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miundombinu ya Mahakama. Kupitia mkopo huo, Mahakama inatarajia kukamilisha ujenzi wa Mahakama za Wilaya 33 na Makama Kuu sita. Kamati inasisitiza Serikali kushirikiana na Mahakama katika utolewaji wa fedha hizo ili hatimaye kuwepo na mazingira mazuri ya kutolea haki katika kila pande za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na miundombinu ya Mahakama za Wilaya, za Mwanzo na Kata; kuna changamoto kubwa ya uhaba wa miundombinu ya Mahakama za Mwanzo katika ngazi za Tarafa na Kata na wakati mwingine Mahakama hulazimika kukodi majengo ya watu binafsi ili kuendesha mashataka. Hali hii siyo nzuri sana kwa chombo kama Mahakama kwa sababu Mahakama inaweza ikashawishika kwenda kinyume na misingi ya utolewaji wa haki mathalani pale inapotokea mwenye jengo ndiyo amepelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, aidha, uhaba wa Mahakama hizo umesababisha adha kubwa kwa wananchi na kuongeza

gharama za kufuatilia mashauri hayo. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza Mpango Mkakati wa Mahakama wa kujenga miundombinu ya Mahakama katika ngazi za Tarafa na Kata ili kuondoa adha kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kamati inapenda kutoa pongezi kwa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Katiba na Sheria na Mahakama kwa mahusiano mazuri ambayo yanajengwa baina yao. Kamati inakiri kuwa haikuwa na wakati mgumu wa kupitisha bajeti Fungu Na. 40 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo kuliwa na mivutano baina ya Taasisi hizi. Hivyo Kamati inaisisitiza mahusiano haya mazuri ambayo yanaonekana kuendelea na hatimaye kuleta tija katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru sana wewe kwa uongozi wako mzuri na kwa kuongoza vizuri mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru pia Mheshimiwa Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga, Waziri wa Katiba na Sheria na Ndugu Mathias Kabunduguru, Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya bajeti kuhusiana na mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Naomba majina yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yanavyosomeka kwenye taarifa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo

pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, Ndugu Michael Kadebe kwa kutupa ushauri wa kitaalam, Kamati hatimaye ikaweza kukamilisha taarifa yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama, Fungu 40 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MFUKO WA MAHAKAMA (FUNGU 40) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu cha 9(c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 pamoja na Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya mwaka 2011 kifungu cha 59, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ili kujadiliana na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama ya Tanzania ni moja kati ya Mihimili mitatu ya Dola na majukumu yake makubwa kwa mujibu wa Katiba ni kutafsiri Sheria na kutolea maamuzi kesi mbalimbali zinazoletwa Mahakamani. kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara 107(A)(1) Mahakama imepewa mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hii inatoa mrejesho kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Mfuko wa Mahakama hadi Februari, 2020, pamoja na vipaumbele na masuala muhimu yanayopendekezwa katika Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2019/20 Mfuko wa Mahakama – **Fungu 40** uliidhinishiwa na Bunge jumla ya kiasi cha **Sh. 126,162,464,756.** Kati ya fedha hizo **Sh. 50,145,970,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Mahakama (PE), **Sh. 2,377,212,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), **Sh. 51,481,382,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), na **Sh. 22,157,900,756** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika fedha za Maendeleo, **Sh. 15,000,0000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 7,157,900,756** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Februari, 2020 Mahakama ilipokea jumla ya **Sh. 80,689,372,935** ambazo ni sawa na **asilimia 63.9** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2019/2020. Kati ya fedha hizo **Sh. 39,130,875,169** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **Sh. 32,664,474,980** kwa ajili ya mishahara ya Mahakama, **Sh. 1,224,864,000** kwa ajili ya Mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA) na **Sh. 10,437,010,014** ni fedha za maendeleo kati ya hizo **Sh. 5,161,158,786** ni fedha ndani na **Sh. 2,508,000,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Mahakama katika mwaka wa fedha 2019/2020 ulipanga kukusanya maduhuli ya **Sh. 12,328,200,862** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2020 kiasi kilichokuwa kimekusanywa ni **Sh. 8,004,020,000** ikiwa ni sawa na **asilimia 63.6** ya lengo la mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo wa utekelezaji wa bajeti hadi kufikia mwezi Februari, 2020 ni wa kuridhisha isipokuwa kwa fedha za maendeleo za ndani na nje ambazo zimetolewa kwa **asilimia 34.1.** Aidha, fedha hizi zililengwa kwenda kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama. Hivyo, kwa mwenendo huu ni wazi kuwa Mahakama haikuweza kutekeleza vipaumbele vyake kwa ukamilifu na hivyo kufifisha jitihada za kusogeza huduma karibu na wananchi. Kwa mantiki hii, Kamati inaendelea kusisitizia Wizara ya Fedha na Mipango ihakikishe kuwa fedha za Mfuko wa Mahakama zinatolewa kwa wakati kulingana na mahitaji ya Mfuko huku ikizingatia maeneo yote ya vipaumbele vya Mfuko.

## 3.0. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/2020 Mahakama katika kutekeleza jukumu lake la msingi la utoaji haki ilijiwekea vipaumbele mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuharakisha usikilizaji wa mashauri, kuimarisha utawala bora, maadili na uwajibikaji; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi; kujenga miundombinu na kuongeza matumizi ya TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia utekelezezaji wa Bajeti ya Mahakama kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mahakama imefanikiwa kutekeleza vipaumbele vyake kama ifuatavyo:-

a) Kumaliza mashauri 271,214 kati ya mashauri 340,137 yaliyokuwepo mwaka 2019 na hivyo kubakia na mashauri 68,923 mwishoni mwa mwezi Desemba, 2019;

b) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali;

c) Kuboresha mfumo wa usajili wa mashauri (Judiciary statistics dashboard system);

d) Kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama Kuu za Kigoma na Mara, Ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi za Manyara, Simiyu, Geita na Njombe na za Wilaya za Longido, Kondoa, Kasulu, Chunya, Bukombe, Chato, Kilwa na Ruangwa. Vilevile, Mahakama za mwanzo za Mkunya (Newala), Magoma (Korogwe), Msanzina Mtowisa (Sumbawanga), Uyole (Mbeya) na Mlowo (Mbozi) zimekamilika;

e) Kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi za Katavi na Lindi na za Wilaya za Kilindi, Sikonge, Rungwe, Bunda, Makete na Wanging'ombe na Mahakama za mwanzo za Mtae (Lushoto), Ngerengere, Mlimba na Mangu'la (Mororgoro); Laele (Sumbawanga) na Lugawala (Ludewa); na

f) Kuanzishwa kwa Mahakama za Wilaya za Kilindi, Kibiti na Mvomero, ambazo awali zilikuwa zinapata huduma kutoka Wilaya za jirani.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Mahakama ilikabiliwa na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2019/2020:-

i. Upungufu wa watumishi kwa kada mbalimbali ikilinganishwa na mahitaji;

ii. Uhaba wa vitendea kazi, hususan magari kwa ajili ya ukaguzi;

iii. Uhaba wa watumishi wenye sifa na maadili kwa kada mbalimbali; na

iv. Maslahi yasiyokidhi hali ya utendaji na mazingira ya kazi ukilinganisha na unyeti wa kazi ya utoaji haki.

**Mheshimiwa Spika,** aidha changamoto hizi zinazoikabili Mahakama zimekuwepo muda mrefu na zimekuwa

zikiripotiwa kila mara. Hivyo, wakati umefika sasa changamoto hizi zikachukuliwa kwa uzito wake na kuweza kutatatuliwa ili Mahakama iweze kufanya kazi kwa ufanisi.

## 4.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MFUKO WA MAHAKAMA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2020/2021, Mfuko wa Mahakama umepanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kutekeleza malengo ya mpango mkakati waliojiwekea. Aidha, katika mwaka 2020/2021, maeneo ambayo yamepewa kipaumbele ni yafuatayo: -

a) Kuharakisha utatuzi wa mashauri ya kawaida na mkakati wa kumaliza mashauri ya muda mrefu (backlog);

b) Kuboresha mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kama nyenzo muhimu ya kuboresha utoaji huduma;

c) Kuimarisha uwezo katika ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama;

d) Kuendelea kutekeleza mpango wa ujenzi wa ukarabati wa Majengo ya Mahakama katika ngazi mbalimbali;

e) Kuanza kwa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania ili kuihamishia Dodoma; na

f) Kuongeza ushirikiano na wadau wa haki jinai ili kuharakisha huduma ya utoaji haki.

## 4.1. Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa Mahakama umepewa ukomo wa jumla ya **Sh. 158,437,977,000** ikiwa ni ongezeko la asilimia **25.68** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/20. Kati ya fedha hizo; **Sh. 50,543,824,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Mahakama, **Sh. 2,264,771,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto, **Sh. 53,754,382,000**

ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo *(OC)* na **Sh. 51,875,000,000** ni kwa ajili ya maendeleo ambapo kati ya kiasi hicho **Sh. 39,000,000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 12,875,000,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** ukomo huu umeongezeka ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/2020, hususan eneo la bajeti ya maendeleo. Nyongeza ya bajeti ya maendeleo ya fedha za ndani ni mahsusi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama Dodoma. Aidha, kati ya fedha hizo ni mkopo kutoka Benki ya Dunia ambao utaelekezwa katika kuboresha miundombinu ya Mahakama ikiwa ni pamoja ujenzi wa Mahakama Kuu, Mahakama za Mwanzo na za Wilaya. Ni matumaini ya Kamati kuwa ikiwa fedha hizo zitatoka kama inavyotarajiwa basi Mahakama itaondokana na changamoto ya uhaba ya miundombinu muhimu na hivyo kuleta karibu huduma za Mahakama kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi mengineyo, kuna nyongeza ya **sh. 2,273,000,000** ambazo ni mahsusi kwa ajili ya kugharamia mashauri yanayotokana na Uchaguzi Mkuu, kwa upande wa wabunge na madiwani, mashauri ambayo yana utaratibu maalum wa kuyashughulikia. Kwa kuzingatia umuhimu wa jambo hili, Serikali iliona umuhimu na haja ya kuiongezea Mahakama kiasi hicho cha fedha kwenye bajeti. Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa suala hili na kulitengea fedha ili kuhakikisha kuwa mashauri ya namna hiyo yatakapojitokeza yanasikilizwa na kumalizwa kwa wakati.

### 4.2. Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa Mahakama umepanga kukusanya maduhuli ya kiasi cha **Sh. 14,571,199,235** ikiwa ni ongezeko la **Sh. 2,000,000,000** ikilinganishwa na makadirio ya **Sh. 12,571,199,235** ya mwaka 2019/2020.

## 5.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 5.1. Changamoto ya Uhaba wa Watumishi

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mahakama unakabiliwa na uhaba wa watumishi wenye sifa zinazotakiwa katika kada mbalimbali hususani Majaji, Mahakimu na Makarani. Aidha, changamoto hii imekuwa ya muda mrefu na kusababisha Mahakama kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza idadi ya watumishi wanaohitajika kwa awamu kwenye kada mbalimbali kulingana na maombi yaliyowasilishwa ili kusaidia kutekeleza majukumu ya Mahakama. Hatua hii iende sambamba na uongezwaji wa mishahara na maslahi ya watumishi ili kuongeza tija katika utendaji kazi.

### 5.2. Changamoto ya Watumishi wenye maadili

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama imekuwa na changamoto ya maadili kwa baadhi ya watumishi wa Mahakama. Na kwa kuwa Tume ya Utumishi wa Mahakama ndio yenye jukumu la kushughulika na maadili ya watumishi, Kamati inasisitizia Tume ya Utumishi kuwatambua na kuwachukulia hatua watumishi ambao wanaenda kinyume na maadili ya utumishi wa Mahakama.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba utaratibu uliowekwa kisheria wa Kamati ya Maadili ya Wilaya chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya umekuwa haufanyiki kutokana na ukosefu wa rasilimali fedha. Kamati hii ya maadili ndiyo inahusika na kusikiliza tuhuma za uvunjifu wa maadili wa watumishi wa mahakama katika ngazi ya Wilaya na kuwachukulia hatua. Hivyo ni wazi kwamba bila kutenga rasilimali fedha za kuwezesha vikao hivi kufanyika kikamilifu tatizo la maadili kwa watumishi wa Mahakama litaendelea kuwepo. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba inatenga fedha ili vikao vya Kamati ya Maadili vifanyike kama sheria inavyotaka.

### 5.3. Posho za Wazee wa Mabaraza ya Mahakama

**Mheshimiwa Spika,** kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuongeze posho zinazolipwa kwa wazee wa mabaraza ya Mahakama. Wazee wa mabaraza wanalipwa kiasi cha sh. 5,000 kwa kila kesi kiasi, ambacho Kamati inaona ni kidogo lakini vivle vile kimekuwa hakilipwi kwa wakati na hivyo kusababisha madeni. Wazee hawa kuendelea kudai posho zao kunawaondolea heshma na kuweka mazingira ya kuhitaji rushwa kutoka kwa watuhumiwa. Hivyo, wakati Serikali inaangalia uwezekano wa kuongeza kiwango hicho iangalie uwezekano wa kuhakikisha kuwa posho hizo zinalipwa kwa wakati na hakuna malimbikizo ya madeni.

### 5.4. Mabaraza ya Usuluhisi

**Mheshimiwa Spika,** mabaraza ya usuluhishi yalianzishwa kwa Sheria namba 5 ya mwaka wa 1985 kwa nia njema ya kusaidia utoaji haki katika maeneo ambayo hayajafikiwa na mahakama lakini mabaraza haya badala yake yamekuwa ya kiongoza katika kuwanyima wananchi haki kutokana na kutawala kwa rushwa na kutokuwa na uelewa wa masuala ya utoaji haki. Aidha, mabaraza haya yanasimamiwa na kamati ya maendeleo ya kata na miongoni mwa kanuni za baraza ni baraza kuundwa na wananchi wa kawaida tu wasio na uelewa wa sheria suala ambalo linapelekea haki kutotolewa kwa usawa.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia changamoto hii Kamati kwanza inaona haja ya kurejea na kupitia upya sheria iliyoanzisha mabaraza ya usuluhishi kwenye ngazi ya chini ili kubadili mfumo huu wa mahakama ikizingatiwa sharia hiyo ni ya muda mrefu. Aidha, mabadiliko haya yanatakiwa kuwa na mawanda mapana zaidi kwa mabaraza mengine yanayotumika kutoa haki mathalani mabaraza ya ardhi ili kuleta haki na usawa kwa wananchi. Pili, Serikali iimarishe usimamizi wa mabaraza husika kwani imebainika kuwa mabaraza haya hayana usimamizi mzuri na mengine kutokukaguliwa na kufuatiliwa utendaji kazi wake na mwisho Serikali kuhakikisha kuwa uteuzi wa mabaraza yaliyopo yalizingatia Sheria iliyozianzisha.

### 5.5. Uboreshaji wa miundombinu ya TEHAMA

**Mheshimiwa Spika,** bado Mahakama ina uhaba mkubwa wa vitendea kazi hasa vitendea kazi vya TEHAMA kwa upande wa vifaa vya kurekodi wa mashauri ya vikao ambao unafanywa kwa kuandika kwa mkono. Majaji kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakiandika mashauri kwa mkono suala ambalo haliendani na hali halisi ya kidigitali iliyopo sasa. Aidha, njia hii pia inachukua muda mrefu na hivyo kupelekea Mahakama kushindwa kuwa shindani na kufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa. Hivyo ni vema Mahakama ikaanzisha programu ya mifumo ya kurekodi mashauri haraka iwezekanavyo.

### 5.6. Utolewaji wa Fedha za Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama inategemea kupata mkopo kutoka Benki ya Dunia ambao utaenda kutekeleza mpango wa maendeleo wa miiundombinu ya Mahakama. Kupitia mkopo huo Mahakama inatarajia kukamilisha ujenzi wa mahakama za wilaya 33 na mahakama kuu 6. Kamati inasisitiza Serikali kushirikiana na Mahakama katika utolewaji wa fedha hizo ili hatimaye kuwepo na mazingira mazuri ya kutolea haki katika kila pande za nchi.

### 5.7. Changamoto ya Miundombinu ya Mahakama za Wilaya, za Mwanzo na Kata.

**Mheshimiwa Spika,** kuna changamoto kubwa ya uhaba wa miundombinu ya Mahakama za mwanzo katika ngazi za tarafa na kata na wakati mwingine Mahakama hulazimika kukodi majengo ya watu binafsi ili kuendesha mashtaka. Hali hii si nzuri sana kwa chombo kama Mahakama kwa sababu Mahakama inaweza ikashawishika kwenda kinyume na misingi ya utolewaji wa haki mathalani pale inapotokea mwenye jengo ndio amepelekwa mahakamani. Aidha, uhaba wa mahakama hizo umesababisha adha kubwa kwa Wananchi nakuongeza gharama za kufuatilia mashauri hayo. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza Mpango Mkakati wa Mahakama wa kujenga miundombinu ya Mahakama

katika ngazi za tarafa na kata ili kuondoa adha kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, Kamati inapenda kutoa pongezi kwa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Katiba na Sheria na Mahakama kwa mahusiano mazuri ambayo yanajengwa baina yao. Kamati inakiri kuwa haikuwa na wakati mgumu wa kupitisha bajeti ya Fungu 40 kwa mwaka wa fedha 2020/21 ukilinganisha na miaka ya nyuma ambapo kulikuwa na mivutano baina ya Taasisi hizi. Hivyo, Kamati inasisitiza mahusiano haya mazuri ambayo yanaonekana kuendelea na hatimaye kuleta tija katika ujenzi wa Taifa.

## 6.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza vema mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali. Namshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga, (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria na Ndg. Mathias Kabunduguru Mtendaji Mkuu wa Mahakama kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Mfuko huu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu Bajeti ya Mfuko wa Mahakama. Naomba kuwatambua wajumbe hao kama ifuatavyo;

1) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – M/Mwenyekiti
2) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
3) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
4) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
5) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
6) Mhe. Dkt. Immaculate Swale Semesi, Mb
7) Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
8) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
9) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb

10) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
11) Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
12) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
13) Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
14) Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
15) Mhe. Hasna Sadi Katunda Mwilima, Mb
16) Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
17) Mhe. Abdallah Majurah Bulembo, Mb
18) Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
19) Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
20) Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
21) Mhe. Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mb
22) Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
23) Mhe. John Kibera Kishimba, Mb
24) Mhe. Andrew John Chenge, Mb
25) Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26) Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb
27) Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo, pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe kwa kuipa ushauri wa kitaalamu Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mfuko wa Mahakama – Fungu 40, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

Mashimba M. Ndaki, Mb
**M/MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
17 Aprili, 2020

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Tunakushukuru sana kwa mawasilisho yako na kwa kazi nzuri ambayo Kamati yako imekuwa ikifanya na majadiliano mazuri ambayo mmekuwa mkiyafanya na upande wa Serikali.

Sasa Msemaji ambaye anapaswa kufuata ni Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Katiba na Sheria. Ninayo hotuba yake na hotuba hii kwa kawaida nakala ninayopewa mimi hapa ndiyo *original* kuliko nyingine yoyote mnayoweza kuiona kwenye mtandao au mahali pengine popote.

Bado meza ina shida na hotuba za Kambi Rasmi za Upinzani. Kama nilivyosema tulipoanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, tusipotafuta namna ya kurekebisha hili tatizo, basi itabidi twende hivyo hivyo, maana mtakuwa mmechagua wenyewe.

Hotuba hii ukiisoma; kwanza tuanze na nini madhumuni ya kikao hiki? Madhumuni ya kikao hiki ni kwamba Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria amewasilisha hoja mbele yetu, kwamba Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Narudia tena, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Hotuba hii ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho haigusi chochote kuhusu bajeti. Hakuna panaposema sijui fungu fulani au nini, hakuna. Ni hotuba inaelekea kama zinaandikwa na watu fulani mahali ambao hawajui hasa kinachoendelea hapa ni nini. *(Makofi)*

Ukitazama hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati iliyosomwa na Mheshimiwa Najma Giga na mnayo humu, tazama utaona inavyojielekeza kwenye *subject matter* ambayo iko mbele yetu. Tazama hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, utaona jinsi gani inavyojielekeza kwenye *subject*. Hotuba ya Upinzani haikataliwi baadhi ya mengine

ambayo mmeyaweka, haikataliwi; lakini basi si ujielekeze kwenye swali? Mmh! Kama ni darasani yaani hujajibu mtihani. Hata kama ulivyoviongea humo ni *point,* lakini uko nje kabisa. Sasa si uwe nje kidogo angalau! Hilo la kwanza.

Kwa hiyo, nawaombeni sana kwa sababu mmeshiriki. Siyo mara ya kwanza nakutana na hivi vitu; mmeshiriki kwenye Kamati kule; marandama, madudu gani vitabu vyote mmevipata mnavyo. Visomeni mjue Mheshimiwa Waziri anakujaje na ninyi mje vipi; na mengine mnayaongezea huko ndani mnayoyaona kwamba yanafaa, hatuwachagulii.

Kubwa zaidi na linalonisumbua zaidi, tumesisitiza mara kwa mara kwamba siyo vizuri Mhimili wa Bunge kuwa ndiyo mahali au *center* ya mashambulizi kwa Mhimili wa Mahakama. Hizi ni taratibu za Kimataifa za *Commonwealth* kwamba mihimili hii inaheshimiana. Ni tofauti sana na Mbunge mmoja mmoja akiongea na hotuba rasmi. Hili ndiyo kubwa zaidi.

Kwa hiyo, utaona kuanzia Fungu 66 Msemaji Mkuu, 67, 68, 69, 70, 71, 72, 74 kila mahali katika maeneo hayo niliyoyataja pamekuwa na lugha ambayo ni ya kutweza Mahakama. Hii ni hotuba ya Kambi Rasmi. Kwa hiyo ni vigumu sana.

Nimetafakari sana, nami sipendi kuona kwamba hamsomi hotuba zenu, sipendi kabisa, lakini katika mazingira haya nafanyaje? Mheshimiwa Suzan mwenyewe anayetaka kusoma hii ni mwanasheria.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Salome.

**SPIKA:** Eeh, Mheshimiwa Salome, sijui kwa nini kila wakati namwita Susan. Ni Mheshimiwa Salome. Itabidi nikubatize hilo jina, maana ni mtani wangu uwe Salome-Susan. Mheshimiwa Salome Makamba ni Mwanasheria *Acting* Kiongozi wa Upinzani ni Mwanasheria.

Wako wanasheria wengine wengi tu, lakini siyo lazima uwe Mwanasheria, hizi ni taratibu ambazo tumejiwekea katika kuendesha mambo yetu hapa kwamba Mhimili wa Mahakama tuuheshimu. Kuonyesha kabisa kwamba Mahakama ya Tanzania siyo lolote wala chochote na kila kutoa mifano kama Mahakama ya mahali fulani, hii haipendezi hata kidogo.

Kwa hiyo, kwa sababu hiyo hasa hii ya pili na ile ya kwanza ya kuwa nje kabisa ya kinachojadiliwa, hotuba hii kwa mara nyingine na yenyewe sitairuhusu kusomwa. Hata hivyo kwa vile mlikuwa na dakika 20 kama nilivyofanya wakati ule, nitawapeni nafasi moja tena ya ziada angalau dakika 10 hivi mnaweza mkaongeza mchangiaji pamoja na wale wawili ambao mlikuwa mmewaweka mwanzo mnaweza mkaweka mmoja, watatu nitahakikisha nawapa nafasi. *Chief Whip* wa Upinzani una hiyo *freedom* kuchukua au kuacha.

Kwa hiyo, tunaendelea na uchangiaji. Mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Rashid Shangazi kutoka hapa na wale ambao wanatakiwa kuwa Msekwa watangulie Msekwa, akiwemo na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma wawe Msekwa.

Mheshimiwa Shangazi tafadhali.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Aah, nilimwona *Chief Whip* wa Upinzani, Mheshimiwa Shangazi subiri kidogo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naheshimu maamuzi yako kwa sababu kiti chako ndicho chenye mamlaka, lakini siyo kila maamuzi yanayotolewa na Kiti kama Kambi tunaridhika nayo; na kwa mujibu wa Kanuni tutatumia Kanuni ya 5 kuleta *official* ofisini kwako.

Mheshimiwa Spika, wakati unatoa maamuzi umesema hatujajielekeza kwenye Bajeti, kwanza

nikuhakikishie hotuba hizo tunaandika wenyewe na tunajua nini tunachokifanya na nini tunataka tueleze kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mbali ya kwamba tutaandika makadirio ya bajeti, ni wajibu wetu kuandika changamoto za Wizara kiujumla mbali tu ya kwenye bajeti. Hivyo tumekuwa tukifanya siku zote hata katika hotuba zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tutakuja kukuona na sisi tuna malalamiko yetu hatutendewi haki kama Kambi. Ningependa nili-*address* hilo mbele ya Bunge lako kama ambavyo wewe umetoa *rulling* na nimesisitiza tunaiheshimu lakini mbali ya kuiheshimu kuna vitu na sisi kama Kambi tutakuja kukuona ili huko tunakokwenda twende vizuri kwasababu na sisi kuna vitu tunahisi hatutendewi haki kabisa kabisa *inclunding* na Ofisi ya Katibu wako. Hayo ningependa niyaweke wazi na tunakuja, tunaomba yafanyiwe kazi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana *Chief Whip* tutapokea maombi yenu na kwa hakika yatatendewa haki na labda itawasaidieni pia wenzenu watakapowasaidia kupitia na kuona jinsi gani ambavyo mpo nje ya msitari kabisa wala siyo nje ya msitari kidogo. Na bahati mbaya sana Spika wenu ni Mwanasayansi ndiyo bahati mbaya nyingine tutasaidiana huko.

Sisi Wanasayansi *we don't waste time.* Nikiulizwa swali elezea kuhusu Azimio la Arusha naanza Azimio la Arusha lilizaliwa tarehe 05.02.1967 Arusha na naendelea. Ukianza na habari ya Carl Peter alikuja Tanzania halafu nani yule, *Chief* Mangungu halafu sijui akaja Mwingereza, Vita Kuu ya Pili ya Dunia halafu sijui nini, yaani, kwanza nikienda ukurasa wa kwanza tayari hiyo karatasi natupa nje, hiyo ni zero kwasababu mimi ninachoangalia Azimio la Arusha ndiyo umeulizwa sasa hapa *topic* hapa ni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria, hakuna chochote cha Makadirio na Matumizi, sasa hapa kuna nini? Haikataliwi zungumza katrika ujumla wake wewe chomeka na haya lakini

soma ya Kamati ya Katiba na Sheria na nyie ni wanakamati mule na ile ya Kamati mnashiriki kuiandika pamoja, kwani Kamati wanaandika wa Chama Tawala pake yake? si mnaandika pamoja? Kamati ya Bajeti wanaandika peke yao? Si mnaandika pamoja? Na hii hivyo hivyo.

Teremka katika utaratibu mtu akuelewe unazungumza nini, katika mafungu gani, katika eneo gani, unataka kurekebisha nini n.k ndiyo maana nasema kwa dalili nyingi inaandikwa na Mtu ambaye hayupo na sisi. Kama kweli huyu Mtu yupo na sisi lazima angejaribu kuteremka katika utaratibu ambao tunauendea na hoja hizi hakuna hata moja ambayo ingekosa kuingia ukiacha zile za kushambulia Mahakama ambazo hazikubaliki katika utaratibu wake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napokea maoni yako itakuwa ni jambo jema tukikaa na kuanza kuambiana kwasababu kwa maoni ya meza ni kwamba yaani mpo nje kabisa ya *range* na mkiendelea hivi basi tutaendelea na utaratibu huo huo. Lazima mbadilike mziandike wenyewe na hata kama ni huyo basi msomesheni kwamba katika hotuba rasmi za Bunge teremka katika utaratibu huu. Hizi hotuba zinakaa mpaka vizazi vijavyo ndiyo maana na *Hansard* n.k watatushangaa watu wa baadaye huko hizi hotuba gani hizi. Mbona Waziri alichowasilisha hapa hoja kingine kabisa *completely.* Kinachokuja kingine na siku hizi hatufanyi siri.

Zamani ilikuwa hotuba ya Wazri haijulikani kwa hiyo ilikuwa sawa ukija maana wewe hujui lakini safari hii au miaka hii mnakuwa nazo. Kila kitu mnakuwa nacho ukiacha *summary* ya hotuba ambayo anaisoma sasa hivi, vitabu vyote mnavyo. Mnajua *estimate* ni zipi, ilikuaje, mmeshapokea *report* za utekelezaji, mmeshapokea Makadirio ya Matumizi ya Mwaka unaofuata kwa hiyo unapokuja hebu.

Mheshimiwa Rashid Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh ambaye yuko kule Msekwa.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuwa mzungumzaji wa kwanza kwenye hoja ambayo iliyoko katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nipende kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana katika eneo hili. Kuna kazi kubwa sana wametufanyia Wananchi wa Jimbo la Mlalo, tumejengewa Mahakama ya mwanzo katika Tarafa ya Mtae. Mahakama hiyo ni ya kisasa sana na sidhani hata kama kule Kongwa ipo na kwa bahati mbaya sikuona hata wakiiweka katika vitabu vyao lakini itoshe kusema ni Mahakama ya kisasa sana, ni nzuri na nadhani hiyo ndiyo *demo* ya Nchi nzima Mahakam zetu zitakuwa katika utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa nafasi hii pia niwapongeze Watendaji Wakuu katika eneo hilo kwa maana ya Katibu Mkuu wa Wizara Prof. Sifuni Mchome lakini na aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Ndugu yangu Katanga.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningetaka lizungumze mahususi leo ni eneo hili la utoaji haki kwa mujibu wa Ibara ya 107; kwanza nimpongeze sana Jaji Kiongozi kwa kazi kubwa aliyoifanya baada ya taharuki hii ya ugonjwa wa *corona* kuingia kuna hatua mahususi walizichukua kama Muhimili. Tunapongeza sana tumeona na Mahakama nazo zinaendeshwa kwa njia ya kidigitali kama ambavyo tunafanya hapa katika Bunge lakini pamoja na jitihada hizo bado naiona changamoto katika Ofisi ya Mdau Mkuu wa Walalamikaji Nchini kwa maana ya Mkurugenzi wa mashitaka. Mkurugenzi wa mashitaka yupo kwa mujibu wa Sheria lakini kuna changamoto kubwa sana katika Ofisi yake:-

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kwanza ni eneo hili la mahabusu bado ni wengi sana katika Magereza yetu na tunaamini kabisa kwamba zipo kesi ambazo kimsingi bado zinadhaminika. Sasa tunaposema tunataka kutoa haki basi ni vizuri haki ikionekana inatendeka kwa manaa ya usimamiaji wa utoaji wa haki yenyewe, usikilizwaji wa mashitaka kwa

haraka, haki ya uwakilishi lakini pia na haki ya kupata dhamana.

Mheshimiwa Spika, sasa kupitia Bunge lako Tukufu tulianzisha Sheria ile ya *plea bargaining* ambayo inawaruhusu watu kadhaa wenye mashitaka kule Magerezani kuweza kuomba na kukiri makosa kasha Ofisi ya Mwendesha Mashitaka iweze kuzungumza nao na kuweza kuziondoa zile kesi. Lakini cha kusikitisha sana ni kwamba eneo hili nalo limeongeza ukiritimba kwasababu hawa watu wamekuwa ni wengi Magerezani. Kwa kufikia mwezi Januari takribani kulikuwa na watu 300 wenye kesi za aina hiyo ambazo wameshakubaliana kwamba wako kwenye *plea bargaining* lakini hakuna kinachofanyika au kinafanyika kwa kusuasua sana.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa hii hali ya ugonjwa wa *corona* ilivyo hii ni hatari kubwa sana kwasababu tunajua kabisa kwamba Magereza yatakuwa yanawapeleka wafungwa Mahakamani, wanapanda katika mabasi, kule inawezekana kwa namna moja au nyingine wakakutana na raia wengine wakachanganyika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata huku Magarezani, Askari Magereza wanaishi uraiani huko wanakutana na watu mbalimbali. Isije ikatokea mahali kwamba tukaingiza huu ugonjwa ndani ya Magereza zetu halafu ukishatoka Magerezani ukalipuka mpaka kufikia huko mahakamani. Kwa hiyo, ningeomba sana Ofisi ya Mwendesha Mashitaka iharakishe hizi kesi na kwa bahati nzuri sana wanazo Sheria kama kifungu namba 91 kwenye hii *Criminal Procedure Act* wanayo mamlaka kupitia kifungu namba 91 kufuta kesi na kushitaki upya. Kwa hiyo, nikaona kwamba kama wanazo kesi ambazo wanadhani kwamba hazina ushahidi wa kutosha basi wangezifuta halafu baadaye kwasababu kifungu hiki kinawapa nafasi watashitaki upya lakini kama mlango huo unaonekana ni mgumu basi watoe dhamana ambayo itawaruhusu watu hawa wawe nje halafu baada ya muda kama hali ya huku nje itaruhusu wanaweza wakaendelea tena na utaratibu unaowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika eneo hili hili kwa upande wa Mahakama zetu, kifungu namba 225 cha Sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai hiyo hiyo kinatoa mamlaka kwa Mahakama na yenyewe kwenye kesi ambazo zimekaa siku 60 na bado hazijaanza kusikilizwa kwamba wana uwezo pia wa kuzifuta. Kwa hiyo, tuombe sana kwasababu *DPP* ana haki ya kurudisha mashitaka haya baadaye kwa mujibu wa kifungu namba 91 basi Mahakama nazo zione zile kesi zote ambazo zimekaa zaidi ya siku 60 hazijaanza kusikilizwa basi kesi zote hizi wawaachie hawa watu ili waweze kuendelea na mambo yao.

Mheshimiwa Spoika, lakini katika eneo hili pia nimemkumbuka sana Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema kwasababu yeye ndiyo Mwenyekiti wa ile *Parol* na muda mrefu sasa amekuwa kimya sana kwa hiyo, nikadhani kwamba eneo hili nalo tumkumbushe Mheshimiwa Mrema arudi sasa akafuatilie huko Magerezani wale wenye kesi ndogo ndogo hizi ambazo nyingine ni za muda mrefu, zingine hazina mashiko yoyote. Kwa mfano; iko kesi moja ya Jamhuri dhidi ya Bwana mmoja anaitwa Jumanne Mikidadi kule Tanga amekamatwa na Mirungi zaidi ya miaka tisa mpaka leo bado yupo ndani, amekamatwa na kifurushi cha Mirungi tu. Kwa hiyo, unaweza ukaona kabisa kwamba huko Magerezani kuna watu ambao wanapoteza muda na hakuna tija yoyote ambayo tunaiona kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningepanda kuchangia ni upande wa *Law School;* tunayo *Law School* yetu tumeanziaha lakini ina changamoto. Changamoto ya kwanza ambayo tunaiona pale ni wataalam hawa wale wanaofundisha (Wakufunzi). Wakufunzi pale bado wanaonekana hawana uzoefu sana, hawana *exposure* ya Kimataifa. Tunatarajia shule ile iboreshwe maana shule ile ndiyo inayokwenda kufunda na kutengeneza Mawakili ambao tunawatarajia.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hata wakati mwingine humu ndani ya Bunge unaona hotuba zinakuwa haziko sawa inawezekana matatizo haya yanaanzia mbali.

Kwa hiyo, niombe sana kwamba eneo hili nalo liboreshwe. Pia na miundombinu ya madarasa. Madarasa yamekuwa ni machache kiasi kwamba wanafunzi wale ni wengi sana wakati mwingine wanasoma huku wengine wakiwa wamesimama. Kwa hiyo, niombe sana ikiwezekana kama bado hatuna nafasi ya kutosha basi angalau hata kwa muda mfupi shule ile ifungwe hata kwa miaka miwili tujipange zaidi tupate wabobezi watakaofundisha Mawakili wetu lakini pia tuboreshe miundombinu ili hata hao wanaokwenda kujifunza pale wakitoka tuone wakiwa wamepikwa na kuiva vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili kiutawala inaonekana kama msimamizi wa Chuo kile ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Inawezekana sijapita sana kuangalia Kisheria kwa maoni yangu ningetamani sana kuona Taasisi kama hizi tungekuwa tunazikabidhi mamlaka hizi angalau kwa Majaji wastaafu wazitazame vizuri kwasababu eneo lile siyo pamoja tu na kufundisha kwenda kwenye Uwakili lakini pia linafunda watu kuwa raia wema na ambao wanakuja kufanya maamuizi makubwa ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningepanda kulizungumza ni suala la uanzishwaji wa Mahakama hizi za video ambalo nalo tumeliona katika baadhi ya Mahakama lakini tungependa sasa kuona kwamba eneo hili linasambaa Nchi nzima kwasababu haki bado inachelewa kupatikana.

Mheshimiwa Spika, sasa niombe nirudi kidogo Jimboni; pamoja na kupata ile Mahakama nzuri sana ambayo ni ya mfano na ninakuombea na wewe angalau kule Kongwa upate moja kwasababu huwezi ukajisemea hapo, basi tunahitaji pia tupate Mahakimu na Makarani.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Lushoto ina Tarafa nane lakini katika Tarafa nane hizo, tatu ndiyo zina Mahakama hizi za mwanzo. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba kuna uhaba mkubwa wa Mahakimu kwasababu kwa mfano; Jimbo zima la Mlalo lina Hakimu mmoja wa Mahakama ya mwanzo kwa hiyo, huyu inabidi azunguke katika Tarafa zote tatu. Azunguke

Tarafa ya Umba, Tarafa ya Mlalo lakini pia na Tarafa ile Mtae kwenye ile Mahakama mpya lakini pia na Makarani. Kwa hiyo, tunaomba sana kwamba pamoja na uboreshaji huu lakini pia tuongeze rasilimali hii ya watu ili waende kwenda kuwahudumia Watanzania katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa nafasi hii. huo ndiyo ulikuwa mchango wnagu kwa siku hii ya leo, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Rashid Shangazi. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Ally Saleh ambaye atachangia kutoka kule Msekwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma kutoka Msekwa huko huko.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii, fursa adhimu na kwanza nataka kusema kwamba uliniweka Kamati hii tangu nimekuja hapa na mpaka leo mwaka huu tunamaliza *inshallah.* Sikuwahi kujuta kuwepo kwenye Kamati hii kwasababu mbali ya kuwa ni fani yangu niliyosomea lakini pia ni maeneo ambayo yalinipanua akili sana kwasababu ya Miswada mingi ambayo ilikuwa inakuja kwetu.

Mheshimiwa Spika, pia niseme kwamba katika wakati nili-*enjoy* kufanyakazi ni wakati wa kipindi cha hawa waliopo sasa yaani timu ya Dkt. Mahiga, Prof. Mchome na Mpanju. Hawa ni waungwana na wamefanyakazi vziuri sana, ni wasikivu kuliko Mawaziri ambao wengine waliotangulia, hilo niseme na tume-*enjoy* sana kufanya kazi nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mambo mawili, matatu na la kwanza ni ujenzi wa Mahakama; katia hili naweza kusema kwamba Serikali inastahili kupongezwa kwa juhudi kubwa ya kujenga Mahakama. Mahakama kuanzia za Rufaa, kuanzia Mahakama Kuu na Mahakama zile ndogo ndogo na ni kazi nzuri ambayo kama nilivyosema inafaa kupongezwa na fedha nyingi zimewekwa huko kwasababu bila ya nchi kuwa na Mahakama hapawezi kuwa na haki na hapawezi kuwa

na Utawala Bora lakini kuna matatizo mawili ambayo yanakabili:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kwamba; hakuna majengo ya Mahakimu au Majaji katika maeneo ambayo Mahakama zimejengwa. Najua itachukua muda hata Mahakama zenyewe mpaka zitosheleze kote kwasababu pengine miaka mitatu, minne itakatwa Wilaya mpya, katika miaka mitatu mingine itakatwa Kata mpya, miaka mitatu mingine utakatwa Mkoa mpya ni *race* ambayo haishii lakini kwa kiasi fulani inaweza ikapunguzwa kasi yake. Kwa hivyo, suala la kuwa na Mahakama ni moja lakini kuwa na nyumba nzuri za Watendaji kukaa pale Mahakimu na Majaji ni suala jingine ambalo hili pengine nalo linapaswa lipewe nguvu kama ujenzi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala zima la *staff* wa Mahakama kwa ujumla; tumekuwa tukilalamikiwa wakija hawa watu kutoka Wizarani wakisema kwamba wana-*under staff* na kwa maana hiyo hawawezi kufikia yale malengo yaliyopangwa. Najua kuna mipango mizuri, kwa mfano; kila Jaji au Hakimu amepewa idadi fulani ya kesi azitekeleze lakini bila utekelezaji pamoja na kupunguza, kusikiliza kwa *video*, kusikiliza kwa nini bado tuna ukosefu. Naamini kuna haja ya kufanya *fast tracking* ya Mahakimu au kuna njia ya kutafuta sijui mnaita Ikama, sijui kitu gani, Ikama zipelekwe kwa wingi watu hawa waweze kuajiriwa ili ile haki na Utawala Bora uonekane kutendeka kwa makini.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili tunasema kwamba bila Mahakama nilisema hapo mwanzo huwezi kupata haki wala huwezi kupata Utawala Bora lakini mwaka jana sisi tulipitisha Sheria juu ya uhujumu uchumi na utakatoishaji wa fedha na Sheria ile ilipitishwa katika wakati ambao kusema ukweli tulifanya makosa kama Bunge kupitisha Sheria ambayo imelata mashaka makubwa katika jamii kwasababu ya namna ambavyo inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano; sitaki kuzungumzia mwenendo wa kesi zinavyokwenda lakini tumeona jinsi

ambavyo kumekuwa na ugumu mkubwa na katikati ikaja na *plea bargain* kwa watu ambao wanashitwakiwa kwa makosa ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi. Mtu anakamatwa kwanza kisha yeye ndiyo anatakiwa a-*prove* kwamba yeye siyo mkosaji na tunasema kwamba ili Mahakama ifanyekazi, Mahakama ndiyo i-*prove* kwamba yule Mtu ana kosa lakini tumekwenda *system* ya Kifaransa uliyekamatwa wewe ndiyo una-*prove* kwamba unakosa kwahivyo unaiita Serikali, unaiambia mimi nalipa milioni kadhaa kwasababu najihisi nina kosa lakini siyo *system* yetu.

Mheshimiwa Spika, s*ystem* yetu inasema Serikali ndiyo im-*prove* mtu siyo yulke mtu aambiwe kwamba a-*enter plea bargain* ili akubali kama ana makosa. Kwa maana hiyo basi hakuna siku Serikali itaingia na makosa kwasababu itakuwa mtu mwenyewe anasema nina makosa kwasababu ya dhiki ya kukaa rumande, kwasababu ya dhiki ya kukaa muda usiojulikana.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria hii hii pia tulipitIsha kipengele kwamba Mahakama tumeipoka mamlaka yake ya asili ya kutoa dhamana, tumeipoka Polisi mamlaka yao ya asili ya kutoa dhamana. Kwa hiyo hakuna *Police bail* wala *Court bail* na mimi kwa kuliona hili nilileta hoja binafsi. Hoja yangu binafsi nikaileta kutaka Serikali sasa ilete mabadiliko na hapa katika Kikao hiki hiki kuna watu wamesema lazima tulete mabadiliko ya kurekebisha namna ya kutoa dhamana la sivyo hatutendi haki na ni dhuluma kabisa kumchukua mtu kumweka hajui lini atatoka, hakuna namna yoyote ya kupata dhamana, analazimishwa ku-*enter pre-bargain,* pengine haitaki lakini kwa sababu tu, jamaa zake wanachanga. Nafikiri hili tulifanya makosa kama Bunge na inapaswa Serikali irekebishe na kabla ya kusubiri Serikali nilileta fikra hiyo kupitia hoja binafsi, lakini mara mbili imekwama.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusiana na suala la *Justice delayed, justice denied.* Kusema kweli kesi nyingi zimekuwa zikirahisishwa sasa zinakwenda kwa haraka, lakini kuna case moja *super case, case* ya watu wa uamsho au *case* ya watu walioshtakiwa

kwa ajili ya suala la uamsho. Hawa wako mahakamani kwa miaka nane, mpaka leo *case* haijaanza, ukiuliza unaambiwa ushahidi haujapatikana. Hivi kweli baada ya miaka nane ushahidi huo haujayeyuka! Ushahidi huo haujapotea! Vipi Taifa au nchi inaweza kuweka raia wake miaka nane bila kesi kuanza, kwa sababu angalau ingekuwa kesi imeanza wangekuwa wameshafika mbali, wakahukumiwa tukajua kwamba wana haki au hawana haki.

Mheshimiwa Spika, leo watoto wao hawajui wazee kama watafia mahakamani, wenye wake zao hawajui kama wake zao hiyo ndoa kama *inaswihi* tena hivi sasa, kama miaka nane haipo tena. Kuna wengine wamefiwa na watoto wao, kuna wengine wamefiwa na wake zao, hata kwenda mtu anaogopa, hakuna watu ambao wanakwenda kuwasaidia, si rahisi mtu anaogopa na yeye atahusishwa. Miaka nane jamani *is a long time*, hata Guantanamo watu hawakukaa miaka nane, walioamuliwa wameamuliwa imekwisha. Kwa hivyo, hii inaitia hila na kuiweka katika nafasi mbaya sana Serikali. Waamue, leo haiwezekani kesi miaka nane nchi ambayo ina utawala bora, nchi ambayo inakwenda kwa misingi ya sheria, nafikiri si vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni kwenye Tume ya Haki za Binadamu. Mimi ni mmojawapo nimekuwa nikipiga kelele kile kipindi ambacho watu wa Tume hawajateuliwa. Baada ya kuteuliwa nilifurahi sana ile timu iliyokuja ni timu nzuri sana, wanafanya vizuri sana, lakini tunawaombe fedha zaidi ili wawe *proactive*, waweze kufika kwa watu. Vituo vingi hawawezi kuvifikia, sehemu nyingi hawawezi kufika, kufika ni mpaka watie mafuta wao wenyewe kwenye gari. Wanafika hawawezi kushughulikia masuala ya haki za binadamu, bila haki za binadamu kusimamia na Tume hii na utawala bora basi kila Serikali itakavyofanya itasemwa nje na Mashirika ya Kimataifa, itasemwa nje na nyingine. Tukitaka tuondoshe tusisemwe na nchi nyingine na tusijidai kwamba sisi ni *sovereign* kwa mujibu wa Mikataba ya Kimataifa mtu mwingine anaweza kuchukua hatua ikiwa wewe unakiuka haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, Gambia imeishtaki Myanmar kwa kuwaua na kuwachoma moto watu wa kabila la Rohingya. Kwa hivyo Mtanzania asijidanganye kusema kwamba sisi ni *sovereign state* hatuwezi kugombwa na nchi yoyote, si kweli, maadam tuaishi katika dunia ya kisasa, tunaishi katika utawala wa kiulimwengu, ni lazima tutasemwa, tukiimarisha tume hii basi tutapunguza kusemwa.

Mheshimiwa Spika,Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh ahsante sana kwa mchango wako mzuri, uliotulia, unaonesha kweli ulikuwa mwanakamati wa Kamati hii.

Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi. Namshukuru Mungu kunipa nguvu na uwezo leo hii nikaweza kusimama kuchangia hotuba hii ya Kamati ya Katiba na Sheria ambayo na mimi tangu nimeingia katika Bunge hili nimekuwa Mjumbe wa Kamati hii, mjumbe wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa dhati ya moyo wangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa umahiri wake katika kusimamia na kuhakikisha kama Tanzania yetu inapaa kiuchumi, kimaendeleo na kimaslahi ya jamii na vilevile kulinda rasilimali zetu. Nampongeza pia Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia, Mheshimiwa Waziri Mkuu jinsi wanavyosaidiana na Mheshimiwa Rais katika kutenda kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha wa mchango wangu leo nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Mahiga, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Watendaji wake Profesa Mchome, Ndugu Mpanju na Watendaji wa Mahakama kwa jinsi tulivyoweza kufanya nao

kazi kwa mashirikiano mazuri mpaka tukapata mafanikio makubwa katika Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda nikiri kuridhishwa na utekelezaji katika uboreshaji mfumo wa utoaji haki nchini unavyofanyika. Kwa kweli tayari kuna Majaji na Mahakimu kadhaa ambao wameweza kuteuliwa na wanafanya kazi zao nzuri. Majaji pamoja na Mahakimu hawa wakiwemo wa jinsia zote, wanawake na wanaume ambao wanafanya kazi kwa weledi kabisa, kwa hivyo kurahisisha mashauri kumalizika kwa haraka sana. Kesi za kuhujumu uchumi zinamalizwa kwa wepesi na jamaa waliotupiga fedha zetu zinaanza kupatikana na tunarudishiwa fedha zetu tunafanyia mambo mengine katika shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nikupe wewe pongezi zako kwa jinsi ulivyowezesha Kamati yetu tukaweza kwenda kukagua miradi katika mikoa yetu inayohusiana na Wizara hii. Mradi wa majengo, majengo mengi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Wilaya yameweza kukamilishwa na yako katika hali nzuri sana ambayo kwa kweli tunaamini kwamba haki itatendeka pale vizuri kwa sababu jengo lenyewe ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Mahakama ya Chato, Mahakama ya Kigoma, Mahakama ya Manyara ambayo kwa wakati fulani tuliitembelea tukaikuta iko shaghalabaghala na Kamati ikatoa ushauri wake pale na ukafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tukuyu, Mahakama ya Kondoa, ambayo ilifunguliwa hapa karibuni ambayo ni nzuri kweli kweli, Mahakama ya Longido na Mahakama ya Ngerengere. Si tu hizi Mahakama ni nzuri, lakini zimezingatia matakwa ya jinsia, ziko Mahabusu za wanawake, wanaume na watoto ambazo hata mabafu yao utafikiri uko katika *Star Hotel* ya nyota tano jinsi yalivyokuwa mazuri. Kwa kweli kazi nzuri katika ujenzi huu nao nitoe pongezi kwa Injinia wa Mahakama Ndugu Katunzi amefanya kazi ya usimamizi mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukamilishwaji wa majengo hayo lakini nina ombi, kwanza ni kujengea uzio kwenye majengo yote ambayo hayana uzio. Kwanza kwa usalama na pili katika kuhakikisha kwamba yanapata sura nzuri, maana huwezi kupaka poda halafu ukasahau kupaka wanja.

Mheshimiwa Spika, ombi langu la pili ni ukosefu wa mahabusu kwenye Mahakama hizi za Mwanzo, kwa mfano Mahakama ya Ngerengere; jengo jipya ni zuri tulikagua hapa juzi lakini mahabusu halina. Kwa hivyo mahabusu inabidi watoke Morogoro waletwe, huku ni mbali sana. Kwa hivyo niiombe Wizara ilitafutie ufumbuzi jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ombi la tatu ni kwa Serikali iweze kutoa fedha zilizotengwa ili mahakama iweze kukamilisha miradi yake bila kukwama. Kwa mfano, Bunge liliidhinisha bilioni 15 fedha za ndani za bajeti mwaka 2019/2020, fedha iliyotoka hadi Februari, 2020 ni bilioni 4.8. Kwa hivyo tuombe fedha hizi zitoke kwa wakati ili kazi za mahakama zisikwame.

Mheshimiwa Spika, ombi la nne, uboreshaji wa maslahi ya Wanasheria, hili ni jambo muhimu sana. Wanasheria wetu wanafanya kazi nzuri sana kama hivyo uandaaji wa Miswada, kushauri Serikali, kwa hivyo mishahara yao izingatiwe ili itazamwe sana na pia mazingira ya kazi zao yazingatiwe na yatazamwe sana. Kwa nafasi ya kipekee pia nimpe pongezi kubwa sana Profesa Juma kwa jinsi anavyosimamia ule Mhimili wake kazi inakwenda vizuri, watu wanamaliziwa kesi zao kwa haraka haraka, kama hivyo tulivyoelezwa na tulivyoshuhudia wenyewe kesi za Mahakama Kuu zinaendeshwa kwa kupitia mitandao. *Big up* kwa Profesa Juma.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo nitapenda kulizungumzia hapa leo ni hili hili kwamba tusisitize kuzingatia maelekezo tunayopewa na Serikali katika vita yetu *corona*. Tufuate mashauri yote, tujitahidi sana ili tuishinde vita hii ya *corona* isije ikatushinda yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno yangu hayo, nashukuru sana kwa jinsi tulivyoshirikiana na wewe katika kipindi chote nilichokuwa Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano. Natoa salamu nyingi kwako na kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri na Viongozi wake. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha Abdullah Juma. Sasa tunarudi hapa ukumbini Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nikuombe radhi kama hotuba yangu mimi ni Msemaji wa Kambi imekukwaza nafikiri itakuwa tu tumetofautiana kwenye mitazamo, lakini lengo letu ni moja kuhakikisha Wizara hii ya Katiba na Sheria ni moja kati ya Wizara inayofanya vizuri kwenye nchi yetu pamoja na ufinyu wa bajeti tulionao.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria kwa bajeti iliyopita ukitazama imepelekewa asilimia 26 tu ya bajeti yake na huo ulikuwa msingi wa hotuba yangu kujaribu kushauri namna ambayo Wizara hii inaweza ikajiendesha bila kuhitaji fedha zaidi kwa kuzingatia mazingira tuliyonayo, bila kuhitaji fedha zaidi na kuokoa gharama ambazo siyo za muhimu.

Mheshimiwa Spika, wakati tunawasilisha hotuba yetu ya Ofisi ya Waziri Mkuu uliuliza maswali mengi na ulikuwa na shauku kubwa ya kujua ni kwa nini Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wanataka Tume Huru ya Uchaguzi kwa hiyo, nikaona ni busara. Wewe kama kiongozi wetu mimi kama Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria nikueleze katika hotuba yangu tunapotaka Tume Huru ya Uchaguzi tunamaanisha nini niliona ni busara.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba hii karibu nusu nzima nimejaribu kujielekeza katika kulifafanua hilo ili Bunge na Watanzania wote wafahamu Kambi Rasmi ya Upinzani ina lengo la kuweka uwanja sawa katika uchaguzi mkuu ulioko mbele yetu; ina lengo wa kuhakikisha Chama cha CCM kipo madarakani, Chama cha Upinzani kipo madarakani, Tume Huru ya Uchaguzi ambayo ndiyo refali yetu anaweza kutenda haki pila kupendelea upande wowote na hilo ndilo lilikuwa lengo la hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mfano vifungu vichache vya Katiba ambavyo vinasimamia uchaguzi; Ibara ya 74(12) na (13) ibara ya 41, 38, 37 na 36 ni Ibara ambazo zina upungufu mkubwa na zinaleta gharama kubwa kwenye Wizara na Taifa kwa ujumla bila sababu yoyote ya msingi.

Mheshimiwa Spika, hoja katika ya maoni sina lengo ya kusoma hotuba ambayo umeifuata moja kati ya maoni makubwa ambayo tumetoa humu ndani tulichokuwa tunakitaka sisi Kambi Rasmi ya Upinzani tulitamani Mheshimiwa Rais baada ya Uchaguzi asitangazwe mpaka pale pingamizi iliyopelekwa hati ya dharura Mahakamani litakapoamuliwa, kwa nini tulitaka hivyo? Ni ili kuepusha gharama kubwa ya kurudia zoezi moja mara mbili kama pingamizi lile litakuwa limefanikiwa.

Mheshimiwa Spika, umesema wewe ni mwanasayansi, mimi ni mwanasanaa, tunatofautiana kwenye *approach* lakini lengo langu ilikuwa ni kuokoa gharama zisizo kuwa na msingi ambazo hata sasa zinaonekana hatuwezi kuzimudu. Hebu tizama kwa mfano kwenye hotuba yangu nilikuwa nimeongelea suala Tanzania kushindwa kuridhia mkataba kuhusu demokrasia na ule Mkataba wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, sisi nchi maskini Tanzania tunategemea *fund* kutoka kwenye Mataifa mbalimbali na ili tupate *fund* lazima tuwe sehemu ya mikataba ambayo inatakiwa iwe imeridhiwa. Hatujaridhia mikataba ile, hotuba yangu ilikuwa imejielekeza kuisisitiza Serikali, Mwanasheria

Mkuu wa Serikali na Waziri wa Katiba na Sheria amshauri Mheshimiwa Rais, aishauri Serikali turidhie ili tuweze kupata pesa kwenye *donar community*.

Mheshimiwa Spika, tukikataa kuyasikia haya mambo leo haimsaidi yoyote kati yetu. Vyama vya Upinzani katika nchi hii vimekuwa vikishinda uchaguzi kwa Tume hii ya Uchaguzi

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome wewe eleza unachotaka kutuambia ukijaribu kujadili maamuzi ya Spika utapata tabu tu. Nimekuelewa unaposema mwanasanaa kwamba unaogopa tarakimu kwa sababu hii ni hotuba ya bajeti, bajeti ni tarakimu, sasa umekwepa tarakimu mwanzo mwisho haina neno nimekuelewa. Sasa wewe jielekeze tu unataka kuiambia nini Serikali na nimekupa nusu ya muda, kule ulikuwa na dakika ishirini sasa peke yako una dakika kumi zinatosha hizo.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli zinanitosha sana.

Mheshimiwa Spika, kwa Tume tuliyonayo ya Uchaguzi vyama za upinzani zimekuwa zikishinda chaguzi mbalimbali na tutaendelea kushinda, kwa Tume hii tuliyonayo. Lengo letu sisi kwenda kushauri Wizara ya Katiba na Sheria katika jukumu kubwa lililoko mbele yake ijielekeze katika kuhakikisha wanaboresha mfumo, wanaleta mabadiliko haraka ambayo yatasaidia tuwe na uwanja sawa wa uchaguzi, lengo letu ilikuwa ni kuokoa gharama katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi hatuna uoga wowote kuhusu hilo nikutolee mfano mdogo, katika kifungu cha 38(7) na (8) cha Sheria ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi inalazimika kuwa nchi nzima, ikasambaze fomu nchi nzima kwa ajili ya uchaguzi ambayo ni gharama kubwa sana na Serikali imethibitisha pesa hiyo hawana. Sisi tumeshauri kwamba kwa sababu za kiusalama kuepuka *biasness* na kwa sababu ya kuhakikisha kunakuwa na uwanja sawa katika uchaguzi unaokuja angalau fomu hizi zitolewe kwa njia ya mtandao, sasa hapo

kuna ubaya gani? Amesema vizuri mnadhimu, atakuja kuzungumza na wewe ili tuweze kurekebisha haya mambo, lakini mwisho wa siku ni lazima tuzungumze.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye suala la *pre- bargain* ambayo inafaywa na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, zipo kesi ambazo zimerundikana mahakamani na watu wako magerezani kwa sababu kuu mbili; ama upelelezi haujakamilika au kesi zao hazina dhamana. Sasa watu hawa mtu amekaa miaka mitatu, mine, mitano, baada ya muda kupita anaitwa, yaani wewe umekaa magereza miaka zaidi ya mitatu, minne, mitano, baada ya muda unaitwa Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali unaambiwa njoo tufanye mazungumzo namna gani unaweza ukatoka gerezani. Baada ya hapo tunaona kwenye vyombo vya habari ameridhia kulipa faini. Utanisaidia hapo maana yake huyo mtu amekutwa na hatia au hana hatia na je, heshima ya mtu huyo bado ipo imepotea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge lako Tukufu liielekeze Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali kwanza watueleze hizo kesi ambazo wanafanya *pre-bargain,* baada ya kulipa zile faini wale watu wanakuwa na hatia au hawana hatia. Pili, pesa ambazo wamezipata kupitia *pre-bargain* ni shilingi ngapi? Bunge hili linajua tumepata shilingi ngapi? Ni *Vote* namba ngapi na kwa nini tusipeleke pesa kwenye Wizara hii ili tupunguze mianya hii ya kugeuza vyombo mbalimbali vya Wizara ya Katiba na Sheria kuwa chanzo cha kukusanya mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vijana wanaitwa Tito Magoti kijana mdogo sana yupo pale amepewa kesi ya utakatishaji fedha sijui uhujumu uchumi, yule ni kijana mdogo sana sasa hivi yupo gerezani kesi yake haisikilizwi nini upelelezi haujakamilika.

**SPIKA:** Sasa si umesema mwenyewe kwamba kesi ikiwa mahakamani hatujadili na wewe Mwanasheria basi, sijui basi busara ikuongoze.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu kuu ni kwamba hili zoezi linaloitwa *pre-bargain* sijui kwa Kiswahili linaitwa mazungumzo kabla kesi haijaendelea mahakamani, wanaitoa ili waende wakazungumze kwanza, waone namna ya kumtoa mtu mahakamani, napata wasiwasi na wasiwasi wangu ni kwamba watu wanakaa magereza miaka mitatu, mine, mitano kazini wametolewa, heshima yao inashuka kwenye jamii, mwisho wa siku wanaenda kwenye mazungumzo, vyombo vya habari vinaandika kwamba, huyu mtu ameridhia kulipa pesa kwa sababu amekubaliana na makosa aliyoyafanya.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa kesi ya Erick Kabendera, juzi amekiri, angalau huyo hayuko Mahakamani, amekiri ametoka jela. Huwezi ukaniita mimi na wewe tufanye mazungumzo kwenye mazingira ambayo uwanja wa kufanya mazungumzo hauko sawa? Hatuwezi kufanya mazungumzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuombe Kiti chako kione busara kuielekeza Wizara, hii inaharibu *future* na *dreams* za Watanzania. Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali inatumika kutafuta pesa kwa ajili ya Serikali na kwa sababu hiyo inaua heshima, utu na ustaarabu tulionao Watanzania. Hakuna *plea- bargaining* kwa mtu aliyekaa miaka minne magereza, hakuna kitu cha namna hiyo. Mtu amekaa miaka minne unamuita huyo ni mnyonge tayari, wewe umeshika mpini yeye ameshika makali, hakuna *negotiation* inaweza ikafanyika kwenye mazingira hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tuko kwenye janga la *Corona,* watu wamejaa mahabusu kwa sababu eti upelelezi haujakamilika. Kwanza umesema nitoe sababu ya kibajeti, ni gharama kubwa kuwalisha mahabusu, ni gharama kubwa sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome, nakumbuka wakati Mzee Mandela yuko magereza walikuwa wanafanya vi-*bargaining* kidogo na wale jamaa.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mandela alikuwa gerezani chini ya uongozi wa Makaburu. Mimi nakushauri tu mambo haya ya siasa uyaache, wewe ni mwanasayansi umesema mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi siyo makaburu, sisi Serikali yetu ni Serikali inayotenda haki, naamini itatenda haki. Kwa hiyo, mimi nasisitiza watu watolewe magereza hatuwezi kujadili kwenye uwanja ambao mtu amekaa magereza miaka minne halafu unamuita ku-*negotiate.*

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Kuna taarifa sijui iko upande gani, nilishairuhusu tayari.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ni mimi.

**SPIKA:** Ooh, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Salome kwamba *plea-bargaining* ni utaratibu unaotumika hata kwenye zile nchi ambazo ndiyo tunaonaga kwamba wanajali haki za binadamu. Utaratibu huu unatumika sana Marekani na Canada, kwa hiyo, siyo mfumo ambao unatumika tu kwa makaburu. Kama kawaida huwa tunasema tukopi kwenye njia za wale ambao tunafikiri wako *progressive* kisheria, kwa hiyo, nimweleze tu *plea-bargaining* siyo kitu kipya.

**SPIKA:** Ulikuwa unasomeshwa shule tu Mheshimiwa Salome na muda wako umeisha. Sekunde chache tu kwa kujibu taarifa hiyo tu.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa siipokei na sitaeleza kwa nini siipokei kwa sababu Mheshimiwa Waziri anajua kwa nini hivyo. Mimi naomba nijielekeze kwenye hoja.

**SPIKA:** Muda wako ulishaisha ilikuwa ni hiyo tu. Ahsante sana Mheshimiwa Salome Makamba. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Mhagama akiwa kule Msekwa atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Mnzava ambaye pia yuko Msekwa.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia leo hotuba ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nikushukuru sana Mheshimiwa Spika katika kipindi hiki cha miaka mitano mimi kama baadhi ya Wabunge ambao wamechangia tumehudumu katika Kamati hii ya Katiba na Sheria na nimepata fursa ya kujifunza mambo mengi sana. Nitumie nafasi hii kukushukuru sana kwa kunijengea uwezo kwa kupitia ushiriki wangu kwenye Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na timu nzima; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya kwa kulijenga Taifa letu na kwa kulinda haki na ustawi wa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi hotuba yangu leo itakuwa fupi kwa kadri itakavyowezekana. Nataka nijikite kwenye eneo moja tu la Mfuko wa Mahakama - Fungu 40. Nchi yetu inaundwa na mihimili mitatu, tunao mhimili wa Mahakama, Bunge na *Executive* ambao ndio mhimili wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mihimili hii mitatu ni kama maksai watatu wanaovuta jembe kwa pamoja, kwa wakati mmoja na kwa kuelekea mwelekeo mmoja. Kazi kubwa ya mhimili wa Serikali ni kutengeneza dira na kazi ya mihimili hii mingine

miwili ya Bunge na Mahakama ni kushirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba ile dira na malengo ambayo tumejiwekea tunayafikia.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imejiwekea malengo ya kukuza uchumi; kuifikisha Tanzania na Watanzania kwenye uchumi wa kati. Inafanya hivi kupitia kujenga uchumi kwa njia ambayo ni shirikishi na jumuishi. Kwa maana hiyo tunajenga uchumi jumuishi. Moja ya nguzo muhimu za uchumi jumuishi ni utawala wa sheria *(the rule of law).* Bila kuwa na utawala wa sheria huwezi kujenga uchumi jumuishi.

Mheshimiwa Spika, katika hili, naomba nimpongeze sanasana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwani mmefaya kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba nchi yetu utawala wa sheria unatamalaki. *The rule of law* imeendelea ku-*rain* Tanzania kwa miaka yote mitano, hii lazima niipongeze sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo Serikali imefanya vizuri kwenye eneo hili la utawala wa sheria ni namna gani inatoa haki kwa Watanzania. Awamu ya Tano imejenga Mahakama nyingi sana, tumeona Mahakama Kuu zimejengwa, tumeona Mahakama za Hakimu Mkazi zimejegwa, tumeona Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo zimeendelea kujengwa. Hii yote inarandana na dhana ya kuijenga Tanzania ambayo ina mfumo wa uchumi shirikishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni katika mazingira ambayo haki imetawala ndipo utapata *incentive* ya kuwekeza. Leo huwezi kumpata mwekezaji Tanzania kama hujajenga mazingira mazuri ya kutoa na kusimamia haki. Leo tunajivunia kwamba Tanzania tumepiga hatua kubwa kwenye uchumi, uchumi wetu unakua kwa asilimia 6.9; leo tunajivunia tuna wawekezaji wengi na wapo Watanzania wanaozidi kuwekeza Tanzania na wapo wageni wanaokuja kuwekeza Tanzania ni kwa sababu tumesimamia utawala wa sheria *(the rule of law).* Hili

naomba nilipigie mstari na haya ni mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna changamoto ambazo naamini kama Serikali itazifanyia kazi tutaboresha zaidi na *incentive* kwenye uchumi itakuwa zaidi kwa watu wetu wa chini. Watanzania wengi wapo vijijini na watafuta haki wengi kama ilivyo kwa asilimia; *proportional* ya Watanzania wengi wapo vijijini maana yake hata wenye changamoto za upatikanaji wa haki wapo vijijini.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia miundombinu ya utoaji haki vijijini ni duni sana. Nenda kwenye Mahakama za Mwanzo zimechoka lakini siyo tu kuchoka kwa miundombinu pia zina watumishi waliokosa weledi na mahali pengine wako wachache hawakidhi akidi inayotakiwa. Niiombe sana Wizara kwenye eneo hili ijitahidi kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, naelewa Serikali kwenye bajeti ya mwaka 2019/2020 imepeleka fedha ndogo sana kwenye Wizara hii. Kwenye eneo hili la Mahakama katika bajeti nzima ambayo Wizara iliomba imepelekewa asilimia 45.24 lakini ukiangalia kwenye uboreshaji wa miundombinu maana yake fedha za maendeleo ni asilimia 23 tu ya fedha za ndani na asilimia 35 tu ya fedha za nje. Hii ni ishara kwamba bado *commitment* yetu kama Serikali kwenye kuhakikisha kwamba Watanzania walio chini wanapata haki ni ndogo. Niombe sana Serikali yangu ninayoiamini sana ihakikishe kwamba inapeleka fedha nyingi kwenda kuboresha miundombinu ya Mahakama maeneo ya vijijini. Pale Madaba tuna Mahakama ambayo nikikuonyesha majengo yake utatupa pole, tuna kazi ya kwenda kufanya.

Mheshimiwa Spika, pia Madaba kama ilivyo katika maeneo mengi ni Wilaya na sehemu zingine ni Halmashauri hatuna Mahakama za Wilaya. Tunaomba Mahakama za Wilaya kwenye ngazi hizi za chini ambapo Watanzania wengi ndio wanahangaika na haki; wanapigania mashamba yao, hata matatizo yao kila siku, migogoro ya nyumbani, haya yanatakiwa yatatuliwe kule chini. Tujifunze pia kwenye sekta

ya afya ambako tumekuwa na uboreshaji wa miundombinu ya afya toka ngazi za vijiji mpaka ngazi za mikoa na hii Mahakama iweze kutoa huduma zilizotukuka toka ngazi ya chini mpaka ya juu.

Mheshimiwa Spika, kwa maslahi ya muda, nijielekeze kwenye eneo la watumishi. Ikama nimetaja kwa kuanzia lakini ni ndogo. Naomba tuendelee kuishauri Serikali kama Wabunge kuhakikisha kwamba tunapata ikama ya kutosha ili tuweze kutoa haki kwa njia iliyo sahihi na tuweze kutengeneza *incentive* kwa Watanzania kuendelea kujishughulisha na shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama kwa mjadala mzuri. *In short* Waziri alikuja mwaka jana akaomba fedha ameenda kutumia ameleta taarifa ya kazi walizofanya na sasa anaomba tena fedha kwa mwaka wa fedha ujao, hapa ndiyo mjadala wetu unapojikita.

Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Timetheo Mnzava kutoka Msekwa atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema anayeendelea kutujalia uzima.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wizara ya Katiba na Sheria, Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wakuu wa taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishauri jambo moja tu kwa upande wa utumishi, juzi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) amezungumzia vizuri kuhusu watu kukaimu nafasi. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ipo Taasisi moja kwa maana ya Wakala wa Udhamini na Ufilisi (RITA),

aliyekuwa Mtendaji Mkuu aliondolewa tangu mwaka 2015 na tumekuwa na Kaimu Mtendaji Mkuu tangu kipindi hicho mpaka sasa karibu miaka mitano (5). Nashauri sana Wizara waliangalie suala hili na mamlaka za uteuzi liweze kufanyiwa kazi, kama aliyepo anafaa aendelee na kama hafai basi awepo mtu kuliko kuendelea kuwa na Kaimu Mtendaji Mkuu kwa muda wa miaka mitano (5).

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu, nimemsikiliza vizuri dada yangu, msomi mwenzangu Mheshimiwa Salome akizungumzia kuhusu uridhiaji wa mkataba. Nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria, tunao utaratibu kama nchi wa namna gani ya kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa pia tunavyo vigezo mbalimbali vya kuangalia kabla hatujakubali kuridhia hiyo mikataba. Ni aibu kuona kwamba tunajielekeza kwenye kigezo kimoja cha kupatiwa fedha na nchi zenye nguvu ili tuweze kuridhia mikataba. Ni vyema tuangalie vigezo vingine vyote vya msingi kama taifa; tuangalie mahitaji yetu kama taifa na mazingira yetu kama taifa. Hayo ndiyo yatuongoze kwenye kuridhia au kutokuridhia mikataba na siyo kuangalia kigezo kimoja pekee cha fedha. Tukiangalia fedha iko siku vitu vingine vya ajabu tutavikubali kwa sababu tunataka kupata fedha.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, pia amesema kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwamba moja ya sababu ya kutaka sijui Mahakama na kitu gani ni ili kuzuia tusipate gharama.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava, kuna taarifa unapewa.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, gharama ni ipi, ni gharama ya zoezi la uapisho au ni gharama

ya zoezi la uchaguzi na ipi ni gharama kubwa? Nadhani kama kuna sababu nyingine ni vyema kama msomi basi aielekeze vizuri ili iweze kueleweka.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Wizara ya Katiba na Sheria...

**SPIKA:** Basi vumilia Mheshimiwa Salome ni kwa sababu ya mawasiliano.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kujenga majengo ya Mahakama kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnzava anapotosha.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Korogwe Vijijini tunashukuru sana tumepata Mahakama mpya ya Mwanzo ya Magoma kwenye Tarafa ya Magoma. Tunayo Tarafa ya Bungwi ...

**SPIKA:** Nitakupa nafasi mwishoni.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ina jengo la muda mrefu sana ambalo halina Hakimu yaani Tarafa nzima ina kata 9 hakuna Hakimu inawalazimisha wananchi wetu watoke kilometa zaidi ya 50 kwenda Korogwe Mjini kufuata huduma ya Mahakama. Jengo lile siyo zuri sana linahitaji ukarabati lakini wakati huu tunaosubiri ukarabati basi tungeweka utaratibu wa kupangiwa Hakimu hata yule wa kutembelea kama ni mara moja au mara mbili ingeweza kutusaidia zaidi ili wananchi wetu waweze kupata huduma hii vizuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tuko kwenye bajeti lakini tunakubaliana kwamba tuko kwenye dharura ya

kidunia ambayo ni *Corona*. Napenda kutumia nafasi hii niseme tu kidogo namna gani Wizara ya Katiba na Sheria kupitia taasisi zake inaweza kutusaidia kwenye harakati zetu za mapambano dhidi ya ugonjwa huu wa *Corona*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba Mahakama ndio chombo chenye mamlaka ya utoaji haki kwa mujibu wa Ibara ya 107 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kutambua kwamba Mahakama imeweza kufanya kazi nzuri katika kujikinga na ugonjwa wa *Corona* lakini lazima tukubaliane kwamba Mahakama hii haiko peke yake, inao wadau ambao inashirikiana nao katika kufanya kazi. Moja ya mdau mkubwa na muhimu anayeshirikiana na Mahakama haswa kwa kesi za jinai ni Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali. Ofisi hii ikishirikiana vizuri na Mahakama itatusaidia kuongeza hatua za namna ya kujikinga na ugonjwa wa *Corona*.

Mheshimiwa Spika, ziko namna nyingi, namna ya kwanza ni hii ya *plea bargaining,* nimemsikia msomi dada yangu Mheshimiwa Salome akizungumza kwamba hata haielewi *plea bargaining* ni nini. Nadhani Profesa Mchome yuko kule atakuwa alikuwa anamsikiliza mwanafunzi wake pengine atakuwa amesikitika kidogo. Kwenye sheria yenyewe tulitafsiri nini maana ya *plea bargaining* na ukiipata ile maana yenyewe ya *plea bargaining* inakuambia kwamba huyo mtu anayefanya *plea bargaining* ikishasajiliwa na akishalipa ni mtu mwenye hatia au asiye na hatia inaeleweka. Kama kuna kitu Bunge lako linapaswa kujivunia ni kuwa sehemu ya mabadiliko haya makubwa ya kuleta mfumo wa *plea bargaining.* Ni mfumo ambao umetusaidia, kama walivyosema wengine hatukuanza nao sisi umeanza maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, pia kwa kumkumbusha tu mfumo wa *plea bargaining* tumeuweka tu rasmi na tumeweka utaratibu mzuri lakini tulikuwa nao hata siku za nyuma. Miaka ya nyuma kwenye kesi za jinai watu wa mashtaka na wale watuhumiwa wanaweza wakakaa chini wakakubaliana namna bora ya kumaliza mashauri yao. Ndiyo maana ziko

kesi za mauaji wakikaa wakikubaliana inakuwa kesi ya kuuwa bila kukusudia, yenyewe hiyo ilikuwa ni namna fulani ya *plea bargaining* lakini ilikuwa haikuwekwa kwenye mfumo huu mzuri.

Mheshimiwa Spika, sasa tushukuru kwamba Bunge hili la Kumi na Moja limekuwa sehemu ya kufanya mabadiliko haya makubwa ya kutanua wigo wa utoaji haki. Lazima kama taifa tujivunie hatua tuliyopiga kwenye kuanzisha *plea bargaining,* imetusaidia kuharakisha usikilizaji wa mashauri, inapunguza gharama kwa pande zote pia kupunguza muda wa kusumbuka na kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la *plea bargaining* naiomba sana Ofisi ya *DPP* mtusaidie, ziko kesi ambazo zimekaa Mahakamani muda mrefu kwa sababu tuna *plea bargaining* na iko kwa mujibu wa sheria tungepata *session* maalum kama ni ya wiki moja au wiki mbili kwa Mahakama za ngazi zote na tusifanye kwa kesi za uhujumu uchumi peke yake tu tufanye kwenye makosa yote watu waende wanaotaka kufanya makubaliano wafanye ili kesi ziishe ili tupunguze msongamano kule kwenye yale magereza yetu, kwa maana ya upande wa mahabusu pia kwa upande wa magereza.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine amelizungumzia kidogo Mheshimiwa Shangazi, kwa mujibu wa kifungu cha 91 cha Sheria ya Taifa ya Mashtaka, Mkurugenzi wa Mashtaka hana *time limit* ya muda wa kushtaki kwa mujibu wa sheria, anaruhusiwa kupeleka shtaka muda wowote na wakati wowote. Kwa wakati huu tukiwa kwenye janga hili la *Corona* kama ziko kezi ambazo tunaona zimekaa muda mrefu na bado upelelezi wake haujakamilika tunaendelea kukusanya ushahidi basi tutumie kifungu cha 91 Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kuwa hafungwi aziondoe kesi hizi Mahakamani kupunguza msongamano wa hawa mahabusu huko Mahakamani. Baada ya kujiridhisha wakipata ushahidi wa kutosha zitarudishwa kwa kuwa sheria inamruhusu kuweza kurudisha kesi hizi Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande mwingine naomba tu Ofisi ya Mwendesha Mashtaka pia itumie wakati huu tuliokuwa nao wa *crisis* hii ya *Corona* kumshauri vizuri Mheshimiwa Rais kuhusu wafungwa ambao wamebakiza muda mdogo wa vifungo vyao kule Magereza. Wako wafungwa wameshakaa Magereza na wamebakiza muda mdogo, tuna uwezo wa kumshauri Mheshimiwa Rais; *DPP* amshauri Mheshimiwa Rais atoe msamaha kwa hao wafungwa, tuendelee kupunguza idadi ya wafungwa na idadi ya mahabusu kwenye Magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba upande wa kesi ambazo zimekaa muda mrefu. Zipo kesi zimekaa muda mrefu ambapo hata zikifika mwisho, vifungo vyake ni kati ya muda wa mwaka sifuri mpaka labda miaka sita au miaka mitano na zimekaa Mahakamani muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba tu niseme, kwa kuwa kuna watu wamekaa mahabusu tayari umekuwa muda mrefu wakiwa wanasubiri kesi zao zisikilizwe na hazijasikilizwa; na hata zikisikilizwa mwisho wake hukumu yao haiwi ya muda mrefu, ni vyema tungetumia hii nafasi kusema tu kwamba hawa kwa kuwa walikaa muda mrefu kwa yale makosa ambayo siyo makubwa, ihesabike kama wameshatumikia vifungo vyao. Wasamehewe tufute hizi kesi ili tuweze kupunguza huu msongamano wa watu wetu kwenye Magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, niliona ni vyema nitumie nafasi hii kushauri mambo hayo machache, lakini pia niendelee kuipongeza Idara ya Mahakama kwa mapinduzi makubwa ya kisayansi wanayoyafanya kwenye namna ya kusikiliza kesi. Naomba tu kwamba miradi ya namna hii iendelee kufikiriwa iendelee kuwa mingi ili tuendelee kusaidia kuipa nguvu Mahakama.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho Mheshimiwa Rais, Kiongozi wetu Mkuu wa Nchi alishatoa mwelekeo wa kurudisha mashauri ya ardhi kwenda kwenye Mahakama zetu. Tunakubaliana kabisa na Mheshimiwa Rais kwamba

moja kati ya sababu zilizofanya tukapeleka kesi za ardhi kwenye Mabaraza ya Ardhi ilikuwa ni kuzidiwa na kuelemewa kwa Mahakama zetu kwa wakati ule. Kwa sasa tunakubaliana kwamba ni kweli Mahakama zimeimarika na ni jambo zuri zikirudi kwenye upande wa Mhimili wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, ipo sababu nyingine ambayo nayo ilikuwa ni ya msingi sana. Sehemu kubwa ya wananchi ambao wana shida na mashauri au migogoro ya ardhi, mingi sana iko kule vijijini na hata maeneo ya mjini. Wengi ni wananchi wa kipato cha chini. Moja ya sababu nyingine ilikuwa ni kuwaondolea wananchi kuumia na *techniques* za kimahakama. Mtu akiangalia kakosa kamoja, kaherufi kamoja, viherufi viwili, anafutiwa kesi, kesi inaondoka.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Rais amesema tunarudi kwenye Idara ya Mahakama. Naiomba tu Wizara, tunapokuwa tunaendelea mbele, basi bajeti zetu na mipango yetu pia i-*reflect* namna ya ku-*incorporate* hizi kesi za ardhi ikiwa ni pamoja na kuangalia namna gani ya kutengeneza kanuni ambazo ni rahisi zitakazowasaidia wananchi wa kipato cha chini wasiumie kwa kuendelea kupata shida ya zile *techniques* za kimahakama.

Mheshimiwa Spika, inaweza kutengenezwa kanuni au waraka ndani ya Mahakama au kupitia kwa Waziri mwenye dhamana kwa namna gani ya kurahisisha na kujaribu kupunguza baadhi ya zile *techniques* za kimahakama ili wananchi walio wengi waweze kupata haki kwenye upande wa mashauri haya ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Wizara inafanya kazi kubwa na nzuri, tunawaunga mkono, tunawapongeza sana. Nakushukuru sana. Pia nakupongeza na wewe maana leo nachangia kutoka Msekwa, naonekana kwenye ukumbi mkubwa. Ni maendeleo makubwa, tunakupongeza sana na tunakutakia kila la heri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava. Mheshimiwa Salome, bahati mbaya kwa sababu ya mawasiliano haya, hamtaweza kujibishana na Mheshimiwa Mnzava. Kwa hiyo, vumilia tu, utamtafuta msomi mwenzio baadaye, mtaelewana tu Kiswahili.

Nilikutaja Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuanza, kwa kuwa Bunge hili halijapata muda mahususi wa kujadili *Corona*, kwa hiyo, kila nitakapopata muda nita- *chip in* kidogo kuhusiana na *Corona*. Katika hili naunga mkono wito wa Mheshimiwa Rais kufanya maombi kuanzia Jumatatu, ingawa sisi wengine tulianza mapema kidogo, tulikuwa tayari tunaomba kila siku na hata hapa nilipokaa naomba.

Mheshimiwa Spika, naomba nikumbushe tu kwamba Mungu tunayemwomba ni Mungu wa ukweli. Kwa hiyo, katika hilo basi, Serikali sasa ije na *data* za ukweli kwamba vifo hasa ni vingapi? Wagonjwa hasa ni wangapi?

Mheshimiwa Spika, utakuwa unafuatilia mitandao pia na *sources* mbalimbali; utakuwa ni shahidi kwamba taarifa ni nyingi sana. Mara tunasikia Mloganzila imeshajaa; Arusha, sijui wapi, kumejaa. Kwa hiyo, Mungu anapenda ukweli; ili atusikilize vizuri, basi tuwe wakweli na tuje na taarifa za ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila mtu amezungumzia kuboreshwa kwa Mahakama. Ni kweli Mahakama zimeboreshwa sana; majengo, kompyuta na kadhalika, lakini katika mfumo wa utoaji haki, hakuna wakati ambapo Mahakama imebomoka kama katika Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya *DPP* ina upungufu mkubwa sana wa kimuundo, lakini tukiwa na *DPP* asiye na weledi na busara, shida inakuwa zaidi. *DPP* anaingilia majukumu ya *AG;* anaingilia majukumu hata ya Mahakama; anageuka *TRA* anakusanya mapato; anawapa watu kesi za uhujumu uchumi, unakaa miaka mitano, sita, saba, anakuita kesi bado iko Mahakamani anakwambia utoe hela, ulipe mabilioni tena *cash.* Unapeleka *cash.*

Mheshimiwa Spika, mfumo wetu sasa hivi ukienda Mahakamani hata kulipia fomu ya maadili ile shilingi 5,000/= wanakwambia nenda kaweke kwenye akaunti, lakini *DPP* peke yake ndio anapelekewa fedha za mnachoita *plea bargaining* kwenye mifuko ya sandarusi halafu mnasema *plea bargaining!* Mnasema ooh, Mandela alifanya *plea bargaining.* Mandela alifanya *plea bargaining* wakati yuko kwenye *strong side...*

**SPIKA:** Ule mfano siyo halisi. Nilikuwa naangalia...

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** ...alikuwa kwenye *strong side;* watu wanavunja madaraja huko, watu wanapambana msituni...

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa Mbilinyi. Ile ilikuwa ni *special* tu kwa Mheshimiwa Salome, mtani wangu, lakini haina uhusinao kabisa na *plea bargaining.* Endelea tu na mchango wako. *It was just a joke,* kwa hiyo *don't take it as an example.*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, *okay* nashukuru sana. ahsante kwa kuliweka sawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huyu *DPP* anawapa watu kesi, anawaita ofisini wanapeleka hela kwenye mifuko ya sandarusi; *that is Mafia style! That is not plea bargaining.* Huo ni umafia kama umafia mwingine wa kule *Sicily*, *Italy* kupora fedha za watu kwa kutumia Ofisi za Serikali. Ndicho kitu wanachokifanya. Sasa hili ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana la kubambikiwa kesi. Zamani suala la kubambikiwa kesi ilikuwa stori za Polisi; wamewakamata masela vijiweni, kambambikia kesi, aende akamtoe shilingi 5,000/= au shilingi 10,000/=. Sasa hivi suala la kubambikiwa kesi limekuwa *systematic.* Wenyewe wanatuambia kabisa, sisi tunapokamatwa Polisi unawaambia wewe *RCO* vipi? Anakwambia, mzee maagizo kutoka juu. S*ystematically* mnawapa watu kesi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nimepewa kesi. Ukitoa kauli ambayo haiifurahishi Serikali unapewa kesi ya uchochezi, unapewa kesi ya uhujumu uchumi. Mimi nimepewa kesi ambayo kwanza ilibadilika kama mara tatu. Kwanza nimeambiwa uchochezi; wakaenda wakarudi wakasema, nimemtukana Rais; wakaenda wakarudi wakasema nimemfedhehesha Rais, hawa jamaa.

Mheshimiwa Spika, baadaye nimekwenda Mahakama Kuu nimekata rufaa, Mahakama ya Rufaa imesema nimefungwa kihuni. Sasa huyu *DPP* hakujua kama hapa hakuna kesi mpaka amempotezea muda Mbunge, nimefungwa, nimekaa Magereza, mama yangu uhai umemtoka kwa sababu ya kufungwa halafu baadaye Mahakama inakuja kuniambia sina kesi!

Mheshimiwa Spika, nimefungwa kwa kesi ya kubumba na waliohusika kunifunga walipandishwa vyeo. Nchi hii, mtu aliyemfunga Mbunge alipandishwa cheo. Sasa Mahakama Kuu imetengua hukumu kwenye rufaa. Kwa taarifa yenu, kisheria ninayo nafasi ya kuwashtaki ndani ya miaka mitatu. Nikiamua kuwashtaki, hamtoboi ninyi kwa kunifunga kihuni. Nitawashitaki kwa kunifunga kihuni au inaitwa *malicious imprisonment. AG take note. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitawafunga, nitawashinda nitakamata ndege halafu mtakuja mtasema ooh, Sugu sio mzalendo. Ila ninyi kumfunga Mbunge ndiyo uzalendo huo katika Taifa hili. Ninyi kumfunga Mbunge ndiyo uzalendo, mimi nitawashitaki. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina *communication* ya Mawakili mpaka kutoka Tel Aviv, Israel, wanasema Sugu *you are an international figure.* Hivi mnadhani mna-*damage image* mnayoiona Bungeni; hizi *images* tumezitengeneza zaidi ya miaka 30 huko nyuma na tunaheshimika Kimataifa halafu mnamchukua Mbunge mnamfungia korokoroni kimzaha tu! Mama anafariki kimzaha tu kwa sababu tu mtu anatafuta kupandishwa cheo amkamate Mbunge kwa kutumia mfumo huu wa sheria!

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Watanzania 2020 tupeni hii nchi sisi CHADEMA twende tukafumue huu mfumo wa sheria na utoaji haki ambao unaonea watu na kukandamiza Watanzania. Kwa muda mrefu sana sasa mmekuwa mnafanya hivi, ingawa Awamu ya Tano imevuka mipaka. Unamfunga Mbunge wa Mbeya Mjini aliyechaguliwa kwa kura nyingi kuliko Wabunge wote katika Bunge la Jamhuri ya Muungano? Unamchukua unakwenda kumfunga ndani kihuni! Kweli! Halafu mnasema tuongelee tu bajeti, hela nini. Sawa hampati hela kama ambavyo Wizara nyingine hazipati hela kwa sababu fedha hakuna, lakini siyo huu uonevu wa kubambikia watu kesi tu ovyo ovyo bila sababu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hakuna Muswada wa Mbunge unao-*proceed,* yote inakwama; ukijaribu kuleta Muswada inakwama, inayoleta ni Serikali tu; sasa basi, Serikali ilete Muswada tuweke sheria hapa ili kuondoa haya mambo ya maagizo kutoka juu. Tuweke sheria Rais yeyote wa nchi hii aweze kushtakiwa Mahakamani kwa makosa atakayoyafanya akiwa ofisini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maana yake ni nini? Akifanya maamuzi ya kutia hasara nchi, Bunge halijajadili mpango fulani yeye akasema kifanyike hiki, huko baadaye ikiparanganyika kama ilivyoparanganyika Gbadolite ya Mobutu; kwa kutoa amri jenga Uwanja wa Kimataifa, jenga Ikulu Gbadolite, halafu baadaye unaondoka inakuwa hasara tupu, nyumba ya popo. Kama hili nilishawahi kusema. Akifanya maamuzi ya hivyo, iwe inawezekana kumpeleka

Mahakamani kwa kutia hasara kwa sababu zile fedha hajatoa mfukoni kufanya hiyo miradi, ni fedha za wananchi, ni fedha za nchi.

Mheshimiwa Spika, akifanya maamuzi yatakayoleta maafa kwa binadamu, yatakayosababisha vifo, ni lazima ifike siku awe *accountable* Mahakamani kwa maamuzi aliyoyafanya na kusababisha maafa ya binadamu na kusababisha vifo kwa namna yoyote ile akiwa katika ofisi yake. Isitakiwe kwamba Rais eti awe juu ya sheria. Halafu mnasema oh, hizi sheria ziko hata Marekani!

Mheshimiwa Spika, wewe unamweka mtu miaka mitano, miaka sita analegea kabisa halafu unamwambia njoo nikutoe, lete shilingi bilioni moja, shilingi bilioni mbili! Hata nyumbani familia itamwambia baba toa tu, si tuna tano, wewe toa. Hata kama iko hiyo hiyo wewe toa, tuuze vitu lakini bora uje huku tuendelee kukutibu hicho kisukari na presha kuliko uendelee kukaa huko jela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu ninyi eti mnasema sisi tunaogopa uchaguzi, sijui hatutatoboa mwaka huu, ninyi! Hivi mamilionea wazalendo wangapi wamekufa kwa *stress* nchi hii chini ya utawla huu? Mamilionea wangapi? Waliajiri watu wangapi? Familia zao, watoto wao, wafanyakazi wao, *organizations* zao, zitawapa kura ninyi? Labda mtegemee kugudua.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hamtaki Tume Huru kwa sababu mnajua kwenye Tume Huru ninyi kati yenu hapa mkirudi sita, saba, sijui ni nani simwoni, labda Mheshimiwa Balozi Mahiga mstaarabu kama atagombea. Siyo Iringa Mjini lakini mzee, Iringa Mjini hautatoboa, wasikuchuuze mzee. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Sugu ukisema namna hiyo maana yake unasema hata Spika hawezi kurudi. Sasa hii unakuwa unavunja kanuni! *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Aah, ujitahidi katika nane, kama hivyo ulivyojitahidi, umetulia kwenye kiti, huniingilii, wananchi wanakuangalia wanasema labda tumfikirie na Spika, anaonekana ameanza kubadilika. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbeya!

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, Mbeya ndiyo kabisa kabisa, hicho kitu hakuna. Nashukuru hata ninyi Serikali, Chama cha Mapinduzi, *system,* wote mnajua kama mkija kuleta mchezo Mbeya ndiyo *civil obedience* itaanzia pale. Utapigwa mtiti pale Mbeya kama ambavyo hamjawahi kuona katika ardhi ya Afrika Kusini mwa Janga la Sahara. Utapigwa mtiti pale utaambukiza Makambako. Ukiambukiza Makambako unaambukiza Mafinga; ukiambukiza Mafinga, wamelidaka sijui Morogoro, Arusha, Ikulu itakuwa ndogo, mtatafuta njia ya Joseph Momoh. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana lakini naomba sana Watanzania *enough is enough,* tupeni hii nchi tukafumue mfumo wa sheria na utoaji haki kwa sababu hii ndiyo *pillar* ya uonevu katika nchi hii. Ukifanya kitu kidogo kesi, nenda ndani; sijui umefanya nini, nitakufunga.

Mheshimiwa Spika, kama kule Mbeya sasa hivi, mmechukua Madiwani lakini mmeshindwa kupata Meya. Mna *majority* lakini Meya bado wa CHADEMA. *Ask how? That is how we do in* Mbeya. Siyo mchezo mchezo! Wale jamaa mliowanunua walichobaki kufanya sasa hivi, ukikutana naye mtaani hata ukimwangalia hivi utaona anakimbilia Polisi, fulani kanitishia kuniua, he! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, Balozi Mahiga wewe ni *international figure,* unajua mifumo ya sheria duniani inavyofanya kazi, hebu mshauri *DPP* atulize wenge. Yeye anatoka *DPP* anakuja kusema, anamhukumu Mheshimiwa Lema kwenye *Press,* kesi haijaenda hata Mahakamani! Mheshimiwa Lema kakamatwa Singida, kesi haijaenda hata Mahakamani anaitisha *Press* anasema Serikali inajua itakachomfanya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ni kengele ya pili. Nakushukuru sana.

Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, yupo? Jacqueline! Hayupo eeh! Basi kama hayupo tunaendelea na Mheshimiwa Ngeleja, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii. Ninaunga na wenzangu kuunga mkono hoja kama vile ambavyo wenzangu waliozungumza kabla yangu walivyoiunga mkono hoja ya Serikali. Nafanya hivi kwa sababu ya kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Mahiga, Waziri, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro; Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote katika mamlaka zote zilizo katika Wizara hii ya Katiba na Sheria.

**MBUNGE FULANI:** Sio Dkt. Ndumbaro.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, samahani, nafahamu kwamba sio Dkt. Ndumbaro. Ahsante kwa kunisahihisha.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme na niwakumbushe wenzangu Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania kwa ujumla, unapozungumzia habari ya sheria maana yake ni kwamba unazungumzia mwongozo katika maisha katika nyanja zozote katika jamii yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili mfumo wa dunia umetengeneza namna ya kutekeleza majukumu yake mbalimali; na moja ya mambo ambayo yamekuwa yakizungumzwa sana duniani ni kuheshimu ama kutii sheria ili mambo yaende mengine yote ambayo jamii inategemea kuendeleza shughuli zake ama ustawi wake kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, sasa leo tuko hapa Bungeni tunajadili Mapendekezo ya Makadirio ya Fedha kwa ajili ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria. Mojawapo ya mambo makubwa kabisa ambayo tunayazungumzia ni uimarishaji wa taasisi zetu zinazosimamia haki, lakini pia tunafahamu kwamba haki inaendana na wajibu.

Mheshimiwa Spika, nataka niwatahadharishe wenzangu, tunapozungumzia eneo hili tuwe makini sana; tujiepushe sana kuwataja watu kwa majina ama kwa nafasi zao kwa sababu ya *emotions* ama hisia zetu tulizonazo. Katika utendaji wote hatuwezi kukosa kasoro ama upungufu na ndiyo maana kuna mifumo ya kusawazisha kasoro zinazojitokeza katika shughuli ama katika taratibu zetu tulizojiwekea katika kuendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, siyo nataka kuwatetea, lakini naomba wenzangu tuwaheshimu sana viongozi wanaoongoza mamlaka ama taasisi mbalimbali za nchi yetu wakiwemo viongozi wetu kutoka Mahakama; Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi, pamoja na Majaji wengine. Tuwaheshimu sana viongozi kama *DPP,* Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Viongozi wa Tume mbalimbali kwa sababu kwao wana jukumu la ku-*balance equation* wanapokuwa wanatenda majukumu yao kuhakikisha kwamba haki inatendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumeweka mfumo, mahali ambapo kama itatokea kwenye ngazi fulani jambo fulani halikuamuliwa vizuri ama linaonekana kuna kasoro, basi ipo mamlaka ya *excretion,* ndiyo maana tumeweka mfumo wa kukata rufaa. Sasa haiwezekani ikitokea kwamba maamuzi fulani yalifanywa katika ngazi fulani, itakapotokea kwamba yanarekebishwa kwenye ngazi ya juu zaidi ya hiyo, tuanze kuwalaumu walio ngazi ya chini. Tukifanya hivyo tutasababisha mgogoro mkubwa sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naliomba Bunge lako Tukufu na Watanzania tuendelee kuziheshimu taratibu tulizonazo kwa sababu pia yapo mambo mengi bila kujali tofauti zetu za itikadi za kisiasa na hata tofauti zetu katika

mambo mbalimbali ambavyo mamlaka hizi, taasisi hizi ambazo zinasimamia haki zilivyotusaidia sisi binafsi lakini pia zilivyosaidia Taifa.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunazungumzia kuiunga mkono Wizara ya Katiba na Sheria kwa sababu ya mambo mengi wanayofanya. Moja tumeboresha mfumo wa uendeshaji wa kesi za jinai katika nchi yetu, lakini hata mfumo wa kesi za *murder,* kesi dawa, mashauri haya ya kawaida ya kudaiana ambayo sio ya kijinai. Yote hiyo ni kwa sababu, tunataka tufikie lengo tulilolikusudia la kutoa haki bila kuwakwaza, lakini bila kuwaumiza ambao wanaingia katika mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo jingine kwa nini tunaiunga mkono bajeti hii, hivi karibuni tumepitisha Sheria ya Usuluhishi, sheria iliyokuwepo ina zaidi ya miaka 70. Katika hali ya kawaida kama hujakumbwa na migogoro yawezekana ukaliona ni jambo dogo sana, lakini nataka nikumbushe Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla; sheria tuliyopitisha hii ya usuluhishi ya mwaka 2020 ina mambo mengi sana ambayo sisi yanarahisisha uendeshaji na utatuzi wa migogoro ambayo inatukumba kama Taifa. Kwa hiyo, ni mambo ya kuisifu Serikali na kuipongeza, lakini kulipongeza Bunge lako Tukufu kwa namna ambavyo umesimamia shughuli hii ikafanyika kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo kubwa ambalo linanishawishi tuunge mkono bajeti hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Wanasema wanaandaa Sera ya Taifa ya Sheria, ni jambo mahususi kwa sababu, hizi sheria ambazo tunazilaamikia, akiwemo Msemaji aliyenitangulia Mheshimiwa Sugu hapa ni kwamba, kwa sera hii tunayokwenda kuitunga sasa na kwa sababu, sera ndio muongozo mkuu kwa sheria kuu zitakazokwenda kutungwa, sheria wezeshi maana yake ni kwamba, hata kasoro ambazo leo tunazihisi kwamba, zimo kwenye sera hiyo itakuwa ndiyo fursa ama daraja la kwenda kuziboresha sheria ambazo zitatuongoza katika nchi hii. Ndio maana nikasema ni muhimu sana kuunga mkono Serikali kwa haya mazuri inayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku mbili zilizopita nchi tajiri duniani zimetoa ahueni kwa nchi masikini zilizokopa katika mataifa haya makubwa na taasisi kubwa za fedha duniani. Zimetoa ahueni ya miezi kadhaa, wamesema kuanzia tarehe 01 Mei, hadi mwishoni mwa mwaka huu madeni yote ambayo nchi hizi zinadaiwa wanasema yasilipwe kwanza, ili tuzielekeze nguvu zetu kwenye utatuzi wa janga hili la corona.

Mheshimiwa Spika, ninacholiomba Bunge lako Tukufu kwa kushauriwa na Serikali, na ninazungumza katika *context* ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa msingi kwamba, madeni haya ya nje ambayo tunalipa sisi nchi na kwa taarifa ambazo ninazo ninaambiwa kwamba, kwa mwaka tunalipa karibu trilioni nne inawezekana wataalam wa Serikali wataweza kunisahihisha, lakini ninachotaka kusisitiza ni kwamba, madeni haya tunayolipa yote yana msingi wake wa kisheria kwa nini yamelipwa na kwa nini mikopo ilichukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ninaliweka hapa ombo langu, ushauri wangu kwako Mezani tuone sisi kama Bunge lako Tukufu pamoja na Serikali tunashaurianaje kwa kipindi hiki ambacho ulipwaji wa deni hilo umesitishwa kwa miezi hii sita au saba? Je, tuiache Serikali iendelee na utaratibu wake wa kawaida? Ama tulitafutie fursa ya kulizungumza hili jambo kwa upana wake kupitia utaratibu wa azimio? Tutafakari vizuri, tuishauri vizuri Serikali namna ambavyo tutaji-*position* vizuri kimkakati namna ya kutumia hii ahueni ya kutolipa ili deni la kwetu la nje ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri kwamba, huko tunakoelekea kwenye siku zijazo, Mungu ajalie kwamba, Bunge liendelee tutafute siku tulijadili. Hili ni jambo kubwa ambalo tunahitaji kuisaidia Serikali kuchanga mawazo na sisi kama wawakilishi wa wananchi nadhani itakuwa ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hilo nilikuwa naomba Benki Kuu itumie mamlaka yake kama benki mama izielekeze sasa benki nyingine ambazo zinatoa mikopo kwa Watanzania wa kada zote wa chini na wa juu na wa kati

kuhakikisha kwamba, na sisi hapa Tanzania tunatafsiri hiyo ahueni iliyotolewa na nchi tajiri kwa mataifa masikini, lakini pia sisi benki zetu za hapa nchini na zenyewe ziwe na utaratibu uleule zisaidie kupunguza hii kadhia ya kuweza kulipa, kulazimisha ama wadaiwa kama wajibu wao, kulipa mikopo yao kwa kila mwezi kwa kipindi cha miezi saba hii kama ambavyo hawa matajiri walivyozipa ahueni hizi nchi masikini.

**SPIKA:** Kwa hilo Mheshimiwa Ngeleja katika kukubaliana nawe niwaombe Kamati ya Bajeti pamoja na Serikali, kwa maana ya Wizara ya Fedha, hebu mliangalie hilo na baadaye mje mtushauri namna gani ya kuendananalo, endelea tu Mheshimiwa Ngeleja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nakushukuru sana. Nadhani litakuwa ni jambo la manufaa sana kwa kauli yako huu ni muongozo mahususi kutoka kwenye Bunge lako Tukufu, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo jingine tuko katika kipindi mahususi ambacho kinahitaji maamuzi mahususi. Moja nafahamu kama nchi yetu sisi tunavyoiendesha tumekuwa katika baadhi ya maeneo tunaachia mambo yetu yajiendeshe kwa utaratibu wa *free market.* Tuna taratibu zetu zina-*regulate* mambo fulani, lakini kuna mambo tunaachia yajiendeshe yenyewe, lakini kuna mazingira mahususi Serikali imefanya *intervation;* ninazungumzia kupanda kwa bei ya bidhaa ya sukari na bidhaa nyingine. Sasa tuko katikati ya corona, lakini pia tunaingia kwenye mwezi mtukufu wa ramadhani. Nilikuwa naomba, ninamshukuru sana nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Bashungwa, ameshatoa muongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika mazingira haya kama ambavyo tunasisitiza Serikali ifanye *intervation* kwenye suala la ahueni iliyotolewa na nchi tajiri, ninaomba katika hili pia Serikali iongeze nguvu kusimamia hili, watakaobainika wachukuliwe hatua kali na ngumu zaidi. La mwisho ni ushauri kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kama Taifa tunahitaji sana maboresho ya kuwa na utamaduni wa kuheshimu sheria tunazojiwekea sisi kama Taifa, lakini pia na utamaduni wa kuheshimu maelekezo yanayotolewa na viongozi wetu, ukiwemo Mheshimiwa Spika wewe na viongozi wengine wakuu wa mihimili. Ninazungumzia kuheshimu maelekezo ynayotolewa na Serikali kwenye janga la corona.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, tutaweka *quaranteen,* tutatunga sheria, tutapiga-*lock down,* lakini jambo mahususi kabisa ni uwajibikaji wa kila mmoja miongoni mwetu sisi Watanzania. Tusipokuwa na utamaduni wa kusikiliza Serikali inasemaje, Mheshimiwa Waziri Mkuu anafanya kazi kubwa sana, Mheshimiwa Waziri Ummy wamefanya kazi kubwa sana pamoja na Serikali nzima chini ya Mheshimiwa Rais Dkt John Pombe joseph Magufuli, kutoa maelekezo tu haitoshi kama sisi Watanzania hatutakuwa na ule utamaduni wa kuheshimu maelekezo haya. Tunaona kwa nchi ambazo zinaheshimu maelekezo yanayotolewa na wataalam kupitia Serikali, tunaona kulikabili hili janga manufaa yake tunaanza kuyaona.

Mheshimiwa Spika, mfano wa nchi ya *South Korea,* mnafahamu Korea Kusini ni mojawapo ya nchi ambazo nadhani haziku-*rush* kwenye *lock down,* lakini wananchi wale wa *South Korea* wana utamaduni, wa Korea Kusini, wana utamaduni wa kuheshimu taratibu walizojiwekea na matokeo yake wamefanikiwa kwa kiasi fulani.

Sasa ombi langu kwa Watanzania Serikali itafanya, Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli amefanya jambo kubwa, ametoa muongozo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri kwa ujumla, Serikali kwa ujumla, lakini Watanzania tuna jukumu la kufanya...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:**...tuna jambo la kufanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, tunakabiliana na hili tatizo. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, tunakushukuru sana kwa mchango wako. Sasa nimuite Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Sabrina Sungura.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kunipa nafasi nichangie Wizara ya Sheria na Katiba. Kwanza nianze kwa kumshukuru sana na kumpongeza Waziri Dkt. Mahiga, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Prof. Sifuni Mchome, Naibu Katibu Mkuu, *DPP* na wote Wizarani kwa kazi kubwa wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilitaka nianze kwa kusema unayoyaona leo yanatokea Wizara ya Sheria kwa kweli, lazima kama ninataka kuwakumbusha kidogo wenzangu, toka Awamu ya Tano imeingia madarakani Wizara ya Sheria alianza pale Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, akatoka Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe akaja Mheshimiwa Prof. Kabudi na sasa Mheshimiwa Dkt. Mahiga. Kama unaona majengo haya ya Mahakama kwa kweli, Mawaziri wote watatu wameshiriki vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Kigoma sisi tumejengewa Mahakama Kuu na tumejengewa nyumba mbili za majaji, *state of the art,* kwa kweli, nawapongeza sana Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayofanya. Napongeza Mfuko wa Mahakama, nampongeza Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Jaji Mkuu na Jaji Kiongozi kwa kazi kubwa wanayofanya. Lakini mwisho wa siku tukubaliane Awamu ya Tano imefanya kazi kubwa sana kwa ajili ya Mahakama Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nitamsema Mheshimiwa Profesa Kabudi, nakumbuka mambo makubwa amefanya, moja ni kuleta *Mobile Court* ambayo nia yake ilikuwa ni kupunguza msongamano hasa kwenye Mahakama za Mwanzo. Lakini la pili ni sheria zile tatu za kulinda maliasili ya Tanzania, ninayo hakika watakaokuja kuandika historia ya Tanzania Mheshimiwa Profesa Kabudi historia itakutendea haki kwa kazi kubwa uliyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini leo nataka niongee jambo moja tu...

**SPIKA:** Mheshimiwa Serukamba yote hayo rafiki zangu wapinzani hawaoni hata moja. Endelea Mheshimiwa!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Tanzania Rais Dkt. Magufuli mwaka jana alikwenda Butimba, alivyokwenda Butimba pale alisononeka sana alivyokuta hali ya wafungwa na hali ya magereza kwa ujumla. Kusononeka kwake akaamua kufanya maamuzi akaongeza fedha magereza, akaongeza baadhi ya kujenga majengo, lakini akafanya jambo kubwa la kihistoria akatoa msamaha kwa wafungwa elfu tano, *unprecedented,* haijawahi kutokea toka nchi yetu imepata uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini alifanya vile? Kwasababu, aliona uchungu na makadhia wanayokumbananayo watu wetu wa magereza pale magerezani. Rais alifanya hayo katika mazingira ya kuona shida zilizokuwepo na ndio maana Rais mwaka huu alipokwenda Siku ya Sheria alisema, namnukuu alisema kwamba, anawaomba wanaofanya upelelezi wahakikishe wanampeleka mtu Mahakamani baada ya kuwa upelelezi umetimia. Na akatumia neno akasema, lakini kuna watu mnawapeleka watu Mahakamani upelelezi bado, anasema kuna watu wengine watapata tabu kuiona Pepo ya Mbinguni, maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, alikuwa anatukumbusha sisi tunaofanya maamuzi tutende haki. Tupeleke watu Mahakamani baada ya kumaliza ushahidi wote. Sasa alisema hayo katika mazingira ambayo hatuna corona; leo Tanzania tuna tatizo la corona, dunia ina tatizo la corona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe umefanya maamuzi ili kuhakikisha tunapambana na corona. Wabunge tunaanza saa nane *social distancing,* tunagawanyika, tuna *sanitizers,* tumetekeleza wajibu wetu. Natamani na wananchi kwa ujumla wao kila mtu atekeleze wajibu wake kulinda familia yake, kulinda watu wa ofisini kwake, kulinda Watanzania

wenzetu kwa sababu, hili ni letu wote, hili sio la Serikali. Ni tatizo, ni janga ni changamoto kubwa tunayotakiwa kupambana nayo kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo nimekuja na ushauri, nimuombe Waziri wa Katiba, naomba mukae Wizarani na watu wa *DPP* na Wizara yako ishiriki kupambana na ugonjwa wa corona; kwa nini nasema haya? Najaribu kutafakari, leo Dar-es-Salaam tumetangaziwa kuna kesi 147, mana yake kila kukicha zinakuwa. Hebu fikirieni kesho ikitokea akatokea mfungwa mmoja au wawili wakapata corona gerezani, hali yetu itakuwa mbaya sana. Na haitaishia kwa wafungwa, kuna askari magereza, kuna askari wa kawaida na familia zao, watu wenyewe wa magereza, lakini mbaya zaidi mahakimu wetu na majaji wetu kule Mahakamani na Wanasheria. *This is very unprecedented situation,* lazima na tuamue *unprecedented decision,* ni zipi? Tutafute namna kupunguza misongamano kwenye magereza yetu, *how? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kesi zile ndogondogo, kwa nini watu wafungwe waende gerezani? Tuwape kazi za kufanya barabarani za kusafisha barabara, kesi zile ndogondogo kupunguza watu wasiende kule magerezani; kuna watu wameshakaa magerezani 75% ya vifungo, tufanye utaratibu watoke, lakini sio hilo tu, kuna watu wana kesi zao ambazo upelelezi haujakamilika, wako kule magerezani wengine wamekaa mwaka mmoja, miaka miwili, miaka mitatu, miaka minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamesema wale *DPP* atumie sheria yake namba 91 afute kesi zile, tukimaliza janga la corona akiamua atawarudisha magerezani au mkae tutafute kwa sababu, hii ni *special circumstance,* ikiwezekana tuone namna wale watu ambao walitakiwa wapate...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, ndio, Mheshimiwa Esther.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nilikuwa nataka tu nimpe Taarifa Mheshimiwa Peter Serukamba kwa wazo lake zuri, nimpe tu Taarifa kwamba, mahabusu kwenye magereza yetu zaidi ya 70% kama sio 80% ni mahabusu ambao kesi zao nyingi zinadhaminika. YaAni ili tuweze kujiepusha na hii corona, nakupa tu taarifa, katika mchango wako washauri Serikali sasa waweze kuwaachia wale mahabusu ambao kesi zao zinadhaminika waendelee na kesi wakiwa majumbani, ni hiyo tu Taarifa ambayo nakupa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Serukamba endelea!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mimi naiomba Serikali ikatafakari hili jambo; hili ni jambo la kwenda kutafakari, wakae vyombo vyote waone namna ambavyo na Wizara ya Sheria na Katiba itashiriki kwenye vita hii ya corona, vita hii ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii Kenya wameanza kupunguza magereza yao...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, iko upande gani Taarifa hii?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Musukuma.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, napenda kumpa Taarifa mchangiaji kwa wazo lake zuri. Na ningependa kuomba Ofisi ya *DPP* ikachukua mfano wa Gereza la Geita ambalo *capacity* yake ni

mahabusu na wafungwa 141, lakini tunavyozungumza wako zaidi ya 500. Na 85% ya kesi zilizoko pale nyingi ni kuingia kwa jinai, vijana wetu wamekutwa maeneo ya mgodi na wengine maeneo ya ziwa ambako kumepigwa marufuku. Sasa ni vizuri angechukua *sample* wale vijana tuko tayari kuwadhamini ili tujikinge na hili janga la corona, ni Taarifa hiyo tu.

**SPIKA:** Ahsante sana, hali ndio hiyo, kila mtu.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, na hii ndio hali halisi. Na ndio maana nawaomba wenzangu wa Serikali tukalitafakari ili tuone namna ambavyo na Wizara hii itashiriki kwa sababu, jambo hili sio la Wizara ya Afya, sio la Wizara ya Waziri Mkuu, sio jambo la Fedha ni jambo la Taifa ni jambo letu wote lazima tushiriki kupambana nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nichuku nafasi hii kwa kweli, kumpongeza sana Mheshimiwa Rais anavyoenenda kwenye jambo la corona. Rais limetokea tatizo, haja-*panick,* hajatupanikisha kama Taifa, ametulia kuliko marais wengine wote ambao wame-*panick.* Matokeo yake, na nasema jamani, atakayekuja kuandika historia ya dunia hii kwa sababu ya ugonjwa wa corona, Rais Dkt. Magufuli atakuwa *vindicated* kwa jinsi alivyo-*act. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii duniani, Marekani Taifa kubwa wanajadili ku-*reopen economy* kwa sababu, *imagine* kwa Taifa letu tunge-*lock down* leo tungekuwa na tatizo jingine kubwa zaidi ambalo ni la umasikini, hali ingekuwa mbaya zaidi. *So* naomba tumsaidie Mheshimiwa Rais na sisi watu wa Wizara ya Sheria, ili tuweze kupunguza tatizo kwenye magereza yetu. Na ninaamini leo hii Kenya wanafanya hivyo, Uturuki wamefanya hivyo, Marekani wamefanya hivyo, sisi ni nani? Lazima tushiriki kwenye vita hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema ninaamini Mheshimiwa Dkt Mahiga ni kati ya Watanzania wachache ambao wanaijua dunia sana. Nikuombe Mheshimiwa Dkt. Mahiga usimamie jambo hili, ili tuweze kufanya hii kazi ni kazi nzuri, *it is a noble job. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na niweze kuchangia, lakini nimalizie kwa kuwapongeza sana kwa kazi kubwa mnayofanya. Asanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Peter Serukamba. Nimeshakutaja Mheshimiwa Sabrina Sungura.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii adhimu. Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Pia, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Salome Makamba kwa ushirikiano ambao amenipa katika kuandaa hotuba yetu pia na kushauriana mambo mbalimbali yanayohusiana na Wizara yetu kivuli ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nina mambo kadhaa na mimi ya kuchangia kwenye Wizara hii na ningependa moja kwa moja nianze na suala zima la Katiba kwa maana ya marekebisho au mabadiliko ya Katiba na Sheria mbalimbali za nchi ambazo zimekuwa ni kilio cha watu wetu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha kuhusiana na Tume ya Uchaguzi ambayo inaundwa kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 74. Tume hii Mwenyekiti wake, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wamekuwa ni wateule ambao wanateuliwa na Mheshimiwa Rais.

Kwa mujibu wa Katiba sisi sote tunajua kwamba Mheshimiwa Rais wetu wa Rais wa Tanzania ni Mheshimiwa Rais lakini pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, lakini pia ndiyo kapewa mamlaka ya kuteua Wenyekiti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira hayo kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali na vyama mbalimbali vya siasa vikiona kwamba wanakosa *fair game* ya kuundwa kwa Tume hii ya Uchaguzi kwa sababu anayeunda Tume tayari na yeye ana upande wa chama cha siasa. Kwa hiyo basi ilikuwa ni mapendekezo kama itaipendeza Serikali walete marekebisho ya Kikatiba ili basi wadau wote wa siasa kwa maana ya vyama vya siasa na viongozi wake na washiriki wake waweze kuhusishwa katika mchakato mzima wa kuchagua viongozi wa kuendesha Tume yetu ya Uchaguzi lakini pia na wajumbe wao ili tuweze kupata Tume Huru itakayoendesha mambo kwa usawa na watu wote watakuwa na amani.

Mheshimiwa Spika, licha ya hiyo, bado Sheria yetu ya Uchaguzi imewaweka Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa, Miji na Halmashauri mbalimbali kama wasimamizi wa chaguzi hizi. Wakurugenzi hawa na wenyewe wamekuwa ni wateule wa Mheshimiwa Rais, hivyo basi inasababisha wakati mwingine na wao kuwa na *interest* na watu waliowateua, lakini pia tumeona Wakurugenzi kadhaa wakitangaza nia katika maeneo mbalimbali na wenyewe wanataka Ubunge, kitu ambacho kinaweza kikasababisha na wao wakaanza kuhujumu kazi za Wabunge wa maeneo mbalimbali kwa sababu na wao wana *interest* za kuwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo basi, ni mapendekezo ambayo ningependa kuiomba Serikali tuone ni namna gani tutaondoa Wakurugenzi kwenye nafasi hizi za kusimamia chaguzi zetu na kutangaza Wabunge kwa sababu na wao wana *interest* na eneo hili na tayari wameanza figisu. Kuna Majimbo tumeyasikia huko Kanda za Juu Kusini, Mbeya na Iringa kuna Majimbo ambayo tayari *clips* za Wakurugenzi zimesikika zikienda kwenye Majimbo ya watu zikitaka na zenyewe nafasi za uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, tukiendelea kuwa na wasimamizi wa aina hii inawezekana kabisa Wabunge wengi, majimbo mbalimbali wakahujumiwa kwa sababu wanaotusimamia, wanaotutangaza na wao wana *interest* ya kuwa Wabunge.

Kwa hiyo napenda kulishauri Bunge na Serikali waone ni kwa jinsi gani tunaweza tukawatoa haa watu na tukaweka watu wengine ambao watakuwa ni mbadala ambao watatenda haki katika kusimamia chaguzi zetu na kutangaza Wabunge wetu ambao watagombea sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia tumeona sheria inatoa mamlaka kwa watumishi wengine wa Serikali kuchaguliwa kama wasaidizi wa usimamizi wa uchaguzi katika maeneo mbalimbali. Kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa tumeshuhudia watu wakiondoka na *form* maofisini, watu wakikimbia na *form* maofisini. Watu wanarudisha *form* za kugombea wanakuta ofisi imefungwa. Hili limekuwa kilio cha muda mrefu, kwa hiyo ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, tuhakikishe kabisa kwamba tunaweka matakwa ya kisheria ya kuwataka wasaidizi, wasimamizi wa uchaguzi waweze kukaa katika maeneo husika, waweze kutoa *form* kwa wakati na *form* zikirudishwa kwa wakati waweze kukutwa ofisini na waweze kupokea *form* hizo ili kutenda haki kwa Watanzania na wagombea wa nafasi mbalimbali za Udiwani, Ubunge na Urais katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye suala zima la mwenendo wa makosa ya jinai. Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wamechangia, tumeona sasa hivi tuna janga la *corona,* kuna watu wengi sana ambao wako mahubusu, kuna watu wengi sana ambao tayari wameshahukumiwa lakini sasa tukibadilisha sheria zetu za mwenendo wa makosa ya jinai kwa mfano, kwa makosa ambayo yana dhamana washtakiwa wasiweze kukamatwa mpaka pale ambapo upelelezi wa kesi zao utakuwa umekamilika. Hili litatusidia kupunguza mrundikano wa mahabusu na wafungwa magerezani na hivyo kutuokoa na janga hili la *corona*.

Mheshimiwa Spika, pia hata kwa kesi zile ambazo hazina dhamana, tunaweza tukaweka utaratibu kwamba ndani ya miezi sita angalau ziweze kuanza kusikilizwa na hili limefanyika na wenzetu sio mbali hapa Zanzibar tu katika sheria yao ya mwenendo wa makosa ya jinai. Tumeona

kabisa mwaka 2004, imeelezea ndani ya miezi sita inatakiwa shauri lianze kusikilizwa. Hii itatufanya tupunguze idadi ya mahabusu na kesi zetu pia ziweze kwenda kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kushauri katika Wizara hii suala ambalo lingeweza kuchukuliwa hatua na lingeweza kusaidia Wizara ni suala zima la hizi *committal proceeding*. Kumekuwa na kesi nyingi sana ambazo zinafanyika kwa kuanzia kwenye Mahakama kama za Mwanzo na kupita kama *committal proceeding* zikisubiri kwenda kuamuliwa katiak Mahakama zetu Kuu. Naiomba Serikali iweze kuweka mkakati na kubadilisha sheria kwamba hizi kesi zinavyopita kwenye Mahakama ya Mwanzo, Mahakama za chini basi Mahakimu wa Mahakama za chini waweze kuwa na uwezo wa kuangalia zile kesi kama kilichoandikwa kwenye kesi na *facts* zilizoko mle ndani zinafanana au wanaweza wakawaachia huru baada ya kuona kwamba ile kesi haina msingi wowote.

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza hivi namaanisha kuwa inawezekana kabisa kichwa cha habari cha kwenye kesi zetu ikawa mtu ameweka labda *money laundering* ama amewekewa *murder,* lakini ndani kwenye *facts* unakuta kwamba labda mtu ameshikwa ugoni. Kwa sababu ni *committal,* Hakimu wa chini hana mamlaka yoyote ya kusema kwamba hiki kitu kimekosewa, kirekebishwe na kadhalika anaichukua anai-*forward* moja kwa moja Mahakama Kuu suala ambalo linasababisha mrundikano mkubwa wa kesi kule. Hivyo basi ushauri wangu aidha, hizi *committal proceeding* zifutwe, na kama zitaendelea kubakia, basi uwekwe utaratibu ambao utawafanya Mahakimu wetu huku chini waweze kufanya *determination* ya zile kesi pale tu zinapopelekwa ama ziruhusu *pre hearing* ili waweze kuandaa mkakati ambao utasaidia kupunguza mrundikano wa kesi huko baadaye.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulichangia ni mwenendo wa shughuli za Mahakama katika kipindi hiki cha *corona*. Wabunge wengi wamegusia kwamba kuna mahabusu wengi, kuna hatari kwa askari magereza

wetu, kuna hatari kwa askari wetu ambao wanaenda kukamata watuhumiwa, tuna hatari kubwa ya Mawakili wetu ambao wanaenda kuwakilisha watu huko Mahakamani, kuna hatari kubwa ya Majaji wetu na wao kupata maambukizi.

Ningependa kujua mkakati wa Serikali dhidi ya kupambana na janga hili la *corona* katika sekta nzima ya usimamizi wa sheria kwa maana tunapoanzia huko polisi, tunapoenda mpaka Mahakamani, tunapokuja mpaka huku juu tuweze kujua ni kwa namna gani sasa Mahakama na Serikali itaweka fungu la fedha la kutosha ili angalau kwa Mahakama zetu zile ambazo zimekuwa na ufinyu wa nafasi, unakuta Mahakama ni finyu sana na watu ni wachache wanahitaji kupata huduma waweze kuhudumiwa bila kuweza kuathirika na suala hili. Au kwa kuwa Serikali sasa hivi inatumia mfumo wa mtandao, waweze kuangalia ni kwa namna gani TEHAMA inaweza ikanusuru hii jamii kutokana na janga la *corona* iweze kutumika kama mbadala kama hiki ambacho leo hii tunafanya hapa tukiwa Bungeni. Hiki kikifanyika kinaweza kikaleta matunda makubwa zaidi na tukaweza kupunguza ugonjwa huu wa corona.

Mheshimiwa Spika, pia niwakumbushe Watanzania kwamba ni wajibu wetu sasa kutumia nguvu zetu zote na maarifa pamoja na jitihada zote zinazofanywa na Serikali. Ni kipindi cha sisi kama Watanzania kumwomba Mungu sana mchana na usiku ili aweze kutupunguzia makali ya ugonjwa huu. Ni dhahiri kwamba kwa miundombinu ya kifedha, kiteknolojia na kwa namna yoyote ile hatuna ujanja mkubwa sana kupambana na janga hili. Kwa hiyo tuendelee kumwomba Mungu wetu, pia tufuate maagizo ambayo yametolewa ya kufunga na kusali kuombea Taifa ili tuweze kufika…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sabreena Sungura…

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kuchangia...

**SPIKA:** Tunakushukuru sana kwa mchango wako. Sasa kwa kifupi sana, Mheshimiwa Lema dakika tano na Mheshimiwa Najma dakika tano.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwenye mchango wangu wa dakika tano sitataka kuisema Mahakama, lakini naomba sana kiti chako na Bunge lielewe kwamba mapungufu yanayoonekana Mahakamani hayawezi kuongewa mahali popote isipokuwa ndani ya Bunge. Sasa kuna tabia inakuwa nzito sana kwwamba ukitaka kutaja mambo unayokutana nayo Mahakamani hasa sisi, mimi toka nimeingia kwenye siasa 2005 mpaka juzi Singida, nimeenda Polisi mara 169. Nahesabu na *wife* ananisaidia kuweka kumbukumbu, kwa hiyo nafahamu sana *issue* za Mahakama na imefika mahali ninaweza hata nikajitetea hata mwenyewe. Kwa hiyo tunapokuja kuwaambia kuhusu Mahakama, hatusemi kwa ajili ya *defense* zetu, kila mtu anahitaji Mahakama yenye *confidence,* Mahakama ambayo Majaji na Mahakimu watasimamia haki.

Mheshimiwa Spika, hii ni muhimu kupita kiasi. *Issue* yangu moja tu, kuna kesi yangu moja ilifutwa Arusha. Wakati nimekwenda Mahakamani saa tatu asubuhi sikuitwa, saa nne na nusu nikapigiwa simu na *RCO* na Mheshimiwa Waziri asikilize hii. Akaniambia njoo polisi, nikamuuliza kuna nini? Akaniambia hiyo kesi iliyofutwa hapo na kesi ilikuwa haijafutwa! Nikasema, ah, leo nafutiwa kesi? Nilipoingia Mahakamani nikafutiwa kesi, nilipotoka nje nikampigia simu *RCO* nikamuuliza kuna haja ya kunikamata? Akasema hapa, tunataka tukupeleke Mahakamani, nikamuuliza Mahakama gani? Akasema, nikamwambia tukutane Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, tumefika Mahakamani, ile kesi nikasomewa *charge sheet,* yaani nimeachiwa saa nne na nusu, saa tano tunakutana Mahakamani nasomewa kesi, maneno yale yale, hadi Hakimu akasema, eh, huyu ameachiwa hapo dakika 20 tu, nyie *State Attorney* mlikuwa

mmeshaandaa na *charge sheet?* Akasema, haya bwana tuendelee!

Mheshimiwa Spika, maana yake kulikuwa na mawasiliano kabla ya kusomewa hiyo *ruling* na Hakimu na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka pamoja na Ofisi ya Polisi. Sasa haya mambo sio ya Wapinzani. *Integrity* ya Mahakama ni kwa ajili ya nchi hii, Mahakama inapokosa *integrity,* kila mtu ataumia. Sasa wewe unaweza usiumie kwa sababu ni Waziri, unaweza usiumie kwa sababu ni Mzee Mkuchika ama ni Spika kwa sababu una *immunity,* shangazi ataenda Mahakamani, baba yako mdogo ataenda Mahakamani, *aunt* yako ataenda Mahakamani na kazi ya Bunge ni ku-*protect future* ya wanaokuja, sio sisi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana mbele ya safari na Mheshimiwa Sugu alisema kati ya nane wewe unaweza ukarudi. Mimi niombe tu Mungu kwa kweli usirudi, kwa sababu na wewe hunitakii mema Arusha, unanitumiaga *message* na naomba Mungu kabisa usirudi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niseme hivi, zimeongelewa hapa kesi za *money laundering* za uhujumu uchumi kwa kesi za uhujumu uchumi na utakatishaji fedha vilivyo, nakuhakikishia hakuna Mbunge ama Waziri hapa akimaliza Uwaziri ama Ubunge akaamua kutafutwa atakuwa sawa! Mimi nimekuta watu magereza wana kesi ya dola 1,200 amekaa jela miaka mitatu. Nimeenda kumsalimia mimi Mzee Kitilya, magereza kule Keko nimekuta mtu ana kesi ya uhujumu uchumi ya 860,000. Sasa hawa waliosemwa akina Tito, tusiongelee mwenendo wa kesi, wana *issue* ya milioni 17, unajiuliza mtu anakaaje ndani miezi mitano au sita kwa *matter* ya 17 million mwajiriwa na *organization* kubwa. Sasa wasipoweka mazingira ya *bail*, nini kinatokea? Ofisi ya *DPP,* inapiga! Mheshimiwa Mahiga, hakuna ofisi inakula fedha kama ofisi ya *DPP,* kwa sababu ukiweka mazingira ya *bail* maana yake kitakachotokea?

Mheshimiwa Spika, kitakachotokea ni kwamba watumishi katika ofisi zao watakuwa wanafanya kazi kufuata

haki. Kinachofanya watu watoe rushwa ni pale mtu anapotafuta dhamana kwa nguvu, lakini mkiweka makosa yote yakawa na dhamana; Uganda makosa yote yana dhamana mpaka *treason,* Mpinzani Mkuu wa Ugana ana kesi ya *treason* lakini yuko nje. Waweke makosa yote kuwa na dhamana, mtu anadaiwa bilioni mbili halafu wanasema ametakatisha fedha bilioni mbili, huku nje ana *property* ya bilioni 15; kwa nini wasizishikilie mali zake kama dhamana yeye wakamwacha nje wakaendelea na kesi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Dakika tano zimeisha Mheshimiwa Lema. Makosa yote yawe na dhamana? Ah! Yaani mtu amebaka binti yako Mheshimiwa Lema, apewe dhamana!

Mheshimiwa Najma, baada yake atafuata Mheshimiwa Profesa Kabudi na *AG* ajiandae.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa upande wangu binafsi pamoja na kwamba pongezi nyingi tumetoa kupitia Kamati, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mawaziri wote waliopita toka Awamu hii imeingia hadi kufikia sasa hivi Profesa Mahiga ambaye ndiyo Waziri wetu pamoja na watendaji wake wote.

Mimi nitazungumza machache sana, niweke sawa kwa faida ya Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kwa vile Kamati hii ya Katiba na Sheria, msingi wake mkuu ni Katiba na naomba nirudie tena kwa mara nyingine katika Bunge hili kwamba Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoundwa mwaka 1977 ni Katiba ambayo imebeba misingi imara ambayo inaweza kuliongoza Taifa letu hata miaka 100 ijayo. Hilo nasema na nataka niwaaminishe Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla kwa sababu yaliyomo humu yameweza kudumisha umoja, mshikamano na upendo wa Watanzania *plus* na hiyo amani na utulivu kwa muda wote wa zaidi ya miaka 40 ya kuundwa kwa Katiba hii. Hilo litoshe kuonesha kwamba hii ni Katiba bora na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais ameona sio kipaumbele kwa mara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo naunganisjha moja kwa moja jambo ambalo linazungumziwa na wenzetu sana kuhusu Tume Huru ya Uchaguzi. Kwa heshima zote naomba ninukuu au Ibara ya 74 (7) kwa uchache sana; kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake yaliyoainishwa katika Ibara hii, Tume ya Uchaguzi itakuwa ni Idara huru inayojitegemea. Kwa hiyo sasa wanachodai sio Tume Huru ya Uchaguzi, kama kuna upungufu ni katika utekelezaji na utekelezaji unapokuwa umekwenda sivyo sheria na taratibu zimewekwa na wenzetu wanazitumia. Wanapokuwa na malalamiko wanakwenda wanasikilizwa na wanafanikiwa. Sasa tatizo ni nini? Jina ama utekelezwaji wa Tume ya Uchaguzi. Wajue hivyo sasa, huo ndiyo ukweli, kwa hiyo anayetaka kukataa hayuko makini na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa narudi kwenye Katiba na Sheria kwenye mambo ambayo yametekelezwa mwaka huu, lakini pia nirudi kwenye miaka mitano ambayo tumeanza nayo toka Bunge hili limeanza, kwenye sehemu ya Mahakama. Wakati tunaingia Bungeni hapa 2015, Tanzania nzima ilikuwa na Mahakama ambazo hazizidi 100, kwenye 80 na kidogo. Leo ninavyozungumza kwenye taarifa hii, Tanzania ina Mahakama zaidi ya 300 ndani ya miaka minne na kidogo. Naamini kabisa tukimpa Mheshimiwa Rais ambaye ndiye msimamizi mkuu wa Serikali na Wizara zote, miaka mitano ijayo, malalamiko yetu Watanzania tutakuwa na Mahakama Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, hilo nawathibitishieni kwa sababu ikiwa ndani ya miaka minne tumeweza kwenda mpaka zaidi ya 300, zikiwemo Mahakama Kuu katika mikoa mikubwa ikiwemo Kigoma, Mara, Mbeya na mingine na Dodoma inakuja kujengwa Mahakama Kuu katika Makao Makuu ya nchi yetu, tena majengo na kila kitu mpaka michoro imeshawekwa, Watanzania tunataka nini? Kweli kuna changamoto na wote tunazijua, mirundikano ya kesi, kesi za *criminal* ambazo tunazijua zinatakiwa zisikae sana Mahakamani, hayo ndiyo ya kufanyiwa kazi na ndiyo tunatakiwa tushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nimalizie kwa kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge tuwe na shukrani na Watanzania wote tuwe na shukrani. Napenda kurudia maneno hayo kila ninapozungumza, shukrani ni neno dogo sana, ukisema neno moja tu shukrani! Lakini thamani yake ni kubwa sana na ndiyo maana hata Mwenyezi Mungu katuambia: Mkinishukuru nitawaongezeeni, nishukuruni niwaongezeeni.

Kwa hiyo sasa hata sisi wabunge tunapofanya wajibu wetu katika Majimbo yetu na maeneo yetu, tukipongezwa tunafurahi na tunakuwa *encouraged* na *motivated,* tunazidi kufanya vizuri. Kwa nini Mheshimiwa Rais asipongezwe kwa wajibu anaouchukua kwa Taifa hili? Kwa hiyo, nami kwa leo hii naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Mawaziri wake wote na Watendaji wake wote katika kipindi chote tulichofanya kazi. Yote yameonekana, sina haja ya kuyazungumza, mwenye macho haambiwi ona. Watanzania tuwe na shukrani ili Mwenyezi Mungu atuongezee. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Najma Giga, kwa kweli umeongea kwa niaba yetu wote kabisa. Tunakushukuru sana kwa maneno ya busara, maneno ambayo yanawakilisha mioyo yetu na wenzetu Serikali basi myapokee kwa mikono miwili maneno haya kwa sababu kwa kweli ndiyo yanawakilisha tulichonacho mioyoni mwetu. Tunawashukuru sana.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri na viongozi wote wa Katiba na Sheria, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya Katiba na Sheria na hasa kurudisha uwabikaji kazini iliopelekea ufanisi mkubwa hasa kwenye usimamizi wa kesi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, napendekeza kuboreshwa kwa miundombinu hasa Mahakama za Mwanzo kwa ajili ya afya na usalama wa watumishi na wateja wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali ijenge Mahakama ya Mwanzo ya Mbalizi ambayo imesongwa na shughuli za soko la Tarafani Mbalizi na pia jengo linalotumika linakumbwa na mafuriko. Napendekeza Serikali ijenge haraka kwenye eneo lililotengwa na kwa kuzingatia mahakama hii inahudumia wakazi zaidi ya 200,000.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalia kuboresha maslahi ya Wazee wa Mahakama ikiwemo kuongeza kiwango cha posho na hata hiyo kidogo ilipwe kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa mchango wangu kwenye hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nakupongeza wewe Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri pamoja na changamoto nyingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa Mahakama mbalimbali unaoendelea nchini tunaomba Wizara iangalie

Wilaya nyingine kama ya Muheza ambapo Wilaya haina Mahakama ya Wilaya rasmi, jengo linalotumiwa ni la Halmashauri wa Wilaya na halina hadhi. Tumekwishatenga eneo maalum kwa ujenzi wa Mahakama hiyo. Tunaomba suala hili lipewe umuhimu unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuiomba Wizara iweke mikakati maalum hususan kuweka vyombo vyenye teknolojia ya kisasa vya kufanya *recording* kwenye uendeshaji wa kesi zote za madai na jinai mahakamani. Uendeshaji wa kesi unaotumika wa kuandika kwa mkono kwa sasa ni wa kizamani na hauendani na teknolojia ya wakati huu. Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara walikwishaonyesha mfano lakini sielewi kwa nini hawaleti bajeti maalum kwa suala hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshwaji wa usikilizwaji wa kesi mbalimbali za jinai ningeshauri utaratibu wa *caseflow,* menejimenti zilizopo mikoani ziimarishwe na kuwezeshwa, naamini zinaweza kusaidia sana kupunguza urundikwaji wa kesi mbalimbali na upungufu wa mahabusu. Aidha, utaratibu wa *High Court Session* uangaliwe upya kwani unachelewesha sana usikilizwaji wa kesi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, suala la dhamana pia inabidi liangaliwe na kuhakikisha tunabakiza kesi chache ambazo hazina dhamana kupunguza msongamano magerezani.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri , Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Nawapongeza sana kwa mipango mizuri iliyowekwa ambayo imewezesha kupungua kwa mrundikano wa kesi mahakamani.

Mheshimiwa Spika, wote tunajua na kuamini kuwa Mahakama ni chombo cha kutoa haki. Lakini maeneo mengi nchini hayana mahakama au kama zipo ziko mbali sana na

wananchi wanashindwa kufikia huduma hizi. Je, ni lini Serikali itahakikisha kuwa huduma za mahakama zinasogezwa karibu na wananchi nchi nzima?

Pia majengo mengi ya mahakama ya mwanzo yamechakaa sana, hayana hadhi ya kuitwa mahakama. Napendekeza fedha zitengwe za kutosha ili mahakama za mwanzo kote nchini zijengwe au zikarabatiwe ili wananchi waweze kukifikia hiki chombo cha utoaji wa haki kirahisi.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa tumepaza sauti zetu, hasa sisi wanawake tukiomba Sheria ya Ndoa Tanzania irekebishwe ili umri wa mtoto wa kike kuolewa usiwe chini ya miaka 18. Huyu mtoto kwa umri chini ya miaka 18 anapaswa kuwa shule, iweje tena kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa aruhusiwe au kwa ridhaa ya mzazi, kuolewa kwa umri mdogo wa miaka chini ya miaka 18? Sheria hii imepitwa na wakati. Ni lini sheria hii itafanyiwa kazi na Tume ya Kurekebisha Sheria ili hatimaye irekebishwe?

Mheshimiwa Spika, katika Afrika Mashariki takwimu zinaonesha kuwa Tanzania ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni kubwa na zinazidi kuongezeka. Wanawake wanatekwa, wanapigwa, wanabakwa, wanafukuzwa, wananyang'anywa mali na kuuawa, watoto wanatumikishwa, wanalawitiwa na kadhalika, je, kuna mpango gani wa makusudi tofauti na *business as usual* wa kuhakikisha tunaliondoa hili tatizo kubwa la unyanyasaji wa wanawake na watoto?

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, uteuzi wa Wajumbe wa Mabaraza ya Kata na uendeshaji wake una matatizo makubwa na hali hiyo imesababisha ukosekanaji wa haki kwenye maeneo mengi. Nashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, dhamana ya Mabaraza ya Usuluhishi ya Kata ambayo hujigeuza kuwa Mabaraza ya Usuluhishi ya Ardhi yanapokuja masuala yanayohusu ardhi iondolewe TAMISEMI badala yake kiuweledi wa tasnia husika ya sheria irejeshwe kwenye Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, sheria iliyoanzisha Mabaraza ya Kata ifanyiwe marekebisho makubwa ili iendane na mahitaji ya sasa kwa kuzingatia pendekezo hilo hapo juu hasa hasa ukweli kwamba sheria hiyo iliandaliwa katika mazingira ya chama kimoja.

Sasa katika kipindi hiki cha vyama vingi na kwa kuwa uendeshwaji wake unasimamiwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kumekuwa na malalamiko mengi ya kuharibiwa haki kupitia misimamo ya kisiasa ya viongozi kwenye maeneo mengi na kusababisha haki kutopatikana kwa wengi kwa sababu tu ya kutofautiana mirengo ya kisiasa. Msilipuuzie suala hili ndugu zangu. Marekebisho makubwa sana yanahitajika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kutuongozea Bunge kwa umahiri mkubwa. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kututoa matongotongo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Augustino Mahiga, Waziri wa Katiba na Sheria kwa kumsaidia vizuri sana Mheshimiwa Rais katika eneo hili la Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri aanzishe mchakato wa kufanya marekebisho ya Katiba hasa kifungu kinachoweka ukomo wa mihula miwili, kifungu hiki kirekebishwe kwa kumruhusu Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli pekee kuendelea kutuongoza hadi akamilishe miradi ya kielelezo aliyoianzisha hususan ujenzi wa mtandao wa reli ya *SGR* ikiwa ni pamoja na inayotoka Mtwara hadi Liganga kupitia Namtumbo. Tafadhali fanya hivyo ili miradi hiyo ikaamilike chini ya usimamizi wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia na naomba kuwasilisha.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba.

Mheshimiwa Spika, naomba kukumbushia kwa mara nyingine maombi kwa mambo matatu; maombi hayo kwa kweli Serikali yangu imekuwa hainitendei haki mimi na wananchi wa Wilaya ya Kwimba. Tangu enzi za Waziri Mama Nagu Serikali imekuwa ikinipa ahadi kila Bunge la bajeti.

Mheshimiwa Spika, ahadi ni hizo ni zifuatazo; kwanza ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo kwa Wilaya ya Kwimba; pili, upungufu wa wafanyakazi katika Mahakama za Mwanzo zote na Mahakama ya Wilaya ya Kwimba na tatu Wilaya ya Kwimba ina majimbo mawili, kata 30, vijiji zaidi ya 130 bila kuwa na usafiri wenye uhakika kwa mahakimu kufika katika Mahakama kutokana na jiografia ya Wilaya ya Kwimba (Jaji Kiongozi wa Tanzania Dkt. E .Feleshi Mbuki) anaifahamu vizuri Kwimba.

Mheshimiwa Spika, mfano, Hakimu atoke Malya kwenda kutoa huduma Mahakama ya Ngulla au atoke Ngudu kwenda Mahakama ya Nyamikoma na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunaomba katika mpango wa kuwapatia usafiri watoa haki Wilaya ya Kwimba iwe mojawapo ya Mahakimu watakaopatiwa usafiri ikiwa ni pamoja na kutekeleza ahadi yake ya muda mrefu ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama katika Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Phillip Mahiga (Mb) kwa hotuba yake nzuri akiwasilisha mpango na makadirio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na jitihada kubwa ya kuboresha utendaji kwenye Mahakama na sehemu nyingine

muhimu katika kutoa haki kwa wananchi. Mimi ninaomba juhudi zaidi ziongezwe ili kutatua migogoro ya ardhi hususan vijijini. Mashauri ya migogoro ya mashamba vijijini yanachukua muda mrefu bila sababu za msingi wakati mwingine hadi wahusika wa kesi hizo wanafariki dunia na kesi hizo wanazirithi wasimamizi wa mirathi na bado kesi hizo wakati mwingine hata kuanza kusikiliza inakuwa bado.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema mimi nina maslahi kwenye suala hili. Kesi ya mgogoro wa shamba dogo tu lenye eneo la chini ya ekari moja lililomhusu mama yangu. Shamba ambalo amelilima mfululizo kwa miaka 19 hadi alipoambiwa na mwananchi mmoja kwamba eneo lile ni eneo lake yeye, Baraza la Kijiji likakagua eneo na kupitia vielelezo vyote ikiwa ni pamoja na mkataba wa ununuzi wa eneo na ushahidi wote wa kijijini na Baraza likaridhia kwamba shamba lile ni mali halali ya mama yangu. Mwananchi huyu kwa kutumia uwezo wake wa pesa akafungua upya kesi Wilayani na kuweka wakili. Miaka mitatu ya usumbufu ilichangia kumwongezea msongo wa akili, mama yangu amefariki akinung'unika kwa nini kesi haiishi akiwa ana uhakika eneo lile ni lake kihalali linalotaka kuporwa kwa njia za hila. Amefariki akiacha kesi na msimamizi wa mirathi nikiwa mimi ndiye nimeachiwa jukumu la kutetea haki ya marehemu. Tunaingia mwaka wa nne sasa.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la ucheleweshaji wa kesi za mirathi na hivyo kusababisha usumbufu mkubwa kwa warithi halali wa mali na madeni ya marehemu. Hakuna faida kutengeneza mlolongo wa mahitaji ya usikilizaji wa kesi hizo za mirathi kama inachukua miaka na miaka mpaka mali zinaharibika. Ninao mfano wa kesi ya namna hiyo iliyochukua miaka 20. Wizara ya Katiba na Sheria iangalie suala hili.

Mheshimiwa Spika, watoto wengi wa mitaani na wengine wanapitia wakati mgumu wa maisha kwa sababu wazazi wao, aidha wote wawili au mmoja wao hasa baba anakwepa wajibu wa kwanza wa malezi mema kwa mtoto. Wapo wazazi hawatunzi watoto wao ila anangoja muda fulani anaenda kudai mtoto wake. Mahakama ziwe na

maamuzi sahihi ya kumlinda mtoto na mama yake ambaye mara nyingi wanaonewa na kunyanyaswa na baadhi yetu sisi kina baba wanaokwepa majukumu muhimu ya malezi mema bora kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Waziri wa Katiba na Sheria. Pia nachukua fursa hii ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimae kuiwasilisha kwa ufasaha wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu elimu kwa watendaji wa Wizara. Wizara hii ni Wizara muhimu katika kulinda na kutoa haki za wananchi. Kutokana na sababu hizo watendaji wake wanatakiwa kuwa na elimu ya uhakika ili waweze kumudu kazi zao. Hivyo basi ushauri wangu katika suala hili kwa Serikali kuendelea kuwapatia elimu wafanyakazi wake ili waweze kutoa huduma kwa kujiamini zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara hii ya Katiba na Sheria kwa kuanza kujenga jengo la Mahakama ya Mwanzo katika Kijiji cha Mwandu na jengo la Mahakama ya Wilaya katika Makao Makuu ya Wilaya Igwachanya. Kwenye hotuba sijaona taarifa ya utekelezaji wa jengo la Mahakama. Ni lini jengo hilo litakamilika?

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Wanging'ombe yenye vijiji 108, kata 21 ina upungufu mkubwa wa utoaji haki kwani kuna Mahakama za Mwanzo tatu tu za Mwandu na Wanging'ombe katika majengo chakavu Mdandu, Kipengere na Wanging'ombe. Kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu na hivyo kusababisha mrundikano wa mashauri na kesi kuchukua zaidi ya miaka mitano mpaka kumi bila kutoelewa hukumu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iajiri mahakimu. Natambua wapo wahitimu wengi wa taaluma ya sheria ngazi ya shahada ambao wamesajiliwa na *Law School* wako mitaani zaidi ya miaka mitano.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii asilimia mia moja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Ssheria pamoja na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya kuhakikisha Wizara hii inaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa mwakilishi wa wanawake wa Mkoa wa dar es Salaam kwa kipindi cha miaka mitano wakati huo Mkoa wetu ulikuwa hakuna Mahakama za Wilaya, lakini mpaka sasa Wilaya zote za Mkoa wa Dar es Salaam zina Mahakama nzuri sana za Wilaya zenye majengo mazuri na ya kisasa. Naipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa ya ujenzi wa Mahakama hizo za Wilaya. Lakini kubwa nashukuru sasa kuona Mahakama za Mwanzo za Mkoa wa Dar es Salaam sasa nazo zimeanza kujengwa ikiwemo Mahakama ya Mwanzo ya Temeke ambayo ilijengwa kabla Mimi sijazaliwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa Kutekeleza Ilani yake ya ujenzi wa mahakama. Pia uanzishwaji wa Mahakama za Magari inasaidia sana katika kupunguza msongamano wa kesi mahakamani. Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kusaidia kufifilisha makosa na kutoa msamaha kwa wenye makosa ya uhujumu uchumi, jambo hili ni kubwa sana na watu hawa walikuwa wanajaza

mahakama na hakuna wanachorudisha kwa Taifa zaidi ya kutia hasara ya kuwalisha na kuwahudumia. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Sasa naishauri Serikali pamoja na juhudi kubwa za Serikali kufanya mabadiliko ya sheria mbalimbali ambazo zimekuwa na ukakasi na kuzifanya kuwa rafiki kwa wananchi na wawekezaji, nakupongeza sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa mliyoifanya kwa kutunga sheria nzuri. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, ombi langu bado kesi ambazo hazina maana zinawekwa muda mrefu, ni vyema sasa tukawa na mahakama za papo kwa papo kwa makosa madogo madogo kuepusha msongamano magerezani. Elimu itolewe juu ya ufifilishaji makosa kwani wananchi walio wengi bado hawajua mabadiliko ya sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi hiyo. Pia naishauri Serikali iwalipe wazee wa Baraza posho zao kwa wakati ili ziweze kuwasaidia na kuepuka kupokea rushwa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuharakisha kesi zisikilizwe ili kuondoa msongamano wa mahabusu katika magereza yetu. Pia naishauri Serikali iboreshe maslahi ya watumishi wa mahakama ili waweze kufanya kazi kwa weledi hii itaepusha na itazuia mianya ya rushwa.

Naishauri Serikali iongeze jitihada ya kujenga mahakama katika Wilaya zote ili kurahisisha kesi kusikilizwa kwa wakati na kuondoa msongamano. Aidha, naishauri

Serikali ijenge vyuo vya kutosha ili kuweza kupata wanasheria wengi na wenye weledi.

Mheshimiwa Spika, mwisho Serikali iajiri wanasheria wengi katika mahakama zetu.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana Wizara kwa kuanza ujenzi wa mahakama katika maeneo ambayo hayana mahakama au mahakama zake ni chakavu. Naomba Wizara isaidie ujenzi wa mahakama katika maeneo ambayo yamesahaulika mfano katika Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe tuna mahakama moja tu inayofanya kazi au ambayo jengo lake linatumika nayo ni Mahakama ya Lupembe. Jengo la Mahakama hii ya Lupembe ni bovu, limechakaa sana na lipo kwenye hifadhi ya barabara, wananchi walitoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa mahakama, lakini mpaka leo haijajengwa. Tunaomba Wizara na Serikali kwa ujumla ione umuhimu wa kujenga mahakama hii ili mazingira ya utoaji haki yaweze kuboreshwa.

Pia tuna mahakama chakavu katika kata yetu ya Mtwango eneo la Sovi, jengo hili ni chakavu na halitumiki tena, hivyo wananchi hutakiwa kwenda Makambako au Njombe Mjini ili kutafuta haki. Hivyo tunaomba eneo hili nalo jengo la mahakama livunjwe na lijengwe upya.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na msongamano mkubwa sana kwenye magereza yetu kutokana na mahakimu kupendelea zaidi hukumu za kifungo cha ndani, Mahakimu waone umuhimu wa kutoa adhabu mbadala kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu bado kuna ucheleweshwaji wa upelelezi wa kesi mbalimbali na kusababisha msongamano mkubwa kwenye mahabusu za

magereza zetu. Napendekeza kuwe na muda maalum wa upelelezi na muda huo ukiisha basi kesi iweze kufutwa. Hii itapunguza msongamano mkubwa uliopo kwenye mahabusu nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Watanzania kupitia nafasi zao tuungane wote kwa kuitikia kauli ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wetu mpendwa, aliyoitoa juzi ya kuliombea Taifa letu na dunia nzima kwa ajili ya janga hili la hatari la Corona. Hakika hili ni janga kubwa sana litakaoathiri ustawi wa jamii, kwa kupoteza maisha ya watu kote duniani.

Mheshimiwa Spika, sisi Bunge kama muhimili wa Serikali tupate nafasi ya kujadili suala la Corona kama ugonjwa kwa ratiba ya siku moja ya muda wa kipindi cha asubuhi kuanzia saa tatu mpaka saa sita ili baadaye saa nane tuendelee na ratiba yetu ya bajeti, pia nashauri Bunge liweze kurushwa na vyombo vya habari muda huo.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, Mawaziri, watendaji na waandamizi wote Serikalini, kwa jinsi alivyoongoza nchi yetu kwa miaka mitano hakika umechelewa kupata. Mungu aendelee kuwabariki wakati wote wa uhai wenu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuishauri Serikali kupitia hoja ya Wizara hii, kwanza nakiri kuwa kuna mabadiliko makubwa sana katika utoaji wa haki kupitia mahakama zetu kuliko tulikotoka. Hivyo basi yanahitajika marekebisho madogo. Pia kuwepo kwa mahabusu katika Mahakama za Mwanzo ili kupunguza mrundikano wa mahabusu katika Magereza ya Wilaya; masharti ya utoaji wa dhamana utazame upya kulingana na uzito wa kesi ulivyo ili kupunguza idadi kubwa ya mahabusu; Serikali iajiri mahakimu wa ngazi za Mahakama ya Mwanzo na Wilaya kwa kuwa ndiko waliko

wahalifu wengi; Serikali ijenge Mahakama za Mwanzo kila tarafa nchini ili kupeleka huduma ya kisheria na maadhimisho ya siku ya sheria nchini zitumike kutathimini huduma ya utoaji haki kwa wananchi kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara ifanye mapitio ya majengo ya mahakama kote nchini kwa kuwa majengo mengi yaliyojengwa wakati wa uhuru yamekuwa hatarishi; Mabaraza ya Ardhi yapewe maelekezo ya muda wa kutoa nakala ya hukumu ili kuondoa urasimu, ubabaishaji na ucheleweshaji usio wa lazima baada ya hukumu kutolewa na Kamati ya Maadili ya Mahakama chini ya Wenyeviti wake ambao ni Wakuu wa Wilaya na Mikoa wafanye vikao vya tathimini walau mara mbili kwa mwaka ili kutazama yaliyojiri katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kuniwezesha kutoa mchango wangu leo kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake kwenye Wizara hii, kwa utendaji wao na kwa namna wanavyoisimamia sekta hii ya kutoa na kusimamia haki hapa nchini.

Pili nichukue fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna anavyoisimamia na kuhakikisha haki na amani ya nchi yetu inadumishwa, kwa kudumisha utawala bora na utoaji haki kwa usawa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi nilizozitoa hapo juu, sasa naomba kuishauri Serikali kwa mambo yafuatayo katika kuboresha ufanisi huo.

Mheshimiwa Spika, kwanza ujenzi wa majengo ya mahakama nchini. Kumekuwa na *speed* ndogo sana za ujenzi wa majengo ya mahakama nchini hasa kwa Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya, kwani kwa sasa kuna uhaba mkubwa wa majengo ya taasisi hii katika Tarafa na Kata mbalimbali hapa nchini. Jambo hili limekuwa likiwanyima haki watu mbalimbali hasa wanapohitajika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hii. Mfano katika Wilaya yangu ya Liwale yenye Tarafa tatu na Kata 20 ina majengo mawili tu ya Mahakama za Mwanzo. Cha kusikitisha zaidi Wilaya hii pamoja na ukongwe wake, kwani Liwale ni Wilaya tangu mwaka 1975, lakini hadi leo haina jengo la Mahakama ya Wilaya. Hapa naomba niishauri Serikali inapogawa hii keki ndogo tuliyonayo ikazingatia mahitaji halisi, kwani ziko Wilaya za hivi karibuni zimepatiwa miradi ya ujenzi wa majengo haya wakati zile Wilaya za zamani zimesahauliwa. Wilaya ya Liwale ina umri wa miaka 45 sasa, lakini haijawahi kuwa na mradi wa majengo ya Mahakama ya Mwanzo wala Mahakama ya Wilaya tangu nchi hii imepata uhuru.

Pili ni kuhusu uhaba wa mahakama na vitendea kazi. Pamoja na uhaba wa ofisi za Mahakama sehemu mbalimbali nchini, liko pia tatizo la uhaba wa mahakimu na vitendea kazi pale ambapo pana hizo ofisi za mahakama. Hii inaenda sambamba na mahakimu wengi kukaa kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu, jambo linaloweza kupelekea kutokupatikana kwa haki kunakosabishwa na baadhi ya mahakimu kukosa weledi kutokana na kukaa muda mrefu kituoni. Mfano Wilaya yangu ya Liwale imekuwa ikiazima mahakimu toka Wilaya jirani ya Nachingwea, kwani pamoja na kukosa jengo la Mahakama ya Wilaya bado kuna uhaba mkubwa wa watumishi wa kada hii. Lakini hata wale waliopo wachache wamekuwepo kituoni kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vitendea kazi bado ziko mahakama ambazo zina uhaba mkubwa wa vitendea licha ya kukosa vitendea kazi vya kisasa, pia baadhi ya mahakama zinakosa hata vile vifaa muhimu kwa uendeshaji wa siku kwa siku.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba nigusie habari za Wazee wa Mahakama kwani wamekuwa wakisahauliwa muda mrefu bila kupewa posho zao, pamoja na kuwa posho hizo bado ni kidogo sana. Naiomba Serikali kuangalia upya utaratibu mzima wa uwendeshaji wa mashauri katika ngazi za Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya ili kutatua tatizo hilo na kupunguza mianya ya rushwa na ucheleweshaji wa mashauri.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu mrundikano wa mahabusu magerezani. Suala la mahabusu kurundikana magerezani bado ni changamoto kubwa hapa nchini. Pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano ya kupunguza tatizo hili bado tatizo hili ni kubwa nchini. Hapa naiomba Serikali kufanya mapitio ya sheria mbalimbali ziletwe hapa Bungeni kufanyiwa marekebisho ili kupunguza tatizo hili ikiwa ni pamoja na kupunguza masharti ya dhamana kwa mahabusu na kuharakishwa kwa mashauri mahakamani na pengine kuweko na ukomo wa upelelezi wa kesi za jinai ili kesi zilizokosa ushahidi wa kimahakama zikafutwa na watuhumiwa kuachiwa huru. Katika hili wako wanaohukumiwa bila hatia, kwani mtu aliyekaa mahabusu kwa miaka zaidi ya mitatu hata akiachiwa kuwa hana kesi ya kujibu, kukaa kwake mahabusu kwa muda mrefu ni sawa na kifungo.

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu kesi kuchukua muda mrefu; pamoja na juhudi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano katika kuhakikisha mashauri hayakai muda mrefu mahakamani, lakini tatizo hili katika baadhi ya mahakama hapa nchini ucheweshaji wa kesi bado ni mkubwa. Inawezekana ucheleweshaji huo ukachangiwa na baadhi sababu nilizoziainisha hapo juu. Hapa pia naiomba Serikali kufanya mapitio ya sheria ili ziletwe hapa Bungeni ili kufanyiwa marekebisho na kuona namna bora ya kuharakisha kasoro hizo na ikiwezekana kukawepo na vifungo vya nje kwa makosa madogo madogo. Hii itasaidia pia kupunguza wafungwa magerezani hasa wale wafungwa wazee, wajawazito na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo hapo juu napenda nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa John J. P. Magufuli kwa kusimamia utawala wa sheria, unaolenga kudumisha haki na amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa 100%.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Mwanzo Tabora Manispaa iko katika hali chakavu wakati wa masika maji hujaa ndani hushindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, pia niiombe Serikali kulipa madai ya Wazee wa Baraza ya muda mrefu na waongezwe posho kidogo.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa ya kuchangia kwa maandishi na nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya katika kusimamia Sheria na Katiba za nchi.

Nampongeza pia Rais kwa usimamizi mzuri wa Serikali, ni kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano tunaona namna nchi inavyoongozwa kwa maadili ya hali ya juu.

Mweshimiwa Spika, natumia fursa hii kuishauri Serikali yangu ya CCM kuhusu namna inavyoweza kuepusha mlipuko wa ugonjwa huu wa COVID-19 unaosumbua dunia kwa ukosefu wa chanjo na tiba.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kuna baadhi ya magereza nchini, hususani ya mijini yamekua na msongamano wa wafungwa. Ni maoni yangu kwamba Serikali ianze kuratibu namna ya kuwasambaza wafungwa kutoka kwenye magereza yenye msongamano mkubwa kwenda kwenye magereza yenye nafasi. Ni matumaini yangu

Serikali italifanyia kazi kabla janga hili la COVID-19 halijavamia magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Kabudi, itabidi uende kwa dakika 10 halafu *AG* na Waziri mtagawana dakika 15, 15.

Mheshimiwa Profesa Kabudi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu ambaye ameturuzuku uhai na kutujalia afya njema katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru na kuwaambia Watanzania mimi ni mzima mpaka sasa kwa neema ya Mungu na sijafungiwa mahali popote kwa sababu ya *Covid19* kama ambavyo baadhi ya mitandao imekuwa inawaambia watu. Mmeniona dhahiri nipo, muendelee kuniombea hilo liniepuke na wale waliodhani sipo, basi wameniona mzima sijafichwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mahiga kwa hotuba nzuri aliyoitoa. Nataka kuanza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunaomfahamu Mheshimiwa Dkt. Mahiga akiwa mwalimu sisi tukiwa wanafunzi wa shule ya sekondari tungeshangaa sana kama asingefanya vizuri kama alivyofanya. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe aliweka msingi, sisi wengine tukawa wajenzi na Mzee Mahiga amefanya *finishing* ya nyumba hiyo vizuri kabisa kama tunavyomfahamu. Ndivyo nilivyowaambia wafanyakazi wa Wizara ya Katiba na Sheria siku namkabidhi ofisi kwamba mmepata bahati sasa ya kupata Waziri atakayeitengeneza hii nyumba ipendeze. Kwa hiyo, nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa msingi mzuri aliouweka, sisi wengine tutabeba lawana lakini nimshukuru kwa dhati kabisa

mwalimu wangu Mheshimiwa Dkt. Mahiga kwa kazi nzuri aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapongeza wafanyakazi wote wa Mahakama na Wizara ya Sheria. Mimi na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe tunayo bahati isiyokuwa ya kawaida ambayo walimu wote huifurahia. *Chief Justice* Ibrahim Juma ni mwanafunzi wangu nimemfundisha *Criminal Law, second year Land Law;* Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Kilangi nimepata heshima ya kumfundisha *Jurisprudence* na *Human Rights Law; Solicitor General,* Clement Mashamba nimepata heshima ya kumfundisha *Jurisprudence* lakini sitaki kuwataja Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Ndumbaro; hakuna fahari kubwa kama hiyo. Mimi na Mheshimiwa Mwakyembe tulipata bahati *rare* kabisa *Faculty of Law*, sisi ndiyo walimu tuliofundisha masomo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Profesa Mchome mwanafunzi wangu wa *Land Law second year* na mwaka huo mimi nafundisha *Land Law,* Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe anafundisha *Administrative Law* na ndiyo mwaka naoa. Kwa hiyo, harusi yangu na Amina, wanafunzi wa *second year* ni pamoja na Mchome walishona sare lakini bado palikuwa na *supplementary* mbili. Kwa hiyo, niwashukuru wale wote ambao bado wameendelea kuniheshimu mimi na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na tunawashukuru wale wote ambao wamebeza tulivyowatengeneza mpaka wakafika kwa sababu wote hao Mwenyezi Mungu amewaweka duniani ili mambo yawe mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tumekuwa kwenye Mkutano wa Haki za Binadamu kule Geneva ulioanza tarehe 24 Februari mpaka tarehe 20 Machi na nilipata heshima ya kwenda kuiwakilisha nchi yetu. Baada ya kuwaeleza hatua kubwa tulizozifanya na jambo kubwa ambalo tumefanikiwa kubadilisha upepo katika *Human Rights Council,* miaka yote mijadala mikubwa imekuwa kwenye haki ya siasa *(civil and political rights)* lakini walisahau haki za kijamii, haki za kiuchumi na haki za kiutamaduni.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya Mheshimiwa Olenasha anisamehe, naye ni mwanafunzi wangu wa *Jurisprudence,* nilikuwa nimemsahau. Naye nilimfundisha *Jurisprudence* na *Environmental Law,* nilisahau kumtaja. Kwa hiyo, ni bahati *very rare* kuna wanafunzi hawa wote ndani ya Baraza la Mawaziri lakini ni pia ni bahati pia *very rare* kwa Mzee Mheshimiwa Mahiga ana wanafunzi wake wa shule ya sekondari ndani ya Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Je, Naibu Spika?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, Naibu Spika yeye nilipata bahati siyo tu ya kumfundisha darasani lakini kumsimamia *Masters.* Miongoni mwa watu ambao nina fahari nao kubwa ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu ambaye nataka nitamke nilihakikisha anakwenda kufanya *PhD* Cape Town. Lengo langu ilikuwa Mheshimiwa Dkt. Tulia awe ndiyo the *first female Dean of Faculty of Law* lakini kumbe Mungu alimpangia makubwa. Mimi nilimuazimia awe *my first female Dean* kumbe Mungu alijua atakuwa Naibu Spika.

Kwa hiyo, kama kuna mtu nina fahari naye kubwa ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, *she is a product of my hands and I am very proud of her and she hasn't let me down. (Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Waziri, wanakulia dakika zako.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, tumefanya mambo makubwa ambayo dunia yote sasa inayakubali katika kusimamia haki ya elimu. Unajua wenzetu wanaona elimu ni huduma, sisi elimu ni haki na tumeifanya ndani ya kipindi hiki, elimu bila malipo shule ya msingi na sekondari. Wafaidika wakubwa wa elimu bila malipo ni watoto kutoka kwenye

familia maskini na familia za kawaida, hiyo nayo ni haki ya binadamu na tume-*score A. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya juhudi kubwa sana kwenye haki ya afya. Idadi ya vituo vya afya, zahanati na hospitali, fedha inayotolewa kwa ajili ya dawa na vifaa tiba haijawahi kutokea. Hiyo nayo ni haki ya binadamu ambayo tumefanikiwa. Vilevile, haki ya kupata majisafi na salama, hiyo nayo tumepiga hatua kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningewaomba Watanzania tunapojadili haki za binadamu, tusisahau kuona maendeleo makubwa ambayo yamefanywa na Tanzania ndani ya miaka hii minne katika hizi haki za msingi kabisa kwa watu wetu. Kwa hiyo, niliona hilo nilieleze ili liwe bayana kwa kila mmoja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Tanzania imesaini na kuridhia mikataba mingi sana. Ipo mikataba ambayo Tanzania haijasaini wala kuridhia na haijafanya hivyo kwa sababu ya kuvunja haki za binadamu, ni kwa sababu inazo sababu za msingi za kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, imezungumzwa sana kuhusu huu Mkataba wa Mambo ya Uchaguzi, Demokrasia *(African Charter on Democracy, Elections and Governance).* Nchi ambazo hazijasaini wala kuridhia mkataba huu ni pamoja na Botswana na huwezi kuiweka Botswana katika ligi ya nchi ambazo zinatiliwa alama ya kuuliza. Nyingine ni Cape Verde, Kenya, Mauritius, Senegal, Tunisia na Uganda na nataja Uganda kwa sababu imetolewa mfano ndani ya Bunge hili lakini zote hizi hazijasaini wala kuridhia mkataba huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu za Tanzania kusita kusaini mkataba huu ni kwa sababu unazo changamoto mbalimbali ambazo zilijidhihirisha hata wakati wa *negotiations.* Tafsiri ya *democracy* mpaka sasa hatujafika kuafikiana, sisi kama Bara la Afrika na ulimwengu *democracy*

ina *constitute* vipi na vipi. Zipo nchi ambazo zina *time limit* ya Marais wao na kuna nchi ambazo hazina *time limit.*

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ibara ya 3 na Ibara ya 23 ya Mkataba huu kuna kitu kinaitwa *unconstitutional change of government* na mpaka sasa hatujaafikiana ni nini inacho-*constitute unconstitutional change of government.* Sasa hamuwezi mkasaini mkataba ambao una dhana ambazo bado hamjakubaliana nyote ni nini *ingredients* za dhana hiyo. Hiyo ndiyo moja ya sababu ambayo iliifanya Tanzania, Botswana, Kenya na nchi nyingine zisisaini kwa sababu bado hatujakubaliana *what constitutes unconstitutional...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Malizia Mheshimiwa Waziri, naona dakika zimeisha.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa...

**SPIKA:** Ndiyo la mwisho, tafadhali.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba Ibara ya 23 pia ina matatizo. Kwa hiyo, nilitaka nieleze kwamba Tanzania haijasita kufanya hivyo eti kwa sababu ya kuogopa uchaguzi, hapana mkataba wenyewe una kasoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga tena mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Profesa Palamagamba Kabudi, ama kweli wewe ni mahiri katika uwanja wa sheria na wakijua hilo ndiyo maana Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi wamekimbia, walipojua unafuata tu wakatoka mbio sana humu ndani na hasa waliposikia Mwanasheria Mkuu

ndio anayefuatia ndiyo kabisa, nimeona ule mlango wanaona kama haufunguki haraka. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tafadhali, tuna robo saa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwa sababu ya muda nitaomba nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge lakini nianze kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wa Mheshimiwa Shangazi alizungumzia majukumu ya *DPP* lakini akiyahusanisha na suala la mrundikano wa mahabusu magerezani. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Shangazi kwamba mrundikano wa mahabusu magerezani hasa kwenye magereza ya mahabusu kuna sababu mbalimbali na moja wapo ikiwa ni ukweli kwamba mahabusu hizo zilijengwa kipindi cha zamani ambapo *population* ya mahabusu na wafungwa ilikuwa ndogo na bado tunaendelea na majengo hayohayo kwa hiyo hayatoshi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, zipo hatua kadhaa ambazo zimechukuliwa na zingine zinafahamika vizuri na Waheshimiwa Wabunge. Ya kwanza ilikuwa ni ile kupitisha Sheria ya *Plea Bargaining* kwa ajili ya kuharakisha ule mfumo wa utoaji wa haki jinai. Hii ina maana kwamba kama kuna mtu anafikiri anataka kukiri basi asisubirishwe mpaka apite kwenye ule mchakato mzima, anaweza kuharakisha huo mchakato na atakuwa amepunguza idadi ya waliopo mahabusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tuliona hata kwenye ile Sheria ya *PCCB* tuliifanyia marekebisho katika Bunge hilihili kwa ajili ya kuweza kutoa *consent* kwa *DPP* katika kesi ambazo siyo kubwa ili kusudi mashtaka yaweze kuendelea katika ngazi za Mikoa na Wilaya huko.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia kulieleza hili pengine inaweza kuwa ngumu kwa Mheshimiwa Waziri kulisemea yeye mwenyewe. Mheshimiwa *DPP* wakishirikiana na Mheshimiwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii wamefanya kazi kubwa sana ya kupita katika magereza mbalimbali nchini kote. Mara nyingi yanayofanyika huko huwa hayatangazwi lakini wamepitia na kukutana na mahabusu wamehojiana na kuzungumza nao na kwa kweli kuna watu wengi tu ambao waliona kwamba hawastahili kuwa mahabusu na hatua zilichukuliwa kwa mujibu wa sheria na wakaweza kutoka. Hizi ni mojawapo ya hatua ambazo zimechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shangazi aligusia kidogo kuhusu suala la *Law School* lakini hasa alikuwa ana-*concern* kuhusu Msimamizi wa Chuo aliposema ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na alipendekeza ingefaa awe Jaji. Napenda tu kumfahamisha kwamba Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria yeye ni Mwenyekiti wa Bodi ya *Law School* na siyo msimamizi wa chuo moja kwa moja. Kwa hiyo, msimamizi wake yupo na vigezo au *qualifications* za huyo msimamizi zipo; anatakiwa awe ni mtu ambaye amefikia ngazi au ana *qualification* za kuweza kuwa *Associate Professor* lakini pia ame-*practice* sheria kama Wakili kwa muda uliotajwa hapo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *qualification* za walimu wa pale, kwa kiasi kikubwa tumejiridhisha kwamba wengi wana-*qualify* vizuri, ni Mawakili wa muda mrefu lakini pia wanayo elimu ya kutosha. Nafikiri wanatosheleza. Pamoja na hayo, kama kuna mahitaji ya maboresho tunayatazama kila siku.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ally Saleh alizungumzia Sheria ya Uhujumu Uchumi na akaihusanisha na suala la *plea bargaining* na akasema ina changamoto. Napenda kusema tu kwamba malengo ya sheria hizi zote mbili ni mazuri kabisa, Sheria ya Uhujumu Uchumi kwa sababu kuna tatizo limekuwepo katika jamii na tunataka tukabiliane nalo lakini pia na *plea bargaining* sheria ambayo kwa kweli kimsingi ni Wabunge wenyewe ndiyo walioleta maombi hapa, nadhani ile Kamati ya Katiba na Sheria ni mashahidi

wamekuwa wakitoa pendekezo hilo na baadaye Serikali ikalitilia maanani.

Mheshimiwa Spika, niseme changamoto huwa zinajionesha wakati wa utekelezaji wa sheria. Hii tumeisema mara nyingi kama zipo changamoto hazituzuii kuzitazama upya na kuangalia kama kuna mahali ambapo panahitaji kufanyiwa marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini aligusia pia kesi ya Uamsho; pengine ni vizuri kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali nilitolee maelezo hili kidogo kwa sababu limekuwa linajirudiarudia. Tulieleza wakati fulani kwamba kulikuwa na mazingira maalum au kuna umaalum wa kimazingira uliokuwa unasababishwa na kesi hizi ambayo yalihitaji utaratibu maalum wa kisheria kuweza kuzisimamia, kwa mfano, utaratibu wa utoaji wa ushahidi.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulileta mapendekezo na mabadiliko ya sheria hapa Bungeni na Bunge liliridhia kupitisha mabadiliko ya utaratibu wa namna ya kuchukua ushahidi na mojawapo ya maeneo lengwa yalikuwa ni maeneo hayo. Kwa hiyo, hilo lilipita sasa baada ya kikwazo hicho kuwa kimeondoka nimefahamishwa na Ofisi ya Mwendesha Mashitaka Mkuu wa Serikali kwamba mashtaka ya watu hawa yanaweza kuanza muda wowote. Kwa hiyo, hili jambo sasa litakuwa limefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salome Makamba, *learned sister* amezungumza kiaina yale yaliyokuwa kwenye hotuba yake. Amezungumzia kwamba kuna upungufu katika Katiba na sheria na hasa zinazogusa masuala ya uchaguzi, nafikiri hata Mheshimiwa Sabreena ameligusia jambo hilo pia.

Mheshimiwa Spika, kimsingi ipo Wizara maalum inayoshughuika na masuala ya uchaguzi, nafikiri masuala haya yalitakiwa kuletwa wakati Wizara hiyo inawasilisha hotuba na hoja yake. Hata hivyo, napenda tu kusema kwa ujumla na hili linajulikana kwamba kama zipo *concern* zozote kuhusu Katiba, sheria na kanuni upo utaratibu katika Katiba

hiyohiyo, sheria na kanuni hizohizo wa kuzileta hizo *concerns* ili ziweze kufanyiwa kazi na Bunge hili. Kwa hiyo, kama zipo *concerns* basi utaratibu upo utumike.

Mheshimiwa Spika, lakini aliibua hoja kuhusu *plea bargaining* tena na alikuwa anaihusanisha ni wazi na suala la mrundikano wa kesi na mrundikano wa mahabusu. Kuna kitu kimoja alichokisema ambacho si sahihi ni lazima nikirekebishe kwamba *DPP* anawaita na kuwalazimisha watuhumiwa wakiri makosa na ili aweze kukusanya fedha. Nimezungumza hapo awali Sheria ya *Plea Bargaining* ilitokana na ushauri na maombi ya Wabunge wenyewe. Kama nilivyosema ile Kamati ya Katiba na Sheria inafahamu hilo vizuri na malengo yake ni mazuri na tulipewa na mifano mingi sana Marekani na kila sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusoma hicho kifungu kinachohusu *plea bargaining* Mheshimiwa Salome anachosema kwamba *DPP* anawalazimisha hawa mahabusu. Iliongezwa katika kile kifungu cha 194A cha *Criminal Procedure Act,* kinasema: *"The accused or his advocate or a public prosecutor may initiate* a *plea bargaining and notify the court of the intention to negotiate a plea agreement."*

Mheshimiwa Spika, kiutaratibu *plea bargaining* inaanzaje pamoja na maneno haya? Inaanza pale mtuhumiwa anapoandika barua kupitia kwa Mkuu wake wa Gereza akielezea nia hiyo ya kufanya *plea bargaining* na hiyo barua hatimaye ndiyo inamfikia *DPP*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, japokuwa sheria iko hivi, lakini kwa kweli katika utendaji ni lazima ianzie kwa mahabusu mwenyewe, anaandika kupitia kwa Mkuu wa Magereza. *DPP* asipopata hiyo barua iliyopitia kwa Mkuu wa Magereza hawezi hata kuitazama. Kwa hiyo, hapo sioni namna yoyote ambayo *DPP* ndio anaweza kwenda kuwashawishi hao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sheria imeruhusu kwamba anaweza akawashauri ingawa kiutendaji haiko

hivyo. Kwa hiyo, alichokisema Mheshimiwa Makamba naomba kiingie katika *record* kwamba siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, uko mchango pia wa Mheshimiwa Mbilinyi ambaye naye alitumia muda mwingi sana kuishambulia Ofisi ya DPP, Ofisi ya Mashitaka ya Taifa. Alisema, *DPP* anaingilia majukumu ya *AG,* lakini hata hakueleza anaingiliaje majukumu hayo. Pengine hafahamu juu ya mabadiliko aliyofanya Mheshimiwa Rais mwaka 2018 ya kuzitenganisha hizi Ofisi ya *AG*, *DPP* na akatoa pia Ofisi ya *Solicitor General.* Namshauri kwamba angeenda kusoma hizo sheria na akaona sasa majukumu ya Ofisi ya *AG* ni yapi, majukumu ya Ofisi ya *DPP* ni yapi na majukumu ya Ofisi ya *Solicitor General* ni yapi na kwa namna gani anaingilia majukumu ya *AG?*

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Mbilinyi alisema *DPP* anaingilia majukumu ya Mahakama, hayo nayo sielewi ni kivipi. Kwa sababu kama ni *plea bargaining* sheria iko wazi, majukumu ya *DPP* ni yapi na majukumu ya Mahakama ni yapi? Mwisho wa siku panapokuwepo makubaliano kati ya mtuhumiwa na *DPP* lazima makubaliano hayo yaende yakasajiliwe Mahakamani kwa Hakimu au Jaji mhusika.

Mheshimiwa Spika, pia Jaji hayapokei tu na kuyapitisha, ana haki ya kuyachunguza, kuyapima na kuweza kutoa uamuzi wake. Pia anaweza akakataa akasema kwamba japokuwa kuna makubaliano haya, lakini mimi naona kuna changamoto hiyo. Kwa hiyo, sioni ni wapi *DPP* anaingilia mamlaka ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, baya kuliko yote na ningependa sana Mheshimiwa Mbilinyi angekuwepo hapa; lile la kusema watu wanakwenda na mifuko ya *sulphate* au sijui na kitu gani wanapeleka zile fedha kwa *DPP,* huu nao ni uongo mkubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya makubaliano haya na yanaposajiliwa na Mahakama, zile fedha zinalipwa kwenye akaunti ya Mahakama. Zile fedha zinalipwa kupitia akaunti

maalum, hazipelekwi mkononi. Kwa hiyo, nilimshangaa sana Mheshimiwa Mbilinyi kwa kusema kwamba zimepelekwa mkononi kwenye sandarusi, basi wakati mwingine unasema kwa kutojua sheria au taratibu unaweza kulazimika kuwahurumia watu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ngeleja ametoa ushauri mwingi ambao ni mzuri kabisa, tunauchukua kama Serikali. Hivyo hivyo Mheshimiwa Serukamba naye ametoa ushauri mwingi mzuri ambao kwa upande wa Serikali tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lema amependa kuiongelea Mahakama Bungeni. Pamoja na mwongozo wako na ushauri wako bado ameona ni muhimu na ni lazima na pengine hakuna sehemu nyingine ya kuweza kuizungumzia Mahakama.

Mheshimiwa Spika, ushauri wako na maelekezo yako yalikuwa yana msingi wake katika sheria na kuanzia katika Katiba. Napenda nimwelekeze Mheshimiwa Lema kwenye Ibara ya 107B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayozungumza juu ya namna ya kuhusiana na huu mhimili wa Mahakama. Kwa hiyo, Mahakama inayo uhuru wake na hii ndiyo misingi ya kidemokrasia na pengine wakati mwingine tunapozungumza juu ya misingi ya kidemokrasia huwa hatujui, lakini uhuru wa Mahakama ni msingi mmojawapo wa kidemokrasia.

Mheshimiwa Spika, Mahakama haina nafasi ya kuja kujitetea wala kuzungumza hapa Bungeni, ndiyo maana hatutumii mhimili wa Bunge kuweza kuzungumzia mhimili wa Mahakama. Kwa upande wa Serikali inajulikana, Bunge linaisimamia Serikali, lakini pia Serikali ipo Bungeni, inaweza kujisemea kama kuna jambo lolote.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kama yapo malalamiko yoyote kuhusiana na utendaji wa Mahakama kwa maana ya mtu mmoja mmoja; Hakimu au Jaji, ipo mifumo na utaratibu wa kuangalia mambo hayo. Ndiyo

maana tunazo Kamati za Maadili ya Watumishi wa Mahakama. Zipo na zinafanya kazi na kama...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja niweze ku-*wind up.*

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kama kuna malalamiko yoyote yanapelekwa huko na hatua zimechukuliwa. Pia zipo Kamati za Maadili kwa ajili ya Majaji, kuna malalamiko yamepelekwa huko, maamuzi yamepitishwa lakini pia kuna Tume ya Utumishi wa Mahakama inafanya kazi zake kuangalia Watumishi wa Mahakama ambao wana tatizo.

Mheshimiwa Spika, vilevile bado kuna taratibu za Kimahakama zenyewe za mtu kukata rufaa, za kuomba *review* pamoja na nafuu nyingine ambazo zinatolewa na sheria.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema pia kwamba tumepokea pia mapendekezo ya kutoka Kamati ya Katiba na Sheria juu ya kuboresha weledi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakili Mkuu wa Serikali, *DPP* na kadhalika. Nimeshaeleza hapa mara nyingi kwamba ipo mipango mingi sana ya kujenga uwezo wa Wanasheria wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada hayo, nashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Profesa Kilangi kwa ufafanuzi mzuri sana ambao umetusaidia kuwa na uelewa mpana zaidi wa baadhi ya mambo muhimu sana.

Sasa nikuite Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga, Waziri wa Katiba na Sheria. Karibu tafadhali, dakika 15. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 15 wamechangia hotuba hii. Kati ya hao, Waheshimiwa Wabunge 16 wamechangia kwa kuzungumza ndani Bunge wakati Waheshimiwa Wabunge 17 wamechangia kwa njia ya maandishi. Haya maandishi yatajibiwa kwa maandishi na nina hakika kabisa kwamba yale ambayo tutayajibu yataridhisha.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe shukrani za pekee kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa mchango wenu mkubwa ambao mmeutoa ambao ni ushauri lakini pia ni mchango wa mawazo kuhusu Wizara yangu ya Katiba na Sheria. Nisingependa kuanza kuzungumzia suala moja moja la Mbunge mmoja mmoja kwa sababu Mwanasheria Mkuu amejitahidi sana kuzungumza na kueleza yale ambayo yaliibuliwa na Waheshimiwa Wabunge humu ndani, lakini kwa ujumla ni kwamba yale ambayo yamezungumzwa hapa yamechukuliwa na tunashukuru sana na tutaendelea kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, kama Waziri napenda kusema yafuatayo: Natoa shukrani kwa wale ambao wamenipa heshima kwamba nafanya nao kazi vizuri. Mheshimiwa Kabudi ananipa cheo kuwa mimi ni mwalimu wake, ni kweli nafurahi kuwa mimi ni mwalimu, lakini yeye alipokuwa shule, nami nilikuwa bado mwanafunzi Chuo Kikuu, nilikuwa napita tu pale Sekondari Tosamaganga natoa *lectures* na wakanipa heshima kwamba ni Mwalimu. Kwa kweli mpaka leo hiyo imeendelea, lakini nilikuwa bado mwanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kikubwa zaidi ni kwamba hawa ni wenzangu ambao nimefanya nao kazi. Katika utendaji kazi Serikalini nimekutana na watu wengi na nimejifunza mambo mengi na ninaendelea kujifunza. Katika nafasi hii ya sasa kama Waziri wa Katiba na Sheria nimethibitisha kwamba katika Serikali bora kuna mihimili mitatu. Mhimili wa Serikali ambayo ni *Executive*, Mhimili wa Utungaji Sheria ambapo ni Bunge hili chini ya Spika wetu na Mhimili wa Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi ambazo zinaendelea na nyingine zimeendelea haziwezi kusema zina ufafanuzi kama ulivyo wazi wa mihimili hii mitatu kama tulivyonayo sisi katika Katiba yetu. Kwa sababu katiba ni kitu hai na kinatekelezwa kwa hatua, mimi kama Waziri ambaye ni sehemu ya *Executive* na sehemu ya Bunge, lakini pia nina Mahakama nao kila siku; nimeshuhudia kwamba katika nchi yetu kweli lazima tujisifie kwamba hiyo *checks and balances* ya hizi nguzo tatu ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii niseme, mengi ambayo mmeyazungumza kuhusu Mahakama yanahusu miundombinu. Mheshimiwa Najma nadhani amesema yote; kwa kulinganisha miundombinu ambayo mliikuta hapa ninyi mnapoingia, nami nimeikuta kama Mbunge kuingia mwaka 2015 na hali ya leo. Mahakama zimejengwa nyingi na idadi kwa kweli ni kubwa. Kama mwenendo huu utaendelea, nina hakika katika miaka mitano ijayo chini ya uongozi wa Mheshimiwa John Pombe Magufuli kila Wilaya na hata Mahakama za Mwanzo zitakuwa zimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo haitoshi tu kujenga Mahakama; namshukuru Mheshimiwa Mbunge Asha ametoa mchango mkubwa sana kwamba hizi Mahakama lazima ziwe na uzio. Kwa hiyo, ni kitu kilikuwa kinakosekana. Hiki ni kitu muhimu, ni sheria ya usalama wa hizi Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mahakama lazima pia ziwe na watu ambao ni wataalam na wanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ameteua Majaji wengi kuliko ilivyo katika historia ya nchi hii na ametuagiza kwamba tuendelee kuhakikisha kwamba Mahakimu na Mahakama hizi tunazozijenga zina watumishi wa kutosha na tukishirikiana na wenzetu Wizara ya Utumishi tunajitahidi tuwezavyo kujaza nafasi hizi. Kwa mwenendo huu na mwelekeo huu, nadhani tutajibu suala la miundombinu na suala la watumishi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuongezea pale alipozungumzia Mheshimiwa Prof. Kabudi kuhusu aina ya haki za binadamu, akasisitiza jinsi Tanzania ambavyo tumezingatia haki za jamii, elimu, afya na makazi na kadhalika. Hizo ni sehemu ambazo hata katika Umoja wa Mataifa zimekuwa na hadhi na zinaitwa *Economic Human Rights.*

Mheshimiwa Spika, nisisitize pia kwamba Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora na Utumishi katika moja ya hotuba zake alieleza kwamba kati ya sifa ambazo nchi yetu inazo Kimataifa ni kuhusu suala la utawala bora kwa maana ya kupambana na rushwa. Katika *Transparency International,* Tanzania iko juu sana kati ya nchi ambazo zinaongoza katika kupambana na rushwa na kuwa na Serikali bora na Serikali yenye kuwajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukijumlisha yote hayo, tunayo Tume yetu ya Haki za Binadamu ambayo imeshakamilika na tumeiombea pesa na inafanya kazi. Katika kipindi kifupi tayari imeshapata utambulisho na kusifiwa kabisa Kimataifa kwa kazi ambayo wanaifanya. Masuala yote haya ni mchakato, masuala yote haya ni hatua. Kwa hiyo, kwa ujumla wote huu, Katiba na Sheria tunadhani tutatekeleza yanayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nisisitize. Kwenye dua kila siku Mheshimiwa Spika anapoomba dua huwa anasema haki na amani. Haki ni huduma muhimu kwa amani na utulivu ndani ya nchi. Mara nyingi haki inakosekana kwa watu wanyonge. Kama Serikali hii imejipambanua kwamba ni Serikali ya kutetea watu wanyonge, sisi kama Wizara ya Katiba na Sheria

lazima tulenge kutoa haki kwa wakati kwa wanyonge. Hilo ndiyo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ametuambia, anatuagiza na tunajaribu kutekeleza kwa kadri tunavyoweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeweza kusema mengi zaidi lakini kwa sababu hatuna muda wa kutosha naomba, mbali na kutoa hizi shukrani ambazo nimezitoa niongelee hili suala la *Corona* na nini Wizara yangu ifanye na hasa jinsi tunavyoweza kudhibiti *Corona* katika Magereza.

Mheshimiwa Spika, nimetembelea Magereza, nimeona hali ya mle ndani tukiwa na *DPP. DPP* amesamehe mahabusu wengi, lakini kwa aina ya mlundikano nilioshuhudia mle ndani katika Magereza mengi niliyotembelea, kama *Corona* itaingia pale watu watateseka, wataumia, wataugua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mapendekezo yaliyotolewa hapa kwamba kweli tukae tufikirie namna ya kutekeleza yale ambayo tumeagizwa katika kuzuia *Corona* hatua za kuchukua kuzuia *Corona* ndani ya Magereza ni muhimu sana; na siyo suala tu la Wizara yangu lakini ni suala tambuka. Hili nadhani lazima tutoe kipaumbele haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza niwatambue kama vile watu wengine walivyonitambua. Kuna baadhi ya watu ambao nao wanastahili kutambuliwa kwa uwezo wao, kwa maandiko yao na michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Salome, maandishi yako ingawa yalikuwa nje ya mstari, lakini umeonyesha ufafanuzi na weledi katika fani ya sheria na nadhani ukijiweka katika mstari sawa sawa *profession* yako itakupeleka mbali. Ila nina hakika kwamba uzalendo wako lazima uwe kitu cha kwanza kabla ya kuwa na misimamo ambayo inaleta utatanishi. Uwe mzalendo kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri hoja imetolewa na imeungwa mkono *over warmly* tunakushukuru sana, ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga mwanadiplamasia mbobevu, Mwanasheria mahiri, Waziri wetu tunakushukuru sana sana. Na hasa ulipomalizia kumpa mawaidha Mheshimwa Salome. Alichokuwa anasema Mheshimiwa Waziri ni kwamba uhamie CCM ili yakae vizuri sasa, napiga mstari kwamba sifa zote amekupa lakini bado moja tu hii akasema ukiwa mzalendo hapa yaani ndiyo alikuwa anamaanisha hivyo. Kwa hiyo, fanyia kazi hilo kabla ya Oktoba mwaka huu, ahsante sana. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge mkiangalia saa yetu mtaona muda hauko upande wetu kabisa, kwa hiyo tuliyokuwa tumejiandaa kwa ajili masuala ya sera basi tena itakuwa haiwezekani tena kwa sababu ya muda na ninyi wenyewe mnaona saa yetu. Kwa jinsi hiyo sasa ni wakati wa Bunge kuamua maombi kupitia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mahiga, kwamba Bunge sasa likubali kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa fedha 2020/2021 na kura zimekwisha pigwa. Waliosema ndiyo wameshinda tena kwa kura nyingi kabisa tangu tuanzie kipindi hiki cha Mkutano huu wa Bunge la Bajeti kura za leo za ndiyo ni nyingi zaidi. *(Makofi)*

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 12 – Tume ya Utumishi ya Mahakama ............................................... Sh.2,603,148,000

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali............................................................Sh. 7,071,723,000
Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu.......................Sh. 11,482,048,000
Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka..........Sh. 22,173,042,000
Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama...................Sh.106,562,977,000
Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria..........Sh. 10,504,398,000
Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.....................................................Sh. 5,659,636,000
Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria.........Sh. 1,980,161,000

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali....................................................................Sh. 433,200,000
Fungu 19 – Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali..........................Sh. 0
Fungu 35 – Ofisi ya Taifa ya Mashtaka............Sh. 3,520,000,000
Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama.................Sh. 69,875,000,000
Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria...........Sh. 8,566,318,000
Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora…….............................…………. Sh. 672,021,000

**SPIKA:** Kwa hiyo nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano ambao tumeendelea kuwa nao, katika kufanya kazi yetu hii na uzalendo mkubwa ambao Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkiuonyesha.

Katika mazingira haya ambayo tunalo janga, *pandemic* duniani ambalo linahusiana na corona tuendelee kushirikiana tuendelee kufanyakazi pamoja huo ndio uzalendo kwa nchi yetu, kwamba na sisi kipande chetu cha uwajibikaji tunahakikisha kinatekelezeka.

Kwa hiyo, kwa niaba yetu Waheshimiwa Wabunge tukushukuru tena Mheshimiwa Waziri na Mawaziri walikuwepo kabla yako Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe na Mheshimiwa Prof. Kabudi tukushukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa *teamwork* Katibu Mkuu Prof. Mchome unatupa kila aina ya ushirikiano sisi Bunge. Rafiki yangu Mpanju Ukumbi huu unaukumbuka wakati wa Bunge la Katiba Karibu sana, Naibu Katibu Mkuu. Lakini pia Mtendaji

Mkuu wa Mahakama karibu sana sana kwa kufanya kazi pamoja nasi vizuri bila tatizo lolote. *(Makofi)*

Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma, pamoja na Jaji Kiongozi, Majaji wote wa Mahakama ya Rufaa, Makahama Kuu na timu nzima ya Makahama wote kabisa.

Muhimili huu umesimama kama muhimili chini ya uongozi wa Jaji Mkuu wamekuwa wakifanya kazi *exemplary* tunawapongeza sana sisi kama Bunge tunajua kwamba bajeti ambayo mtaipata kama Wizara lakini kama mahakama ni ndogo. Lakini mnajitahidi katika udogo wake kutekeleza majukumu yenu vizuri sana mahakama zimejengwa baadhi yenu Waheshimiwa Wabunge hamjaziona mahakama hizi ambazo zinajengwa hivi sana. Kwa kweli ukuzitembelea mahakama hizi ni *master peace* zimejengwa vizuri sana hata *furniture* zake ni nzuri sana, zuri kabisa na mnakumbuka wengi mnafahamu hali ya mahakama majengo ya mahakama yalivyokuwa ni majengo makuu kuu, yamejaa popo *crack* ni machakavu mno yalikuwa. Mpaka wakati fulani zikawa zinatolewa hoja kwamba halmashauri za wilaya za sasa tuanze kujijengea mahakama za tofali za kuchoma na nini angalau maana yake zingekuwa bora bado kuliko hali ilivyokuwepo, yalikuwa ni majengo chakavu mno. *(Makofi)*

Lakini serikali hii ya Awamu ya Tano na uongozi huu kwa kweli mmejenga mahakama za heshimiwa, katika ngazi zote kabisa kabisa kabisa katika hili tunawapongezeni mno katika bajeti hii ya mwisho ya Bunge la Kumi na Moja kwa kazi hii kubwa sana ambayo mahakama wameifanya na wizara mmeifanya kwa ujumla wake. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais katika eneo hili tunajua ungwe bado ni kubwa yapo maeneo mengi yanahitaji kujengwa mahakama tunaamini kabisa zoezi hili litaendelea. *(Makofi)*

Lakini manaingia katika historia kama watu mmefanya mabadiliko makubwa sana katika majengo ya kimahakama. Lakini vilevile katika mfumo wa kimfumo

mtandao wa uendeshaji wa baadhi ya shughuli za mahakama ni jambo ambalo limerahisha mambo mengi sana ya utoaji haki kwa wananchi wetu wa Tanzania.

Mtendaji Mkuu nakukumbusha tu mahakama ya Kibaigwa bado bwana, tulikubaliana mwezi huu wa nne inaanza kujengwa Kibaigwa ni mji ambao hauna mahakama. Sasa pale sio mahali pa mahakama ya mwazo ya kijiji pale ni mji unaokuwa kwa haraka. Kwa hiyo, naomba ahadi hii Mheshimiwa Waziri naomba ahadi hii unisaidie kuisimamia.

*DPP* na *Solicitor General* hongereni sana kwa kazi, kazi zenu ni ngumu ni kubwa haya maneno ya hapa yasiwape tabu sana haya madogo ya humu ndiyo utamaduni wetu humu ndani. Lakini ninyi yawatie moyo zaidi mzidi kufanya kazi, kazi yenu ni kazi ya lawama kuna kazi duniani hapa ni za lawama, sasa hata ufanyaje basi wewe ndiyo unakuwa Mnyamwezi lazima ubebe huo mzigo sasa abebe nani? Kama siyo *DPP* na wenzako? *(Makofi)*

Mwisho Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe kwamba Mheshimiwa Rais ametushauri Watanzania na kutuomba sana kwamba tutumie siku hizi tatu kwa ajili ya maombi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge pia tujiunge na ushauri huu wa Mheshimiwa Rais, leo Ijumaa, kesho Jumamosi na Jumapili kila watu katika *level* ya familia, mmoja mmoja, kupitia madhehebu yetu mbalimbali ya dini na kadhalika kila mtu mahali pake tuiombee nchi yetu tulipombee Taifa letu. Kwa sababu ni ukweli tunapita mahali kuna tishio la janga hili. *(Makofi)*

Lakini Mheshmiwa Rais wetu ametutia moyo sana kama baba kwa kutuambia msitishike kuweni na moyo tufuate utaratibu tunaoambiwa na serikali. Sasa watu wengine oooh! ulitegemea atuambieje Rais wetu kwamba tuingie uvunguni sasa basi si litakuwa ni Taifa la ajabu sana

kwa hiyo ametupa moyo na tunapaswa kuwa na moyo. Lakini hakumaanisha kwamba sasa tufanye mambo valuvalu bila kujali tahadhali ambazo zitatakiwa kuchukuliwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tahadhali zinatakiwa kuchukuliwa lakini tujipe moyo tuchape kazi tuendeleza Taifa letu. Tusinyooshe tu mikono tukabakia yala yala hapa, tumuombe Mwenyenzi Mungu tuwajibike tuchukue hatua tuzingatie ushauri ambao tunaupata tusisahau kujiombea wenyewe na kuiombea nchi yetu tuweze kupita katika hili nalo kwa salama na hakika wale wenye imani kwa Mwenyezi Mungu lazima tunaamini kwamba hili nalo litapita mwenye matatizo ni yule ambaye hana imani maana ukiwa huna imani basi. *(Makofi)*

Mwisho niwajulishwe kwamba Mheshimiwa Nsanzugwanko alipata msiba mkubwa wa kufiwa na wadogo zake wawili kwa mpigo kwenye ajali ya gari kwa hiyo, ameelekea kule Kasulu kwa ajili ya mazishi tunawaombea kwa mwenyenzi Mungu aziweke mahali pepo peponi roho za marehemu hawa ambao ni wadogo zake na Mheshimiwa mwenzetu ni ajali kubwa na mbaya.

Lakini pia Mheshimiwa Waziri Simbachawene amefiwa na Baba yake Mzazi mapema leo mazishi yatakuwa jumatatu kule Kijiji cha Pwaga katika Wilaya ya Mpwapwa. Kwa hiyo, na yeye pia tunamuombea mzee wetu ili roho yake iweze kupokelewa na kukaa Mahali Pema Peponi. Amina.

Baada ya kuwa shughuli zilizopangwa katika shughuli za leo zimekamika hapa mezani, basi nichukue nafasi hii kuwatakia kila kheri katika *weekend* hii ushauri ni ule ule kutulia majumbani *social distance* kutoji-*expose* na masuala na makundi makundi na maeneo ambayo yana watu wengi bila sababu, safari za Dar es Salaam zisizokuwa na tija tuziache. Mheshimiwa Naibu alisoma hapa jana ushauri ambao tunautoa ikiwezekana wale wenye familia dogo kule Dar es Salaam basi mkiagiza waje Dodoma, kidogo Dodoma pana usalama salama kidogo kwa hiyo, sio mbaya sana ni ushauri tu unapima mwenyewe.

Basi naomba niarishe shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu tarehe 20 Aprili, 2020 siku ya ambayo tutakuwa na bajeti ya Wizara ya Madini.

*(Saa 12.13 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku Jumatatu, Tarehe 20 Aprili, 2020 Saa Nane Mchana)*